

شرح كتاب التوحيد

Sharh Kitaab-it-Tawhiyd

Mwandishi:

Imaam, Faqiyh, 'Allaamah na Shaykh
'Abdul-'Aziyz bin 'Abdillaah bin Baaz

Tarjama:

www.firqatunnajia.com

1. Haki ya Allaah juu ya waja na haki ya waja kwa Allaah	6
2. Fadhila za Tawhiyd na madhambi yanayosamehewa kwayo.....	16
3. Mwenye kuhakikisha Tawhiyd basi ataingia Peponi bila ya hesabu.....	24
04. Kuogopa shirki.....	36
05. Kulingania katika kushuhudia ya kwamba hakuna mungu wa haki isipokuwa Allaah	42
06. Tafisiri ya Tawhiyd na kushuhudia ya kwamba hapana mungu wa haki isipokuwa Allaah	49
07. Kuvaa cheni, uzi na mfano wavyo kwa ajili ya kuondosha au kuzuia dhara ni shirki	58
08. Kuhusu matabano na hirizi	60
09. Kufanya Tabarruk kwa mti, jiwe na mfano wake.....	67
10. Kuchinja kwa ajili ya mwingine asiyekuwa Allaah.....	72
11. Hakuchinjwi kwa ajili ya Allaah mahali ambapo kunachinjwa kwa ajili ya mwingine asiyekuwa Allaah	80
12. Kuweka nadhiri kwa asiyekuwa Allaah ni katika shirki	85
13. Kutafuta kinga kwa asiyekuwa Allaah ni katika shirki	88
14. Kutaka uokozi kwa asiyekuwa Allaah au kumuomba mwingine asiyekuwa Yeye ni katika shirki	92
15. Tawhiyd na ugeni wa dini.....	98
16. Mlango kuhusu maneno Yake (Ta'ala) "Mpaka itakapoondolewa fazaiko nyoyoni mwao [baada ya kuzimia]; watasema [wakiulizana]: "Amesema nini Mola wenu?" – waseme: "Ya haki; Naye yujuu, Mkubwa kabisa."	105
17. Uombezi	111
18. Mlango kuhusu maneno Yake (Ta'ala) "Hakika wewe huwezi kumwongoza umpendaye"	122
19. Kuchupa mipaka kwa waja wema ndio lililopelekea kukufuru kwa wanaadamu	127
20. Makatazo ya kuabudu makaburi au kumuabudu Allaah kwenye kaburi la mtu mwema .	133

21. Mlango kuhusu kuchupa mipaka katika makaburi ya watu wema hupelekea huyafanya kama masanamu yaabudiwayo badala ya Allaah	141
22. Himaya ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) kuihami Tawhiyd na kufunga kila njia inayopelekea katika shirki.....	145
23. Baadhi ya watu katika Ummah huu wataabudu masanamu	150
24. Mlango kuhusu uchawi	161
25. Mfano wa aina za uchawi.....	169
26. Kuhusu makuhani na mfano wao	178
27. Mlango kuhusu kuagua na kuondosha uchawi	184
28. Mlango kuhusu kuamini mkosi na nuksi	188
29. Mlango kuhusu unajimu	191
30. Mlango kuhusu kuomba kunyeshewa mvua kwa sayari	194
31. Mlango kuhusu maneno Yake (Ta'ala) "Miongoni mwa watu wako wenye kuchukua asiye kuwa Allaah kuwa ni mungu mshirika ambapo wanawapenda kama mapenzi wanavyompenda Allaah... "	201
32. Mlango kuhusu maneno Yake (Ta'ala) "Hakika huyo ni shaytwaan anawakhofisha marafiki zake. Basi msiwakhofu - na nikhofuni Mimi - mkiwa ni waumini!"	210
33. Mlango kuhusu maneno Yake (Ta'ala) "Kwa Allaah pekee tegemeeni ikiwa nyinyi ni waumini!"	216
34. Mlango kuhusu maneno Yake (Ta'ala) "Je, wameaminisha na mipango ya Allaah? Basi hawaaminishi mipango ya Allaah isipokuwa watu wenye kukhasirika."	221
35. Kuwa na subira kwa makadirio ya Allaah ni katika kumuamini Allaah.....	225
36. Kujionyesha.....	232
37. Mtu kufanya kitendo kwa ajili ya dunia ni katika shirki.....	236
38. Mwenye kuwatii wanachuoni na viongozi katika kuharamisha aliyohalalisha au kuhalalisha aliyoharamisha Allaah amewafanya ni waungu badala ya Allaah.....	241
39. Mlango maneno Yake (Ta'ala) "Je, huoni wale ambao wanadai kwamba wao wameamini yaliyoteremshwa kwako na yale yaliyoteremshwa kabla yako, wanataka wahukumiane	

kwa Twaaghuut na hali wameamrisha wakanushe hiyo, na shaytwaan anataka awapoteze upotofu wa mbali kabisa”	246
40. Anayepinga kitu katika majina na sifa za Allaah.....	254
41. Mlango kuhusu maneno Yake (Ta’ala) “Wanazitambua vyema neema za Allaah, kisha wanazikanusha - na wengi wao ni makafiri”	261
42. Mlango kuhusu maneno Yake (Ta’ala) “Hivyo basi msimfanyie Allaah washirika, na hali ya kuwa nyinyi mnajua.”.....	266
43. Mlango kuhusu ambaye hakuridhika kuapiwa kwa Allaah.....	274
44. Mlango kuhusu kusema “Akitaka Allaah na wewe”	277
45. Mwenye kutukana wakati amemuudhi Allaah.....	282
46. Kuitwa “qaadhi wa maqaadhi” na mfano wake.....	285
47. Kuyaheshimu majina ya Allaah na kubadilisha jina kwa ajili aa hilo.....	287
48. Mlango kuhusu anayekifanyia mzaha kitu kilichotajwa ndani yake jina la Allaah, Qur-aan au Mtume	290
49. Mlango kuhusu maneno Yake (Ta’ala) “Tunapomuonjesha rehema kutoka Kwetu baada ya dhara iliyomgusa, bila shaka husema: “Haya nayastahiki mimi na sidhani kama Saa itatokea.”	295
50. Mlango kuhusu maneno Yake (Ta’ala) “Lakini anapowapa [mtoto mzima na] mwema [waliyemuomba], wanamfanyia washirika katika kile alichowapa! Ametukuka Allaah kutokana na yale yote wanayoshirikisha!”	300
51. Mlango kuhusu maneno Yake (Ta’ala) “Allaah ana majina mazuri mno; hivyo basi muombeni kwayo”.....	305
52. Hakusemwi “as-Salaam iwe juu ya Allaah”	308
53. Mlango kuhusu msemu “Ee Allaah! Nisamehe Ukitaka”	310
54. Mlango wa kutosema “Mja wangu, kijakazi wangu”	314
55. Mwenye kuomba kitu kwa jina la Allaah asirudishwe nyuma.....	317
56. Hakuombwi kwa Uso wa Allaah isipokuwa Pepo tu.....	321
57. Mlango kuhusu ‘lau`	323

58. Makatazo ya kutukana upepo.....	328
59. Mlango kuhusu maneno Yake (Ta'ala) "Wakamdhanja Allaah pasi na haki, dhana ya kipindi cha kikafiri"	331
60. Mlango juu ya mwenye kupinga Qadar	337
61. Mlango kuhusu picha.....	344
62. Mlango kuhusu kuapa kwa wingi	350
63. Mlango kuhusu ahadi za Allaah na Mtume Wake.....	357
64. Mlango kuhusu kumuapia Allaah	364
65. Haombwi Allaah kupitia viumbe Wake.....	367
66. Mtume (صلى الله عليه وسلم) kuihami Tawhiyd na kuziba njia zote za shirki	369
67. Mlango kuhusu maneno Yake (Ta'ala) "Hawakumkadiria Allaah inavyostahiki kukadiriwa!"	373

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

1. Haki ya Allaah juu ya waja na haki ya waja kwa Allaah

Shaykh-ul-Islaam Muhammad bin 'Abdil-Wahhaab (Rahimahu Allaah) amesema:

1- Allaah (Ta'ala) amesema:

وَمَا خَلَقْتُ الْجِنَّ وَالْإِنْسَ إِلَّا لِيَعْبُدُونِ

"Na Sikuumba majini na watu wa isipokuwa waniabudu." (ad-Dhaariyaat 51: 52)

وَلَقَدْ بَعَثْنَا فِي كُلِّ أُمَّةٍ رَسُولًا أَنِ اعْبُدُوا اللَّهَ وَاجْتَنِبُوا الطَّاغُوتَ

2- "Na kwa yakini Tulituma katika kila ummah Mtume [awaamrishe watu wake] kwamba: "Mwabuduni Allaah na jiepusheni na Twaaghuut." (an-Nahl 16 : 32)

وَقَضَىٰ رَبُّكَ أَلَّا تَعْبُدُوا إِلَّا إِيَّاهُ وَبِالْوَالِدَيْنِ إِحْسَانًا

3- "Na Mola wako Ameamrisha ya kwamba, msiabudu yeyote isipokuwa Yeye Pekee. Na [amekuamrisheni] kuwatendea wema wazazi wawili." (al-Israa' 17 : 23-24)

وَاعْبُدُوا اللَّهَ وَلَا تُشْرِكُوا بِهِ شَيْئًا

4- "Na mwabuduni Allaah na wala msimshirikishe Yeye na chochote." (an-Nisaa' 04:36)

قُلْ تَعَالَوْا أَتْلُ مَا حَرَّمَ رَبِّي عَلَيْكُمْ ۖ أَلَّا تُشْرِكُوا بِهِ شَيْئًا ۖ وَبِالْوَالِدَيْنِ إِحْسَانًا ۖ وَلَا تَقْتُلُوا أَوْلَادَكُمْ

مَنْ إِمْلَاقٍ ۖ نَحْنُ نَرْزُقُكُمْ وَإِيَّاهُمْ ۖ وَلَا تَقْرُبُوا الْفَوَاحِشَ مَا ظَهَرَ مِنْهَا وَمَا بَطَنَ ۖ وَلَا تَقْتُلُوا النَّفْسَ الَّتِي
حَرَّمَ اللَّهُ إِلَّا بِالْحَقِّ ۚ ذَلِكُمْ وَصَّاكُمْ بِهِ لَعَلَّكُمْ تَعْقِلُونَ وَلَا تَقْرُبُوا مَالَ الْيَتِيمِ إِلَّا بِالَّتِي هِيَ أَحْسَنُ حَتَّىٰ يَبْلُغَ
أَشُدَّهُ ۖ وَأَوْفُوا الْكَيْلَ وَالْمِيزَانَ بِالْقِسْطِ ۖ لَا تَكْلَفُ نَفْسًا إِلَّا وُسْعَهَا ۖ وَإِذَا قُلْتُمْ فَاعْدِلُوا وَلَوْ كَانَ ذَا
قُرْبَىٰ ۖ وَبِعَهْدِ اللَّهِ أَوْفُوا ۚ ذَلِكُمْ وَصَّاكُمْ بِهِ لَعَلَّكُمْ تَذَكَّرُونَ وَأَنَّ هَذَا صِرَاطِي مُسْتَقِيمًا فَاتَّبِعُوهُ ۖ وَلَا
تَتَّبِعُوا السُّبُلَ فَتَفَرَّقَ بِكُمْ عَن سَبِيلِهِ ۚ ذَلِكُمْ وَصَّاكُمْ بِهِ لَعَلَّكُمْ تَتَّقُونَ

5- "Sema: "Njoooni nikusomeeni yale Aliyoyaharamisha Mola wenu kwenu kwamba: Msimshirikishe na chochote; na muwafanyie wema wazazi wawili; na wala msiwaue watoto wenu kutokana na umasikini - Sisi Tunakuruzukuni pamoja nao - na wala msikaribie machafu, yaliyo dhahiri na yaliyo siri; na wala msiue nafsi ambayo Ameiharamisha Allaah isipokuwa kwa haki. Hivyo ndivyo Alivyokuusieni [Allaah] kwayo mpate kutia akilini. Na wala msiikaribie mali ya yatima isipokuwa kwa njia bora [ya kumtengenezea hicho chake] mpaka afikie kubalege. Na timizeni kipimo na mizani kwa uadilifu - Hatukalifishi nafsi isipokuwa vile inavyoweza. - Na mnaposema [katika kushuhudia] basi semeni kwa uadilifu, japokuwa ni jamaa wa karibu. Na timizeni ahadi ya Allaah." Hivyo ndivyo Alivyokuusieni [Allaah] kwayo mpate kukumbuka. Allaah anasema: "Hii ndio njia Yangu, [njia] iliyonyooka; basi ifuateni na wala msifuate njia [nyinginezo] vitakufarikisheni na njia Yake!" Hivyo ndivyo Alivyokuusieni kwayo mpate kuwa na kucha." (al-An'aam 06 : 151-153)

6- Ibn Mas'uud (Radhiya Allaahu 'anh) amesema:

"Yule anayetaka kuona wasia wa Muhammad (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) ambao Mtume ameweka muhuri wake, basi asome Kauli Yake (Ta'ala):

قُلْ تَعَالَوْا أَتْلُ مَا حَرَّمَ رَبِّي عَلَيْكُمْ ۖ أَلَّا تُشْرِكُوا بِهِ شَيْئًا ۖ وَبِالْوَالِدَيْنِ إِحْسَانًا ۖ وَلَا تَقْتُلُوا أَوْلَادَكُمْ
مَنْ إِمْلَاقٍ ۖ نَحْنُ نَرْزُقُكُمْ وَإِيَّاهُمْ ۖ وَلَا تَقْرُبُوا الْفَوَاحِشَ مَا ظَهَرَ مِنْهَا وَمَا بَطَنَ ۖ وَلَا تَقْتُلُوا النَّفْسَ

الَّتِي حَرَّمَ اللَّهُ إِلَّا بِالْحَقِّ ۚ ذَلِكُمْ وَصَّاكُمْ بِهِ لَعَلَّكُمْ تَعْقِلُونَ وَلَا تَقْرَبُوا مَالَ الْيَتِيمِ إِلَّا بِالَّتِي هِيَ أَحْسَنُ
حَتَّىٰ يَبْلُغَ أَشُدَّهُ ۗ وَأَوْفُوا بِالْعَهْدِ ۗ إِنَّكُمْ لَعَلَّكُمْ تَكُونُونَ رَاغِبِينَ ۗ وَإِذَا قُلْتُمْ فَاعْدِلُوا
وَلَوْ كَانَ ذَا قُرْبَىٰ ۗ وَبِعَهْدِ اللَّهِ أَوْفُوا ۗ ذَلِكُمْ وَصَّاكُمْ بِهِ لَعَلَّكُمْ تَذَكَّرُونَ ۗ هَذَا صِرَاطٌ مُسْتَقِيمٌ
فَاتَّبِعُوهُ ۗ وَلَا تَتَّبِعُوا السُّبُلَ فَتَفَرَّقَ بِكُمْ عَن سَبِيلِهِ ۗ ذَلِكُمْ وَصَّاكُمْ بِهِ لَعَلَّكُمْ تَتَّقُونَ

"Sema: "Njoooni nikusomeeni yale Aliyoyaharamisha Mola wenu kwenu kwamba: Msimshirikishe na chochote; na muwafanyie wema wazazi wawili; na wala msiwaue watoto wenu kutokana na umasikini - Sisi Tunakuruzukuni pamoja nao - na wala msikaribie machafu, yaliyo dhahiri na yaliyo siri; na wala msiue nafsi ambayo Ameiharamisha Allaah isipokuwa kwa haki. Hivyo ndivyo Alivyokuusieni [Allaah] kwayo mpate kutia akilini. Na wala msiikaribie mali ya yatima isipokuwa kwa njia bora [ya kumtengenezea hicho chake] mpaka afikie kubalege. Na timizeni kipimo na mizani kwa uadilifu - Hatukalifishi nafsi isipokuwa vile inavyoweza. - Na mnaposema [katika kushuhudia] basi semeni kwa uadilifu, japokuwa ni jamaa wa karibu. Na timizeni ahadi ya Allaah." Hivyo ndivyo Alivyokuusieni [Allaah] kwayo mpate kukumbuka. Allaah anasema: "Hii ndio njia Yangu, [njia] iliyonyooka; basi ifuateni na wala msifuate njia [nyinginezo] vitakufarikisheni na njia Yake!" Hivyo ndivyo Alivyokuusieni kwayo mpate kuwa na kucha."¹ (al-An'aam 06 : 151-153)

7- Mu'aadh bin Jabal (Radhiya Allaahu 'anh) amesema:

"Nilikuwa nimekaa nyuma ya Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) juu ya punda. Akanambia: "Ee Mu'aadh! Je, unajua ni ipi haki ya Allaah juu waja na haki ya waja kwa Allaah?" Nikasema: "Allaah na Mtume Wake ndio wanajua zaidi." Akasema: "Haki ya Allaah juu ya waja wamuabudu Yeye na

¹ at-Tirmidhiy (3070), al-Bayhaqiyy katika "Shu'ab-ul-Iymaan" (7918) na at-Twabaraaniyy katika "al-Awsat" (1186). Dhaifu kwa mujibu wa al-Albaany katika "Dhwa'iyf Sunan at-Tirmidhiy".

wala wasimshirikishe na chochote. Na haki ya waja kwa Allaah ni kutomuadhibu yule ambaye hakumshirikisha Yeye na chochote." Nikasema: "Ee Mtume wa Allaah! Nisiwabashirie watu?" Akasema: "Usiwabashirie wakaja kutegemea hivyo."²

Ameipokea al-Bukhaariy na Muslim.

MAELEZO

1- Maana ya Tawhiyd ni kumpwekesha Allaah na 'ibaadah.

Allaah (Ta'ala) amesema:

وَمَا خَلَقْتُ الْجِنَّ وَالْإِنْسَ إِلَّا لِيَعْبُدُونِ

"Na Sikuumba majini na watu wa isipokuwa waniabudu." (**adh-Dhaariyaat 51: 52**)

Hii ndio hekima ya Kishari'ah ya wao kuumbwa. Allaah hakuwaumba ili waje kuongeza idadi. Amewaumba ili awape majaribio. Alalah (Ta'ala) amesema:

الَّذِي خَلَقَ الْمَوْتَ وَالْحَيَاةَ لِيَبْلُوَكُمْ أَيُّكُمْ أَحْسَنُ عَمَلًا ۗ وَهُوَ الْعَزِيزُ الْعَفُورُ

"Ambaye Ameumba mauti na uhai ili akujaribuni ni nani kati yenu mwenye matendo mazuri zaidi. Naye ni Mwenye nguvu kabisa, Mwingi wa kusamehe." (**al-Mulk 67 : 02**)

لِتَعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ وَأَنَّ اللَّهَ قَدْ أَحَاطَ بِكُلِّ شَيْءٍ عِلْمًا

"Ili mjue kwamba Allaah juu ya kila kitu ni Muweza na kwamba Allaah Amekwishakizunguka kila kitu kwa ujuzi Wake." (**atw-Twalaah 65 : 12**)

² al-Bukhaariy (2856) na Muslim (30).

Allaah amewaumba ili awafunze kuwa Yeye ndio Muumbaji, Mrukuzakaji na Muwezaji. Allaah amewapa majaribio kwa maamrishi, makatazo na majukumu ili waweze kumuabudu kwa ujuzi. Kwa ajili hiyo ndio maana amewatuma Mitume na akateremsha Vitabu ili aweze kujifunza haki Yake na washikamane nayo:

2- Allaah (Ta'ala) amesema:

وَلَقَدْ بَعَثْنَا فِي كُلِّ أُمَّةٍ رَّسُولًا أَنِ اعْبُدُوا اللَّهَ وَاجْتَنِبُوا الطَّاغُوتَ

"Na kwa yakini Tulituma katika kila ummah Mtume [awaamrishe watu wake] kwamba: "Mwabuduni Allaah na jiepusheni na Twaaghuut." (an-Nahl 16 : 32)

Bi maana muabuduni Allaah pekee na jiepusheni na Twaaghuut. Twaghuut ni kila chenye kuabudiwa badala ya Allaah na huku kimeridhia hilo. Kuhusiana na wale wenye kuabudiwa badala ya Allaah pasi kuridhia hilo, kama Mitume na Manabii, sio Twaahuut. Kwa sababu wao hawakuamrishah ilo.

3- Allaah (Ta'ala) amesema:

وَقَضَىٰ رَبُّكَ أَلَّا تَعْبُدُوا إِلَّا إِيَّاهُ وَبِالْوَالِدَيْنِ إِحْسَانًا

"Na Mola wako Aameamrisha ya kwamba, msiabudu yeyote isipokuwa Yeye Pekee. Na [amekuamrisheni] kuwatendea wema wazazi wawili." (al-Israa' 17 : 23-24)

Bi maana amekuamrisheni na kukuusieni kumuabudu Allaah Pekee. Yeye ndiye ambaye anastahiki 'ibaadah. Hakuna muabudiwa wa haki isipokuwa Allaah. Hii ina maana ya kwamba hakuna zaidi ya Allaah ambaye ana haki ya kuabudiwa. Hivyo basi muabudu Yeye peke yake na wala usimshirikishe Yeye katika 'ibaadah Zake na chochote sawa ikiwa ni Mtume, Malaika, walii au mtu mwingine. Ni juu ya mtu kutahadhari na aina zote za shirki.

4-

وَاعْبُدُوا اللَّهَ وَلَا تُشْرِكُوا بِهِ شَيْئًا

“Na mwabuduni Allaah na wala msimshirikishe Yeye na chochote.” (an-Nisaa’ 04:36)

5-

قُلْ تَعَالَوْا أَنَا وَالْحَرَمَ رَبُّكُمْ عَلَيْكُمْ ۖ أَلَّا تُشْرِكُوا بِهِ شَيْئًا ۖ وَبِالْوَالِدَيْنِ إِحْسَانًا ۖ وَلَا تَقْتُلُوا أَوْلَادَكُمْ
مِّنْ إِمْلَاقٍ ۖ نَّحْنُ نَزَرُكُمْ وَإِبَاهُمْ ۖ وَلَا تَقْرَبُوا الْفَوَاحِشَ مَا ظَهَرَ مِنْهَا وَمَا بَطَنَ ۖ وَلَا تَقْتُلُوا النَّفْسَ الَّتِي
حَرَّمَ اللَّهُ إِلَّا بِالْحَقِّ ۚ ذَلِكُمْ وَصَّاكُمْ بِهِ لَعَلَّكُمْ تَعْقِلُونَ وَلَا تَقْرَبُوا مَالَ الْيَتِيمِ إِلَّا بِالَّتِي هِيَ أَحْسَنُ حَتَّىٰ يَبْلُغَ
أَشُدَّهُ ۖ وَأَوْفُوا الْكَيْلَ وَالْمِيزَانَ بِالْقِسْطِ ۖ لَا تَكْلَفُ نَفْسًا إِلَّا وُسْعَهَا ۖ وَإِذَا قُلْتُمْ فَاعْدِلُوا وَلَوْ كَانَ ذَا
قُرْبَىٰ ۖ وَبِعَهْدِ اللَّهِ أَوْفُوا ۚ ذَلِكُمْ وَصَّاكُمْ بِهِ لَعَلَّكُمْ تَذَكَّرُونَ وَأَنَّ هَذَا صِرَاطِي مُسْتَقِيمًا فَاتَّبِعُوهُ ۖ وَلَا
تَتَّبِعُوا السُّبُلَ فَتَفَرَّقَ بِكُمْ عَن سَبِيلِهِ ۚ ذَلِكُمْ وَصَّاكُمْ بِهِ لَعَلَّكُمْ تَتَّقُونَ

”Sema: “Njoooni nikusomeeni yale Aliyoyaharamisha Mola wenu kwenu kwamba: Msimshirikishe na chochote; na muwafanyie wema wazazi wawili; na wala msiwaue watoto wenu kutokana na umasikini - Sisi Tunakuruzukuni pamoja nao - na wala msikaribie machafu, yaliyo dhahiri na yaliyo siri; na wala msiue nafsi ambayo Ameiharamisha Allaah isipokuwa kwa haki. Hivyo ndivyo Alivyokuusieni [Allaah] kwayo mpate kutia akilini. Na wala msiikaribie mali ya yatima isipokuwa kwa njia bora [ya kumtengenezea hicho chake] mpaka afikie kubalege. Na timizeni kipimo na mizani kwa uadilifu - Hatukalifishi nafsi isipokuwa vile inavyoweza. - Na mnaposema [katika kushuhudia] basi semeni kwa uadilifu, japokuwa ni jamaa wa karibu. Na timizeni ahadi ya Allaah.” Hivyo ndivyo Alivyokuusieni [Allaah] kwayo mpate kukumbuka. Allaah anasema: “Hii ndio njia Yangu, [njia] iliyonyooka; basi ifuateni na wala msifuate njia [nyinginezo] vitakufarikisheni na njia Yake!” Hivyo ndivyo Alivyokuusieni kwayo mpate kuwa na kucha.” (al-An’aam 06 : 151-153)

Allaah anamwamrisha Mtume kuwaeleza watu yale aliyoharamisha na awesomee kwa elimu na yakini na sio kwa shaka na dhana. Jambo la kwanza katika mambo haya yaliyoharamishwa ni shirki. Allaah ameharamisha shirki kama ambavyo vilevile ameharamisha mambo ya haramu mengine yote. La kwanza katika mambo ya haramu yote haya ni shirki. Shirki maana yake ni kufanya aina yoyote ile ya 'ibaadah kumfanyia asiyekuwa Allaah. Aayah hizi zimebeba mambo kumi:

La kwanza: Shirki.

La pili: Kuwatendea wema wazazi wawili. Kutajwa kwao baada ya Allaah kunatolea dalili kuonesha ukubwa wa haki zao. Kuwatunza vibaya wazazi wawili ni moja katika madhambi makubwa. Allaah ametaja haki zao sambamba pamoja na haki Yake katika Aayah nyingi.

La tatu: Kutowaua watoto.

La nne: Kutoyakaribia machafu kama usengenyaji, uvumi, uzinifu na wizi.

La tano: Kutoiua nafsi yoyote iliyoharamishwa na Allaah kuia pasi na haki.

La sita: Kutokula mali ya yatima. Yatima ni yule ambaye amefisha baba yake kabla ya kubaleghe.

La saba: Kutimiza kipimo na mizani.

La nane: Kutimiza ahadi ya Allaah. Ahadi ya Allaah ni 'ibaadah aliyoamrisha na apwekeshwe katika 'ibaadah na kuepuka makatazo Yake.

La tisa: Ahadi.

Wasia ni maamrishi yenye kukaziwa. Mtu anausia jambo pale anapolikokoteza. Wenye busara ni wale wenye kuyafahamu mambo haya na wakashikamana nayo kwa akili zao.

Allaah amesema:

وَأَنَّ هَذَا صِرَاطِي مُسْتَقِيمًا فَاتَّبِعُوهُ

"Hii ndio njia Yangu, [njia] iliyonyooka; basi ifuateni... "

Njia ya Allaah ni kutekeleza maamrisho Yake, kujiepusha na makatazo Yake na kumtakasia Yeye katika 'ibaadah. Ni wajibu kwa watu kushikamana bara bara na njia hii. Allaah (Ta'ala) amesema:

وَلَا تَتَّبِعُوا السُّبُلَ

"... na wala msifuate njia [nyinginezo]."

Njia nyinginezo ni Bid'ah, matamania na shahawa za haramu. Allaah ameanza kutaja akili kwa sababu mwanaadamu huanza kufikiri kwanza. Kisha anatafakari, anajifunza na kukumbuka. Halafu baada ya hapo ndio anaogopa na kufanya yale yenye kumnufaisha na kujiepusha na yale yenye kumdhuru na kumkasirikisha Mola Wake.

6- Ibn Mas'uud (Radhiya Allaahu 'anh) amesema:

"Yule anayetaka kuona wasia wa Muhammad (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) ambao Mtume ameweka muhuri wake, basi asome... "

Bi maana ni kana kwamba aliandika na kupiga saini yake. Huu ndio wasia wa Allaah na wasia wa Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam). Maswahabah walihuzunishwa pindi walipomuona Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) anataka kuacha anausia. Hatimaye akawa ameacha kufanya hivo. Alipotaka kuacha anausia baadhi yao walionelea aletewe karatasi na wengine wakaonelea asisumbuliwe kwa vile anaumwa. Ndipo Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) akawaamrisha watoke na kusema:

"Haitakiwi walumbane kwangu."³

Ibn 'Abbaas amesema:

"Ni ajali kubwa kuona Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) hakuacha anaandika wasia."

Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

"Je, si mnipe kiapo cha usikivu na utiifu kwa Aayah hizi?"⁴

7- Mu'aadh bin Jaba (Radhiya Allaahu 'anh) amesema:

"Nilikuwa nimekaa nyuma ya Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) juu ya punda.. "

Katika Hadiyth hii kunaonesha unyenyekevu wake Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) na tabia nzuri aliokuwa nayo kwa njia mbali mbali. Kwa mfano kupanda kwake juu ya punda, kuwa na mtu mwingine nyuma yake ambaye anazungumza naye tofauti na wanavofanya baadhi ya watu waliokuwa na kiburi.

Katika Hadiyth hii kunaonesha pia jinsi faida na hukumu zinavyotolewa kupitia kwa njia ya maswali. Hili hushika kwenye mioyo ya wasikilizaji. Vilevile ni jambo linalomuandaa na kumpa moyo wa kujibu swali msikilizaji. Tofauti na lau mada itanza kutajwa moja kwa moja. Kuna khatari ya mtu kutoizingatia.

Mu'aadh bin Jabal amesema:

"Allaah na Mtume Wake ndio wanajua zaidi."

³ al-Bukhaariy (114).

⁴ al-Haakim (3240) na al-Marwaziyy katika "Ta'dhwiym Qadr-is-Swalaah" (2/615).

Kuna tabia nzuri ya Mu'aadh ambapo hakujikakama kwa kitu asichokijua. Ikiwa mtu hawezi kujibu swali ni wajibu kwake kusema "Sijui" au "Allaah na Mtume Wake ndio wanajua zaidi" ikiwa Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) bado yuhai. Baada ya kufa kwa Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) mtu anatakiwa kusema "Allaah ndio anajua zaidi" au "Sijui". Asiseme "Allaah na Mtume Wake ndio wanajua zaidi" kwa vile Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) hajui yale waliyoyafanya watu baada ya kufa kwake. Katika Hadiyth ya Hodhi Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) anasema: "Maswahabah zangu! Maswahabah zangu!" Ndipo ataambiwa: "Hakika wewe hujui waliyoyafanya baada yako."⁵

⁵ al-Bukhaariy (4625) na Muslim (2860).

2. Fadhila za Tawhiyd na madhambi yanayosamehewa kwayo

Shaykh-ul-Islaam Muhammad bin 'Abdil-Wahhaab (Rahimahu Allaah) amesema:

1- Allaah (Ta'ala) amesema:

الَّذِينَ آمَنُوا وَلَمْ يَلْبِسُوا إِيمَانَهُمْ بِظُلْمٍ أُولَٰئِكَ هُمُ الْأَمَنُ وَهُمْ مُهْتَدُونَ

"Wale ambao wameamini na hawakuchanganya imani zao na dhulma. Hao ndio watakaopata amani nao ndio walioongoka." (al-An'aam 06 : 82)

2- 'Ubaadah bin as-Swaamit (Radhiya Allaahu 'anh) ameeleza kuwa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

"Mwenye kushuhudia ya kwamba hakuna mungu wa haki isipokuwa Allaah, hali ya kuwa ni mmoja asiyekuwa na mshirika, na kwamba Muhammad ni mja na Mtume Wake na kuwa 'Iysa ni mja, Mtume Wake na ni Neno Lake Alilompelekea Maryam na roho iliyotoka Kwake na kwamba Pepo ni kweli na Moto ni kweli, basi Allaah Atamuingiza Peponi pasi na kujali atachofanya."⁶

Ameipokea al-Bukhaariy na Muslim.

3- al-Bukhaariy na Muslim wamepokea wote wawili Hadiyth kupitia kwa 'Utbaan (Radhiya Allaahu 'anh):

"Hakika Allaah kamharamishia Moto yule mwenye kusema hakuna mungu wa haki isipokuwa Allaah akikusudia kwa kufanya hivo Uso wa Allaah."⁷

⁶ al-Bukhaariy (3435) na Muslim (28).

⁷ al-Bukhaariy (425) na Muslim (33).

4- Abu Sa'iyd al-Kudriy (Radhiya Allaahu 'anh) ameeleza kuwa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

"Muusa alisema: "Ee Mola Wangu! Nifunze kitu ambacho nitakukumbuka kwacho na kukuomba kwacho." Akamwambia: "Ee Muusa! Sema: "Hakuna mungu wa haki isipokuwa Allaah." Akasema: "Ee Mola! Waja Wako wote wanasema hivi." Akasema: "Ee Muusa! Lau mbingu saba na vyote vilivyomo ndani yake mbali na Mimi na ardhi saba na vyote vilivyomo ndani yake vitawekwa kwenye kitanga kimoja cha mzani na "hakuna mungu wa haki isipokuwa Allaah" ikawekwa kwenye kitanga kingine, basi "hakuna mungu wa haki isipokuwa Allaah" ingevizidi uzito."

Ameipokea Ibn Hibbaan na al-Haakim ambaye ameisahihisha.

5- at-Tirmidhiy amepokea na kuifanya kuwa ni nzuri kutoka kwa Anas (Radhiya Allahu 'anh) ambaye ameeleza kuwa amemsikia Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) akisema:

"Allaah (Ta'ala) amesema: "Ee mwanaadamu! Lau utanijia kwa madhambi yaliyojaa ardhi kisha ukakutana na Mimi pasi na kunishirikisha na chochote, basi ningelikujia na kiasi hicho hicho cha msamaha."

MAELEZO

Mwandishi anachotaka ni kuonesha

وَمَا يُؤْمِنُ أَكْثَرُهُمْ بِاللَّهِ إِلَّا وَهُمْ مُشْرِكُونَ

fadhila za Tawhiyd na kuwa hakuna kitendo kinachofuta madhambi kama Tawhiyd. Kwa sababu Tawhiyd ndio asli na ndio msingi wa matendo. Matendo hayasihi bila ya Tawhiyd. Ameitaja ili muumini aweze kuitambua na kuipupia na kuitamani.

1- Allaah (Ta'ala) amesema:

الَّذِينَ آمَنُوا وَلَمْ يَلْبِسُوا إِيمَانَهُمْ بِظُلْمٍ أُولَئِكَ لَهُمُ الْأَمْنُ وَهُمْ مُهْتَدُونَ

"Wale ambao wameamini na hawakuchanganya imani zao na dhulma. Hao ndio watakaopata amani nao ndio walioongoka." (al-An'aam 06 : 82)

Wameamini ina maana ya kwamba wamempwekesha Allaah na kumtakasia Yeye 'ibaadah na kuwamini kuwa Yeye ndiye mungu wao wa haki. Imani maana yake Tawhiyd. Hawakuchanganya imani zao na shirki. Bali wanamuabudu tu Yeye (Subhaanah) peke yake. Hao ndio watakaopata amani na uongofu mkamilifu kwa sababu imano zao zilisalimika na sampuli zote za shirki na yote yaliyo chini yake katika maasi na kuwadhulumu waja.

Pindi ilipoteremshwa Aayah hii Maswahabah wa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) iliwayatiza. Wakaenda kwa Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) na kumuuliza ni nani hajapatae kuitendea nafsi yake dhuluma. Walidhani kuwa Allaah anamaanisha madhambi. Ndipo Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) akasema:

"Je, hamkusikia maneno ya mja mwema alivyosema:

إِنَّ الشِّرْكَ لَظُلْمٌ عَظِيمٌ

"Hakika shirki ni dhulma kubwa mno!"⁸ (Luqmaan 31 : 13)

Makusudio ya dhuluma hapa ni shirki. Hili ni tofauti na mshirikina. Hatopata amani yoyote. Ataingia Motoni. Muumini mwenye kusalimika na shirki kubwa na ndogo na kuwadhulumu waja basi huyo ana uongofu na amani kamilifu duniani na Aakhirah. Yule mwenye kusalimika na shirki kubwa na asisalimike na shirki ndogo na akatumbukia katika baadhi ya maasi hapati uongofu na amani kamilifu. Kuna khatari kwa mtu huyo akaingia Motoni kutokana na

⁸ al-Bukhaariy (4776) na Muslim (124).

madhambi aliyokufa juu yake. Pindi Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) alipoifasiri Aayah alibainisha ya kwamba uongofu na amani kamilifu havipatikani isipokuwa kwa kuepuka shirki kubwa. Hata hivyo kuna dalili zingine zenye kuonesha kuwa uongofu na amani kamilifu havipatikani isipokuwa kwa kuepuka maasi, kuwadhulumu waja na aina nyinginezo za shirki na ndogo.

2- 'Ubaadah bin as-Swaamit (Radhiya Allaahu 'anh) ameeleza kuwa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

"Mwenye kushuhudia ya kwamba hakuna mungu wa haki isipokuwa Allaah, hali ya kuwa ni mmoja asiyekuwa na mshirika, na kwamba Muhammad ni mja na Mtume Wake na kuwa 'Iysa ni mja, Mtume Wake na ni Neno Lake Alilompelekea Maryam na roho iliyotoka Kwake na kwamba Pepo ni kweli na Moto ni kweli, basi Allaah Atamuingiza Peponi pasi na kujali atachofanya."

Ameipokea al-Bukhaariy na Muslim.

Roho kutoka Kwake ina maana ya kwamba ni roho iliyoubwa na Allaah.

Mwenye kushuhudia haya kikweli basi Allaah atamuingiza Peponi. Hadiyth hii ni miongoni mwa Hadiyth ambazo hazikufungamanishwa [Mutlaq] zenye kuonesha fadhila za Tawhiyd. Lakini pamoja na hivyo kuna dalili zingine zenye kuonesha kuwa hukumu hii ambayo haikufungamanishwa imefungamanishwa na kule kutekeleza haki ya Shahaadah. Shahaadah yenye maazimio ambayo ndani yake kuna kumtakasia 'ibaadah Allaah peke yake kwa ukweli, unyenyekeaji, mapenzi, kukubali na kwa nia safi kwa kumfuata na kumtii Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam). Mwenye kushuhudia Shahaadah hii na akaichafua na maasi na madhambi au akaitamka kwa ulimi tu na huku anashirikisha kwa moyo au matendo yake, kama wanafiki, huyu Shahaadah haitomfaa kitu. Shahaadah ni lazima itamkwe kwa maazimio na kutekeleza maamrishi na kujiepusha na makatazo. Kadhalika ni lazima Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) afuatwe. Vingenvyo Shahaadah itakuwa ni yenye

kuchafuliwa na haitoweza kumwingiza mwenye nayo Peponi isipokuwa kwa kutaka Kwake Allaah.

3- al-Bukhaariy na Muslim wamepokea wote wawili Hadiyth kupitia kwa 'Utbaan (Radhiya Allaahu 'anh):

"Hakika Allaah kamharamishia Moto yule mwenye kusema hakuna mungu wa haki isipokuwa Allaah akikusudia kwa kufanya hivo Uso wa Allaah."

Anayetamka Shahaadah kwa ukweli na akafa katika hali hiyo Allaah atamwingiza Peponi. Ama kuhusu yule mwenye kufanya madhambi bila ya kutubu hilo anaachiwa Allaah kama atamsamehe au kumuadhibu.

Mwenye kutamka Shahaadah kwa nia safi na kwa ukweli habaki kwenye madhambi. Imani na *Ikhlāasw* yake kamilifu inamzuia na kuendelea kwa madhambi. Huyu ataingia Peponi pamoja na wale wa kwanza wataoingia. Dalili yenye kuonesha kuwa mwenye kufa hali ya kuwa ni mtendaji madhambi anaingia katika matakwa ya Allaah ni Kauli Yake (Ta'ala):

إِنَّ اللَّهَ لَا يَغْفِرُ أَنْ يُشْرَكَ بِهِ وَيَغْفِرُ مَا دُونَ ذَلِكَ لِمَنْ يَشَاءُ

"Hakika Allaah hasamehi kushirikishwa na anasamehe yaliyo chini ya hayo kwa amtae." (**an-Nisaa' 04:48**)

Kuna Hadiyth zenye kuonesha kuwa mtenda madhambi kuna khatari juu yake akaadhibiwa na kutumbukia Motoni. Kisha watatolewa kutokana na uombezi wa Mitume na wengine. Watu hawa Tawhiyd yao ilikuwa dhaifu. Waliichafua kwa madhambi. Huu ndio mfumo wa Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa'ah na uelewa sahihi ambao Ahl-ul-Bid'ah kama Khawaarij, Mu'tazilah na Murji-ah wameuacha. Pamoja na hivyo yule mwenye kukufuru Shahaadah haitomfaa kitu hata kama ataitamka.

4- Abu Sa'iyd al-Kudriy (Radhiya Allaahu 'anh) ameeleza kuwa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

"Muusa alisema: "Ee Mola Wangu! Nifunze kitu ambacho nitakukumbuka kwacho na kukuomba kwacho." Akamwambia: "Ee Muusa! Sema: "Hakuna mungu wa haki isipokuwa Allaah." Akasema: "Ee Mola! Waja Wako wote wanasema hivi." Akasema: "Ee Muusa! Lau mbingu saba na vyote vilivyomo ndani yake mbali na Mimi na ardhi saba na vyote vilivyomo ndani yake vitawekwa kwenye kitanga kimoja cha mzani na "hakuna mungu wa haki isipokuwa Allaah" ikawekwa kwenye kitanga kingine, basi "hakuna mungu wa haki isipokuwa Allaah" ingevizidi uzito."

Ameipokea Ibn Hibbaan na al-Haakim ambaye ameisahihisha.

Hadiyth hii inaonesha fadhila za neno hili na kuwa ni Dhikr na du'aa yote mawili kutokana na kwamba Muusa (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) alisema:

"Nifunze kitu ambacho nitakukumbuka kwacho na kukuomba kwacho."

Mtu anamdhukuru Allaah kwa neno hili na kushuhudia kupwekeka Kwake. Neno hili vilevile ni du'aa kwa sababu yule mwenye kulitamka anatarajia thawabu. Kama ilivyo kwa du'aa nyenginezo kama "Subhaan Allaah", "al-Hamdu lillaah" na "Laa hawlaa wa laa quwwata illa billaah". Hadiyth inaonesha vilevile nafasi ya neno hili. Neno hili ni Dhikr na du'aa. Hadiyth inaonesha pia kuwa fadhila Zake zinaweza kuwa hata hazijulikana kwa baadhi ya Mitume. Inaonesha pia ukubwa wa neno hili kwa kumuhakikishia 'ibaadah Allaah peke yake, kumthibitishia nayo na kumkanushia nayo mwingine yeyote. Neno hili maana yake ni hakuna muabudiwa wa haki isipokuwa Allaah. Bi maana kubatilisha waungu wengine wote.

Allaah amesema "Lau mbingu saba na vyote vilivyomo ndani yake mbali na Mimi... ". Allaah (Subhanaah) Amejiondoa kwa kuwa Yeye ni Mkubwa. Hakika Yeye (Subhaanah) Yuko juu ya mbingu. Ameumba mbingu na ardhi. Yeye ndiye

mwenye kuzizuia na kuzisimamisha, 'Arshi na Kursiy. Yeye ndiye amevsimamisha viumbe Hivi. Allaah (Ta'ala) amesema:

وَمِنْ آيَاتِهِ أَنْ تَقُومَ السَّمَاءُ وَالْأَرْضُ بِأَمْرِهِ

"Miongoni mwa alama Zake ni kwamba mbingu na ardhi zimesimama kwa amri Yake." (ar-Ruum 30:25)

إِنَّ اللَّهَ يُمَسِّكُ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضَ أَنْ تَزُولَا

"Hakika Allaah anazuia mbingu na ardhi zisitoweke." (Faatwir 35:31)

Lau vyote vingeliwekwa kwenye kitanga cha mzani na "hakuna mungu wa haki isipokuwa Allaah" ikawekwa kwenye kitanga kingine, basi "hakuna mungu wa haki isipokuwa Allaah" ingevizidi uzito. Kwa maana ya kwamba maana ingelikuwa na uzito zaidi na sio vitu hivi. Kutokamana na maana na uhakika neno la Tawhiyd ni kubwa, la kweli na muhimu zaidi. Ndio maana lina uzito zaidi kuliko vitu vyote. Kama jinsi neno hili lina uzito zaidi kuliko viumbe basi linafanya vilevile kwa yule mwenye kulitamka kushinda madhambi yake yote.

5- at-Tirmidhiy ameipokea na kuifanya kuwa ni nzuri kutoka kwa Anas (Radhiya Allahu 'anh) ambaye ameeleza kuwa amemsikia Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) akisema:

"Allaah (Ta'ala) amesema: "Ee mwanaadamu! Lau utanjia kwa madhambi yaliyojaa ardhi kisha ukakutana na Mimi pasi na kunishirikisha na chochote, basi ningelikujia na kiasi hicho hicho cha msamaha."

Hadiyth inaonesha kuwa madhambi yote yanashindwa na neno la Tawhiyd lenye kuhakikishwa kama jinsi neno hilo lilivyo na uzito zaidi kuliko viumbe vingine vyote. Wanachuoni wameifasiri Hadiyth hii kwa njia mbili:

Ya kwanza: Inahusu yule ambaye ataitamka kwa ukweli na kwa nia safi pasi na kuendelea juu ya maasi. Huyu analitendea kazi neno hili mpaka anatekeleza mambo yote ya wajibu, kuacha mambo yote yaliyokatazwa na kushikamana na Shari'ah ya Allaah katika mambo yote.

Ya pili: Inahusu yule mwenye kuitamka na akamjia Allaah hali ya kuwa ameshatubu kwa madhambi yake na kujivua nayo. Madhambi yote yanaondoka kwa neno hili.

Hadiyth hii ni lazima ifahamike namna hii. Kuna Aayah na Hadiyth zenye kuonesha kuwa watenda madhambi kuna khatari juu yao wakaadhibiwa na kutumbukizwa Motoni. Maandiko haya hayagongani. Ndio maana ni wajibu Hadiyth hizi zikafasiriwa namna hii ili kuepuka tofauti na mgongano.

Kuna wajinga ambao wameshikamana na maandiko haya ambayo hayakufungamanishwa na kufikiri ya kwamba inatosha kwa mtu kutamka Shahaadah hata kama ataacha mambo ya wajibu na kufanya maasi. Hili linakwenda kinyume na maafikiano ya Salaf wa Ummah huu yenye kusema kuwa ni lazima kufanya mambo ya wajibu, kujiepusha na mambo ya haramu na kusimama katika mipaka ya Allaah. Mwenye kuacha mambo ya wajibu na akafanya mambo yaliyokatazwa kuna khatari akaadhibiwa na Allaah (Ta'ala). Katika hali hii haijalishi kitu hata kama atatamka na kuyakinisha neno hili. Ikiwa atafanya kitu kinachotengua Uislamu wake anakuwa kafiri aliyeritadi. Hapa hatonufaika na neno hili. Kwa msemu mwingine ni lazima kuhakikisha yale yenye kulazimishwa na neno hili. Vinginevyo mtu yuko katika hali ya khatari ikiwa hakutubia.

3. Mwenye kuhakikisha Tawhiyd basi ataingia Peponi bila ya hesabu

Shaykh-ul-Islaam Muhammad bin 'Abdil-Wahhaab (Rahimahu Allaah) amesema:

1- Allaah (Ta'ala) amesema:

إِنَّ إِبْرَاهِيمَ كَانَ أُمَّةً قَانِتًا لِلَّهِ حَنِيفًا وَّم يَكُ مِنَ الْمُشْرِكِينَ

"Hakika Ibraahiym alikuwa ni mfano mwema, mnyenyekevu kwa Allaah na mwenye imani safi na ya asli. Hakuwa miongoni mwa washirikina." (an-Nahl 16:120)

2-

وَالَّذِينَ هُمْ بِرَبِّهِمْ لَا يُشْرِكُونَ

"... na wale ambao Mola wao hawamshirikishi na chochote." (al-Mu'minuun 23 :59)

3- Huswayn bin 'Abdir-Rahmaan amesema:

"Nilikuwa kwa Sa'iyd bin Jubayr pindi aliposema: "Ni nani kati yenu aliyeona kimondo [nyota] jana usiku?" Nikasema: "Mimi." Halafu nikaeleza kwamba sikuwa nikiswali wakati ule kwa sababu nilikuwa nimedonolewa [na mdumu mwenye sumu]. Akasema: "Sasa ulifanya nini?" Nikasema: "Nilijitibu." Akasema: "Kipi kilichokupelekea ufanye hivyo?" Nikasema: "Ni kutokana na Hadiyth aliyotuelezea ash-Sha'biy." Nikasema: "Alikuelezeni nini?" Nikasema: "Ametueleza kutoka kwa Buraydah bin al-Huswayb ambaye amesema: "Ruqyah hairuhusiwi isipokuwa kwa ajili ya kijicho au homa." Akasema: "Amefanya vyema kukomea kwenye alosikia. Lakini hata hivyo Ibn 'Abbaas ametusimulia ya kwamba Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Ummah zote zilipitishwa mbele yangu, nikamuona Mtume akiwa na kundi dogo la watu, na Mtume akiwa na mtu mmoja au wawili, na Mtume akiwa hana mtu yeyote. Kisha nikaonyeshwa idadi kubwa ya watu niliodhania ni katika Ummah wangu, lakini nikaambiwa: “Huyo ni Muusa na watu wake.” Kisha nikatazama nikaona kundi kubwa ambalo nikaambiwa: “Hawa ni watu wako, miongoni mwao kuna 70.000 watakaolingia Peponi bila ya kufanyiwa hesabu wala adhabu.” Kisha akainuka na kwenda nyumbani. Huku nyuma watu wakaanza kujadiliana ni nani hao watakaoweza kuwa? Baadhi yao wakasema: “Pengine ni Maswahabah wa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam).” Wengine wakasema: “Pengine ni wale waliozaliwa katika Uislamu na hawakumshirikisha Allaah na chochote.” Wakataja mengine kadhaa. Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) akatoka na kuja na wakamweleza waliyokuwa wakiyajadili. Akasema: “Ni wale wasioomba kusomewa Ruqyah, hawajichomi chuma cha moto na wala hawaamini rajua nzuri na mbaya, bali wanamtegemea Mola Wao.” ‘Ukaashah bin Mihswan (Radhiya Allaahu ‘anh) aliposikia alisimama akasema: “Muombe Allaah anijaalie kuwa mmoja wao.” Akasema: “Wewe ni katika wao.” Kisha akasimama mtu mwengine na kusema: “Muombe Allaah anijaalie kuwa mmoja wao.” Akasema: “‘Ukaashah amekutangulia.”⁹

MAELEZO

Kuhakikisha Tawhiyd maana yake ni kuisafisha na shirki, Bid’ah na maasi. Mwenye kuhakikisha Tawhiyd na akasalimika na shirki, Bid’ah na maasi ataingia Peponi bila ya hesabu wala adhabu. Shirki kubwa inaitengua Tawhiyd na shirki ndogo inatengua ukamilifu wa Tawhiyd. Bid’ah na maasi yanaiathiri Tawhiyd na kupunguza thawabu zake.

1- Allaah (Ta’ala) amesema:

⁹ al-Bukhaariy (5705) na Muslim (220).

إِنَّ إِبْرَاهِيمَ كَانَ أُمَّةً قَانِتًا لِلَّهِ حَنِيفًا وَلَمْ يَكُ مِنَ الْمُشْرِكِينَ

“Hakika Ibraahiym alikuwa ni mfano mwema, mnyenyekevu kwa Allaah na mwenye imani safi na ya asli. Hakuwa miongoni mwa washirikina.”

Allaah amemsifu kipenzi Chake Ibraahiym kwa sifa kubwa. Inafahamisha ukamilifu wa Tawhiyd na imani yake. Mosi:

إِنَّ إِبْرَاهِيمَ كَانَ أُمَّةً

“Hakika Ibraahiym alikuwa ni mfano mwema...”

Ina maana ya kwamba alikuwa peke yake akilingania katika mema na kwamba alikuwa na subira. Hivyo ndivyo walivyofasiri wanachuoni. Alilingania katika haki na hali ya kuwa imara juu yake pindi watu walipokuwa wameharibika. Mambo haya mawili yalikuwa yamekusanyika kwa Ibraahiym. Alikuwa peke yake juu ya kufuata haki. Hakuna yeyote aliyekuwa pamoja naye. Pamoja na hivyo alilingania katika haki peke yake.

2-

أُمَّةً قَانِتًا لِلَّهِ

“Mnyenyekevu kwa Allaah...”

Bi maana alikuwa siku zote ni mwenye kumtii Allaah na mwenye kuendelea kufanya matendo mema. Alikuwa ni mwenye kutii siku zote na akimuabudu Allaah peke yake. Hakuwa akimuabudu mwengine yeyote zaidi Yake.

3-

حَنِيفًا

“... mwenye imani safi na ya asli.”

Bi maana mwenye kuemelea kwa Allaah. Aliwapa mgongo waungu wote kwa ajili ya kumuabudu Allaah (‘Azza wa Jall) peke yake. Kisha Akakazia hilo kwa kusema:

وَأَمْ يَكُ مِنَ الْمُشْرِكِينَ

“Hakuwa miongoni mwa washirikina.”

Alitofautiana nao katika ‘Aqiydah yake, matendo, maneno na nyumba yake. Muislamu anatakiwa kuwa katika njia iliyonyooka na kuihakikisha Tawhiyd yake. Kwa sifa hizi ndio Ibraahiym (‘alayhis-Swalaatu was-Salaam) alihakikisha ukamilifu wa Tawhiyd yake.

2-

وَالَّذِينَ هُمْ بِرَبِّهِمْ لَا يُشْرِكُونَ

“... na wale ambao Mola wao hawamshirikishi na chochote.” (al-Mu‘minuun 23:59)

Hii ni moja katika sifa za wapwekeshaji na watu wa imani. Wanampwekesha Allaah na kumtakasia Yeye dini. Hawachanganyi ‘ibaadah zao na shirki. Wanamuabudu Allaah na kumwogopa. Huu ndio ukamilifu wa Tawhiyd. Ikiwa Ibraahiym (‘alayhis-Swalaatu was-Salaam) alihakikisha Tawhiyd basi Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) alifanya zaidi ya hivo. Kwa sababu yeye ndiye mchaji Allaah na mwenye kumtakasia ‘ibaadah Allaah zaidi katika watu.

3- Huswayn bin ‘Abdir-Rahmaan amesema:

“Nilikuwa kwa Sa‘iyd bin Jubayr pindi aliposema: “Ni nani kati yenu aliyeona kimondo [nyota] jana usiku?” Nikasema: “Mimi.” Halafu nikaeleza kwamba sikuwa nikiswali wakati ule kwa sababu nilikuwa nimedonolewa [na mdumu mwenye sumu]. Akasema: “Sasa ulifanya nini?” Nikasema: “Nilijitibu.” Akasema: “Kipi kilichokupelekea ufanye hivyo?” Nikasema: “Ni kutokana na

Hadiyth aliyotuelezea ash-Sha'biy." Nikasema: "Alikuelezeni nini?" Nikasema: "Ametueleza kutoka kwa Buraydah bin al-Huswayb ambaye amesema: "Ruqyah hairuhusiwi isipokuwa kwa ajili ya kijicho au homa." Akasema: "Amefanya vyema kukomea kwenye alosikia. Lakini hata hivyo Ibn 'Abbaas ametusimulia ya kwamba Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema: "Ummah zote zilipitishwa mbele yangu, nikamuona Mtume akiwa na kundi dogo la watu, na Mtume akiwa na mtu mmoja au wawili, na Mtume akiwa hana mtu yeyote. Kisha nikaonyeshwa idadi kubwa ya watu niliodhania ni katika Ummah wangu, lakini nikaambiwa: "Huyo ni Muusa na watu wake." Kisha nikatazama nikaona kundi kubwa ambalo nikaambiwa: "Hawa ni watu wako, miongoni mwao kuna 70.000 watakaoingia Peponi bila ya kufanyiwa hesabu wala adhabu." Kisha akainuka na kwenda nyumbani. Huku nyuma watu wakaanza kujadiliana ni nani hao watakaoweza kuwa? Baadhi yao wakasema: "Pengine ni Maswahabah wa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam)." Wengine wakasema: "Pengine ni wale waliozaliwa katika Uislamu na hawakumshirikisha Allaah na chochote." Wakataja mengine kadhaa. Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) akatoka na kuja na wakamweleza waliyokuwa wakiyajadili. Akasema: "Ni wale wasioomba kusomewa Ruqyah, hawajichomi chuma cha moto na wala hawaamini rajua nzuri na mbaya, bali wanamtegemea Mola Wao." 'Ukaashah bin Mihswan (Radhiya Allaahu 'anh) aliposikia alisimama akasema: "Muombe Allaah anijaalie kuwa mmoja wao." Akasema: "Wewe ni katika wao." Kisha akasimama mtu mwengine na kusema: "Muombe Allaah anijaalie kuwa mmoja wao." Akasema: "'Ukaashah amekutangulia."¹⁰

Kauli yake "Halafu nikaeleza kwamba sikuwa nikiswali wakati ule" ni sifa miongoni mwa sifa za Salaf. Walikuwa wakiogopa kudhihirisha matendo yao ili wasije kutumbukia katika kujionyesha na mtu kuisifu nafsi yake.

¹⁰ al-Bukhaariy (5705) na Muslim (220).

Kauli yake "Nilikuwa nimedonolewa" inaonesha ilikuwa ni nge, nyoka na mfano wake.

Kauli yake "Nilijitibu" inaonesha kuwa alimuomba mtu mwingine amtibu kwa Ruqyah. Allaah hunufaisha kwa Ruqyah.

Kauli yake "Kipi kilichokupelekea ufanye hivyo?" ni swali juu ya dalili kwa alichokifanya. Salaf walikuwa hivyo na masomo yao na pupa yao juu ya dalili.

Kauli yake "... kutoka kwa Buraydah bin al-Huswayb" ina maana ya kwamba Hadiyth hii imepokelewa na Buraydah na kwamba imepokelewa kutoka kwa Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam).

Kauli yake "Amejanya vyema kukomea kwenye alosikia" ni dalili ya kwamba alifanya kwa ujuzi na hakufanya kwa ujinga au kinyume na alivyojifunza.

Kauli yake "Ruqyah hairuhusiwi isipokuwa kwa ajili ya kijicho au homa" ni dalili yenye kuonesha kuwa mwenye kusibiwa na nge, nyoka au maradhi mengine ni sawa akajifanyia mwenyewe Ruqyah na akawaomba wengine wamfanyie Ruqyah. Hadiyth haikukoma kwa hayo yaliyotajwa peke yake. Wanachuoni wanaifasiri kama kipaumbele na kwamba hakuna kinachotibu kijicho na homa kama Ruqyah. Kwa sababu kuna Hadiyth zingine zinazoruhusu Ruqyah katika mnasaba wa mambo mengine mbali na kijicho na homa peke yake. Kwa mfano Hadiyth:

"Kujitibu [kwa Ruqyah] kunaruhusu midhali sio shirki."¹¹

Imethibiti pia ya kwamba Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) alifanya matabano na akafanyiwa matabano. Ni dalili inayofahamisha kuwa ni sawa kumnufaisha mgonjwa na kumsomea Aayah za Qur-aan.

¹¹ Muslim (2200) na Abu Daawuud (3886).

Kauli yake "... kijicho au homa" yaani kijicho cha mwenye kufanya kijicho, mtazamo wake na yeye mwenyewe na homa imefungamana na kudona kwa nyoka au nge.

Tiba hii ni yenye kunufaisha kwa maandiko na uzowefu. Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

"Anayeweza kumnufaisha ndugu yake kwa kitu basi na amnufaishe."¹²

Lililo bora ni mtu kutoomba kufanyiwa Ruqyah. Lakini hata hivyo inafaa wakati wa haja. Ndio maana Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) aliomba Ruqyah kwa mtoto wa Ja'far na kumwambia mama yao Asmaa' wakati waliposibiwa na kijicho:

"Wasomee Ruqyah."¹³

Kisha Sa'iyd akataja kilicho bora kuliko kuomba Ruqyah na akasimulia Hadiyth ya Ibn 'Abbaas.

Maneno yake (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) "Ummah zote zilipitishwa mbele yangu" imesemekana kwa mujibu wa maoni sahihi ya kwamba ni katika usiku wa Israa'.

Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) akasema "Mtume akiwa hana mtu yeyote". Kuna baadhi ya Mitume waliouawa na watu wao. Ni dalili yenye kuonesha kuwa ni wachache ndio wenye kufuata haki. Allaah (Ta'ala) amesema:

وَمَا أَكْثَرُ النَّاسِ وَلَوْ حَرَصْتَ بِمُؤْمِنِينَ

"Na wengi wa watu hawatoamini japokuwa utafanya hima."¹⁴

¹² Muslim (2199) na Ahmad (13819).

¹³ Muslim (2198) na Ahmad (14163).

Maneno yake (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) "Huyo ni Muusa na watu wake" ni dalili yenye kuonesha fadhila za Muusa na kwamba wana wa Israaiyl wengi walimuitikia.

Maneno ya Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) "Nikaona kundi kubwa" na katika upokezi mwingine imekuja "Nikaona kundi kubwa la watu lililofunika upeo" na katika upokezi mwingine imekuja "Nikaona kundi kubwa la watu lililofunika upeo mwingine" ni dalili yenye kuonesha ukubwa wa Ummah huu na kwamba una wafuasi wengi. Kwa sababu ndio Ummah wa mwisho na Mtume wao ndio Mtume wa mwisho. Wao ndio watakuwa nusu ya wafuasi wa Peponi au theluthi, kama ilivyokuja katika Hadiyth.

Maneno ya Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) "... miongoni mwao kuna 70.000... ". Imekuja katika Hadiyth nyingine kuwa kila mmoja katika hawa 70.000 wataingia 70.000 Peponi bila ya hesabu¹⁵ kutokana na ukamilifu wa uchaji Allaah wao, imani na msimamo wao. Kadri jinsi mtu atavyokuwa na msimamo ndivyo itavyozidi kuwa sahali kuingia Peponi.

Maneno yake (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) "Huku nyuma watu wakaanza kujadiliana..." bi maana juu ya sifa zao na ni kina nani. Hapa kuna dalili juu ya kufanya utafiti, kusoma na kupeleleza maandiko kwa ajili ya elimu.

Maneno ya Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) "Ni wale wasioomba kusomewa Ruqyah" bi maana ya kwamba hawamuombi mtu awesomee. Ni dalili yenye kuonesha kuwa lililo bora ni kutowaomba watu kitu ikiwa ni pamona na Ruqyah. Pamoja na hivyo hakukataza hilo. Lililo bora tu ni kutowaomba hilo. Wakati wa haja ni sawa kuomba tiba na ni bora kutofanya hivo ikiwa hakuna haja hiyo.

¹⁴ 12:103

¹⁵ Ahmad (22). Swahiyh kwa mujibu wa al-Albaaniy katika "Swahiyh-ul-Jaami" (1057).

Maneno ya Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) "... hawajichomi chuma cha moto... ". Bora ni kuacha kufanya hivo ikiwa ni pasi na haja kwa sababu ni aina fulani ya kujiadhibu. Ikiwa mtu anaweza kujitibu kwa kutumia dawa nyingine bora ni kufanya hivo. Ikiwa kuna haja ya kufanya hivo hakuna machukizo kuitumia kutokana na Hadiyth:

"Dawa iko katika mambo matatu; kujichoma kwa chuma cha moto, asali na kuumikwa."

Katika matamshi mengine Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

"Ninaukataza Ummah wangu na kujichoma kwa chuma cha moto."¹⁶

Hata hivyo makatazo haya ni kwa ya machukizo na si kwamba ni haramu. Kwa ajili hiyo kuna baadhi ya Maswahabah waliojitibu kwa kujichoma pindi walipokuwa wagonjwa. Ni jambo lenye kujuzu wakati wa haja lakini ni bora zaidi kwa dawa nyingine. Hii ni moja katika sifa za wale watu 70.000. Lakini hata hivyo kama jinsi tulivyosema inajuzu wakati wa haja.

Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema "... na wala hawaamini rajua nzuri na mbaya... ". Ni shirki. Kuamini rajua nzuri na mbaya maana yake ni mtu kuamini mkosi pale anapona au kusikia kitu na hiyo inakuwa ni sababu ya kumzuia kufanya kitu alichokuwa amepanga. Huu ni uovu uliyokatazwa. Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

"Kuamini rajua nzuri au mbaya ni shirki."¹⁷

Amesema (Swalla Allaahu 'alayhi wa salam) tena:

"Haifai ikamzuia muislamu."¹⁸

¹⁶ al-Bukhaariy (5681) na Muslim (2205).

¹⁷ Abu Daawuud (3910), Ibn Maajah (3538) na Ahmad (3687). Swahiyh kwa mujibu wa al-Albaaniy katika "Swahiyh-ul-Jaami" (3960).

Kadhalika amesema:

"Mmoja wenu akiona kitu chenye kumchukiza aseme: "Ee Allaah! Hakuna mwengine mwenye kuleta mema isipokuwa Wewe. Hakuna mwengine mwenye kuzuia mabaya isipokuwa Wewe. Hakuna nguvu za kufanya utiifu wala kuacha maasi isipokuwa kwa msaada Wako."¹⁹

Mema ni neema na mabaya ni majanga na shida. Vilevile amesema kuwa kafara ya kuamini rajua nzuri au mbaya ni mtu kusema:

"Ee Allaah! Hakuna kheri isipokuwa kheri Yako. Hakuna makadirio isipokuwa ya Kwako. Hakuna mungu wa haki isipokuwa Wewe."²⁰

Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

"... bali wanamtegemea Mola Wao... " bi maana ni wenye kumtegemea Allaah. Wanamwachia mambo yao Allaah. Hizi ndio hali zao. Wanamtegemea Allaah na kumwamini. Wanatambua kuwa hakuna kitakachowafika isipokuwa kile alichowaandikia. Aidha wanajiepusha na aina zote za shirki na mambo ya kuchukiza kama kujichoma na kuomba kusomewa Ruqyah kwa sababu wanamtegemea Yeye, wanamtegemea na ni wenye kupigania kuwa na dini kamilifu na salama.

Hizi ndio sifa walonazo wale watu 70.000. Ni wale waliotekeleza mambo ya wajibu, wakaachana na mambo ya haramu na ya shirki, wanamtegemea Allaah na kumwachia mambo yote Allaah na pamoja na kuwa wakati huo huo wanafanya sababu zilizoruhusiwa katika kutafuta riziki, kufanya biashara na dawa. Wanaacha yale mambo yenye kuwafanya kuwa na haja na watu wengine kama kuwaomba wawasomee Ruqyah na aina za kujiadhibu maadamu si wenye

¹⁸ Abu Daawuud (3919). Dhaifu kwa mujibu wa al-Albaaniy katika "Silsilat-ul-Ahaadiyth adh-Dhwa'iyfah (1619).

¹⁹ Abu Daawuud (3919). Dhaifu kwa mujibu wa al-Albaaniy katika "Silsilat-ul-Ahaadiyth adh-Dhwa'iyfah (1619).

²⁰ Ahmad (7045). Nzuri kwa mujibu wa Shu'ayb al-Arnaa'uut katika "Musnad Ahmad".

dharurah ya kufanya hivo. Wanaacha mambo fulani yaliyoruhusiwa kwa sababu tu yana mapungufu. Malipo yao Allaah awaingize Peponi pasi na hesabu wala adhabu.

FAIDA

Ruqyah pasi na kuomba inafaa. Ikiwa Ruqyah imefungamana na mtu kuomba lililo bora zaidi ni mtu kuacha kufanya hivo midhali hakuna haja. Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Kujitibu [kwa Ruqyah] kunaruhusu midhali sio shirki.”

Ruqyah inajuzu kwa sharti tatu:

- 1- Iwe kwa lugha yenye kufahamika.
- 2- Isiwe na mambo yasiyojuzu katika Shari'ah.
- 3- Ifanywe kwa kutarajia ya kwamba Allaah ndiye mponyaji. Mtu asitegemee Ruqyah yenyewe.

Katika hali hii Ruqyah inajuzu.

Kadhalika kujichoma kunajuzu wakati wa haja. Lakini hata hivyo kuacha hilo ni bora zaidi kwa sababu ni aina ya kujiadhibu.

Sababu zingine zote ni lazima zifanywe. Ni lazima kula na kunywa. Riziki ni lazima itafutwe. Mambo ya wajibu ni lazima yafanywe na madhambi ni lazima yaepukwe ili mtu aweze kuingia Peponi. Sababu zilizo na mapungufu, kama mfano wa kujichoma na kuomba kusomewa Ruqyah, bora zaidi ni kuziepuka.

Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema “'Ukaashah amekutangulia" ili kufunga mlango wasije kuwaomba wale wasiostahiki. Wanachuoni wanatumia Hadiyth hii ili kutolea dalili kuonesha kuwa inajuzu kutaka udhuru kwa ajili ya kuzuia kitu kibaya pasi na kumuumbua wala kumfedhehesha mtu.

Ni jambo lisilokuwa na ubaya kwa mtu kujifanyia Ruqyah mwenyewe na ni bora kutumuomba yeyote akusomee. Ni sawa kwa mtu akamuomba ndugu yake amuombee du'aa. Imetajwa katika Hadiyih:

"Usitusahau katika du'aa yako."²¹

Ni jambo limewekwa katika Shari'ah kujitenga mbali na mambo yote yenye kudhuru ikiwa ni pamoja na mtu mgonjwa ambaye ana maradhi ya kuambukiza. Ajitenga naye. Imetajwa katika Hadiyih:

"Mgonjwa asiyende kwa ambaye ana afya njema."²²

Hata hivyo inafaa kwa mtu kufanya hivo ikiwa mtu huyo anamwamini Allaah na kumtegemea Yeye kutokana na imani yake ya wazi. Imethibiti ya kwamba (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) aliika na kula pamoja na mtu mwenye ukoma na kusema:

"Kula kwa jina la Allaah kwa kumtegemea Allaah."²³

Inafaa vilevile kuyasomea maji na kuyatemea cheche za mate. Imethibiti kuwa Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) alitemea cheche za mate kwenye maji ya Thaabit bin Qays²⁴. Kisomo kinatakiwa kiwe kile ambacho ni chepesi kwa mtu kusoma kutoka katika Qur-aan.

²¹ Ahmad (195), Abu Daawuud (1498) na Ibn Maajah (2894). Dhaifu kwa mujibu wa al-Albaaniy katika "Dhwa'iyf-ul-Jaami'" (14425).

²² al-Bukhaariy (5771) na Muslim (2221).

²³ Abu Daawuud (3925), at-Tirmidhiy (1817) na al-Haakim (7196). Dhaifu kwa mujibu wa al-Albaaniy katika "Dhwa'iyf Sunan at-Tirmidhiy" (307).

²⁴ Abu Daawuud (3885). Dhaifu kwa mujibu wa al-Albaaniy katika "Dhwa'iyf Sunan Abiy Daawuud" (836).

04. Kuogopa shirki

Shaykh-ul-Islaam Muhammad bin 'Abdil-Wahhaab (Rahimahu Allaah) amesema:

1- Allaah ('Azza wa Jall) amesema:

إِنَّ اللَّهَ لَا يَغْفِرُ أَنْ يُشْرَكَ بِهِ وَيَغْفِرُ مَا دُونَ ذَلِكَ لِمَنْ يَشَاءُ

"Hakika Allaah hasamehi kushirikishwa na anasamehe yaliyo chini ya hayo kwa amtakae." (an-Nisaa' 04:48)

2- Ibraahiym ('alayhis-Salaam) amesema:

وَاجْتَنِبْنِي وَبَنِيَّ أَنْ نَعْبُدَ الْأَصْنَامَ

"Uniepushe mimi na wanangu kuabudu masanamu." (Ibraahiym 14:35)

3- Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

"Kikubwa ninachokikhofieni juu yenu ni shirki ndogo." Alipoulizwa juu yake akasema: "Kujionyesha."²⁵

4- Ibn Mas'ood (Radhiya Allaahu 'anh) ameeleza kuwa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

"Anayekufa ilihali ni mwenye kuomba wenza pamoja na Allaah ataingia Motoni."²⁶

Ameipokea al-Bukhaariy.

²⁵ Ahmad (23680). Swahiyh kwa mujibu wa al-Albaaniy katika "Swahiyh-ul-Jaami" (1555).

²⁶ al-Bukhaariy (4497).

5- Muslim amepokea kuwa Jaabir (Radhiya Allaahu 'anh) amesimulia kwamba Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Mtu ambaye atakutana na Allaah ilihali hamshirikishi na chochote ataingia Peponi. Na atakayekutana Naye ilihali ni mwenye kumshirikisha na chochote ataingia Motoni.”²⁷

MAELEZO

Mlango unahusiana na uwajibu wa kuogopa shirki. Ni wajibu kwa muumini kuiogopa shirki na maasi. Ajitenge nayo mbali na khaswa shirki. Asijiami nayo juu ya nafsi yake.

Shirki maana yake ni kumshirikisha Allaah na mwengine katika 'ibaadah pasi na kujali inahusiana na 'ibaadah ipi. Ndio maana ikaitwa kuwa ni shirki. 'Ibaadah ni haki ya Allaah Pekee. Baya zaidi kuliko hilo ni kumfanyia 'ibaadah aina zote asiyekuwa Allaah.

1- Allaah ('Azza wa Jall) amesema:

إِنَّ اللَّهَ لَا يَغْفِرُ أَنْ يُشْرَكَ بِهِ وَيَغْفِرُ مَا دُونَ ذَلِكَ لِمَنْ يَشَاءُ

“Hakika Allaah hasamehi kushirikishwa na anasamehe yaliyo chini ya hayo kwa amtakae.”

Hapa kumbainishwa ukubwa na ukhatari wa shirki. Mtu akifa katika hali hiyo hasamehewi. Atadumishwa Motoni milele. Hilo ni tofauti na madhambi mengine. Ni jambo liko chini ya utashi wa Allaah akitaka atamuadhibu kisha baadae amwingize Peponi na akitaka atamsamehe. Lakini inapokuja katika shirki Allaah (Ta'ala) anasema:

²⁷ al-Bukhaariy (129) na Muslim (93).

إِنَّهُ مَنْ يُشْرِكْ بِاللَّهِ فَقَدْ حَرَّمَ اللَّهُ عَلَيْهِ الْجَنَّةَ وَمَأْوَاهُ النَّارُ

“Hakika yule atakayemshirikisha Allaah, bila shaka Allaah atamharamishia Pepo na makazi yake yatakuwa ni motoni.”²⁸

2- Ibraahiym (‘alayhis-Salaam) amesema:

وَاجْتُنِبْنِي وَبَنِيَّ أَنْ تَعْبُدَ الْأَصْنَامَ

“Na Uniepushe na wanangu kuabudu masanamumu.”

Hapa kuna ukhatari wa shirki. Bwana wa Mitume baada ya Mtume wetu (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) alikuwa ni mwenye kuiogopa shirki. Ni wajibu kuwaiga na kuiogopa shirki zaidi kuliko walivyokuwa.

Masanamu ni kitu kilicho kwa aina kama ya mtu na wanyama. Kulikuwepo aina mbalimbali za washirikina. Kuna ambao walikuwa wakiabudu masanamumu. Wengine walikuwa wakiabudu yasiyokuwa masanamumu kama mti, bahari, jua na mwezi. Wote kitu kimoja ndio kilikuwa chenye kuwakutanisha ambacho ni kumtekelezea ‘ibaadah asiyekuwa Allaah (‘Azza wa Jall). Sanamu inaweza kuitwa pia "mzimu".

03- Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) amesema:

“Kikubwa ninachokikhofieni juu yenu ni shirki ndogo.” Alipoulizwa juu yake akasema: "Kujionyesha."

Hadiyth hii imepokewa na Ahmad kwa mlolongo wa wapokezi mzuri kupitikia kwa Mahmuud bin Lubayd kutoka kwa Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam). Imepokelewa vilevile kupitia njia zingine na milolongo ya wapokezi ilio na nguvu. Zote zinatolea dalili kuonesha kuwa ni wajibu kuwa na tahadhari na

²⁸ 05:72

kujionyesha na kwamba ni jambo la khatari. Kuna watu wema wenye kutumbukia ndani yake. Wanaweza kutumbukia katika kujionyesha pindi wanaposwali, wanapota zakaah, wanapoamrisha mema na kukataza maovu. Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

"Mwenye kutaka kusikika basi Allaah atamfichua na yule mwenye kutaka kuonekana na yeye Allaah atamfichukua."²⁹

Utimilifu wa Hadiyith ni:

"Allaah atawaambia wale wenye kujionyesha siku ya Qiyaamah: "Nendeni kwa wale mliokuwa mkijionyesha kwao duniani na mtazame kama watakupeni malipo yoyote."³⁰

Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

"Allaah (Ta'ala) amesema: "Mimi ni Mwenye kujitosheleza ambaye sina haja ya washirika. Hivyo basi, yule mwenye kufanya kitendo na akanishirikisha Mimi pamoja na wengine nitamwacha yeye na shirki yake."³¹

Imepokelewa na Muslim. Kwa ajili hiyo ni wajibu kwa mtu amtakasie 'ibaadah Allaah peke yake.

4- Ibn Mas'uud (Radhiya Allaahu 'anh) ameeleza kwamba Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

"Anayekufa ilihali ni mwenye kuomba wenza pamoja na Allaah ataingia Motoni."

Imepokelewa na al-Bukhaariy.

²⁹ al-Bukhaariy (6499) na Muslim (93).

³⁰ Ahmad (23680). Swahiyh kwa mujibu wa al-Albaaniy katika "Swahiyh-ul-Jaami" (1555).

³¹ Muslim (2985).

Mwenzwa ni mshirika anayeombwa msaada na kutakwa uokozi pamoja na Allaah. Mtu kama huyu atadumishwa Motoni milele. Katika upokezi mwingine imekuja ya kwamba Ibn Mas'uud amesema:

"Na anayekufa ilihali si mwenye kuomba wenza pamoja na Allaah ataingia Peponi."

Bi maana yule mwenye kufa juu ya Tawhiyd ataingia Peponi. Ni dalili yenye kuonesha kuwa yule mwenye kujichukulia wenza katika watu wema, Mitume, miti na mawe akawaabudu pamoja na Allaah ataingia Motoni.

5- Muslim amepokea kuwa Jaabir (Radhiya Allaahu 'anh) amesimulia kwamba Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

"Mtu ambaye atakutana na Allaah ilihali hamshirikishi na chochote ataingia Peponi. Na atakayekutana Naye ilihali ni mwenye kumshirikisha na chochote ataingia Motoni."

Hapa kuna ukhatari wa shirki na kwamba ni wajibu kuigopa na kutahadhari nayo.

Hadiyth ndani yake mna mambo mawili yanayopelekea:

1- Mwenye kukutana na Allaah pasi na kumshirikisha na chochote ataingia Peponi.

2- Mwenye kukutana na Allaah ilihali ni mshirikina ataingia Motoni. Kwa ajili hii ndio maana imetajwa katika upokezi mwingine ya kwamba Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

"Je, nisikujuzeni juu ya mambo mawili yanayohitajika?" Wakasema: "Ndio." Akasema: "Mtu ambaye atakutana na Allaah ilihali hamshirikishi na chochote ataingia Peponi. Na atakayekutana Naye ilihali ni mwenye kumshirikisha na chochote ataingia Motoni."

05. Kulingania katika kushuhudia ya kwamba hakuna mungu wa haki isipokuwa Allaah

Shaykh-ul-Islaam Muhammad bin 'Abdil-Wahhaab (Rahimahu Allaah) amesema:

1- Allaah (Ta'ala) amesema:

قُلْ هَذِهِ سَبِيلِي أَدْعُو إِلَى اللَّهِ ۚ عَلَىٰ بَصِيرَةٍ أَنَا وَمَنِ اتَّبَعَنِي

"Sema: "Hii ndio njia yangu: nalingania kwa Allaah kwa ujuzi - mimi na anayenifuata." (Yuusuf 12:108)

2- Ibn 'Abbaas (Radhiya Allaahu 'anhumaa) ameeleza kuwa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) pindi alipomtuma Mu'aadh Yemen alimwambia:

"Hakika wewe unawaendea watu katika watu wa Kitabu, basi iwe kitu cha kwanza utakachowalingania kwacho iwe ni kushuhudia ya kwamba hapana mungu wa haki isipokuwa Allaah... "

Katika upokezi mwingine imekuja:

"... wampwekeshe Allaah. Ikiwa watakutii kwa hilo, basi wafundishe ya kwamba Allaah amewafaradhishia swalah tano kila mchana na usiku. Ikiwa watakutii kwa hilo, wafundishe ya kwamba Allaah amewafaradhisha zakaah itayochukuliwa kutoka kwa matajiri wao na wapewe mafakiri wao. Ikiwa watakutii kwa hilo, tahadhari na kuwachukulia mali yao. Iogope du'aa ya

mwenye kudhulumiwa, kwani hakika hakuna baina yake na baina ya Allaah kizuizi.”³²

Imepokelewa na al-Bukhaariy na Muslim.

3- al-Bukhaariy na Muslim wamepokea kupitia kwa Sahl bin Sa'd (Radhiya Allaahu 'anh) ya kwamba Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) alisema siku ya Khaybar:

“Kuna mtu nitampa bendera kesho, ni mtu anampenda Allaah na Mtume Wake na Allaah na Mtume Wake wanampenda. Allaah atafungua mji kwa mikono yake.” Watu wakabaki macho usiku ule na kutafakari ni nani atapewa nayo. Ilipofika asubuhi wakaamkia mapema kwa Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) kila mmoja akitaraji atapewa yeye. Akasema: “Yuko wapi 'Aliy bin Abiy Twaalib.” Akaambiwa: “Ni mgonjwa wa macho.” Akamtumia ujumbe. Akaletwa. Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) akamtemea mate machoni mwake na kumuomba du'aa. Akapona papo hapo kana kwamba hakuwa mgonjwa. Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) akampa bendera na kumwambia: “Nenda zako taratibu na kwa upole mpaka ufike maeneo yao, kisha uwalinganie katika Uislamu na uwaeleze haki za Allaah (Ta'ala) ambazo ni wajibu kwao. Naapa kwa Allaah! Lau Allaah atamuongoza mtu mmoja kupitia kwako ni bora kwako kuliko ngamia wekundu.”³³

MAELEZO

Mlango unahusiana na ni wajibu kulingania katika kushuhudia ya kwamba hapana mungu wa haki isipokuwa Allaah na kwamba Muhammad ni Mtume wa Allaah. Shahaadah mbili hizi ni zenye kulazimiana. Makusudio ya mwandishi ni kulingania katika Tawhiyd na kumfuata Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam). Hili ni wajibu kwa wanachuoni. Mwandishi amethibitisha hilo kwa Qur-aan na Sunnah kama maneno Yake (Ta'ala):

³² al-Bukhaariy (1395) na Muslim (19).

³³ al-Bukhaariy (309) na Muslim (405).

ادْعُ إِلَى سَبِيلِ رَبِّكَ بِالْحُكْمَةِ وَالْمَوْعِظَةِ الْحَسَنَةِ ۗ وَجَادِلْهُمْ بِالَّتِي هِيَ أَحْسَنُ

“Lingania katika njia ya Mola wako kwa hekima na mawaidha mazuri na jadiliana nao kwa ambayo ni mazuri zaidi.” (Ibraahiym 16:125)

قُلْ هَذِهِ سَبِيلِي أَدْعُو إِلَى اللَّهِ ۚ عَلَىٰ بَصِيرَةٍ أَنَا وَمَنِ اتَّبَعَنِي

”Sema: “Hii ndio njia yangu: nalingania kwa Allaah kwa ujuzi - mimi na anayenifuata.” (Yuusuf 12:108)

وَمَنْ أَحْسَنُ قَوْلًا مِّمَّن دَعَا إِلَى اللَّهِ

“Na nani aliye na kauli nzuri zaidi kuliko yule anayelingania kwa Allaah.” (Fuswswilat 41:33)

Ni wajibu kwa wanachuoni kulingania katika Tawhiyd na Allaah atakasiwe 'ibaadah shirki iachwe. Vilevile ni wajibu kulingania katika kumuamini Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam), kusadikishwa, kufuatwa yale aliyokuja nayo na kutomkhalifu.

1- Allaah (Ta'ala) amesema:

قُلْ هَذِهِ سَبِيلِي أَدْعُو إِلَى اللَّهِ ۚ عَلَىٰ بَصِيرَةٍ أَنَا وَمَنِ اتَّبَعَنِي

”Sema: “Hii ndio njia yangu: nalingania kwa Allaah kwa ujuzi - mimi na anayenifuata.” (al-Baqarah 12:108)

Mzungumzishwa hapa ni Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) na Ummah wake. Sema ya kwamba hii ndio njia yangu ninayopita ambapo nampwekesha Allaah na kumtakasia 'ibaadah, kutoa zakaah na mengineyo. Hii ndio njia ya Allaah iliyonyooka, uongofu na imani.

أَدْعُو إِلَى اللَّهِ ۖ عَلَىٰ بَصِيرَةٍ

“... nalingania kwa Allaah kwa ujuzi... “

Ninalingania katika dini ya Allaah na sio katika ufalme, maslahi, mali au mambo ya kidunia. Ninalingania katika kumpwekesha Allaah Pekee na kufuata Shari'ah Yake na ninafanya hivo kwa ujuzi na uongofu.

أَنَا وَمَنْ اتَّبَعَنِي

“... mimi na anayenifuata... “

Bi maana wafuasi wangu vilevile wanalingania kwa ujuzi na umaizi. Wafuasi wake wana ujuzi na umaizi. Wanachuoni ambao wanalingania ulinganizi wao wanafanya hivo kwa ujuzi na umaizi. Wanachuoni ambao hawalinganii katika njia ya Allaah sio katika wafuasi zake kihakika. Kwa sababu wafuasi zake hawanyamazi na wala hawalinganii kwa ujinga. Allaah (Ta'ala) amesema:

ادْعُ إِلَى سَبِيلِ رَبِّكَ بِالْحُكْمَةِ وَالْمَوْعِظَةِ الْحَسَنَةِ

“Lingania katika njia ya Mola wako kwa hekima... “

Bi maana kwa ujuzi. Hii ndio kazi ya Mitume, wanachuoni na wema wote. Hili ni wajibu kwa yule ambaye yuko na elimu. Anatakiwa kulingania kila mahali ikiwa ni pamoja vilevile na msikitini na sehemu nyenginezo na awe na subira.

2- Ibn 'Abbaas (Radhiya Allaahu 'anhumaa) ameeleza kuwa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) pindi alipomtuma Mu'aadh Yemen alimwambia:

“Hakika wewe unawaendea watu katika watu wa Kitabu, basi iwe kitu cha kwanza utakachowalingania kwacho iwe ni kushuhudia ya kwamba hakuna mungu wa haki isipokuwa Allaah... “

Katika upokezi mwingine imekuja:

“... wampwekeshe Allaah. Ikiwa watakutii kwa hilo, basi wafundishe ya kwamba Allaah amewafaradhishia swalah tano kila mchana na usiku. Ikiwa watakutii kwa hilo, wafundishe ya kwamba Allaah amewafaradhisha zakaah itayochukuliwa kutoka kwa matajiri wao na wapewe mafakiri wao. Ikiwa watakutii kwa hilo, tahadhari na kuwachukulia mali yao. Iogope du'aa ya mwenye kudhulumiwa, kwani hakika hakuna baina yake na baina ya Allaah kizuizi.”

Maneno yake Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) “Hakika wewe unawaendea watu katika watu wa Kitabu” yanaonyesha kuwa hawakuwa wajinga. Wana elimu na utata. Anamzindua ili amuandae na kufikisha maamrishi ya Allaah.

Maneno ya Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) “Basi iwe kitu cha kwanza utakachowalingania kwacho iwe ni kushuhudia ya kwamba hakuna mungu wa haki isipokuwa Allaah” ina maana ya kwamba asibabaike na utata wao na elimu yao. Anachotakiwa ni kuhakikisha amewafikishia Tawhiyd na kuwa wanamuabudu Yeye peke yake na si mwingine kama 'Uzayr, 'Iysaa, marabi na watawa wao. Katika upokezi mwingine imekuja ya kwamba awalinganie katika kumuabudu Allaah peke yake. Hii ndio tafsiri ya kushuhudia ya kwamba hapana mungu wa haki isipokuwa Allaah.

Maneno ya Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) “Ikiwa watakutii kwa hilo...” bi maana wakimuabudu Allaah peke yake na si mwingine.

Maneno ya Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) “... basi wafundishe ya kwamba Allaah amewafaradhishia swalah tano kila mchana na usiku” ni dalili yenye kuonesha kuwa mshirikina kwanza anatakiwa kulinganiwa katika Tawhiyd. Akiikubali ndio alinganiwe katika swalah. Akikubali na kuisimamisha ndio analinganiwa katika zakaah ambayo inachukuliwa kutoka kwa matajiri na kupewa mafukara. Wametajwa mafukara kwa sababu ndio muhimu wenye

kustahiki zaidi kupewa zakaah. Kadhalika ndio ambao Allaah ameanza pale aliposema:

إِنَّمَا الصَّدَقَاتُ لِلْفُقَرَاءِ وَالْمَسْكِينِ وَالْعَامِلِينَ عَلَيْهَا وَالْمُؤَلَّفَةِ قُلُوبُهُمْ وَفِي الرِّقَابِ وَالْغَارِمِينَ وَفِي سَبِيلِ اللَّهِ
وَأَبْنِ السَّبِيلِ ۖ فَرِيضَةً مِّنَ اللَّهِ ۗ وَاللَّهُ عَلِيمٌ حَكِيمٌ

“Hakika Zakaah ni kwa ajili ya mafakiri na masikini na wanaozitumikia na wanaotiwa nguvu nyoyo zao [kwa ajili ya Uislamu] na kuwakomboa mateka na wenye deni na katika njia ya Allaah na msafiri [aliyeharibikiwa]. Ni faradhi itokayo kwa Allaah; na Allaah ni Mjuzi, Mwenye hekima.” (at-Tawbah 09:60)

Maneno ya Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) “Ikiwa watakutii kwa hilo, tahadhari na kuwachukulia mali yao” bi maana usichukue mali yao yenye thamani kwa nguvu. Chukua kati kwa kati. Kuna mali tukufu, mali ya kati kwa kati na mali isiyokuwa na maana. Hata hivyo lililo bora kwao ni kutoa mali yao tukufu kwa khiyari yao.

Maneno ya Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) “Iogope du´aa ya mwenye kudhulumiwa” bi maana tahadhari na kuwadhulumu wakaja kuomba dhidi yako na kuitikiwa. Du´aa ya mwenye kudhulumiwa ni yenye kuitikiwa.

Mtume (Swalla ALlaahu ´alayhi wa sallam) alitosheka na mambo haya matatu kwa sababu ndio muhimu zaidi. Mwenye kuyakubali hukubali hajji, swawm na mengineyo. Wakiyakubali mambo hayo matatu ya kwanza basi watafanya hivo kwa imani na kukinaika. Imani hiyo hiyo itawafanya kutekeleza mambo mengine ya Shari´ah. Ndio maana Allaah amekomeka nayo kwa kusema:

فَإِنْ تَابُوا وَأَقَامُوا الصَّلَاةَ وَآتَوُا الزَّكَاةَ فَخَلُّوا سَبِيلَهُمْ

“Lakini akitubu na wakasimamisha swalah na wakatoa zakaah, basi waacheni huru.” (at-Tawbah 09:05)

وَمَا أُمِرُوا إِلَّا لِيَعْبُدُوا اللَّهَ مُخْلِصِينَ لَهُ الدِّينَ خُنَفَاءَ وَيُقِيمُوا الصَّلَاةَ وَيُؤْتُوا الزَّكَاةَ

“Hawakuamrisha jengine isipokuwa wamuabudu Allaah pekee hali ya kumtakasia yeye dini kwa imani safi kabisa na ya asli na wasimamishe swalah na watoe zakah.” (al-Bayyinah 98:05)

Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) amesema:

“Nimeamrisha kuwapiga watu vita mpaka washuhudie ya kwamba hapana mungu wa haki isipokuwa Allaah na mimi ni Mtume wa Allaah, wasimamishe swalah na watoe zakaah.”

Misingi hii mitatu ndio muhimu zaidi.

3- al-Bukhaariy na Muslim wamepokea kupitia kwa Sahl bin Sa’d (Radhiya Allaahu ‘anh) ya kwamba Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) alisema siku ya Khaybar:

“Kuna mtu nitampa bendera kesho, ni mtu anampenda Allaah na Mtume Wake na Allaah na Mtume Wake wanampenda. Allaah atafungua mji kwa mikono yake.” Watu wakabaki macho usiku ule na kutafakari ni nani atapewa nayo. Ilipofika asubuhi wakaamkia mapema kwa Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) kila mmoja akitaraji atapewa yeye. Akasema: “Yuko wapi ‘Aliy bin Abiy Twaalib.” Akaambiwa: “Ni mgonjwa wa macho.” Akamtumia ujumbe. Akaletwa. Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) akantemea mate machoni mwake na kumuomba du’aa. Akapona papo hapo kana kwamba hakuwa mgonjwa. Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) akampa bendera na kumwambia: “Nenda zako taratibu na kwa upole mpaka ufike maeneo yao, kisha uwalinganie katika Uislamu na uwaeleze haki za Allaah (Ta’ala) ambazo ni wajibu kwao. Naapa kwa Allaah! Lau Allaah atamuongoza mtu mmoja kupitia kwako ni bora kwako kuliko ngamia wekundu.”

06. Tafsiri ya Tawhiyd na kushuhudia ya kwamba hapana mungu wa haki isipokuwa Allaah

1- Allaah (Ta'ala) amesema:

أُولَئِكَ الَّذِينَ يَدْعُونَ يَبْتَغُونَ إِلَىٰ رَبِّهِمُ الْوَسِيلَةَ أَيُّهُمْ أَقْرَبُ

“Hao wanaowaomba [wao wenyewe] wanatafuta kwa Mola wao njia [na] kumkurubia kadri wanavyoweza.” (al-Israa' 17:57)

2-

وَإِذْ قَالَ إِبْرَاهِيمُ لِأَبِيهِ وَقَوْمِهِ إِنَّنِي بَرَاءٌ مِّمَّا تَعْبُدُونَ إِلَّا الَّذِي فَطَرَنِي فَإِنَّهُ سَيَهْدِينِ

“Ibraahiym alipomwambia baba yake na watu wake: “Hakika mimi najitoa dhima na yale yote mnayoyaabudu [ya batili]! [Simwabudu mwengine yeyote] isipokuwa Yule ameniumba, basi hakika Yeye ataniongoa.” (az-Zukhruf 43:26-28)

3-

اتَّخَذُوا أَحْبَابَهُمْ وَرُهْبَانَهُمْ أَرْبَابًا مِّنْ دُونِ اللَّهِ

“Wamewafanya marabi wao na watawa wao kuwa ni waungu badala ya Allaah.” (at-Tawbah 09:31)

4-

وَمِنَ النَّاسِ مَن يَتَّخِذُ مِنْ دُونِ اللَّهِ أَنْدَادًا يُحِبُّونَهُمْ كَحُبِّ اللَّهِ

“Wapo katika watu ambao wanafanya badala ya Allaah washirika [na] wanawapenda kama mapenzi [yapasavyo] ya kumpenda Allaah.” (**al-Baqarah 02:165**)

5- Katika Swahiyh imepokelewa kutoka kwa Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) ya kwamba amesema:

“Atakayesema hapana mungu wa haki isipokuwa Allaah na akakufuru kwa vinavyoabudiwa badala ya Allaah, basi imeharamika mali na damu yake na hesabu yake iko kwa Allaah ('Azza wa Jall).”

Maelezo kuhusu mlango huu na ile milango mingine ilio baada yake ndani yake kumetajwa mambo makubwa na ya muhimu. Nayo ni tafsiri ya Tawhiyd na tafsiri ya shahaadah ambayo yamefasiriwa kwa njia ya wazi kabisa.

Katika hayo ni Aayah ya Suurah al-Israa' ambayo imewaraddi washirikina ambao wanawaomba waja wema. Imebainisha ya kwamba hii ndio shirki kubwa.

Katika hayo ni Aayah ya Suurah al-Baraa' inayobainisha ya kwamba watu wa Kitabu waliwafanya marabi wao na watawa wao kuwa ni waungu badala ya Allaah. Allaah amebainisha vilevile ya kwamba hakuwaamrisha jengine isipokuwa wamuabudu Mungu Mmoja. Haya pamoja na kuwa tafsiri ya Aayah isiyokuwa na utatizi ndani yake inahusiana na kuwaabudu wanachuoni na waja wema katika maasi na kwamba hawakuwaomba.

Katika hayo ni maneno ya Ibraahiym ('alayhis-Salaam) kwa makafiri:

إِنِّي بَرَاءٌ مِّمَّا تَعْبُدُونَ إِلَّا الَّذِي فَطَرَنِي

“Hakika mimi najitoe dhima na yale yote mnayoyaabudu [ya batili]! [Simwabudu mwengine yeyote] isipokuwa Yule ameniumb.”

Kwa vile vyote vinavyoabudiwa amemvua Mola Wake. Allaah (Subhaanah) ameeleza kuwa chuki hii na mapenzi haya ndio tafsiri ya shahaadah na kwamba hapana mungu wa haki isipokuwa Allaah na akasema:

وَجَعَلَهَا كَلِمَةً بَاقِيَةً فِي عَقْبِهِ لَعَلَّهُمْ يَرْجِعُونَ

"Na akalifanya ni neno lenye kubakia katika kizazi chake ili [wale wanaopinda kutoka katika ile imani safi] wapate kurejea." (**az-Zukhruf 43:28**)

Katika hayo ni Aayah ya Suurah al-Baqarah inayohusiana na makafiri ambao Allaah (Ta'ala) amesema juu yao:

وَمَا هُمْ بِخَارِجِينَ مِنَ النَّارِ

"Wala hawatokuwa wenye kutoka Motoni." (**al-Baqarah 02:167**)

Ametaja namna ambavyo wanawapenda washirika wao kama wanavyompenda Allaah. Haya yanafahamisha ya kwamba wao walikuwa na mapenzi makubwa kabisa. Pamoja na hivyo hayakuwafanya kuwa waislamu. Vipi kuhusu yule ambaye anampenda mshirika zaidi kuliko anavyompenda Allaah? Vipi kuhusu yule ambaye hampendi isipokuwa mshirika peke yake na akawa hampendi Allaah?

Katika hayo ni maneno yake (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam):

"Atakayesema hapana mungu wa haki isipokuwa Allaah na akakufuru kwa vinavyoabudiwa badala ya Allaah, basi imeharamika mali na damu yake na hesabu yake iko kwa Allaah ('Azza wa Jall)."

Hadiyth hii ndio tafsiri bora kabisa iwezayo kufasiri maana ya hapana mungu wa haki isipokuwa Allaah. Hakufanya kule kutamka tu ndio kunamsalimisha mtu maisha yake na damu yake. Wala kule kutambua, kukubali na kwamba hamuombi mwengine asiyekuwa Allaah pekee. Uhakika wa mambo ni kuwa

mali na damu yake havisalimiki mpaka vilevile akanushe vile vyote vinavyoabudiwa badala ya Allaah. Iwapo atakuwa na mashaka au akanyamaza juu ya suala hili basi havisalimiki mali wala damu yake. Suala hili ni kubwa na tukufu zaidi. Ni jambo liko wazi kabisa. Ni hoja yenye kukata kabisa dhidi ya wapinzani.

MAELEZO

Hapa mwandishi amebainisha tafsiri ya Tawhiyd na kushuhudia ya kwamba hapana mungu wa haki isipokuwa Allaah kwa njia inayoafikiana na matamshi yake na kuonyesha yanayopingana nayo. Kwa sababu mambo hufahamika kwa kinyume chake. Ametaja mlango huu ili uweze kuelewa uhakika wa Tawhiyd. Uhakika wake ni kumpwekesha Allaah kwa 'ibaadah na kumtekelezea aina zote Yeye. Unatakiwa kuamini hilo kwa moyo na kulitendea kazi kwa viungo vya mwili:

1- Allaah (Ta'ala) amesema:

أُولَئِكَ الَّذِينَ يَدْعُونَ يَبْتَغُونَ إِلَىٰ رَبِّهِمُ الْوَسِيلَةَ أَيُّهُمْ أَقْرَبُ

“Hao wanaowaomba [wao wenyewe] wanatafuta kwa Mola wao njia [na] kumkurubia kadri wanavyoweza.” (al-Israa' 17:57)

Kabla ya hapo Allaah (Ta'ala) amesema:

قُلْ ادْعُوا الَّذِينَ زَعَمْتُمْ مِّنْ دُونِهِ فَلَا يَمْلِكُونَ كَشْفَ الضَّرِّ عَنْكُمْ وَلَا تَحْوِيلًا

"Sema: “Iteni wale ambao mnadai [ni waabudiwa] badala ya Allah, basi [mtaona kuwa] hawamiliki kukuondesheeni dhara na wala kuihamisha [kwa mwengine].” (1-Israa' 17:56)

Kumuomba asiyeweza kumiliki kuondosha dhara wala kuleta manufaa badala ya Allaah ndio shirki na kinyume chake ndio Tawhiyd. Allaah anamwamrisha

Muhammad (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) kuwaambia wale wanaowaomba waungu wao badala ya Allaah kwa njia ya kuwakemea:

فَلَا يَمْلِكُونَ كَشْفَ الضُّرِّ

"... hawamiliki kukuondesheeni dhara..."

Bi maana aina zote za madhara.

وَلَا تَحْوِيلاً

"... na wala kuihamisha [kwa mwengine]."

Bi maana hawawezi kuhamisha dhara kutoka sehemu moja kwenda nyingine kama kutoka kichwani kwenda miguuni. Hili ni kwa Allaah pekee ndiye awezaye kuondosha mara na kuleta manufaa. Allaah (Ta'ala) amesema:

أُولَئِكَ الَّذِينَ يَدْعُونَ يَبْتَغُونَ إِلَىٰ رَبِّهِمُ الْوَسِيلَةَ أَيُّهُمْ أَقْرَبُ

"Hao wanaowaomba [wao wenyewe] wanatafuta kwa Mola wao njia [na] kumkurubia kadri wanavyoweza." (al-Israa' 17:57)

Anamaanisha wale wanaowaomba Malaika, Mitume na waja wema. Kwa ajili hiyo amesema:

يَبْتَغُونَ إِلَىٰ رَبِّهِمُ الْوَسِيلَةَ

"... wanatafuta kwa Mola wao njia..."

Bi maana pamoja na kuwa wale wanaoombwa ni wema hawamiliki kuondosha dhara wala kuliamisha. Ina maana kwamba masanamu mengine yote wana haki zaidi ya kutoweza kufanya hivo. Njia maana yake ni kujikurubisha kwa Allaah

kwa utiifu. Wao wenyewe wanajitahidi kuwa karibu na Allaah kwa kufanya aina mbalimbali za utiifu.

وَيَرْجُونَ رَحْمَتَهُ وَيَخَافُونَ عَذَابَهُ

"... wanataraji Rahmah Yake na wanakhofu adhabu Yake... " (al-Israa' 17:57)

Kwa sababu ni waja Wake. Wanamtarajia Yeye na wanamuogopa. Ni vipi basi wataombwa?

2-

وَإِذْ قَالَ إِبْرَاهِيمُ لِأَبِيهِ وَقَوْمِهِ إِنَّنِي بَرَاءٌ مِّمَّا تَعْبُدُونَ إِلَّا الَّذِي فَطَرَنِي فَإِنَّهُ سَيَهْدِينِ

"Ibraahiym alipomwambia baba yake na watu wake: "Hakika mimi najitoa dhima na yale yote mnayoyaabudu [ya batili]! [Simwabudu mwengine yeyote] isipokuwa Yule ameniumba, basi hakika Yeye ataniongoa." (az-Zukhruf 43:26-28)

Hii ndio tafsiri ya Tawhiyd. Maneno Yake:

إِنِّي بَرَاءٌ مِّمَّا تَعْبُدُونَ

"Hakika mimi najitoa dhima na yale yote mnayoyaabudu [ya batili]!..."

ni sawa na maneno yetu "Hapana mungu wa haki" na maneno yake:

إِلَّا الَّذِي فَطَرَنِي

"... [Simwabudu mwengine yeyote] isipokuwa Yule ameniumba..."

ni sawa na maneno yetu "isipokuwa Allaah". Haya yanamaanisha kwamba tafsiri ya Tawhiyd ni kujitenga mbali na vile vyote vinavyoabudiwa badala ya

Allaah na kuvitupilia mbali na kuvikemea na kumuabudu Allaah peke yake kwa kumtekelezea aina zote za 'ibaadah.

3-

اتَّخَذُوا أَحْبَابَهُمْ وَرُهْبَانَهُمْ أَرْبَابًا مِّن دُونِ اللَّهِ

"Wamewafanya marabi wao na watawa wao kuwa ni waungu badala ya Allaah."
(at-Tawbah 09:31)

Amebainisha kwamba huku pia ni kumshirikisha Allaah na kwamba Tawhiyd ni kutomuabudu mwengine asiyekuwa Allaah pekee na si watawa, marabi, Mitume wala waja wema. Hayo ni tofauti na yale yaliyofanywa na mayahudi na ambao waliwafanya marabi na manaswara ambao wamewafanya watawa kuwa ni waungu badala ya Allaah kwa njia ya kwamba wamewahalalishia yale ambayo Allaah ameharamisha na wakaharamisha yale ambayo Allaah amehalalisha pasi na dalili ijapokuwa yatakuwa ni yenye kwenda kinyume na Sharii'ah ya Allaah na yale waliyokuja nayo Mitume. Kwa hivyo ndipo wakawa ni wenye kuwaabudu kwa vile wamewatii kwa yale yanayopingana na Shari'ah na wakayatanguliza. 'Addiy bin Haatim ameeleza kwamba Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

"Huku ndio kuwaabudu."³⁴

Mwenye kufanya hivo anakuwa mshirikina. Allaah amesema baada ya hapo:

سُبْحَانَهُ عَمَّا يُشْرِكُونَ

"Ametakasika na ametukuka kutokamana na yale yote wanayomshirikisha." **(al-Hujuraat 49:31)**

³⁴ at-Twabaraaniy (218) na al-Bayhaqiyy (20137). Swahiyh kwa mujibu wa al-Albaaniy katika "Silsilaat-ul-Ahaadiyth as-Swahiyhah" (3293).

Faida

Waabudu makaburi wameyafanya makaburi kuwa ni waungu badala ya Allaah. Kwa hiyo ni wajibu kuwabainishia haki. Kwa sababu kitendo chao ni aina kubwa ya ukafiri. Hata hivyo wasiuawe. Inatakiwa kwanza kuwabainishia haki na kuwasimamishia hoja. Endapo wataendelea basi hapo ndipo wanatakiwa kuuawa ikiwa kuna yeyote ambaye anaweza kuwasimamishia adhabu hiyo.

4-

وَمَنْ النَّاسِ مَنْ يَتَّخِذُ مِنْ دُونِ اللَّهِ أَنْدَادًا يُحِبُّونَهُمْ كَحُبِّ اللَّهِ

"Wapo katika watu ambao wanafanya badala ya Allaah washirika [na] wanawapenda kama mapenzi [yapasavyo] ya kumpenda Allaah." (**al-Baqarah 2:165**)

Aayah hii pia inafasiri Tawhiyd kwa kuelezea kinyume chake. Wale wanaojifanyia waungu wanawapenda, kuwaadhimisha, wanawaomba, wanawataka msaada na wanawapenda mapenzi maalum ambayo yanapelekea kuwaabudu badala ya Allaah. Hii ni shirki kubwa. Allaah amewasema vibaya watu hawa na akawatishia Moto kama alivosema mwishoni mwa Aayah:

كَذَلِكَ يُرِيهِمُ اللَّهُ أَعْمَالَهُمْ حَسَرَاتٍ عَلَيْهِمْ وَمَا هُمْ بِخَارِجِينَ مِنَ النَّارِ

"Hivyo ndivo Allaah atakavyowaonyesha matendo yao kuwa ni majuto juu yao. Wala hawatokuwa wenye kutoka Motoni." (**al-Baqarah 02:167**)

5- Imepokelewa Hadiyith Swahiyh kutoka kwa Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) ambaye amesema:

"Atakayesema hapana mungu wa haki isipokuwa Allaah na akakufuru kwa vinavyoabudiwa badala ya Allaah, basi imeharamika mali na damu yake na hesabu yake iko kwa Allaah ('Azza wa Jall)."

Ameipokea Muslim kupitia kwa Sa'd bin Twaariq al-Ashjaa'iy.

Katika upokezi mwingine imekuja: "Atakayesema hapana mungu wa haki isipokuwa Allaah" na upokezi mwingine imekuja: "Yule ambaye atampwekesha Allaah". Haya yanabainisha maana ya shahaadah na kwamba maana yake ni kuwa 'ibaadah anatakiwa kufanyiwa Allaah pekee.

Maneno yake Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam): "... na akakufuru kwa vinavyoabudiwa badala ya Allaah" ni kwamba amekanusha vile vyote vyenye kuabudiwa badala ya Allaah na akaamini hivo moyoni mwake.

Maneno yake Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam): "... basi imeharamika mali na damu..." maana yake ni kwamba amekuwa muislamu na hivyo amelazimika kutekeleza Shari'ah za Allaah.

Maneno yake Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam): "... na hesabu yake iko kwa Allaah ('Azza wa Jall)" ni kwamba akiwa ni mkweli ataingia Peponi na kama amesema kwa ulimi wake tu, na si kutoka kwenye moyo wake, anakuwa ni katika wanafiki. Hukumu yake ni kama hukumu ya wanawake duniani na Aakhirah ataingia Motoni.

07. Kuvaa cheni, uzi na mfano wavyo kwa ajili ya kuondosha au kuzuia dhara ni shirki

Shaykh-ul-Islaam Muhammad bin 'Abdil-Wahhaab (Rahimahu Allaah) amesema:

1- Allaah (Ta'ala) amesema:

أُولَئِكَ الَّذِينَ يَدْعُونَ يَبْتَغُونَ إِلَىٰ رَبِّهِمُ الْوَسِيلَةَ أَيُّهُمْ أَقْرَبُ

"Sema: "Je, mnaonaje wale mnaowaomba badala ya Allaah ikiwa Allaah atanitakia dhara, je, wao wataweza kuondosha dhara Yake?" (az-Zumar 39:38)

2- 'Imraan bin Husayn (Radhiya Allaahu 'anh) amesimulia kwamba Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) alimuona mtu mkononi mwake kavaa kicheni [cha mfano wa pete] ya shaba. Akamuuliza: "Ni kitu gani hichi?" Mtu yule akajibu: "Kinanikinga na udhaifu." Akasema: "Kivue. Kwani hakika hakikuzidishii isipokuwa udhaifu. Lau ungekufa nawe bado wakivaa usingelifaulu kamwe."

Ameipokea Ahmad kwa mlolongo wa wapokezi usiokuwa na neno. Amepokea vilevile kupitia kwa 'Uqbah bin 'Aamir (Radhiya Allaahu 'anh) kwamba Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

3- "Yeyote atakayevaa hirizi, basi Allaah hatomtimizia na yule atakayevaa au kutundika chaza ndogo, Allaah asimpe raha yoyote."³⁵

Katika upokezi mwingine imekuja:

³⁵ Ahmad (17440), Abu Ya'laa (1759) na at-Twahaawiy (6660). Nzuri kwa mujibu wa Shu'ayb al-Arnaa'uut katika "Musnad-ul-Imaam Ahmad".

4- "Yeyote atakayevaa hirizi ameshirikisha."³⁶

5- Ibn Abiy Haatim amepokea kutoka kwa Hudhayfah (Radhiya Allaahu 'anh) alimuona mtu ambaye mkononi mwake kulikuwa kipande cha uzi anataka umponye homa. Akaukata ule uzi na akasoma maneno Yake:

وَمَا يُؤْمِنُ أَكْثَرُهُمْ بِاللَّهِ إِلَّا وَهُمْ مُشْرِكُونَ

"Wengi kati yao hawamwamini Allaah isipokuwa wao ni wenye kufanya shirki."
(Yuusuf 12:106)

MAELEZO

Mlango huu haukusomwa kwa Imaam Ibn Baaz (Rahimahu Allaah).

³⁶ Ahmad (17458). Swahiyh kwa mujibu wa al-Albaaniy katika "Swahiyh-ul-Jaami" (11340).

08. Kuhusu matabano na hirizi

Shaykh-ul-Islaam Muhammad bin 'Abdil-Wahhaab (Rahimahu Allaah) amesema:

1- Imesihi kupokelewa kutoka kwa Abu Bashiyr al-Answaariy (Radhiya Allaahu 'anh) kwamba alisafiri mara kadhaa pamoja na Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) ambapo akaagiza mjumbe kupeleka ujumbe usemao:

“Pasiachwe katika shingo ya ngamia kidani cha kamba au mkufu isipokuwa kikatwe.”³⁷

2- Ibn Mas'uud (Radhiya Allaahu 'anh) amesimulia kwamba amemsikia Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) akisema:

“Hakika matabano, hirizi na *Tiwalah* ni shirki.”³⁸

Ameipokea Ahmad na Abu Daawuud.

3- 'Abdullaah bin 'Ukaym amepokea ya kwamba Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Atakayevaa/atakayejifungamanisha na kitu basi huwakilishwa kwacho.”³⁹

Ameipokea Ahmad na at-Tirmidhiy.

Hirizi ni kitu huvalishwa watoto ili kimkinge na kupatwa na kijicho. Lakini ikiwa kilichotundikwa ni kitu kilicho na Qur-aan, basi wako baadhi ya Salaf ambao wameonelea kuwa inaruhusu na baadhi yao wengine, akiwemo Ibn Mas'uud

³⁷ al-Bukhaariy (3005) na Muslim (2115).

³⁸ Abu Daawuud (3883), Ibn Maajah (3530), Ahmad (3615), at-Twabaraaniy (10503) na al-Bayhaqi (19387). Swahiyh kwa mujibu wa al-Albaaniy katika "Silsilat-ul-Ahaadiyth as-Swahiyhah" (331).

³⁹ at-Tirmidhiy (2027), an-Nasaa'iy (4079) na Ahmad (18803). Dhaifu kwa mujibu wa al-Albaaniy katika "Dhwa'iyf-ul-Jaamiy" (12477).

(Radhiya Allaahu 'anh) pia, wameona kuwa hairuhusu na wamefanya kuwa ni katika mambo yaliyokatazwa.

Matabano ndio ile inayoitwa "formula". Kuna dalili zinazofahamisha kwamba matabano yasiyokuwa na shirki yanafaa. Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) ameruhusu kujitibu kwa matabano dhidi ya kijicho na homa.

Tiwalah ni kitu kinachotengenezwa na wanadai kwamba humpendezea mke kwa mume wake au mume kwa mke wake.

4- Ahmad amepokea kutoka kwa Ruwayfiy' ambaye amesema:

"Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) alinambia: "Ee Ruwayfiy'! Huenda ukaishi muda mrefu. Hivyo waeleze watu kwamba ambaye anazifunga fundo ndevu zake, akatundika kidani cha kamba ya upinde au akajisafisha kwa choo cha mnyama au mfupa, basi hakika Muhammad (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) yuko mbali naye."⁴⁰

5- Sa'iyd bin Jubayr (Rahimahu Allaah) amesema:

"Mwenye kukata hirizi kutoka kwa mtu atakuwa ni kama ambaye kaacha mtumwa huru."⁴¹

Ameipokea Wakiy'.

6- Amepokea vilevile kwamba Ibraahiym amesema:

"Walikuwa wakichukizwa na hirizi zote; ni mamoya za Qur-aan na zisizokuwa za Qur-aan."⁴²

MAELEZO

⁴⁰ Abu Daawuud (36), an-Nasaa'iy (5067) na Ahmad (17037). Swahiyh kwa mujibu wa al-Albaaniy katika "Swahiyh-ul-Jaamiy" (13869).

⁴¹ Ibn Abiy Shaybah (23473).

⁴² Ibn Abiy Shaybah (23467).

1- Mlango unaozungumzia maandiko yaliyokuja kuharamisha hirizi na kupambanua kuhusu matabano. Kuna baadhi ambao wameharamisha hirizi za aina fulani na wamehalalisha za aina nyingine. Maoni sahihi ni kwamba hirizi zote ni haramu. Hirizi ni kitu kinachoningizwa kwa mtoto dhidi ya kijicho. Dalili zimefahamisha kwamba ni haramu, kama itavyokuja huko mbele kwa mgonjwa na mtoto.

2- Kuhusu matabano, kunahitajia maelezo. Inafaa kwa kupatikana sharti tatu:

1- Iwe kwa lugha yenye kufahamika kwa Aayah za Qur-aan na du'aa zenye kutambulika.

2- Isiwe na kitu kinachopingana na Shari'ah.

3- Asiamini kwamba yenyewe ndio inayonufaisha. Katika Hadiyth iliyotangulia imekuja:

“Matabano yanafaa midhali ndani yake hamna shirki.”

Tiwalah mwandishi ameeleza maana yake. Ni jambo linalofanywa kwa kuchukua msaada kutoka kwa majini na mashaytwaan. Wanaita “uchawi”, “uvutwaji”, “ukimbizaji”. Uchawi wote ni ukafir:

إِنَّمَا نَحْنُ فِتْنَةٌ فَلَا تَكْفُرْ

“Hakika sisi ni mtihani, basi usikufuru.” (al-Baqarah 02:102)

3- 'Abdullaah bin 'Ukaym amepokea ya kwamba Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Atakayevaa/atakayejifungamanisha na kitu basi huwakilishwa kwacho.”

Ameipokea Ahmad na at-Tirmidhiy.

Mtu anatakiwa kumtegemea Allaah pekee. Hili ndilo jambo litalomnufaisha pamoja vilevile na kufanya sababu. Kama ilivyokuja katika Hadiyth:

“Pupie kile kinachokunufaisha na taka msaada kwa Allaah (‘Azza wa Jall) na wala usikate tamaa.”⁴³

Kufanya sababu ni jambo la lazima katika kuomba du‘aa, kufuata Shari‘ah ya Allaah, kutafuta sababu zitazomfanya mtu kupona na kutafuta riziki. Kufanya sababu ima ikawa ni wajibu au jambo lenye kujuzu. Kwa hiyo mtu anatakiwa kuhakikisha amefanya zile sababu zenye kujuzu na za wajibu. Kufanya hivo hakuitii kasoro Tawhiyd ya mtu. Bali mambo ni kinyume chake. Kuacha kufanya sababu kunatia kasoro akili na Tawhiyd vyote viwili.

Hirizi ikiwa ni ya Qur-aan wako baadhi ya Salaf waliojuzisha hilo, kama ‘Abdullaah bin ‘Amr, wengine wakaikataza, kama ‘Abdullaah bin Mas‘uud. Maoni haya ya mwisho ndio ya sawa yanayofahamishwa na dalili. Lililo la wajibu ni kufunga mlango huu kwa ajili ya kuzuia njia zote zinazopelekea katika shirki na kutendea kazi dalili. Haitakiwi kuwavalisha watoto hirizi. Bali mtu anatakiwa awesome du‘aa kama ambavo Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) alivomsomea al-Hasan na al-Husayn⁴⁴.

Wako baadhi ya Salaf ambao wameandika Qur-aan katika karatasi na kwenye sahani. Imepokelewa kutoka kwa Ibn ‘Abbas, lakini haikuthibiti. Hata hivyo haina neno. Ibn-ul-Qayyim ametaja katika “Zaad-ul-Ma‘aad”. Hata hivyo matabano ndio bora zaidi.

Kujitibisha pia hakuna neno. Imekuja katika Hadiyth:

⁴³ Muslim (2664).

⁴⁴ al-Bukhaariy (3371).

“Enyi waja wa Allaah! Jitibisheni na wala msijitibishe kwa kitu cha haramu.”⁴⁵

Maoni sahihi ni kwamba imependekezwa. Maalik amesema:

“Ni jambo liko sawasawa.”

Bi maanal limeruhusiwa.

4- Ahmad amepokea kutoka kwa Ruwayfiy' ambaye amesema:

“Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) alinambia: “Ee Ruwayfiy'! Huenda ukaishi muda mrefu. Hivyo waeleze watu kwamba ambaye anazifunga fundo ndevu zake, akatundika kidani cha kamba ya upinde au akajisafisha kwa choo cha mnyama au mfupa, basi hakika Muhammad (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) yuko mbali naye.”

Hapa kuna mambo mane:

1- “...ambaye anazifunga fundo ndevu zake... “ Wanachuoni wamesema kuwa maana yake ni kwamba mtu anazifunga ndevu zake kwa kuzitengeneza kwa ajili ya kutafuta kiburi na ukuu. Imesemekana vilevile kwamba ili mtu asijifanani na wanawake na mashoga. Kuhusu kuzijali kwa kuzichanua na kuzihudumia hakuna neno. Katika Hadiyith kuna udhaifu lakini hata hivyo imepokelewa kupitia zengine zinazoitolea ushahidi.

2- “... akatundika kidani... “ Kinachotengenezwa kwa matumbo na vyengine. Wakati wa kabla ya kuja Uislamu walikuwa wakiwaninginiza ngamia na watoto ili wasipatwe na kijicho.

⁴⁵ Abu Daawuud (3874), at-Twabaraaniy (649) na al-Bayhaqiy (19465). Swahiyh kwa mujibu wa al-Albaaniy katika “Swahiyh-ul-Jaamiy” (2643).

3- "... au akajisafisha kwa choo cha mnyama au mfupa... ". Kuna Hadiyth zimekuja zikikataza mambo hayo. Kwa sababu ni mambo yasiyosafisha na isitoshe ni kujifananisha na kipindi kabla ya kuja Uislamu.

4- "... basi hakika Muhammad (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) yuko mbali naye.... " Hapa kuna makemeo makali. Hata hivyo haina maana kwamba anakuwa mshirikina. Hadiyth hii ni kama mfano wa Hadiyth isemayo:

"Si katika sisi yule anayejipiga kwenye mashavu, kuchana nguo zake au akaita kwa wito wa kipindi kabla ya kuja Uislamu."

Kinacholengwa hapa ni kukatazwa kutundika kidani, uzi na vyengine ambavo mtu anadhani kuwa vinanufaisha. Lililo la wajibu ni mtu kumtegemea Allaah pekee.

5- Sa'iyd bin Jubayr (Rahimahu Allaah) amesema:

"Mwenye kukata hirizi kutoka kwa mtu atakuwa ni kama ambaye kaacha mtumwa huru."

Ameipokea Wakiy'.

Wakiy' bin al-Jarraah alifariki 196.

Katika Hadiyth kuna fadhilah za kukata hirizi na kwamba ni sawa na kuacha mtumwa huru. Kwa sababu katika hali hii amemsalimisha mtumwa huyu kutokamana na Moto na shirki. Kwa ajili hiyo inakuwa ni bora kuliko kuacha mtumwa huru kwa kujitolea mwenyewe. Inawezekana maneno haya ya Sa'iyd yamepokelewa kupitia cheni ya wapokezi. Ni jambo ambalo lina wasaa ndani yake kwa sababu Sa'iyd hazungumzi hivo kutoka kichwani mwake. Inawezekana vilevile kwamba alitamka hivo kutokana na Ijtihad na uelewa wake. Lakini baada ya uhakiki na upekuzi imeonyesha kwamba kitendo hicho ni bora zaidi kuliko kumwacha mtumwa huru kwa kujitolea mwenyewe.

Kutundika hirizi ni shirki ndogo na ni jambo lenye khatari kubwa. Inaweza vilevile kupelekea katika shirki kubwa.

6- Amepokea vilevile kwamba Ibraahiym amesema:

“Walikuwa wakichukizwa na hirizi zote; ni mamoja za Qur-aan na zisizokuwa za Qur-aan.”

Anaitwa Ibraahiym bin Yaziyd an-Nakha'iy. Ni mtu aliyekuja baada ya Maswahabah (Taabi'iy) na alikuwa ni mwanafunzi wa 'Abdullaah bin Mas'uud (Radhiya Allaahu 'anh). Walikuwa wakichukizwa na hirizi na vivyo hivyo mwalimu wao Ibn Mas'uud. Alikuwa anachukizwa na jambo hilo kutokana na sababu mbili:

1- Hadiyth zimekuja kwa njia ya jumla.

2- Kwa sababu kufunga njia zote zinazopelekea katika shirki. Kwa hivyo haitakiwi kutundika Qur-aan, Aayah za Qur-aan, Hadiyth, talasimu wala mifupa. Yote haya ni shirki.

09. Kufanya Tabarruk kwa mti, jiwe na mfano wake

Shaykh-ul-Islaam Muhammad bin 'Abdil-Wahhaab (Rahimahu Allaah) amesema:

1- Allaah (Ta'ala) amesema:

أَفَرَأَيْتُمُ اللَّاتَ وَالْعُزَّىٰ وَمَنَاةَ الثَّالِثَةَ الْأُخْرَىٰ أَلَكُمُ الذَّكْرُ وَلَهُ الْأُنثَىٰ

“Je, mmeona al-Laat na al-'Uzzaa na Manaat, mwengine wa tatu [mliokuwa mkiwaabudu]? Je, nyinyi mna wana wa kiume Naye ana wana wa kike?” (an-Najm 53:19-21)

2- Abu Waaqid al-Laythiy amesema:

“Tulitoka pamoja na Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) kuelekea Hunayn na sisi ndio bado karibuni tulikuwa tumetoka katika ukafiri. Washirikina walikuwa na mkunazi wakikaa hapo kwa muda mrefu na wakitundika silaha zao juu ambao ulikuwa ukiitwa Dhaat an-Waatw. Tukapita kwenye mti mwengine wa mkunazi tukasema: “Ee Mtume wa Allaah! Tufanyie na sisi Dhaat an-Waatw kama ambavyo wao wako na Dhaat an-Waatw?” Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) akasema: “Allaahu ni mkubwa! Ndio zilezile njia [za makafiri]. Ninaapa kwa Yule ambaye nafsi yangu iko mikononi Mwake, kwa hakika mmesema kama walivosema wana wa israaiyl kumwambia Muusa:

اجْعَلْ لَّنَا إِهًّا كَمَا هُمْ آهَةٌ قَالَ إِنَّكُمْ قَوْمٌ بَجْهَلُونَ

“Tufanyie mungu kama ambavyo wao wako na miungu!” Akasema: “Hakika nyinyi ni watu wajinga!” (al-A'raaf 07:138)

Hakika mtafuata njia za wale waliokuwa kabla yenu.”⁴⁶

Ameipokea at-Tirmidhiy na ameisahihisha.

MAELEZO

Mfano wake kunamaanisha makaburi, masanamu na vyenginevyo.

Tabarruk maana yake ni kule mtu kutafuta baraka kutoka katika vitu hivyo. Kama wanavofanya waabudu makaburi, waabudu mawe na waabudu miti. Ameacha kutaja hukumu yake ili mwanafunzi aweze kuzingatia hukumu kupitia maandiko. Hukumu ya kitendo hicho ni shirki, kama atavyotaja mwandishi. Tabarruk hii ni miongoni mwa matendo ya watu wa kipindi cha kikafiri na ni jambo linachengua Uislamu. Baadhi waliitikia, nao ni wachache, ilihali wengi walipinga:

وَمَا أَكْثَرَ النَّاسِ وَلَوْ حَرَصْتَ بِمُؤْمِنِينَ

“Wengi wa watu hawatoamini ijapokuwa utalitilia hima.” (Yuusuf 12:103)

Kuhusiana na kisiwa cha kiarabu wengi wao waliingia katika Uislamu baada ya kufunguliwa mji wa Makkah.

1- Allaah (Ta'ala) amesema:

أَفَرَأَيْتُمُ اللَّاتَ وَالْعُزَّىٰ وَمَنَاةَ الثَّالِثَةَ الْأُخْرَىٰ أَلَكُمُ الذَّكْرُ وَلَهُ الْأُنثَىٰ

“Je, mmeona al-Laat na al-'Uzzaa na Manaata, mwengine wa tatu [mliokuwa mkiwaabudu]? Je, nyinyi mna wana wa kiume Naye ana wana wa kike?”

⁴⁶ Ahmad (21947), at-Tirmidhiy (2180), Ibn Hibbaan (6702) na at-Twabaraaniy (3291). Swahiyh kwa mujibu wa al-Albaaniy katika "Mishkaat-ul-Maswaabiyh" (5408).

Je, masanamu haya yamenufaisha na kudhuru? Maana yake ni kwamba hayakunufaisha wala hayakudhuru. Walikuwa wakiyaabudu, wakiyaomba baraka na msaada. Matendo yanachengua Uislamu. al-'Uzzaa lilikuwa ni salamua la watu wa Makkah na majirani wao. Manaat lilikuwa ni sanamu la watu wa al-Madiynah. al-Laah lilikuwa ni sanamu la watu wa at-Twaa-if na wale wenye kuwafuata. Masanamu haya yaliondoshwa na kuvunjwa siku ileile ulipofunguliwa mji wa Makkah. Pamoja na hivyo Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Hayatoenda masiku na michana mpaka aabudiwe al-Laah na al-'Uzzaa.”

2- Abu Waaqid al-Laythiy amesema:

“Tulitoka pamoja na Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) kuelekea Hunayn na sisi ndio bado karibuni tulikuwa tumetoka katika ukafiri. Washirikina walikuwa na mkunazi wakikaa hapo kwa muda mrefu na wakitundika silaha zao juu ambao ulikuwa ukiitwa Dhaat an-Waatw. Tukapita kwenye mti mwengine wa mkunazi tukasema: “Ee Mtume wa Allaah! Tufanyie na sisi Dhaat an-Waatw kama ambavyo wao wako na Dhaat an-Waatw?” Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) akasema: “Allaahu ni mkubwa! Ndio zilezile njia [za makafiri]. Ninaapa kwa Yule ambaye nafsi yangu iko mikononi Mwake, kwa hakika mmesema kama walivosema wana wa israaiyl kumwambia Muusa:

اجْعَلْ لَنَا إِهًا كَمَا هُمْ آهَةٌ قَالَ إِنَّكُمْ قَوْمٌ بَجْهَلُونَ

“Tufanyie mungu kama ambavyo wao wako na miungu!” Akasema: “Hakika nyinyi ni watu wajinga!” (al-A'raaf 07:138)

Hakika mtafuata njia za wale waliokuwa kabla yenu.”⁴⁷

Ameipokea at-Tirmidhiy na ameisahihisha.

Maneno yake “na sisi ndio bado karibuni tulikuwa tumetoka katika ukafiri” hii ni aina fulani ya udhuru. Ni kama vile anataka kusema kwamba ndio maana hatukujua kitendo hichi.

Maneno yake “wakitundika silaha zao juu” kwa ajili ya kutafuta baraka. Wanadai kwamba wakifanya hivo basi silaha zinakuwa na nguvu na makali sana.

Maneno yake “Tufanyie na sisi Dhaat an-Waatw kama ambavyo wao wako na Dhaat an-Waatw” bi maana ili nao waweze kupata baraka.

Ndipo Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) akakasirika na kusema: “Allaahu ni mkubwa!” Hii ilikuwa ni ada yake pindi anapona jambo analolilekea basi husema: “Allaahu ni mkubwa!” au “Allaah ametakasika kutokamana na mapungufu”. Hii ndio Sunnah pindi mtu anapona jambo analolikemea au jambo lililompendeza. Wakati Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) aliposema: “Nyinyi ni robo ya watu wa Peponi” Maswahabah wakasema: “Allaahu ni mkubwa!”⁴⁸

Maneno yake (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam): “Ndio zilezile njia [za makafiri]” bi maana za kuabudu miti, mawe na kufanya Tabarruk kwa vitu hivyo. Huu ndio mfumo unaotambulika kwa watu waliotangulia hapo kale. Kwa msemu mwingine ndio mfumo wa watu tangu hapo kale na siku zote walikuwa ni wenye kufanya hivo.

⁴⁷ Ahmad (21947), at-Tirmidhiy (2180), Ibn Hibbaan (6702) na at-Twabaraaniy (3291). Swahiyh kwa mujibu wa al-Albaaniy katika “Mishkaat-ul-Maswaabiyh” (5408).

⁴⁸ al-Bukhaariy (3348) na Muslim (222).

Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) akasema: “mmesema kama walivosema wana wa israaiyl”. Israaiyl, Israel, ni Ya'quub mwana wa Ishaq mwana wa Ibraahiym. Wana wa israaiyl ni mayahudi ambao wanajinasibisha na israaiyl, israel. Mayahudi walimwambia Muusa:

اجْعَلْ لَنَا إِهًّا كَمَا هُمْ آهَةٌ قَالَ إِنَّكُمْ قَوْمٌ بَجْهَلُونَ

“Tufanyie mungu kama ambavyo wao wako na miungu!” Akasema: “Hakika nyinyi ni watu wajinga!”

Muusa akawakaripia na akawakumbusha Tawhiyd. Vivyo hivyo Maswahabah hawa waliwaiga wale kwa sababu ya ujinga. Hawakuwa wanajua hukumu ya kitendo hichi kwa sababu punde tu ndio wametoka katika ukafiri. Hii ni dalili inayofahamisha kwamba kinachozingatiwa ni uhalisia wa mambo na sio matamshi. Kwa sababu wameomba kitu ili wakiadhimishe na watafute baraka kwacho kama walivofanya wana wa israaiyl japokuwa matamshi yao ni yenye kutofautiana. Batili ni batili ijapokuwa matamshi ni yenye kutofautiana.

Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema: “Hakika mtafuata njia za wale waliokuwa kabla yenu.” Bi maana mienendo yao. Hii ina maana kwamba Ummah huu utapewa majaribio kama walivyopewa majaribio watu walioshi katika kipindi cha kikafiri katika kuiabudu miti na mawe na kufanya Tabarruk kwavyo. Haya tayari ni mambo yamekwishatokea. Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema hivo ili kueleza kwamba yatatokea. Ametahadharisha mambo hayo na akaashiria kwamba jambo la wajibu ni kuwa na thabati katika kumuabudu Allaah peke yake kama walivyofanya Mitume. Ama kuyaabudu makaburi ni miongoni mwa matendo ya mayahudi, manaswara na washirikina wengine.

10. Kuchinja kwa ajili ya mwingine asiyekuwa Allaah

Shaykh-ul-Islaam Muhammad bin 'Abdil-Wahhaab (Rahimahu Allaah) amesema:

1- Allaah (Ta'ala) amesema:

قُلْ إِنَّ صَلَاتِي وَنُسُكِي وَمَحْيَايَ وَمَمَاتِي لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ لَا شَرِيكَ لَهُ ۖ وَبِذَلِكَ أُمِرْتُ وَأَنَا أَوَّلُ الْمُسْلِمِينَ

"Sema: "Hakika swalah yangu na kichinjwa changu na uhai wangu na kufa kwangu ni kwa ajili ya Allaah pekee, Mola wa walimwengu, hali ya kuwa hana mshirika; na kwa hayo ndio nimeamrisha, nami ni muislamu wa kwanza." (al-An'aam 06:162-163)

2-

فَصَلِّ لِرَبِّكَ وَانْحَرْ

"Basi swali kwa ajili ya Mola wako na [pia ukichinja] na chinja [kwa ajili Yake]!" (at-Takaathuur 108:02)

3- 'Aliy (Radhiya Allaahu 'anh) amesema:

"Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amenieleza kuhusu mambo mane; Allaah amemlaani yule mwenye kuchinja kwa ajili ya asiyekuwa Allaah. Allaah amemlaani yule mwenye kuwalaani wazazi wake wawili. Allaah amemlaani yule mwenye kumpa himaya mzushi. Allaah amemlaani yule mwenye kubadili alama ya ardhi."

Ameipokea Muslim.

4- Twaariq bin Shihaab amesimulia kwamba Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Kuna mtu aliyeingia Motoni kwa sababu ya nzi na kuna mtu mwengine aliingia Peponi kwa sababu ya nzi.” Wakasema: “Ilikuweje, ee Mtume wa Allaah?” Akasema: “Watu wawili waliwapitia watu waliokuwa na sanamu ambalo ilikuwa haijuzu kwa mtu yeyote kulipita mpaka mtu alitolee swadaqah. Wale watu wakamwambia mmoja wao: “Litolee swadaqah.” Akasema: “Sina chochote cha kutoa.” Wakamwambia: “Litolee ijapokuwa ni nzi.” Hivyo akalitolea nzi. Wakamwacha kwenda zake na akaingia Motoni. Wakamwambia yule mwengine: “Litolee.” Akasema: “Siwezi kamwe kutoa swadaqah kwa ajili ya yeyote yule asiyekuwa Allaah ('Azza wa Jall).” Hivyo wakamkata shingo yake na akaingia Peponi.”⁴⁹

Ameipokea Ahmad.

MAELEZO

Bi maana ukhatari wa kitendo hichi na kwamba ni katika shirki kubwa, kama zilivyofahamisha dalili.

1- Allaah (Ta'ala) amesema:

قُلْ إِنَّ صَلَاتِي وَنُسُكِي وَمَحْيَايَ وَمَمَاتِي لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ لَا شَرِيكَ لَهُ ۖ وَبِذَلِكَ أُمِرْتُ وَأَنَا أَوَّلُ الْمُسْلِمِينَ

“Sema: “Hakika swalah yangu na kichinjwa changu na uhai wangu na kufa kwangu ni kwa ajili ya Allaah pekee, Mola wa walimwengu, hali ya kuwa hana mshirika; na kwa hayo ndio nimeamrisha, nami ni muislamu wa kwanza.” (al-An'aam 06:162-163)

⁴⁹ Ibn Abiy Shaybah (33037) kutoka kwa Salmaan, al-Bayhaqiy katika "Shu'b-ul-Iymaan" (7343) na Ahmad katika "az-Zuhd" (1715).

قُلْ

“Sema!”

Bi maana sema, ee Muhammad.

نُسْكِي

“... kichinjwa changu...”

Kichinjwa. Imesemekana vilevile kwamba ni 'ibaadah zote kukiwemo kuchinja.

فَصَلِّ لِرَبِّكَ وَأَنْحَرْ

“... na uhai wangu na kufa kwangu...”

Bi maana zile 'ibaadah na matendo ninayoishi ndani yake ni kwa ajili ya Allaah pekee. Aayah inabainisha kwamba kuchinja ni 'ibaadah na hivyo ni lazima afanyiwe Allaah pekee na haitakikani kumfanyia mwingine. Yule mwenye kumchinjia mwingine asiyekuwa Allaah kama vile jini, masanamu na wafu waliyomo ndani ya makaburi ni kama mfano wa mwenye kuswali kwa ajili ya asiyekuwa Allaah. Kwa sababu swalah na kuchinja yote mawili ni 'ibaadah kwa kwa vile Allaah ameyataja kwa pamoja na kusema:

وَبَدِّلْ أَمْرُتُ

“... na kwa hayo ndio nimeamrisha...”

Allaah ndiye kamwamrisha.

2-

فَصَلِّ لِرَبِّكَ وَأَنْحَرْ

“Basi swali kwa ajili ya Mola wako na [pia ukichinja] na chinja [kwa ajili Yake]!”
(at-Takaathuur 108:02)

Bi maana swali na uchinje kwa ajili Allaah kushukuru kwa ajili ya mto mkubwa Kawthar. Hii ni dalili inayofahamisha kwamba kuchinja na swalah vyote viwili ni 'ibaadah kwa sababu ameviamrisha vyote viwili. Mwenye kuchinja kwa ajili ya asiyekuwa Allaah ni shirki kama ambavyo mtu ataswali kwa ajili ya mwingine asiyekuwa Allaah. Mwenye kuchinja kwa ajili ya masanamu, majini au vyenginevyo ameshirikisha.

3- 'Aliy (Radhiya Allaahu 'anh) amesema:

“Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amenieleza kuhusu mambo mane; Allaah amemlaani yule mwenye kuchinja kwa ajili ya asiyekuwa Allaah. Allaah amemlaani yule mwenye kuwalaani wazazi wake wawili. Allaah amemlaani yule mwenye kumpa himaya mzushi. Allaah amemlaani yule mwenye kubadili alama ya ardhi.”⁵⁰

Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) ameanza na: “Allaah amemlaani yule mwenye kuchinja kwa ajili ya asiyekuwa Allaah” kwa sababu shirki ndio dhambi kubwa. Laana maana yake ni kuwekwa mbali na rehema ya Allaah. Ni dalili inayofahamisha kwamba shirki ndio dhambi kubwa kabisa. Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Dhambi kubwa ni kumshirikisha Allaah.”⁵¹

⁵⁰ Muslim (1978).

⁵¹ al-Bukhaariy (2654) na Muslim (87).

Kuwalaani wazazi wawili ni katika dhambi kubwa pia. Inahusiana vilevile na yule mwenye kuwatukana wazazi wa mtu mwingine na mtu huyo akawatukana wazazi wake. al-Bukhaariy na Muslim wamepokea kupitia kwa 'Abdullaah bin 'Amr ambaye ameeleza kwamba Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Miongoni mwa dhambi kubwa ni mtu kuwatukana wazazi wake.” Wakasema: “Ee Mtume wa Allaah! Vipi mtu atawatukana wazazi wake?” Akajibu: “Ndio. Mtu atamtukana baba wa mwingine na yeye mtu huyo amtukanie baba yake, na mtu atamtukana mama wa mwingine na yeye mtu huyo amtukanie mama yake.”⁵²

Kuwatukana watu pasi na haki ni katika madhambi makubwa. Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Kumtukana muislamu ni dhambi nzito na kumuua ni ukafiri.”⁵³

al-Bukhaariy amepokea kupitia kwa Thaabit bin adh-Dhwahhaak maneno yake Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam):

“Kumlaani muumini ni kama kumuua.”⁵⁴

Muslim amepokea kwamba Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Watu wenye [kupenda] kulaani hawatokuwa mashahidi wala waombezi siku ya Qiyaamah.”⁵⁵

Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema “mwenye kumpa himaya mzushi”. Bi maana yule mwenye kuwalinda Ahl-ul-Bid'ah na watenda maasi na

⁵² al-Bukhaariy (5973) na Muslim (90).

⁵³ al-Bukhaariy (48) na Muslim (64).

⁵⁴ al-Bukhaariy (6105) na Muslim (110).

⁵⁵ Muslim (2598).

akawanusuru. Huyu amelaaniwa. Vilevile yule mwenye kuzuia wasisimamishiwe adhabu ya Kishari'ah. Kadhalika yule mwenye kusimamisha Bid'ah ba kuzinusuru.

Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema "mwenye kubadili alama ya ardhi". Alama hizi zinawekwa kwa ajili ya kupambanua ardhi za watu. Yule mwenye kubadili alama hizi amelaaniwa kwa sababu jambo hili linaweza kupelekea katika matatizo, mabalaa na vita. Katika hayo kunaingia vilevile zile alama zinazowaelekeza watu barabara. Yule mwenye kuzibadili amelaaniwa.

4- Twaariq bin Shihaab amesimulia kwamba Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

"Kuna mtu aliyeingia Motoni kwa sababu ya nzi na kuna mtu mwengine aliingia Peponi kwa sababu ya nzi." Wakasema: "Ilikuweje, ee Mtume wa Allaah?" Akasema: "Watu wawili waliwapitia watu waliokuwa na sanamu ambalo ilikuwa haijuzu kwa mtu yeyote kulipita mpaka mtu alitolee swadaqah. Wale watu wakamwambia mmoja wao: "Litolee swadaqah." Akasema: "Sina chochote cha kutoa." Wakamwambia: "Litolee ijapokuwa ni nzi." Hivyo akalitolea nzi. Wakamwacha kwenda zake na akaingia Motoni. Wakamwambia yule mwengine: "Litolee." Akasema: "Siwezi kamwe kutoa swadaqah kwa ajili ya yeyote yule asiyekuwa Allaah ('Azza wa Jall)." Hivyo wakamkata shingo yake na akaingia Peponi."⁵⁶

Ameipokea Ahmad.

Twaariq huyu alikuwa ni miongoni mwa Maswahabah wadogo. Mara nyingi anapokea kutoka kwa Abu Muusa al-Ash'ariy. Upokezi huu ni kupitia kwa

⁵⁶ Ibn Abiy Shaybah (33037) kutoka kwa Salmaan, al-Bayhaqiy katika "Shu'b-ul-Iymaan" (7343) na Ahmad katika "az-Zuhd" (1715).

Swahabah ambaye hakutajwa. Wakati Swahabah anapopokea kutoka kwa Swahabah mwenzie pasi na kumtaja upokezi unakuwa Swahiyh.

Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema "kwa nzi", bi maana kwa sababu ya nzi.

Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema "sanamu". Sanamu ni kitu kilichochongwa kwa sura. Kitu kilichochongwa pasi na sura huitwa "mzimu". Masanamu pia huitwa "mizimu".

Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema "hajuzu kwa mtu yeyote kulipita". Bi maana hawamwachi akapita.

Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema kwamba mmoja wao akasema "Sina chochote cha kutoa". Hakukemea kitendo hicho. Ndipo wakawa na matumaini kwake na wakamwamrisha alitolee swadaqah ijapo nzi tu. Kwa sababu hiyo akaingia Motoni. Hii ni dalili inayofahamisha kwamba kulitolea swadaqah sanamu hata kama itakuwa ni kitu kisichokuwa na maana yoyote ni shirki. Kwa sababu kuchinja na 'ibaadah nyenginezo hafanyiwi mwingine asiyekuwa Allaah pekee.

Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema kwamba walipomuomba yule mwingine kufanya hivo akasema "Siwezi kamwe kutoa swadaqah kwa ajili ya yeyote yule asiyekuwa Allaah ('Azza wa Jall)". Mtu huyu amepinga na akawabainishia kuwa kitendo hicho hakijuzu. Matokeo yake akaingia Peponi. Hili linaweza kuwa na maana mbili:

1- Katika Shari'ah yao mtu alikuwa hapewi udhuru kwa kutenzwa nguvu. Kwa ajili hiyo ndio maana hakuchukua ruhusa ili aweze kujinasua na shari yao.

2- Inawezekana vilevile aliacha kuchukua ruhusa hiyo kwa sababu ya imani na yakini yake yenye nguvu, ndipo wakamua.

Ama katika Shari'ah yetu mtu akitenzwa nguvu kufanya shirki na akafanya kwa ajili ya kujinasua na shari yao na wakati huohuo moyo wake ukawa umetua juu ya imani yake hakuna neno. Allaah (Ta'ala) amesema:

مَنْ كَفَرَ بِاللَّهِ مِنْ بَعْدِ إِيمَانِهِ إِلَّا مَنْ أُكْرِهَ وَقَلْبُهُ مُطْمَئِنٌّ بِالْإِيمَانِ وَلَكِنْ مَنْ شَرَحَ بِالْكُفْرِ صَدْرًا فَعَلَيْهِمْ
عَذَابٌ مِّنَ اللَّهِ وَهُمْ عَذَابٌ عَظِيمٌ

“Atakayemkufuru Allaah baada ya kuamini kwake - isipokuwa yule aliyetenzwa nguvu na huku moyo wake umetua juu ya imani - lakini aliyekifungulia ukafiri kifua chake, basi hao juu yao wana ghadhabu kutoka kwa Allaah na watapata adhabu kuu.” (an-Nahl 16:106)

Katika hali hiyo inafaa kuchukua ruhusa hata kama atahitajia kutamka kufuru kwa ulimi wake.

Hadiyth ya Twaariq ameipokea Ahmad katika “az-Zuhd”. Ibn-ul-Qayyim ameitaja kwa cheni ya wapokezi yenye nguvu.

11. Hakuchinjwi kwa ajili ya Allaah mahali ambapo kunachinjwa kwa ajili ya mwingine asiyekuwa Allaah

Shaykh-ul-Islaam Muhammad bin 'Abdil-Wahhaab (Rahimahu Allaah) amesema:

1- Allaah (Ta'ala) amesema:

لَا تَقُمْ فِيهِ أَبَدًا

“Usisimame huko kamwe!” (at-Tawbah 09:108)

2- Thaabit bin adh-Dhwahhaak (Radhiya Allaahu 'anh) amesema:

“Kuna mtu aliweka nadhiri ya kuchinja mahali kunapoitwa Bawaanah. Akamuuliza Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) kuhusu hilo ambapo akasema: “Je, mahali hapo kulikuwepo sanamu lolote katika masanamu ya kipindi cha kikafiri likiabudiwa?” Wakasema: “Hapana.” Akasema (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam): “Je, kulikuwepo sikukuu yoyote iliyofanywa katika sikukuu zao?” Wakasema: “Hapana.” Ndipo Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) akasema: “Tekeleza nadhiri yako. Kwani hakika hakuna kutekeleza nadhiri katika kumuasi Allaah wala katika kitu ambacho hakimiliki mwanaadamu.”⁵⁷

Ameipokea Abu Daawuud na cheni ya wapokezi wake iko kwa mujibu wa masharti ya al-Bukhaariy na Muslim.

MAELEZO

⁵⁷ Abu Daawuud (3313). Swahiyh kwa mujibu wa al-Albaaniy katika “Swahiyh Abiy Daawuud” (2834).

Anachomaanisha na mlango huu ni kwamba haijuzu kwa waumini kujifananisha na watenda maasi wala kuwepo sehemu za maasi na sehemu za 'ibaadah za makafiri hata kama itahusiana na mambo mengine mbali na kuchinja. Haya ili mtu asinasibishwe nao na akashirikishwa nao. Mtu akichinja mahali ambapo kunachinjwa kwa ajili ya mwingine asiyekuwa Allaah basi anaweza kunasibishwa na watu waovu au akadhiniwa vibaya. Muumini anatakiwa kujiepusha na yote hayo.

1- Allaah (Ta'ala) amesema:

لَا تَعْمَلُوا فِيهِ آثًا

“Usisimame huko kamwe!”

Aayah hii iliteremshwa kuhusiana na msikiti wa Dhwiraar uliojengwa na wanafiki kwa ajili ya kuwalinda baadhi ya makafiri. Walikuwa wakikusanyika huko na wakisaidizana juu ya namna gani watamuua Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam). Lakini hata hivyo wakayaficha hayo. Badala yake wakadhihirisha kuwa wameujenga msikiti kwa ajili ya kuwasaidia madhaifu na masikini wakati wa nyusiku za wakati wa majira ya baridi. Wakamuomba Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) aswali ndani yake kabla ya kwenda Tabuuk. Lakini akawataka udhuru na kuwaambia kwamba ataswali ndani yake pale ataporudi kutoka Tabuuk. Wakati alipokuwa njiani anarudi nyumbani ndipo Allaah akamteremshia yenye kufedhehesha na kubainisha njama zao mbaya. Ndipo Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) akawatuma watu kwenda kuubomoa.

Hiyo ina maana kwamba sehemu ambazo kunafanywa kufuru na upotevu zinatakiwa kuondoshwa na kutobakizwa ili zisisaidie kueneza ufiisadi. Mtunzi wa kitabu ametumia kama dalili kuonyesha kwamba sehemu ambazo kunachinjwa au kuswaliwa kwa ajili ya mwingine asiyekuwa Allaah au kunafanywa maasi zinatakiwa zisibakizwe ili zisije kuwaharibu waislamu na

kunasibishwa nao. Hiki ni kipimo, Qiyaash, kilichothibiti. Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Huenda mtoto wako huu asili yake ni hivo.”⁵⁸

2- Thaabit bin adh-Dhwahhaak (Radhiya Allaahu 'anh) amesema:

“Kuna mtu aliweka nadhiri ya kuchinja mahali kunapoitwa Bawaanah. Akamuuliza Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) kuhusu hilo ambapo akasema: “Je, mahali hapo kulikuwepo sanamu lolote katika masanamu ya kipindi cha kikafiri likiabudiwa?” Wakasema: “Hapana.” Akasema (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam): “Je, kulikuwepo sikukuu yoyote iliyofanywa katika sikukuu zao?” Wakasema: “Hapana.” Ndipo Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) akasema: “Tekeleza nadhiri yako. Kwani hakika hakuna kutekeleza nadhiri katika kumuasi Allaah wala katika kitu ambacho hakimiliki mwanaadamu.”⁵⁹

Bawaanah ni sehemu ilioko kusini mwa Makkah. Imesemekana vilevile kwaba iko karibu na Yanbuu'.

Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema “Je, mahali hapo kulikuwepo sanamu lolote katika masanamu ya kipindi cha kikafiri likiabudiwa?” na “Je, kulikuwepo sikukuu yoyote iliyofanywa katika sikukuu zao?” Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) alichelea asije kuwa amefanya sehemu hiyo kuwa maalum kwa sababu kuna mzimu katika mizimu ya kipindi cha kikafiri au sikukuu miongoni mwa sikukuu zao na kwamba muulizaji anataka kuwaiga. Wakati alipojuzwa (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) kwamba hakuna mambo hayo ndipo akamwamrisha kutekeleza nadhiri yake. Ni dalili inayofahamisha kwamba ni wajibu kutekeleza nadhiri ikiwa mtu lengo lake sio kujifananisha na washirikina, makafiri na mfano wao.

⁵⁸ al-Bukhaariy (5305) na Muslim (1500).

⁵⁹ Abu Daawuud (3313). Swahiyh kwa mujibu wa al-Albaaniy katika “Swahiyh Abiy Daawuud” (2834).

Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema “Kwani hakika hakuna kutekeleza nadhiri katika kumuasi Allaah”. Kwa mfano mtu akaweka nadhiri ya kunywa pombe. Haifai kuitekeleza. Wanachuoni wametofautiana kama ni wajibu kuitolea kafara ya kiapo. Maoni ya kwanza yanasema kuwa ni nadhiri batili na kwamba haina kafara. Dalili zao ni zile zenye kuenea. Lakini hata hivyo kumekuja mapokezi mengi yanayofahamisha juu ya uwajibu wa kuitekeleza. Haya ndio maoni ya pili na ndio yenye nguvu.

Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema “wala katika kitu ambacho hakimiliki mwanaadamu”. Kwa mfano mtu akaweka nadhiri kwa jina la Allaah kumwacha mtumwa wa fulani. Nadhiri hii ni batili.

Kwa kifupi ni kwamba haitakikani kwa muumini kufanya 'ibaadah sehemu za kipindi cha kikafiri au sehemu za shirki na maasi isipokuwa kukibadilishwa na kukafanywa kwa mfano msikiti au kukajengwa nyumba au kukaondoshwa athari za kipindi cha kikafiri. Katika hali hiyo itakuwa inafaa. Kama ambavyo Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) alivyoamrisha avunjwe al-Laah na badala yake kujengwe msikiti sehemu hiyo⁶⁰. Katika hali hiyo itafaa kufanya 'ibaadah mahali hapo.

Kukifanywa shirki au Bid'ah makaburini haina maana kwamba haitofaa kuyatembelea makaburi hayo kwa mujibu wa Shari'ah. Kama ambavo haitokatazwa kuswali kwenye msikiti ambapo kunafanywa maasi.

'Umar bin al-Khattwaab aliamrisha kuswali makanisani kwa sababu manaswara ni wenye kuyafanya ni sehemu ya kumuabudia Allaah. Lakini 'ibaadah zao zina makosa na hazina maana yoyote na ndani yake zina shirki. Huenda alisema hivo kwa sababu ni wenye kuyafanya ni sehemu ya kumuabudia Allaah, au kwa sababu waislamu walikuwa ni wenye kulazimika kuswali ndani yake wakati

⁶⁰ Abu Daawuud (450) na Ibn Maajah (743).

wanaposafiri, au kwa sababu aina ya 'ibaadah ni yenye kufanana baina yao inapokuja katika swalah.

12. Kuweka nadhiri kwa asiye kuwa Allaah ni katika shirki

Shaykh-ul-Islaam Muhammad bin 'Abdil-Wahhaab (Rahimahu Allaah) amesema:

1- Allaah (Ta'ala) amesema:

يُؤْفُونَ بِالنَّذْرِ

“Ambao wanatimiza nadhiri zao.” (al-Insaan 76:07)

2-

وَمَا أَنْفَقْتُمْ مِّنْ نَّفَقَةٍ أَوْ نَذَرْتُمْ مِّنْ نَّذْرٍ فَإِنَّ اللَّهَ يَعْلَمُهُ

“Na chochote mtoacho katika matumizi au mkiwekacho nadhiri katika nadhiri, basi Allaah anakijua.” (al-Baqarah 02:270)

3- Imepokelewa Swahiyh kutoka kwa 'Aishah (Radhiya Allaahu 'anhaa) ya kwamba Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Mwenye kuweka nadhiri ya kumtii Allaah na amtii na mwenye kuweka nadhiri ya kumuasi Allaah na asimulasi.”⁶¹

MAELEZO

Bi maana ni katika shirki kubwa. Hii ni shirki iliokuwa ikifanywa katika kipindi cha kikafiri na inafanywa na waabudu makaburi ambao wanayawekea nadhiri makaburi na kuyataka uokozi na mengineyo. Mitume wametumilizwa ili

⁶¹ al-Bukhaariy (6696).

kukataza shirki hii iliouwa ikifanywa katika kipindi cha kikafiri. Ama shirki ndogo ni kama mfano wa kujionyesha, kuapa kwa Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) na kusema "akitaka Allaah na wewe".

1-

يُوفُونَ بِالنَّذْرِ

"Ambao wanatimiza nadhiri zao."

Hapa wanasifiwa wale waumini ambao wanazitekeleza nadhiri zao nzuri zilizoafikiana na Shari'ah. Hii ni dalili inayoonyesha kuwa nadhiri ni 'ibaadah ambayo ni wajibu kumtekelezea nayo Allaah pekee.

2-

وَمَا أَنْفَقْتُمْ مِّنْ نَّفَقَةٍ أَوْ نَذَرْتُمْ مِّنْ نَّذْرٍ فَإِنَّ اللَّهَ يَعْلَمُهُ

"Na chochote mtoacho katika matumizi au mkiwekacho nadhiri katika nadhiri, basi Allaah anakijua."

Ina maana kwamba Allaah anajua matumizi na nadhiri za waja. Allaah anawalipa kwayo ikiwa yamefanywa kwa ajili Yake. Ni dalili inayofahamisha kuwa nadhiri ni 'ibaadah kwa sababu imetajwa pamoja na matumizi. Matumizi, kama kuwapa swadaqah mafukara na masikini, ni 'ibaadah yakitolewa kwa ajili ya Allaah. Mtu akiliwekea nadhiri au kulitolea swadaqah kaburi, kujengwa kwake au waungu maalum, kitendo hicho kinakuwa ni shirki kubwa.

3- Imepokelewa Swahiyh kutoka kwa 'Aaishah (Radhiya Allaahu 'anhaa) ya kwamba Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Mwenye kuweka nadhiri ya kumtii Allaah na amtii na mwenye kuweka nadhiri ya kumuasi Allaah na asimuasi.”

Hii ni dalili inayofahamisha kwamba ni wajibu kutekeleza nadhiri ambayo ni 'ibaadah kwa Allaah. Mfano wa hilo ni kama mtu kusema:

“Najifaradhishia mwenyewe kufanya kitu kadhaa kwa ajili ya Allaah.”

Kuhusiana na nadhiri ya maasi haifai kuitekeleza.

13. Kutafuta kinga kwa asiyekuwa Allaah ni katika shirki

Shaykh-ul-Islaam Muhammad bin 'Abdil-Wahhaab (Rahimahu Allaah) amesema:

1- Allaah (Ta'ala) amesema:

وَأَنَّهُ كَانَ رِجَالٌ مِّنَ الْإِنسِ يَعُوذُونَ بِرِجَالٍ مِّنَ الْجِنِّ فَزَادُوهُمْ رَهَقًا

“Na kwamba walikuwa wanaume miongoni mwa watu wanajikinga na wanaume miongoni mwa majini, basi wakawazidishia mzigo.” (al-Jinn 72:06)

2- Khawlah bint Hakiym (Radhiya Allaahu 'anhaa) ameeleza kwamba amemsikia Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) akisema:

“Yeyote atakayetua mahali na akasema:

أَعُوذُ بِكَلِمَاتِ اللَّهِ التَّامَّاتِ مِنْ شَرِّ مَا خَلَقَ

“Najikinga kwa maneno ya Allaah yaliyotimia dhidi ya maovu Aliyoyaumba.”

hakitomdhuru kitu mpaka atapoondoka mahali hapo.”⁶²

Ameipokea Muslim.

MAELEZO

Bi maana kitendo hichi ni shirki kubwa kama mfano wa 'ibaadah zengine anazofanyiwa asiyekuwa Allaah. Kwa sababu kuomba ulinzi ni 'ibaadah. Allaah (Ta'ala) amesema:

⁶² Muslim (2708).

وَأِمَّا يَنْزِعَنَّكَ مِنَ الشَّيْطَانِ نَزْعٌ فَاسْتَعِذْ بِاللَّهِ

“Na pindi utakapokuchochea uchochezi kutokana na shaytwaan, basi mtake kinga Allaah.” (al-A’raaf 07:200)

قُلْ أَعُوذُ بِرَبِّ النَّاسِ

”Sema: “Najikinga na Mola wa watu.” (an-Naas 114:01)

قُلْ أَعُوذُ بِرَبِّ الْعَلَقِ

”Sema: “Najikinga na Mola wa mapambazuko.” (al-Falaq 113:01)

Kuhusu kuomba ulinzi kutoka kwa viumbe waliohai, mbele yako na wenye uwezo, hakuna neno. Kama ambavyo mtu anaomba kutokamana na mtumwa wa mtu au mtoto wake. Allaah (Ta’ala) amesema:

فَاسْتَعَاثَهُ الَّذِي مِنَ شِيعَتِهِ عَلَى الَّذِي مِنْ عَدُوِّهِ

“Akamsaidia yule ambaye katika kundi lake dhidi ya yule ambaye ni katika adui wake.” (al-Qaswasw 28:15)

1- Allaah (Ta’ala) amesema:

وَأَنَّهُ كَانَ رِجَالٌ مِّنَ الْإِنْسِ يَعُوذُونَ بِرِجَالٍ مِّنَ الْجِنِّ فَزَادُوهُمْ رَهَقًا

”Na kwamba walikuwa wanaume miongoni mwa watu wanajikinga na wanaume miongoni mwa majini, basi wakawazidishia mzigo.”

Aayah hii iliteremshwa juu ya watu ambao walikuwa wakiwaomba ulinzi wale viongozi wa majini. Hivo ndivyo walivyokuwa waarabu katika kipindi cha kikafiri. Wanapotua sehemu basi wanasema:

“Tunamuomba ulinzi kiongozi wa bonde hili kutokamana na wale wapumbavu katika watu wake.”

Kitendo hichi ni katika matendo ya watu wa kipindi cha kikafiri. Ni wajibu kumtekelezea hayo yote Allaah pekee. Allaah amesema:

1- Allaah (Ta'ala) amesema:

فَزَادُوهُمْ رَهَقًا

“... basi wakawazidishia mzigo.”

Bi maana majini waliwazidishia watu uwoga zaidi. Watu watu walipowaogopa majini basi majini yalizidi kuwa na kiburi. Kuna baadhi ya Salaf wamesema kinyume na hivyo kwamba watu waliwazidishia majini kiburi na jeuri. Maana zote mbili ni za sawa. Pindi mwanadamu anapowaomba majini ulinzi basi huingiwa na majivuno na jeuri na huku mwanadamu anaingiwa na woga zaidi kuwaogopa majini. Allaah amewataja katika mazingira ya kuwakaripia, kwa hiyo ina maana kwamba ni wajibu kuachana na kitendo hicho.

2- Khawlah bint Hakiym (Radhiya Allaahu 'anhaa) ameeleza kwamba amemsikia Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) akisema:

“Yeyote atakayetua mahali na akasema:

أَعُوذُ بِكَلِمَاتِ اللَّهِ التَّامَّاتِ مِنْ شَرِّ مَا خَلَقَ

“Najikinga kwa maneno ya Allaah yaliyotimia dhidi ya maovu Aliyoyaumba.”

hakitomdhuru kitu mpaka atapoondoka mahali hapo.”

Ameipokea Muslim.

Imependekezwa kusoma du'aa hii wakati mtu anapotua mahali fulani. Hadiyth inaonyesha fadhilah za du'aa hii ya kinga na kwamba inachangia kumlinda mtu na shari ya majini na watu. Kadhalika mtu anatakiwa kusema wakati anapoingia ndani ya ndege, anapokaa kwenye gari, anapoingia ndani ya treni na mfano wake. Imekuja katika Hadiyth kwamba imependekezwa kuisoma mara tatu. Wakati Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) alipokuwa anaomba kitu basi anaomba mara tatu.

Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema “maneno”. Maana yake ni kwamba maneno ya Allaah yenye kutekelezeka na ya kilimwengu ambayo hayawezi kurudishwa na chochote. Wapo baadhi ya Salaf waliosema “maneno” maana yake ni yale maneno ya Allaah ya Kishari'ah na ya Qur-aan kwa sababu ni maneno makubwa na matukufu zaidi na ni maneno ya Allaah. Tafsiri zote hizi ni haki na zote ni sifa za Allaah (Subhaanah). Maneno Yake ya kilimwengu ni yenye kutekelezeka na maneno Yake ya Kishari'ah ndio maneno bora zaidi.

Katika Hadiyth hii kuna kufanya Tawassul kwa sifa za Allaah. Salaf wameitumia Hadiyth hii kama dalili kuthibitisha kwamba maneno ya Allaah hayakuumbwa kwa sababu haijuzu kuomba kinga kwa asiyekuwa Allaah. Hadiyth inathibitisha kwamba maneno ya Allaah ni sifa miongoni mwa sifa Zake, inafaa kutaka ulinzi kwayo na kwamba hayakuumbwa.

Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema “hakitomdhuru kitu”. Neno “kitu” imetajwa katika mazingira ya kuenea na inahusiana na kila kitu. Hii inaonyesha fadhilah za du'aa hii na kwamba inatakiwa kuitendea kazi. Kuhusu kuomba ulinzi kwa asiyekuwa Allaah na kwa sifa zake, haijuzu kwa maafikiano. Kwa sababu ni shirki.

14. Kutaka uokozi kwa asiye kuwa Allaah au kumuomba mwingine asiye kuwa Yeye ni katika shirki

Shaykh-ul-Islaam Muhammad bin 'Abdil-Wahhaab (Rahimahu Allaah) amesema:

1- Allaah (Ta'ala) amesema:

وَلَا تَدْعُ مِنْ دُونِ اللَّهِ مَا لَا يَنْفَعُكَ وَلَا يَضُرُّكَ ۚ فَإِنْ فَعَلْتَ فَإِنَّكَ إِذَا مِنْ الظَّالِمِينَ وَإِنْ يَمْسَسْكَ اللَّهُ بِضُرٍّ فَلَا كَاشِفَ لَهُ إِلَّا هُوَ

“Wala usiombe badala ya Allaah asiye kufaa na wala asiye kudhur; na ukifanya hivyo, basi hakika utakuwa miongoni mwa madhalimu. Allaah akikugusisha dhara, basi hakuna awezaye kuiondosha isipokuwa Yeye.” (Yuunus 10:106-107)

2-

فَابْتَغُوا عِنْدَ اللَّهِ الرِّزْقَ وَاعْبُدُوهُ وَاشْكُرُوا لَهُ ۚ إِلَيْهِ تُرْجَعُونَ

“Basi tafuteni riziki kwa Allaah na mwabuduni na mshukuruni; Kwake ndio mtarejea.” (al-Ankabuut 29:17)

3-

وَمَنْ أَضَلُّ مِمَّن يَدْعُو مِنْ دُونِ اللَّهِ مَنْ لَا يَسْتَجِيبُ لَهُ إِلَى يَوْمِ الْقِيَامَةِ وَهُمْ عَنِ دُعَائِهِمْ غَافِلُونَ

“Ni nani aliyepotea zaidi kuliko yule anayemwomba badala ya Allaah, ambao hatowaitikia mpaka siku ya Qiyaamah nao hawatambui maombi yao.” (al-Ahqaaf 46:05-06)

4-

أَمَّنْ يُجِيبُ الْمُضْطَرَّ إِذَا دَعَاهُ وَيَكْشِفُ السُّوءَ

"Au Yule anayemuitika mwenye dhiki anapomwomba na akamuondoshea uovu?" (an-Naml 27:62)

5- at-Twabaraaniy amepokea kwa cheni ya wapokezi wake:

"Katika zama za Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) kulikuwepo mnafiki akiwaudhi waumini. Baadhi yao wakasema: "Simameni tumwendee Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) kumtaka msaada kutokana na mnafiki huyu. Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) akasema: "Hakika mimi siye niombwaye uokozi. Isipokuwa uokozi unaombwa kwa Allaah pekee."⁶³

MAELEZO

Mlango huu ni maalum baada ya ujumla uliotangulia. Kwa sababu kutaka uokozi ni katikad du'aa. Kila mwenye kuomba uokozi anakuwa ameomba na si kila mwenye kuomba anakuwa ameomba uokozi. Mtu anayeomba uokozi ni yule anayeomba wakati wa matatizo, kama ilivyotajwa katika Aayah:

فَاسْتَعَاثَهُ الَّذِي مِنْ شِيعَتِهِ عَلَى الَّذِي مِنْ عَدُوِّهِ

"Akamsaidia yule ambaye katika kundi lake dhidi ya yule ambaye ni katika adui wake." (al-Qaswasw 28:15)

إِذْ تَسْتَغِيثُونَ رَبَّكُمْ

⁶³ al-Haytamiy amesema: "Ameipokea at-Twabaraaniy. Wanaume wake ni wanaume wa al-Bukhaariy isipokuwa Ibn Lahiy'ah ambaye hata hivyo hupokea Hadiyth nzuri." (Majma'-uz-Zawaa-id (17276)).

“Pindi mlipomuomba uokovu Mola wenu.” (al-Anfaal 08:09)

Yule ambaye ni mgonjwa au anaogopa kuzama ndani ya maji na akaomba uokozi kwa Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) au kwa al-Badawiy amefanya shirki kubwa. Washirikina wakati wa kipindi cha kikafiri walikuwa wakimuomba Allaah peke yake wakati wa matatizo. Kwa sababu walikuwa wakijua kuwa hakuna awezaye kuwaokoa isipokuwa Allaah pekee. Kuhusu washirikina katika wakati wetu huu wanashirikisha katika kipindi cha raha na katika kipindi cha matatizo. Yule anayefanya hivo wakati wa matatizo anazingatiwa ametaka uokozi na yule anayefanya hivo wakati wa raha anazingatiwa ameomba. Lakini hivyo matendo yote mawili ni shirki. Dalili ya hayo ni:

1-

وَلَا تَدْعُ مِنْ دُونِ اللَّهِ مَا لَا يَنْفَعُكَ وَلَا يَضُرُّكَ ۚ فَإِنْ فَعَلْتَ فَإِنَّكَ إِذَا مِنْ الظَّالِمِينَ

“Wala usiombe badala ya Allaah asiyekufaa na wala asiyekudhur; na ukifanya hivyo, basi hakika utakuwa miongoni mwa madhalimu.”

Bi maana miongoni mwa washirikina.

وَالْكَافِرُونَ هُمُ الظَّالِمُونَ

“Makafiri wao ndio madhalimu.” (al-Baqarah 02:254)

Allaah amebainisha hukumu juu ya yule mwenye kuomba badala ya Allaah kisichoweza kumnufaisha wala kumdhuru. Hukumu hii ni yenye kuenea na inawahusu viumbe wote wasioweza kunufaisha wala kudhuru wao wenyewe. Allaah ndiye awezaye kudhuru na kunufaisha kivyake. Allaah amebainisha kwamba yule mwenye kumuomba asiyekuwa Allaah basi ni mshirikina. Hata

hivyo kunavuliwa katika hayo yule mwenye kumuomba aliyehai, muweza na wakati huohuo yuko mbele yake. Waislamu wameafikiana kwamba sio shirki. Mfano wa hilo ni kama mtu akamuomba mwingine kubeba kitu, kumsaidia kutua kitu chini na mfano wa hayo. Allaah (Ta'ala) amesema:

وَإِنْ يَمْسَسْكَ اللَّهُ بِضُرٍّ فَلَا كَاشِفَ لَهُ إِلَّا هُوَ

“Allaah akikugusisha dhara, basi hakuna awezaye kuiondosha isipokuwa Yeye.”

Haya ni kujengea juu ya kwamba viumbe si waweza wa kuleta manufaa wala kuzuia madhara. Vipi mtu atamuabudu mwingine asiyekuwa Yeye ilihali si muweza?

2-

فَابْتَغُوا عِنْدَ اللَّهِ الرِّزْقَ وَاعْبُدُوهُ وَاشْكُرُوا لَهُ إِلَيْهِ تُرْجَعُونَ

“Basi tafuteni riziki kwa Allaah na mwabuduni na mshukuruni; Kwake ndio mtarejea.”

Ameamrisha riziki na uokozi aombwe Yeye peke yake na asiabudiwe mwingine yeyote asiyekuwa Yeye. Kunavuliwa katika hayo yale yaliyotangulia.

3-

وَمَنْ أَضَلُّ مِمَّن يَدْعُو مِن دُونِ اللَّهِ مَن لَّا يَسْتَجِيبُ لَهُ إِلَى يَوْمِ الْقِيَامَةِ وَهُمْ عَن دُعَائِهِمْ غَافِلُونَ

“Ni nani aliyepotea zaidi kuliko yule anayemwomba badala ya Allaah, ambao hatowaitikia mpaka siku ya Qiyaamah nao hawatambui maombi yao.”

Aayah inathibitisha kwamba hakuna yeyote ambaye ni mpotevu zaidi kuliko yule anayemwomba mwingine asiyekuwa Allaah. Mtu kama huyo hakufaulu

hapa duniani na huko Aakhirah ni mwenye kukhasirika na kutupwa Motoni. Ameeleza mambo mane kuhusu yule mwenye kumuomba badala ya Allaah:

1- Hawawezi kumuitikia mpaka siku ya Qiyaamah.

2- Hawatambui maombi yao. Imaa kwa sababu ni wafu, vitu visivyokuwa na uhai na havina hisia, wako hai lakini wameshughulishwa au Malaika wasiotambua ni nani mwenye kuwaomba.

3- Watakuwa ni maadui wa wale wawaombao siku ya Qiyaamah.

4- Watajitenga mbali na 'ibaadah zao na kuzikemea.

أَمَّنْ يُجِيبُ الْمُضْطَرَّ إِذَا دَعَاهُ وَيَكْشِفُ السُّوءَ

"Au Yule anayemuitika mwenye dhiki anapomwomba na akamuondoshea uovu?"

Bi maana hakuna yeyote awezaye hayo. Kwa ajili hiyo haitakikani kumuomba yeyote asiyekuwa Allaah.

5- at-Twabaraaniy amepokea kwa cheni ya wapokezi wake:

"Katika zama za Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) kulikuwepo mnafiki akiwaudhi waumini. Baadhi yao wakasema: "Simameni tumwendee Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) kumtaka msaada kutokana na mnafiki huyu. Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) akasema: "Hakika mimi siye niombwaye uokozi. Isipokuwa uokozi unaombwa kwa Allaah pekee."

Imekuja katika upokezi mwingine kwamba 'Ubaadah bin as-Swaamit ndiye aliyesema hivo na kwamba mnafiki huyo alikuwa 'Abdullaah bin Abiy Saluu. Hata hivyo katika cheni ya wapokezi wake kuna baadhi ya udhaifu.

Maswahabah hawakumuomba uokozi Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) isipokuwa ni kwa sababu walijua kuwa anaweza kuwaokoa naye aidha kwa kumuua au kumfunga. Walitambua kuwa inafaa kumuomba msaada ambaye yuhai na muweza. Kwa ajili hiyo ndio maana wakaenda kwake. Maneno ya Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) "Hakika mimi siye niombwaye uokozi" yanaweza kufasiriwa kwa njia mbili:

1- Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) hawezi kumuua kwa sababu ilikuwa imekatazwa ili watu wasije kusema kuwa Muhammad (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) anawaua Maswahabah wake. Kwa ajili hiyo ndio maana akaacha kumuua.

2- Upokezi huu ukiwa ni Swahiyh basi inawezekana alisema hivo kwa sababu ya kuziba njia ijapokuwa alikuwa ni muweza wa kuwaondoshea naye. Alisema hivo ili wasitamke namna hiyo katika mambo asiyoyaweza.

Kinacholengwa ni kwamba uokozi hauombwi kutoka kwa mwingine asiyekuwa Allaah isipokuwa katika yale mambo ambayo aliyehai anayaweza.

15. Tawhiyd na ugeni wa dini

Shaykh-ul-Islaam Muhammad bin 'Abdil-Wahhaab (Rahimahu Allaah) amesema:

1- Allaah (Ta'ala) amesema:

أَيْشْرِكُونَ مَا لَا يَخْلُقُ شَيْئًا وَهُمْ يُخْلَقُونَ وَلَا يَسْتَطِيعُونَ لَهُمْ نَصْرًا وَلَا أَنْفُسُهُمْ يَنْصُرُونَ

“Je, wanawashirikisha wale ambao hawaumbi kitu, na hali wao wenyewe wameumbwa, na wala hawawezi kuwanusuru na wala hawawezi kujinusuru nafsi zao?” (al-A'raaf 07:191-192)

2-

وَالَّذِينَ تَدْعُونَ مِنْ دُونِهِ مَا يَمْلِكُونَ مِنْ قِطْمِيرٍ

“Na wale mnaowaomba badala Yake hawamiliki japo kijiwavu cha kokwa ya tende.” (Faatwir 35:13-14)

3- Imesihi kupokelewa kupitia kwa Anas (Radhiya Allaahu 'anh) ya kwamba Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) alipasuliwa siku ya Uhud na yakavunjwa meno yake mane. Akasema:

“Vipi watafaulu watu ambao wamempasua Mtume wao?”

Ndipo kukateremshwa:

لَيْسَ لَكَ مِنَ الْأَمْرِ شَيْءٌ

“Si juu yako katika amri kuamua lolote.”⁶⁴ (Aal 'Imraan 03:128)

⁶⁴ al-Bukhaariy na Muslim (1791).

4- Imepokelewa kupitia kwa Ibn 'Umar (Radhiya Allaahu 'anhumaa) ya kwamba amemsikia Mtume wa Allah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) akisema wakati akiinua kichwa chake kutoka katika Rukuu' katika Rak'ah ya mwisho ya Fajr:

“Ee Allaah! Mlaani fulani na fulani!”

Haya aliyasema baad ya kusema:

“Allaah amemsikia mwenye kumhimidi. Mola wetu! Sifa zote njema ni Zako.”

Ndipo Allaah akateremsha:

لَيْسَ لَكَ مِنَ الْأَمْرِ شَيْءٌ

“Si juu yako katika amri kuamua lolote.”⁶⁵ (Aal 'Imraan 03:128)

Katika upokezi mwingine imekuja ya kwamba (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) alikuwa akiomba dhidi ya Swafwaan bin Umayyah, Suhayl bin 'Amr na al-Haarith bin Hishaam.” Ndipo kukateremka:

لَيْسَ لَكَ مِنَ الْأَمْرِ شَيْءٌ

“Si juu yako katika amri kuamua lolote.”⁶⁶ (Aal 'Imraan 03:128)

5- Imesihi kupokelewa kupitia kwa Abu Hurayrah (Radhiya Allaahu 'anh) ambaye amesema:

“Alisimama Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) wakati alipotemshiwa:

وَأَنْذِرْ عَشِيرَتَكَ الْأَقْرَبِينَ

⁶⁵ al-Bukhaariy (4070).

⁶⁶ at-Tirmidhiy (3004), Ahmad (5674) na al-Bayhaqiy (2948).

“Na waonye jamaa zako wa karibu.” (ash-Shu'raa 26:214)

na akasema (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam): “Enyi Quraysh - au maneno mfano wa haya - Zinunueni nafsi zenu! Hakika sintokufaeni mbele ya Allaah na chochote. Ee 'Abbaas bin 'Abdil-Muttwalib! Sitokufaa mbele ya Allaah na chochote! Ee Swafiyyah, shangazi yake Mtume wa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) Sitokufaa mbele ya Allaah na chochote. Ee Faatwimah, binti ya Muhammad! Niombe chochote katika mali yangu utakacho. Sitokufaa mbele ya Allaah na chochote.”

MAELEZO

1-

أَيْشُرْكُونَ مَا لَا يَخْلُقُ شَيْئًا وَهُمْ يُخْلَقُونَ وَلَا يَسْتَطِيعُونَ لَهُمْ نَصْرًا وَلَا أَنْفُسَهُمْ يَنْصُرُونَ

“Je, wanawashirikisha wale ambao hawaumbi kitu, na hali wao wenyewe wameumbwa, na wala hawawezi kuwanusuru na wala hawawezi kujinusuru nafsi zao?”

Anachokusudia mtunzi kwa mlango huu ni kubainisha yale waliyokuwemo washirikina katika zama za Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) wakati alipowalingania na kuwapiga vita. Anabainisha ubatilifu wa hali zao inapokuja katika kumuabudu mwingine asiyekuwa Allaah walio na sifa hii. Mtu aliye na sifa kama hii hastahiki kuabudiwa. Swali limeulizwa kwa lengo la kuwakemea. Wao hawawezi kuumba hata nzi. Bali wao wenyewe wameumbwa. Ni vipi basi watawanufaisha wengine wasiokuwa wao? Wao ima ni viumbe visivyokuwa na uhai na visivyokuwa na akili au viumbe vilivyo hai lakini hawasikii au wafu wasiowatikia wale wenye kuwaomba. Katika Aayah wamesifiwa wale wanaowabudiwa badala ya Allaah kwa njia nne:

1- Hawaumbi kitu.

2- Wao wenyewe wameumbwa na wanaendeshwa.

3- Hawawezi kuwanusuru.

4- Wao wenyewe hawawezi kujinusuru.

2-

وَالَّذِينَ تَدْعُونَ مِنْ دُونِهِ مَا يَمْلِكُونَ مِنْ قِطْمِيرٍ

“Na wale mnaowaomba badala Yake hawamiliki japo kijiwavu cha kokwa ya tende.”

Allaah amewasifu waungu wao kwa sifa nne:

1- Hawamiliki chochote japo kijiwavu cha kokwa ya tende.

2- Hawasikii maombi ya wale wenye kuwaomba.

3-Hata kama watasikia hawatoweza kuwajibu.

4- Siku ya Qiyaamah watakanusha ushirikina wa watu hawa. Hii ndio hali ya washirikina. Hakika wamekhasirika duniani na Aakhirah.

3- Imesihi kupokelewa kupitia kwa Anas (Radhiya Allaahu 'anh) ya kwamba Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) alipasuliwa siku ya Uhud na yakavunjwa meno yake mane. Akasema:

“Vipi watafaulu watu ambao wamempasua Mtume wao?”

Ndipo kukateremshwa:

لَيْسَ لَكَ مِنَ الْأَمْرِ شَيْءٌ

“Si juu yako katika amri kuamua lolote.”

Ikiwa kiumbe huyu mbora na Mtume ndiye ana manzilah ya karibu zaidi kwa Allaah hawezi kuitetea nafsi yake mwenyewe wala Maswahabah zake ambao ndio watu wa karne bora kabisa, basi ni dalili inayofahamisha kwamba hastahiki kuabudiwa badala ya Allaah wala kushirikishwa pamoja Naye. Yale yaliyomtokea Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) na Maswahabah zake kwa sababu ya dhambi zao yalitokea kwa sababu ya hekima kubwa. Ni vipi Muhammad (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) na Maswahabah zake, seuze wengine, wataombwa ikiwa wao wenyewe hawakuweza kujitetea nafsi zao wenyewe? Dhambi waliofanya ni kwenda kinyume na maamrisha ya Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) pale alipowaamrisha wapiganaji juu ya mlima kubaki katika nafasi zao.

4- Imepokelewa kupitia kwa Ibn 'Umar (Radhiya Allaahu 'anhumaa) ya kwamba amemsikia Mtume wa Allah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) akisema wakati akiinua kichwa chake kutoka katika Rukuu' katika Rak'ah ya mwisho ya Fajr:

“Ee Allaah! Mlaani fulani na fulani!”

Haya aliyasema baad ya kusema:

“Allaah amemsikia mwenye kumhimidi. Mola wetu! Sifa zote njema ni Zako.”

Ndipo Allaah akateremsha:

لَيْسَ لَكَ مِنَ الْأَمْرِ شَيْءٌ

“Si juu yako katika amri kuamua lolote.”

Aliomba dhidi ya al-Haarith bin Hishaam, Swafwaan bin Umayyah na viongozi wengine wa Quraysh. Baada ya hapo wakaingia katika Uislamu. Allaah aliwaongoza na hakuitikia du'aa na laana dhidi yao. Ikiwa kiongozi na bwana wa wanaadamu hakukubaliwa du'aa yake na du'aa yake haikuwadhuru, vipi kuhusu wengine? Allaah ni mjuzi zaidi juu ya hali za waja Wake.

5- Imesihi kupokelewa kupitia kwa Abu Hurayrah (Radhiya Allaahu 'anh) ambaye amesema:

“Alisimama Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) wakati alipotoremshiwa:

وَأَنْذِرْ عَشِيرَتَكَ الْأَقْرَبِينَ

“Na waonye jamaa zako wa karibu.”

na akasema (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam): “Enyi Quraysh – au maneno mfano wa haya - Zinunueni nafsi zenu! Hakika sintokufaeni mbele ya Allaah na chochote. Ee 'Abbaas bin 'Abdil-Muttwalib! Sitokufaa mbele ya Allaah na chochote! Ee Swafiyah, shangazi yake Mtume wa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) Sitokufaa mbele ya Allaah na chochote. Ee Faatwimah, binti ya Muhammad! Niombe chochote katika mali yangu utakacho. Sitokufaa mbele ya Allaah na chochote.”

Amewakanushia kuwa udugu wao hautowafaa kitu ikiwa hatowamini. Amewaamrisha kuamini na kufuata yale aliyokuja nayo (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) na akawabainishia Tawhiyd na kwamba ndio njia ya uokozi. Tawhiyd ndio itakayowafanya kufaulu. Ama kuhusu mali yake, anaweza akawafaa nayo. Hili linatufahamisha kwamba 'ibaadah anastahiki kufanyiwa Allaah (Ta'ala) pekee na si mwingine. Ikiwa Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) hawezi kumnufaisha yeyote mbele ya Allaah basi wengine wote wana haki zaidi ya kutoweza kufanya hivo.

Katika haya kuna Radd kwa washirikina ambao wanaomba manufaa kwa wengine asiye kuwa Allaah na huku wanasema:

مَا نَعْبُدُهُمْ إِلَّا لِيُقَرِّبُونَا إِلَى اللَّهِ زُلْفَىٰ

“Hatuwaabudu isipokuwa ili wapate kutukurubisha kwa Allaah karibu” (**az-Zumar 39:03**)

Allaah ameita kitendo chao hichi kuwa ni shirki na akamwamrisha Mtume Wake kuwapiga vita kwa sababu walikuwa washirikina.

Kuhusu kumuomba kitu ambaye yuhai na muweza ni sawa. Ni miongoni mwa sababu zenye kuhisiwa na zenye kuingia akilini na hazina mahusiano yoyote na mambo yaliyofichikana wala wafu.

16. Mlango kuhusu maneno Yake (Ta'ala) “Mpaka itakapoondolewa fazaiko nyoyoni mwao [baada ya kuzimia]; watasema [wakiulizana]: “Amesema nini Mola wenu?” – waseme: “Ya haki; Naye yujuu, Mkubwa kabisa.”

Shaykh-ul-Islaam Muhammad bin 'Abdil-Wahhaab (Rahimahu Allaah) amesema:

1- Allaah (Ta'ala) amesema:

حَتَّىٰ إِذَا فُزِّعَ عَن قُلُوبِهِمْ قَالُوا مَاذَا قَالَ رَبُّكُمْ ۖ قَالُوا الْحَقُّ ۖ وَهُوَ الْعَلِيُّ الْكَبِيرُ

“Mpaka itakapoondolewa fazaiko nyoyoni mwao [baada ya kuzimia]; watasema [wakiulizana]: “Amesema nini Mola wenu?” – waseme: “Ya haki; Naye yujuu, Mkubwa kabisa.” (Sabaa' 34:23)

2- Imesihi kupokelewa kupitia Abu Hurayrah (Radhiya Allaahu 'anh) kwamba Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Allaah anapotoa amri huko juu ya mbingu Malaika hupiga mbawa zao kwa kunyenyekevu maneno Yake. Kama vile ni mnyororo juu ya mlima. Huwapita amri hiyo hali wamezimia mpaka inapoondolewa ile fazaiko kwenye nyoyo zao wanasema [wakiulizana]: “Amesema nini Mola wenu?” – waseme: “Ya haki; Naye yujuu, Mkubwa kabisa.” Husikia Neno hilo wale waibao usikizi na hawa waibao usikizi wanakuwa wamepandiana namna hii. Sufyaan bin 'Uyaynah alionyesha kwa kunyanyua mkono wake na kutawanya vidole. Wadukuzi wa usikizi huliagiza neno hili kwa kwa aliye chini yake, kisha huyo mwingine

humuagizia aliye chini yake mpaka humfikishia kuhani au mchawi. Wakati mwingine humpata kimondo kabla ya kuifikisha na wakati mwingine huenda akaifikisha kabla ya kimondo hicho kumpata. Hapo ndipo huongezewa neno hilo uongo mia moja. Kunasemwa: “Kwani sialitwambia hivi na hivi siku kadhaa na kadhaa?” Husadikishwa kwa neno hilo alilolisikia kutoka mbinguni.”⁶⁷

3- an-Nawwaas bin Sam'aan (Radhiya Allaahu 'anh) ameeleza kwamba Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Allaah (Ta'ala) anapotaka kufunua amri ya jambo fulani basi Huzungumza. Hapo ndipo mbingu hutetemeka sana - au alisema radi kali - kwa sababu ya kumuogopa Allaah ('Azza wa Jall). Wanapoyasikia hayo wakazi wa mbinguni basi huanguka chini hali ya kusujudu. Wa kwanza wao ambaye hunyanyua kichwa chao anakuwa ni Jibriyl ambaye Allaah anamzungumzisha kwa Wahy kwa Ayatakayo. Kisha Jibriyl anawapitia Malaika wengine katika mbingu mbalimbali. Katika kila tabaka anayopita basi Malaika humuuliza: “Kasema nini Mola Wetu, ee Jibriyl?” Jibriyl anasema: [wakiulizana]: “Amesema nini Mola wenu?” - waseme: “Ya haki; Naye yujuu, mkubwa.” Jibriyl hujibu: “Ya haki; Naye yujuu, Mkubwa kabisa.” Baada ya hapo wote husema vile alivyosema Jibriyl. Jibriyl humalizia kwa Wahy vile Alivyoamrisha na Allaah ('Azza wa Jall).”⁶⁸

MAELEZO

1- Allaah (Ta'ala) amesema:

حَتَّىٰ إِذَا فُزِّعَ عَن قُلُوبِهِمْ قَالُوا مَاذَا قَالَ رَبُّكُمْ ۖ قَالُوا الْحَقُّ ۖ وَهُوَ الْعَلِيُّ الْكَبِيرُ

⁶⁷ al-Bukhaariy (7481).

⁶⁸ at-Twabaraaniy katika "Musnad-ush-Shaamiyyiyn" (591).

“Mpaka itakapoondolewa fazaiko nyoyoni mwao [baada ya kuzimia]; watasema [wakiulizana]: “Amesema nini Mola wenu?” – waseme: “Ya haki; Naye yujuu, Mkubwa kabisa.”

Alichokusudia mtunzi wa kitabu kwa mlango huu ni kuwaraddi waabudu makaburi, masanamu, Malaika na wengineo. Anabainisha namna Malaika wanavyomuogopa Allaah na adhabu Yake pindi ikiwa watakwenda kinyume na amri Yake. Ni vipi basi watashahiki kuabudiwa?

إِنَّ الَّذِينَ تَدْعُونَ مِنْ دُونِ اللَّهِ عِبَادٌ أَمْثَلُكُمْ

“Hakika wale muowaombao badala ya Allaah ni waja kama nyinyi.” (al-A’raaf 07:194)

2- Imesihi kupokelewa kupitia Abu Hurayrah (Radhiya Allaahu ‘anh) kwamba Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) amesema:

“Allaah anapotoa amri huko juu ya mbingu Malaika hupiga mbawa zao kwa kunyenyekevu maneno Yake. Kama vile ni mnyororo juu ya mlima. Huwapita amri hiyo hali wamezimia mpaka inapoondolewa ile fazaiko kwenye nyoyo zao wanasema [wakiulizana]: “Amesema nini Mola wenu?” – waseme: “Ya haki; Naye yujuu, Mkubwa kabisa.” Husikia Neno hilo wale waibao usikizi na hawa waibao usikizi wanakuwa wamepandiana namna hii. Sufyaan bin ‘Uyaynah alionyesha kwa kunyanyua mkono wake na kutawanya vidole. Wadukuzi wa usikizi huliagiza neno hili kwa kwa aliye chini yake, kisha huyo mwingine humuagizia aliye chini yake mpaka humfikishia kuhani au mchawi. Wakati mwingine humpata kimondo kabla ya kuifikisha na wakati mwingine huenda akaifikisha kabla ya kimondo hicho kumpata. Hapo ndipo huongezewa neno hilo uongo mia moja. Kunasemwa: “Kwani sialitwambia hivi na hivi siku kadhaa na kadhaa?” Husadikishwa kwa neno hilo alilolisikia kutoka mbinguni.”

Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) ametaja fazaiko na namna inavyowaondoka Malaika, kama ilivyokuja katika Hadiyth. Wanapopata fahamu husema: "Amesema nini Mola wenu?" Waseme hali ya kujibu: "Ya haki." Bi maana wanaambizana. Ya haki kinachokusudiwa ni yale aliyosema Allaah kuhusu hili na lile.

Wakati Malaika wanaposikia neno la Mola ('Azza wa Jall) basi huanza hupiga mbawa zao huku wakiogopa na wakinyenyekea mbele ya Allaah ('Azza wa Jall). Kama kwamba ni minyororo iliyopigwa juu ya mlima. Hapo ndipo wadukuzi wa usikizi huiba maneno haya yaliyosemwa na Malaika. Wanakuwa wamepandiana na baadhi huwaagizia wengine neno hilo mpaka wa mwisho kumfikia huwa ni kuhani au mchawi. Hupatwa na kimondo. Wakati fulani kuna ambao hupatwa na kimondo kabla ya kulifikisha neno lile kwa mchawi na wakati mwingien kuna ambao hulifikisha baada ya kuwa wameshalifikisha. Hivi ndivyo Allaah anawapa mtihani waja Wake. Lau Allaah angetaka basi wasingelisikia chochote. Maneno haya yanamfikia mchawi na anayachanganya na uongo mia moja na ilihali ukweli ni mmoja tu. Ndipo watu wanaanza kuambizana namna kuna siku aliyosema kweli. Matokeo yake wanasadikisha maneno mengi kwa sababu ya neno moja tu la kweli. Kwa ajili hiyo ndio maana haitakiwi kwa mtu akadanganyika na watu hawa. Haitakiwi kuwaamini kunatokamana ima na jambo la kidunia lililonukuliwa kutoka kwa mashaytwaan au kutoka kwa wadukuzi wa usikizi. Kwa hivyo ni wajibu kutowasikiliza japokuwa watakuwa ni wenye kusema kweli wakati fulani.

3- an-Nawwaas bin Sam'aan (Radhiya Allaahu 'anh) ameeleza kwamba Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

"Allaah (Ta'ala) anapotaka kufunua amri ya jambo fulani basi Huzungumza. Hapo ndipo mbingu hutetemeka sana - au alisema radi kali - kwa sababu ya kumuogopa Allaah ('Azza wa Jall). Wanapoyasikia hayo wakazi wa mbinguni basi huanguka chini hali ya kusujudu. Wa kwanza wao ambaye hunyanyua

kichwa chao anakuwa ni Jibriyl ambaye Allaah anamzungumzisha kwa Wahy kwa Ayatakayo. Kisha Jibriyl anawapitia Malaika wengine katika mbingu mbalimbali. Katika kila tabaka anayopita basi Malaika humuuliza: “Kasema nini Mola Wetu, ee Jibriyl?” Jibriyl anasema: [wakiulizana]: “Amesema nini Mola wenu?” – waseme: “Ya haki; Naye yujuu, mkubwa.” Jibriyl hujibu: “Ya haki; Naye yujuu, Mkubwa kabisa.” Baada ya hapo wote husema vile alivyosema Jibriyl. Jibriyl humalizia kwa Wahy vile Alivyoamrisha na Allaah (‘Azza wa Jall).”

Sam‘aan inaweza pia kusomwa Sim‘aan.

Jibriyl pia inaweza kusomwa kama Jabraaiyl. Yeye ndiye wa kwanza anayepata fahamu kwa sababu yeye ndiye Malaika mtukufu zaidi na ndiye mjumbe kati ya Allaah na Mitume Wake. Kila anapopita katika mbingu basi humuuliza Malaika wa mbingu hiyo. Wadukuzi wa usikizi husikia maneno wanayoambizana Malaika. Wakati mwingine huenda wakahifadhi kitu na wakawafikishia wachawi na makuhani. Wakati mwingine huenda wakachomwa na wasifikishe kitu. Allaah ndiye mwamuzi.

Ni wajibu kumuabudu Allaah peke yake. Si Malaika, Mitume wala mwengineo hawaistahiki. Hapa kuna dalili ya kuogopa kwa Malaika na kufazaika kwao.

Yule mwenye kuamini kuwa makuhani wanajua mambo yaliyofichikana ni kafiri.

Katika Hadiyth kuna kuthibiti kwa sifa ya Allaah kuwa na maneno na utashi na fadhilah za Malaika.

Hadiyth inathibitisha vilevile kwamba mashaytwaan hudukua usikizi. Hali ilikuwa hivo hata kabla ya utume. Wakati alipotumilizwa Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) ndipo wakawekewa mkazo. Wakati (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) alipokufa wakawa ni wenye kuendelea kusikiliza. Wakati

fulani wanapatwa na kimondo kabla ya kuwahi kusikiliza na wakati mwingine wanapatwa na kimondo baada ya kuwahi kusikiliza.

17. Uombezi

Shaykh-ul-Islaam Muhammad bin 'Abdil-Wahhaab (Rahimahu Allaah) amesema:

1- Allaah (Ta'ala) amesema:

وَأَنْذِرْ بِهِ الَّذِينَ يَخَافُونَ أَنْ يُخْشَرُوا إِلَىٰ رَيْبِهِمْ ۚ لَيْسَ لَهُمْ مَنَّ دُونِهِ وَلِيٌّ وَلَا شَفِيعٌ لَّعَلَّهُمْ يَتَّقُونَ

"Na waonye kwayo [Qur-aan] wale wanaokhofu ya kwamba watakusanywa kwa Mola wao; hawana badala Yake mlinzi wala mwombezi ili wapate kumcha." (al-An'aam 06:51)

2-

قُلْ لِلَّهِ الشَّفَاعَةُ جَمِيعًا

"Sema: "Uombezi wote ni wa Allaah." (az-Zumar 39:44)

3-

مَنْ ذَا الَّذِي يَشْفَعُ عِنْدَهُ إِلَّا بِإِذْنِهِ

"Nani huyu ambaye anashufai mbele Yake bila ya idhini Yake?" (al-Baqarah 02:255)

4-

وَكَمْ مِنْ مَّلَكٍ فِي السَّمَاوَاتِ لَا تُعْنِي شَفَاعَتُهُمْ شَيْئًا إِلَّا مِنْ بَعْدِ أَنْ يَأْذَنَ اللَّهُ لِمَنْ يَشَاءُ وَيَرْضَىٰ

"Na Malaika wangapi mbinguni haitowafaa kitu chochote uombezi wao isipokuwa baada ya kuwa Allaah ametolea idhini kwa Amtakaye na kumridhia." (an-Najm 53:26)

5-

قُلْ ادْعُوا الَّذِينَ زَعَمْتُمْ مِّنْ دُونِ اللَّهِ لَا يَمْلِكُونَ مِثْقَالَ ذَرَّةٍ فِي السَّمَاوَاتِ وَلَا فِي الْأَرْضِ وَمَا لَهُمْ فِيهَا مِن شِرْكٍَ وَمَا لَهُ مِنْهُمْ مِّن ظَهِيرٍ وَلَا تَنْفَعُ الشَّفَاعَةُ عِنْدَهُ إِلَّا لِمَنْ أَذِنَ لَهُ حَتَّىٰ إِذَا فُزِّعَ عَن قُلُوبِهِمْ قَالُوا مَاذَا قَالَ رَبُّكُمْ قَالُوا الْحَقُّ وَهُوَ الْعَلِيُّ الْكَبِيرُ

”Sema: “Waombeni wale mnadai [kuwa ni waungu] badala ya Allaah. Hawamiliki uzito wa atomu mbinguni wala ardhini na wala wao hawana humo ushirika na wala Hana msaidizi miongoni mwao.” Na wala hautofaa uombezi mbele Yake isipokuwa kwa yule Aliyempa idhini. Mpaka itakapoondolewa fazaiko nyoyoni mwao [baada ya kuzimia]; watasema [wakiulizana]: “Amesema nini Mola wenu?” – waseme: “Ya haki; Naye yujuu, Mkubwa kabisa.” (Sabaab 34:22-23)

6- 'Abul-'Abbaas amesema:

“Allaah amekanusha vyote visivyokuwa Yeye ambavyo washirikina wamejiambatanisha navyo. Amekanusha kwa yeyote badala Yake kuwa na mamlaka au ushirika wowote wa hilo badala Yake au msaidizi wowote kwa Allaah. Hapakubaki isipokuwa uombezi. Hivyo amebainisha ya kwamba hautomfaa yeyote isipokuwa kwa yule ambaye Mola kampa idhini. Kama alivyosema (Ta'ala):

وَلَا يَشْفَعُونَ إِلَّا لِمَنِ ارْتَضَىٰ

“Na wala hawamuombei yeyote yule isipokuwa kwa yule ambaye Amemridhia.” (al-Anbiyaa 21:28)

Uombezi huu ambao washirikina wanatumai umekanushwa kuwepo kwake siku ya Qiyaamah, kama ulivyokanushwa na Qur-aan. Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi

wa sallam) ameeleza kwamb atakuja na kumsujudia Mola wake na kumhimidi. Hatoanza kuombea moja kwa moja. Baada ya hapo ndipo Ataambiwa:

“Nyanyua kichwa chako. Sema na utasikizwa. Omba na utapewa. Shufai utakubaliwa.”⁶⁹

7- Abu Hurayrah (Radhiya Allaahu ‘anh) alimuuliza Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam):

“Ni nani katika watu atakayekuwa na furaha zaidi kwa uombezi wako?” Akasema (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam): “Ni yule atakayesema: “Hapana mwabudiwa wa haki isipokuwa Allaah” akiwa ni wenye kutakasika kutoka moyoni mwake.”⁷⁰

Kwa hivyo uombezi huu ni kwa wale wenye Ikhlaasw baada ya idhini ya Allaah. kwa idhini ya Allaah na hautokuwa kwa wale waliomshirikisha Allaah. Ukweli wa mambo ni kwamba Allaah (Subhaanah) ndiye atakayetoa fadhilah Zake kuwapa wale wenye Ikhlaasw na awasamehe kupitia du’aa za waombeaji wataopewa idhini ya kushufai kwa ajili ya kumkirimu na kufikia nafasi yenye kusifiwa. Uombezi ambao umekanushwa na Qur-aan ni ule ambao ndani yake kuna shirki. Kwa ajili hii ndio maana uombezi umethibiti kwa idhini Yake katika maeneo mbalimbali. Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) amebainisha ya kwamba hautokuwa isipokuwa kwa watu wa Tawhiyd na Ikhlaasw.

MAELEZO

Watu wamezungumzia kuhusu uombezi na wakafikia katika maoni mbalimbali. Wazushi wamepondoka kwa ‘Aqiydah zao batili. Kwa ajili hiyo ndio maana wanachuoni wakalazimika kuizungumzia mada hii maalum ili muumini aweze kutambua haki na awe na imani sahihi juu yake. Mlango unaozungumzia

⁶⁹ al-Bukhaariy (7510) na Muslim (193).

⁷⁰ al-Bukhaariy (99).

uombezi ni wenye kubainisha uombezi uliohibitishwa na uliokanushwa pamoja na haki na batili ndani yake.

1- Allaah (Ta'ala) amesema:

وَأَنْذِرْ بِهِ الَّذِينَ يَخَافُونَ أَنْ يُخْشَرُوا إِلَىٰ رَيْبٍ ۚ لَيْسَ لَهُمْ مِّنْ دُونِهِ وَايٌّ وَلَا شَفِيعٌ لَّهُمْ يَتَّقُونَ

“Na waonye kwayo [Qur-aan] wale wanaokhofu ya kwamba watakusanywa kwa Mola wao; hawana badala Yake mlinzi wala mwombezi ili wapate kumcha.”

Bi maana, ee Muhammad, waonye kwa Qur-aan wale wanaokhofu kwamba ipo siku watafufuliwa kwa Mola wao. Inawahusu waislamu kwa sababu makafiri hawakusikia na wala hawakuitikia. Maonyo ni matangazo yanayoambatana na makhofisho. Allaah (Ta'ala) amesema:

لَيْسَ لَهُمْ مِّنْ دُونِهِ وَايٌّ وَلَا شَفِيعٌ لَّهُمْ يَتَّقُونَ

“... hawana badala Yake mlinzi wala mwombezi ili wapate kumcha...”

Huu ni uombezi batili. Waja hawatokuwa na walinzi wala waombezi kabisa isipokuwa wale atakaowaridhia Allaah. Makafiri wanadhani kuwa watakuwa na walinzi na waombezi ambao watawaokoa kutokamana na Moto kwa sababu walikuwa wakiwaabudu. Kwa sababu hiyo ndio maana walikuwa wakiwaabudu badala ya Allaah:

هَؤُلَاءِ شُفَعَاؤُنَا عِنْدَ اللَّهِ

“Hawa ni waombezi wetu mbele ya Allaah.” (Yuunus 10:18)

مَا نَعْبُدُهُمْ إِلَّا لِيُقَرِّبُونَا إِلَى اللَّهِ زُلْفَىٰ

“Hatuwaabudu isipokuwa ili wapate kutukurubisha kwa Allaah karibu” (**az-Zumar 39:03**)

Ndipo Allaah akabainisha kuwa watu hawatokuwa na walinzi wala waombezi badala Yake na kwamba uombezi huu wa makafiri ni batili na kwamba uombezi wa haki ni ule ambao Allaah atawaidhinisha Mitume na mawalii kuwaombea wapwekeshaji na waumini na sio makafiri na wanafiki. Allaah (Ta'ala) amesema:

لَعَلَّهُمْ يَتَّقُونَ

“... ili wapate kumcha.”

Bi maana kwa ajili wamche Allaah na wawe na msimamo juu ya dini Yake pale watapotambua kuwa hakuna uombezi wala mlinzi yeyote badala ya uombezi na ulinzi Wake. Kwa ajili hiyo ndio maana wanatakiwa kumuabudu Yeye pekee na watahadhari kutokamana na ghadhabu Zake.

2-

قُلْ لِلَّهِ الشَّفَاعَةُ جَمِيعًا

“Sema: “Uombezi wote ni wa Allaah.”

Waambie watu kwamba uombezi wote ni wa Allaah. Kabla ya hapo amewakemea wale wenye kudai kuwa na waombezi badala ya Allaah. Wakimaanisha waombezi wao kuwa masanamu, mawe na waungu wao wengine. Allaah akawakanushia hilo:

فَمَا تَنْفَعُهُمْ شَفَاعَةُ الشَّافِعِينَ

“Basi haitowafaa uombezi wowote wa waombezi.” (**al-Muddaththir 74:48**)

وَأَنْذِرْ بِهِ الَّذِينَ يَخَافُونَ أَنْ يُخْشَرُوا إِلَىٰ رَبِّهِمْ ۗ لَيْسَ لَهُمْ مَن دُونِهِ وَيٰٓأَيُّهَا الَّذِينَ يَتَّقُونَ

“Na waonye kwayo [Qur-aan] wale wanaokhofu ya kwamba watakusanywa kwa Mola wao; hawana badala Yake mlinzi wala mwombezi ili wapate kumcha.”

Uombezi ni Wake pekee. Mitume na waja wema watashufai kwa idhini Yake. Anampa idhini yule Amtakaye. Hivyo ni wajibu kumuomba Yeye na kumuomba ampe idhini Mtume na waja wema wakuombezi.

Hakuna ubaya kumuombezi uombezi aliyehai wakati wa uhai wake. Mfano wa hilo ni kumuomba mtu mwema akuombezi kwa Allaah akusamehe au akuongoze. Ama kuhusu masanamu, wafu, viumbe visivyoonekana, kama mfano wa Malaika, hawatakiwi kuombwa mambo hayo. Kwa sababu hawatambui hali yako. Hawajui mambo yaliyofichikana tofauti na wanavyoamini wajinga na makafiri.

3-

مَنْ ذَا الَّذِي يَشْفَعُ عِنْدَهُ إِلَّا بِإِذْنِهِ

“Nani huyu ambaye anashufai mbele Yake bila ya idhini Yake?”

4-

وَكَمْ مِّن مَّلَكٍ فِي السَّمَاوَاتِ لَا تُغْنِي شَفَاعَتُهُمْ شَيْئًا إِلَّا مَن بَعَدَ أَنْ يَأْذَنَ اللَّهُ لِمَن يَشَاءُ وَيَرْضَىٰ

“Na Malaika wangapi mbinguni haitowafaa kitu chochote uombezi wao isipokuwa baada ya kuwa Allaah ametolea idhini kwa Amtakaye na kumridhia.”

5-

قُلْ ادْعُوا الَّذِينَ زَعَمْتُمْ مِّنْ دُونِ اللَّهِ لَا يَمْلِكُونَ مِثْقَالَ ذَرَّةٍ فِي السَّمَاوَاتِ وَلَا فِي الْأَرْضِ وَمَا لَهُمْ فِيهِمَا مِنْ شِرْكٍَ وَمَا لَهُ مِنْهُمْ مِّنْ ظَهِيرٍ وَلَا تَنْفَعُ الشَّفَاعَةُ عِنْدَهُ إِلَّا لِمَنْ أَذِنَ لَهُ حَتَّىٰ إِذَا فُزِّعَ عَن قُلُوبِهِمْ قَالُوا مَاذَا قَالَ رَبُّكُمْ قَالُوا الْحَقُّ وَهُوَ الْعَلِيُّ الْكَبِيرُ

”Sema: “Waombeni wale mnadai [kuwa ni waungu] badala ya Allaah. Hawamiliki uzito wa atomu mbinguni wala ardhini na wala wao hawana humo ushirika na wala Hana msaidizi miongoni mwao.” Na wala hautofaa uombezi mbele Yake isipokuwa kwa yule Aliyempa idhini. Mpaka itakapoondolewa fazaiko nyoyoni mwao [baada ya kuzimia]; watasema [wakiulizana]: “Amesema nini Mola wenu?” – waseme: “Ya haki; Naye yujuu, Mkubwa kabisa.” (Saba’ 34:23)

Allaah (Subhaanah) amebainisha kwamba hakuna yeyote atakayeombea mbele Yake isipokuwa baada ya idhini Yake na kwamba hatoombewa yeyote isipokuwa kwa yule Aliyemridhia. Hata Malaika hawamiliki uombezi. Bali ni Allaah pekee ndiye anamiliki. Ikiwa hiyo ndio hali ya Malaika, Manabii na Mitume kwamba hawawezi kushufai isipokuwa baada ya Allaah kuwapa idhini na kumridhia yule mwombewaji, basi waja wema, watoto na wengineo wana haki zaidi ya kutoweza kufanya hivo.

Wale waliofungamana na watu hawa ambao wanawaomba badala ya Allaah wanafungamana nao kwa sababu ya mambo mane ambayo kayabainisha Allaah:

قُلْ ادْعُوا الَّذِينَ زَعَمْتُمْ مِّنْ دُونِ اللَّهِ لَا يَمْلِكُونَ مِثْقَالَ ذَرَّةٍ فِي السَّمَاوَاتِ وَلَا فِي الْأَرْضِ وَمَا لَهُمْ فِيهِمَا مِنْ شِرْكٍَ وَمَا لَهُ مِنْهُمْ مِّنْ ظَهِيرٍ وَلَا تَنْفَعُ الشَّفَاعَةُ عِنْدَهُ إِلَّا لِمَنْ أَذِنَ لَهُ حَتَّىٰ إِذَا فُزِّعَ عَن قُلُوبِهِمْ قَالُوا مَاذَا قَالَ رَبُّكُمْ قَالُوا الْحَقُّ وَهُوَ الْعَلِيُّ الْكَبِيرُ

”Sema: “Waombeni wale mnadai [kuwa ni waungu] badala ya Allaah. Hawamiliki uzito wa atomu mbinguni wala ardhini na wala wao hawana humo ushirika na wala Hana msaidizi miongoni mwao.” Na wala hautofaa uombezi mbele Yake isipokuwa kwa yule Aliyempa idhini. Mpaka itakapoondolewa fazaiko nyoyoni mwao [baada ya kuzimia]; watasema [wakiulizana]: “Amesema nini Mola wenu?” – waseme: “Ya haki; Naye yujuu, Mkubwa kabisa.”

1- Mamlaka. Wanadhani kuwa wanamiliki kitu. Uhakika wa mambo Allaah ndiye ana mamlaka yote.

2- Ushirika. Wanadhani kuwa ni washirika wa Allaah.

3- Msaidizi. Wanadhani kuwa wanamsaidia Allaah, jambo ambalo ni batili.

4- Uombezi. Wanadahni kuwa waungu wao watawaombea.

Allaah akabainisha kwamba hakuna yeyote awezaye kuombea isipokuwa kwa idhini Yake na kwamba hakuna uombezi wenye kujitegemea kama hali ilivyo duniani. Duniani mtu anaweza kukubali uombezi wa mwingine kwa sababu ya kumuogopa na kumuhitajia, mambo ambayo Allaah ametakasika nayo.

6- 'Abul-'Abbaas amesema:

“Allaah amekanusha vyote visivyokuwa Yeye ambavyo washirikina wamejiambatanisha navyo. Amekanusha kwa yeyote badala Yake kuwa na mamlaka au ushirika wowote wa hilo badala Yake au msaidizi wowote kwa Allaah. Hapakubaki isipokuwa uombezi. Hivyo amebainisha ya kwamba hautomfaa yeyote isipokuwa kwa yule ambaye Mola kampa idhini. Kama alivyosema (Ta'ala):

وَلَا يَشْفَعُونَ إِلَّا لِمَنْ ارْتَضَىٰ

“Na wala hawamuombei yeyote yule isipokuwa kwa yule ambaye Amemridhia.”
(al-Anbiyaa' 21:28)

Uombezi huu ambao washirikina wanatumai umekanushwa kuwepo kwake siku ya Qiyaamah, kama ulivyokanushwa na Qur-aan. Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) ameeleza kwamb atakuja na kumsujudia Mola wake na kumhimidi. Hatoanza kuombea moja kwa moja. Baada ya hapo ndipo Ataambiwa:

“Nyanyua kichwa chako. Sema na utasikizwa. Omba na utapewa. Shufai utakubaliwa”

Abul-'Abbaas ni Shaykh-ul-Islaam [Ibn Taymiyyah]. Uombezi huu wanaotarajia washirikina siku ya Qiyaamah umekanushwa, kama ilivyotajwa katika Qur-aan. Baadhi yao wanafikiria kwamba masanamu na waungu wao watawaombea kilazima, kwamba hawatohitajia idhini, uombezi wao utakubaliwa, kwamba wataingia Peponi kwa sababu yao na kwamba watasalimishwa kutokamana na Moto. Haya ni kwa haki ya yule ambaye anaamini Aakhirah. Kuhusu yule asiyeamini Aakhirah wanawaomba kwa ajili ya mambo ya kidunia. Malengo yao ya uombezi ni manufaa ya kidunia. Waarabu wengi walikuwa hawaamini Aakhirah.

7- Abu Hurayrah (Radhiya Allaahu 'anh) alimuuliza Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam):

“Ni nani katika watu atakayekuwa na furaha zaidi kwa uombezi wako?” Akasema (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam): “Ni yule atakayesema: “Hapana mwabudiwa wa haki isipokuwa Allaah” akiwa ni wenye kutakasika kutoka moyoni mwake.”

Kwa hivyo uombezi huu ni kwa wale wenye Ikhlaasw baada ya idhini ya Allaah. kwa idhini ya Allaah na hautokuwa kwa wale waliomshirikisha Allaah. Ukweli wa mambo ni kwamba Allaah (Subhaanah) ndiye atakayetoa fadhilah Zake kuwapa wale wenye Ikhlaasw na awasamehe kupitia du'aa za waombeaji wataopewa idhini ya kushufai kwa ajili ya kumkirimu na kufikia cheo chenye kusifiwa. Uombezi ambao umekanushwa na Qur-aan ni ule ambao ndani yake kuna shirki. Kwa ajili hii ndio maana uombezi umethibiti kwa idhini Yake katika

maeneo mbalimbali. Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amebainisha ya kwamba hautokuwa isipokuwa kwa watu wa Tawhiyd na Ikhlaasw."

Watu wataokuwa na furaha zaidi kwa sababu ya uombezi ni wapwekeshaji. Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

"Kila Mtume ana maombi yenye kuitikiwa. Maombi yangu nimeyaweke kwa ajili ya Ummah wangu siku ya Qiyaamah. Atayapata - Allaah akitaka - katika Ummah wangu yule mwenye kufa na huku hamshirikishi na Allaah na chochote."⁷¹

Amebainisha (Swalla Allaahu 'alayhi w sallam) kwamba hautomfaa katika Ummah wake isipokuwa yule aliyekuwa akimpwekesha Allaah. Kuhusu yule aliyekufa katika dini nyingine mbali na Uislamu hatopata uombezi wowote. Uhakika wa mambo Allaah ndiye atatoa fadhilah Zake kuwapa watu wa Ikhlaasw na hivyo awasemehe.

Ametaja nafasi yenye kusifiwa. Ni yenye kuthibiti kwa Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam). Ni nafasi ambayo atasifiwa na wale wa mwanzo na wa mwisho. Allaah (Ta'ala) amesema:

وَمِنَ اللَّيْلِ فَتَهَجَّدْ بِهِ نَافِلَةً لَّكَ عَسَىٰ أَنْ يَبْعَثَكَ رَبُّكَ مَقَامًا مَّحْمُودًا

"Na amka sehemu ya usiku na uswali ni ziada ya sunnah kwako; bila shaka Mola wako atakuinua cheo kinachosifika." (**al-Israa' 17:79**)

Cheo chenye kusifiwa ni ule uombezi mkubwa kwa mujibu wa maoni sahihi. Imesemekana vilevile kwamba nafasi yenye kusifiwa ni kwamba Allaah atamkalisha pamoja Naye juu ya 'Arshi Yake siku ya Qiyaamah. Hata hivyo

⁷¹ al-Bukhaariy (5945).

usahihi wa Hadiyth hii unatakiwa kutazamwa vizuri. Maoni yanayotambulika ni yale ya kwanza.

Uombezi ni fadhilah anayopewa yule mwenye kuombewa. Ni fadhilah ya Allaah anayompa yule mwenye kuombewa ili aweze kuingia Peponi. Huu ndio uhakika wa uombezi. Hapa kuna Radd kwa waabudu makaburi. Bali wao ni wenye kunyimwa uombezi kwa sababu wanafuata ule uombezi uliokanushwa.

18. Mlango kuhusu maneno Yake (Ta'ala) ”Hakika wewe huwezi kumwongoza umpendaye”

Shaykh-ul-Islaam Muhammad bin 'Abdil-Wahhaab (Rahimahu Allaah) amesema:

1- Allaah (Ta'ala) amesema:

إِنَّكَ لَا تَهْدِي مَنْ أَحْبَبْتَ

”Hakika wewe huwezi kumwongoza umpendaye.” (al-Qaswasw 28:56)

2- Imesihi kupokelewa kutoka kwa Ibn-ul-Musayyab ambaye ameeleza kutoka kwa baba yake aliyesimulia:

”Wakati mauti yalipomfikia Abu Twaalib alimjia Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) na alikuwepo 'Abdullaah bin Abiy Umayyah na Abu Jahl. Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) akamwambia: “Ewe ami yangu! Sema: “Hapana mwabudiwa wa haki isipokuwa Allaah”. Ni maneno ambayo nitakutetea kwayo mbele ya Allaah. Wakamwambia: “Hivi kweli unataka kuacha dini ya 'Abdul-Muttwalib?” Akamrudilia Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) nao wawili wakamrudilia. Mwishowe neno lake la mwisho alilosema ni kwamba yeye yuko katika dini ya 'Abdul-Muttwalib na akakataa kusema kwamba hapana mwabudiwa wa haki isipokuwa Allaah. Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) akasema: “Nitakuombea msamaha midhali sijakatazwa.” Ndipo Allaah ('Azza wa Jall) akateremsha:

مَا كَانَ لِلنَّبِيِّ وَالَّذِينَ آمَنُوا أَنْ يَسْتَغْفِرُوا لِلْمُشْرِكِينَ

“Haimpasii Nabii na wale walioamini kuwaombee msamaha washirikina.” (**at-Tawbah 09:113**)

Allaah akateremsha pia kuhusu Abu Twaalib:

إِنَّكَ لَا تَهْدِي مَنْ أَحْبَبْتَ وَلَكِنَّ اللَّهَ يَهْدِي مَنْ يَشَاءُ

“Hakika wewe huwezi kumwongoza umpendaye lakini Allaah ndiye anamwongoza mtakaye.” (**al-Qaswasw 28:56**)

MAELEZO

Katika mlango huu alichokusudia mtunzi wa kitabu ni kwamba Mitume, akiwemo mbora wao Muhammad (Swalla Allaahu ‘alayhii wa sallam) hawawezi kujiamualia lolote isipokuwa yale aliyowapa Allaah. Wao hawawezi kuwaongoza watu isipokuwa wale walio-ongozwa na Allaah. Wao ni wenye kuongozwa na wako chini ya uendeshaji Wake. Hawawezi kufanya chochote isipokuwa kwa msaada wa Allaah. Kwa ajili hiyo hawasilihi kuabudiwa badala ya Allaah. Wao ni kama watu wengine wote. Lakini hata hivyo Allaah amewafadhilisha kwa ujumbe na unabii. Wao wana ziada ya utukufu, lakini hili haliwafanyi kuwa washirika wa Allaah katika kuendesha ulimwengu, kujua mambo yaliyofichikana, kumwongoza wampendaye na mengineyo. Ikiwa Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) hakuweza kuwaongoza baba zake wadogo Abu Twaalib na Abu Lahab basi hiyo ni dalili inayoonyesha kwamba kuongoka kuko mikononi mwa Allaah. Kwa hivyo ni wajibu kumuomba Yeye (Subhaanah) pekee uongofu. Mlango huu unazungumzia juu ya kwamba uongofu (ambao una maana ya kukubali haki na kuiridhia) hakuna yeyote anayeumiliki isipokuwa Allaah.

Ama uongofu wenye maana ya kuelekeza na kubainisha, uko mikononi mwa Mitume na wafuasi wake katika wanachuoni na walinganizi. Allaah (Ta’ala) amesema:

وَلَكِنْ جَعَلْنَاهُ نُورًا نَهْدِي بِهِ مَنْ نَشَاءُ مِنْ عِبَادِنَا ۗ وَإِنَّكَ لَتَهْدِي إِلَى صِرَاطٍ مُسْتَقِيمٍ

“Lakini Tumeifanya ni nuru tunaongoa kwayo tumtakaye katika waja Wetu; na hakika wewe bila shaka unaongoza kuelekea njia iliyonyooka.” (ash-Shuura 42:52)

Bi maana unaelekeza, unaita na kulingania katika njia iliyonyooka. Lakini hata hivyo hawawezi kuziathiri nyoyo ili ziweze kukubali haki. Bali Allaah pekee ndiye anaweza hilo.

2- Imesihi kupokelewa kutoka kwa Ibn-ul-Musayyab ambaye ameeleza kutoka kwa baba yake aliyesimulia:

“Wakati mauti yalipomfikia Abu Twaalib alimjia Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) na alikuwepo ‘Abdullaah bin Abiy Umayyah na Abu Jahl. Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) akamwambia: “Ewe ami yangu! Sema: “Hapana mwabudiwa wa haki isipokuwa Allaah”. Ni maneno ambayo nitakutetea kwayo mbele ya Allaah. Wakamwambia: “Hivi kweli unataka kuacha dini ya ‘Abdul-Muttwalib?” Akamrudilia Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) nao wawili wakamrudilia. Mwishowe neno lake la mwisho alilosema ni kwamba yeye yuko katika dini ya ‘Abdul-Muttwalib na akakataa kusema kwamba hapana mwabudiwa wa haki isipokuwa Allaah. Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) akasema: “Nitakuombea msamaha midhali sijakatazwa.” Ndipo Allaah (‘Azza wa Jall) akateremsha:

مَا كَانَ لِلنَّبِيِّ وَالَّذِينَ آمَنُوا أَنْ يَسْتَغْفِرُوا لِلْمُشْرِكِينَ

“Haimpasii Nabii na wale walioamini kuwaombe msamaha washirikina.”

Allaah akateremsha pia kuhusu Abu Twaalib:

إِنَّكَ لَا تَهْدِي مَنْ أَحْبَبْتَ وَلَكِنَّ اللَّهَ يَهْدِي مَنْ يَشَاءُ

"Hakika wewe huwezi kumwongoza umpendaye lakini Allaah ndiye anamwongoza mtakaye."

al-Musayyab pia inaweza kuandikwa al-Musayyib, lakini lililoenea zaidi kwa wanachuoni wa Hadiyth ni al-Musayyab.

Wakati Abu Twaalib kulipoonekana kwake alama za kutaka kukata roho, Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) alimwendea kumlingania ulinganizi maalum. Hapo kabla alikuwa ameshamlingani sana. Pamoja na kwamba alijua kuwa ni haki hakukubaliwa kwa madai kwamba eti asije kutukanywa na watu wake. Kwa ajili hiyo akasema katika mashairi yake:

Nilijua kuwa dini ya Muhammad

ndio dini bora ya viumbe

Isingekuwa kwa ajili ya lawama na kuogopwa kutukanywa

basi ungeniona ni mwenye kufunguka waziwazi na kukubali

Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema "Hapana mwabudiwa wa haki isipokuwa Allaah". Ni maneno ambayo nitakutetea kwayo mbele ya Allaah." Bi maana ningekushuhudilia na kufanya niwezayo kukuokoa.

Wakasema "Hivi kweli unataka kuacha dini ya 'Abdul-Muttwalib?" Bi maana 'ibaadah ya kuabudu mizimu na masanamu.

Hatimaye maneno ya mwisho ikawa kwamba yeye yuko katika dini ya 'Abdul-Muttwalib. Kwa sababu alikuwa alikuwa ameshahukumiwa kwamba atakuwa na mwisho mbaya. Allaah hakutaka kumwongoza kwa sababu ya hekima kubwa. Hivyo akafa katika dini ya watu wake. Ni kweli. Kumekuja Hadiyth Swahiyh zinazosimulia jinsi Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) alimuona namna anavyozama kwenye Moto ambapo akamuombea na akatumbukizwa

kwenye Moto wa afueni ambapo ubongo wake unachemka⁷². Maoni yanayosema kuwa aliingia katika Uislamu hayana msingi wowote.

Hadiyth inathibitisha kwamba Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) hawezi kumwongoza kiumbe yeyote. Aayah:

إِنَّكَ لَا تَهْدِي مَنْ أَحْبَبْتَ وَلَكِنَّ اللَّهَ يَهْدِي مَنْ يَشَاءُ

"Hakika wewe huwezi kumwongoza umpendaye lakini Allaah ndiye anamwongoza mtakaye."

ni liwazo kwa Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) na waislamu wengine ambao ndugu zao hawakusilimu.

⁷² al-Bukhaariy (3883) na Muslim (209).

19. Kuchupa mipaka kwa waja wema ndio lililopelekea kukufuru kwa wanaadamu

Shaykh-ul-Islaam Muhammad bin 'Abdil-Wahhaab (Rahimahu Allaah) amesema:

1- Allaah ('Azza wa Jall) amesema:

يَا أَهْلَ الْكِتَابِ لَا تَغْلُوا فِي دِينِكُمْ

“Enyi Ahl-ul-Kitaab! Msipindukie mipaka katika dini yenu.” (an-Nisaa’ 04:171)

2- Imesihi kupokelewa kupitia kwa Ibn 'Abbaas (Radhiya Allaahu 'anhumaa) ambaye amesema kuhusiana na maneno ya Allaah (Ta'ala):

وَقَالُوا لَا تَذَرُنَّ آلِهَتَكُمْ وَلَا تَذَرُنَّ وَدًّا وَلَا سُوَاعًا وَلَا يَغُوثَ وَيَعُوقَ وَنَسْرًا

“Wakasema: “Msiwaache waungu wenu - na wala msimwache Wadd na wala Suwaa’ na wala Yaghuuth na Ya’uuq na Nasr!” (Nuuh 71:23)

“Haya ni majina ya waja wema katika watu wa Nuuh. Walipokufa shaytwaan aliwapendezea watu wake watengeneze masanamu na kuyaweka mahali ambapo walikuwa wakikaa na kuyapa majina yao. Wakafanya hivyo na hawakuyaabudu mpaka walipofariki watu wale na elimu ikasahaulika, hivyo ndipo wakaabudiwa.”

3- Ibn-ul-Qayyim (Rahimahu Allaah) amesema:

“Wengi katika Salaf wamesema: “Walipokufa wakawa ni wenye kukaa kwa muda mrefu kwenye makaburi yao kisha wakatengeneza masanamu yenye sura zao. Kulipopita muda mrefu ndipo wakaanza kuwaabudu.”

4- 'Umar (Radhiya Allaahu 'anh) ameeleza kwamba Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Msipindukie kwangu kama walivyopindukia manaswara kwa 'Iysaa mwana wa Maryam. Hakika mimi ni mja. Hivyo semeni “Mja wa Allaah na Mtume Wake”.”⁷³

Ameipokea al-Bukhaariy na Muslim.

5- Ameeleza kwamba Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Nakutahadharisheni na kupetuka mipaka. Hakika kilichowafanya kuangamia waliokuwa kabla yenu ni kupetuka mipaka.”⁷⁴

6- Muslim amepokea kutoka kwa Ibn Mas'uud (Radhiya Allaahu 'anh) ambaye amesimulia ya kwamba Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Wameangamia waliochupa mipaka.”

Alisema hivyo mara tatu⁷⁵.

MAELEZO

Mtunzi wa kitabu amebainisha sababu iliowapelekea watu wengi kukufuru ni kuchupa mipaka kwa watu wema. Zipo sababu zengine vilevile kama hasadi na ukandamizaji. Kwa ujumla ni kwamba watu hawa waliwapenda Mitume na waja wema sana kiasi cha kwamba wakachupa mipaka kwao na wakakufuru.

⁷³ al-Bukhaariy (3445).

⁷⁴ an-Nasaa'iy (3057), Ibn Maajah (3029), Ahmad (1851) na Ibn Hibbaan. Swahiyh kwa mujibu wa al-Albaaniy katika “Swahiyh Sunan Ibn Maajah” (2455).

⁷⁵ Muslim (2670).

1- Allaah (‘Azza wa Jall) amesema:

يَا أَهْلَ الْكِتَابِ لَا تَغْلُوا فِي دِينِكُمْ

“Enyi Ahl-ul-Kitaab! Msipindukie mipaka katika dini yenu.” (an-Nisaa’ 04:171)

Hapa wanazungumzishwa manaswara na mayahudi, lakini manaswara ni wenye kupindukia zaidi.

Malengo ya mlango huu ni matahadharisho ya kupindukia katika kuwapenda Mitume na waja wema. Kuwapenda kwao ni dini kwa vile Allaah amesema:

لَا تَغْلُوا فِي دِينِكُمْ

“Msipindukie mipaka katika dini yenu.”

Kupenda na kuchukua kwa ajili ya Allaah ni katika dini. Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) amesema:

“Haamini mmoja wenu mpaka Allaah na Mtume Wake wawe ni wenye kupendwa zaidi kwake kuliko mwingine yeyote.”

Hata hivyo mapenzi haya hayatakiwi kuwa na upindukaji. Mapenzi haya yanatakiwa yawe kwa sampuli ya kuwafuata na kuwatii, sio kuwaasi na kuwaabudu badala ya Allaah. Kadhalika mapenzi ya kuwapenda wanachuoni na waja wema yanatakiwa yawe kwa kuwatakiya radhi na kufuata mwenendo wao. Kwa msemu mwingine ni kwamba mapenzi yanatakiwa yawe ya Kishari’ah.

2- Imesihi kupokelewa kupitia kwa Ibn ‘Abbaas (Radhiya Allaahu ‘anhumaa) ambaye amesema kuhusiana na maneno ya Allaah (Ta’ala):

وَقَالُوا لَا تَذَرُنَّ آلِهَتَكُمْ وَلَا تَذَرُنَّ وَدًّا وَلَا سُوَاعًا وَلَا يَئُوثَ وَيَعُوقَ وَنَسْرًا

“Wakasema: “Msiwaache waungu wenu - na wala msimwache Wadd na wala Suwaa’ na wala Yaghuuth na Ya’uuq na Nasr!”

“Haya ni majina ya waja wema katika watu wa Nuuh. Walipokufa shaytwaan aliwapendezea watu wake watengeneze masanamu na kuyaweka mahali ambapo walikuwa wakikaa na kuyapa majina yao. Wakafanya hivyo na hawakuyaabudu mpaka walipofariki watu wale na elimu ikasahaulika, hivyo ndipo wakaabudiwa.”

Shaytwaan aliwatia wasiwasi watu wa Nuuh ya kutengeneza picha zao ili wawakumbuke katika ‘ibaadah. Walipofariki ndipo shaytwaan akawaenda kwa wale waliokuwepo wakati ule na kuwaambia kwamba baba zao walikuwa wakiwaabudu na wakiwaomba uokozi. Ndipo wakawaabudu. Hii ndio sababu iliopelekea katika kuvuka mipaka. Kumewafanya watu kupotea na kuwaangamiza duniani na Aakhirah.

Elimu kusahulika ina maana kwamba ilipotea. Katika upokezi mwingine imekuja kwamba ilifutwa. Elimu ilipotea na wakaja watu wasiojua lolote. Matokeo yake wakatumbukia katika shirki. Katika Hadiyith kuna dalili inayothibitisha juu ya umuhimu wa elimu na kwamba inapiga vita ujinga. Elimu inapoondoka watu wanatumbukia katika batili na ujinga. Ndani yake kuna fadhilah za elimu ya Kishari’ah.

3- Ibn-ul-Qayyim (Rahimahu Allaah) amesema:

“Wengi katika Salaf wamesema: “Walipokufa wakawa ni wenye kukaa kwa muda mrefu kwenye makaburi yao kisha wakatengeneza masanamu yenye sura zao. Kulipopita muda mrefu ndipo wakaanza kuwaabudu.”

Maneno yake yanaweza kuwa na maana kwamba wale waliotengeneza masanamu yenye sura zao ndio wale waliowaabudu kulipopita muda na hali zikabadilika. Anaweza kuwa anamaanisha vilevile kwamba waliowaabudu ni

kizazi kilichokuja baada yao. Bid'ah shari yake ni kubwa kwa yule mwenye kuizua na kwa wale wataokuja baada yake.

4- 'Umar (Radhiya Allaahu 'anh) ameeleza kwamba Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Msipindukie kwangu kama walivyopindukia manaswara kwa 'Iysaa mwana wa Maryam. Hakika mimi ni mja. Hivyo semeni “Mja wa Allaah na Mtume Wake”.”

Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) anatahadharisha juu ya kusifu kwa kupindukia na kueleza kusikofaa. Mfano wa hayo ni kama mtu kusema kwamba anajua mambo yaliyofichikana au kwamba anaendesha ulimwengu. Anatakiwa kusifiwa kwa mambo yanayotakikana na kwa haki. Mfano wa hayo ni kama vile kusema kwamba yeye ndiye Mtume bora, kiumbe bora, Mtume wa mwisho, mfikishaji wa ujumbe na mfano wa hayo. Miongoni mwa kuvuka mipaka ni yale aliyosema al-Buswayriy kwamba Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) anatakiwa kusifiwa kwa njia zote isipokuwa tu mtu asiseme kuwa ni mwana wa Allaah. Huu ni ujinga na upotevu. Si Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) wala mwengine yeyote haifai kumsifu kwa sifa alizopwekeka nazo Allaah pekee. Wakati 'Aishah (Radhiya Allaahu 'anhaa) alipopoteza cheni yake akaipata chini ya ngamia. Si Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) wala yeyote katika Maswahabah wake hakuna aliyejua wapi ilipo. Ni dalili inayoonyesha kuwa hawajui mambo yaliyofichikana isipokuwa tu yale aliyowafunulia Allaah.

5- Ameeleza kwamba Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Nakutahadharisheni na kupetuka mipaka. Hakika kilichowafanya kuangamia waliokuwa kabla yenu ni kupetuka mipaka.”

Haya yalisemwa na Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) katika hajj ya kuaga wakati alipomwamrisha Ibn 'Abbaas (Radhiya Allaahu 'anhumaa) vijiwe

saba. Hadiyth ameipokea Ahmad na baadhi ya waandishi wa Sunan. Cheni ya wapokezi wake ni nzuri na Hadiyth ni Swahiyh.

Kuvuka mipaka na kuongeza. Hivyo katika mazingira haya itahusiana na kuongeza katika dini yale ambayo Allaah hakuyaidhinisha. Ni wajibu kukomeka katika yale yaliyoko katika Qur-aan na Sunnah pasi na kuongeza wala kupunguza. Watu wanapozidisha watatumbukia katika shirki na Bid'ah.

6- Muslim amepokea kutoka kwa Ibn Mas'ud (Radhiya Allaahu 'anh) ambaye amesimulia ya kwamba Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Wameangamia waliochupa mipaka.”

Alisema hivyo mara tatu.

Mwenye kuchupa mipaka ni yule mwenye kupindukia na mwenye kujikakama anayezidisha katika mambo. Kimsingi maana yake ni kujikakama wakati wa kuongea. Hivo ndivyo anavyokuwa mwenye kuvuka mipaka katika mambo. Mtu kama huyu ni mwenye kujikakama. Ni wajibu kwa mtu kuwa kati na kati anapozungumza na katika mambo mengine yote. Si ruhusa kwa mtu yeyote kuzidisha katika dini wala kupunguza. Ni mamoja awe Malaika, raisi, mwanachuoni wala mwengine yeyote.

20. Makatazo ya kuabudu makaburi au kumuabudu Allaah kwenye kaburi la mtu mwema

Shaykh-ul-Islaam Muhammad bin 'Abdil-Wahhaab (Rahimahu Allaah) amesema:

1- Imesihi kupokelewa kutoka kwa 'Aishah (Radhiya Allaahu 'anhaa) ambaye amesimulia kwamb Ummah Salamah (Radhiya Allaahu 'anhaa) alimtajia Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) kanisa aliyoiona Habashah na namna ilivyokuwa mapicha. Akasema:

“Hao ndio wale ambao wanapofiwa na mtu mwema au mja mwema, basi hujenga juu ya kaburi lake msikiti na huchora ndani yake picha hiyo. Hao ndio viumbe waovu kabisa mbele ya Allaah.”⁷⁶

2- Watu hawa wamekusanya kati ya fitina mbili; fitina ya makaburi na fitina ya masanamu.

3- al-Bukhaariy na Muslim kumepokelewa ya kwamba 'Aishah (Radhiya Allaahu 'anhaa) amesema vilevile:

“Wakati Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) alipokuwa anataka kufa alikuwa akijifunika kitambara usoni mwake. Anapohisi joto hukifunua na anasema akiwa katika hali hiyo: “Laana ya Allaah iwe juu ya mayahudi na manaswara. Wameyafanya makaburi ya Mitume wao kuwa ni sehemu ya kuswalia.” Mtume akitahadharisha yale waliyokuwa wakiyafanya. Lau

⁷⁶ al-Bukhaariy (434) na Muslim (528).

sikuchelea hilo basi kaburi lake lingewachwa nje, isipokuwa yeye alikhofia lisije kufanywa kuwa ni mahali pa kuswalia.”⁷⁷

Ameipokea al-Bukhaariy na Muslim.

4- Muslim amepokea kupitia kwa Jundub bin 'Abdillaah (Radhiya Allaahu 'anh) ambaye amesimulia kwamba amemsikia Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) kabla ya kufa kwake kwa siku tano akisema:

“Hakika mimi najitakasa kwa Allaah kuwa na kipenzi wa karibu katika nyinyi. Kwani hakika Allaah amenifanya kuwa kipenzi Wake wa karibu kama alivyomfanya Ibraahim kuwa kipenzi Wake wa karibu. Na lau ningemchukua yeyote katika Ummah wangu kuwa kipenzi wangu wa karibu, basi ningelimfanya Abu Bakr kuwa kipenzi wangu wa karibu. Tanabahini! Hakika wale waliokuwa kabla yenu walikuwa wakiyafanya makaburi ya Mitume wao kuwa mahali pa kuswalia. Tanabahini! Msiyafanye makaburi kuwa mahali pa kuswalia. Hakika mimi nawakatazeni na hilo.”⁷⁸

Amekataza hilo mwishoni wa uhai wake. Baada ya makatazo haya halafu akamlaani yule mwenye kufanya hivo. Kuswali kwenye makaburi kunaingi katika hayo hata kama hakukujengwa juu yake msikiti. Hii ndio maana ya maneno yake:

“... isipokuwa yeye alikhofia lisije kufanywa kuwa ni mahali pa kuswalia.”

Hakika Maswahabah (Radhiya Allaahu 'anhum) hawakujenga msikiti pembezoni mwa kaburi lake. Kila sehemu ambayo kunaswaliwa basi kunakuwa kumefanywa msikiti. Bali kila nafasi ambapo kunaswaliwa ndio kunaitwa msikiti. Kama alivyosema (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam):

⁷⁷ al-Bukhaariy (436) na Muslim (531).

⁷⁸ Muslim (532).

“Nimefanyiwa ardhi yote kuwa msikiti na safi.”⁷⁹

5- Ahmad amepokea kwa cheni ya wapokezi nzuri kupitia kwa Ibn Mas'ud (Radhiya Allaahu 'anh) kutoka kwa Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) ambaye amesema:

“Hakika waovu katika watu ni wale ambao Qiyaamah kitawakuta nao wako hai na wale wenye kuyafanya makaburi kuwa ni mahali pa kuswalia.”⁸⁰

Ameipokea Abu Haatim katika “as-Swahiyyh” yake.

MAELEZO

Mlango huu ni mkubwa kama ule uliokuwa kabla yake. Dalili zinazokemea. Ikiwa dalili zimekuja zikikaripia kumuabudu Allaah kwenye makaburi ya waja wema, vipi ikiwa wataabudiwa na wakafanywa kuwa ni waungu badala ya Allaah? Katika hali hii makemeo yanakuwa na nguvu zaidi. Kwa sababu katika hali ya kwanza kitendo kinapelekea katika shirki na katika hali ya pili kitendo chenyewe ni shirki kubwa.

1- Imesihi kupokelewa kutoka kwa 'Aaishah (Radhiya Allaahu 'anhaa) ambaye amesimulia kwamb Ummah Salamah (Radhiya Allaahu 'anhaa) alimtaja Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) kanisa aliyoiona Habashah na namna ilivyokuwa mapicha. Akasema:

“Hao ndio wale ambao wanapofiwa na mtu mwema au mja mwema, basi hujenga juu ya kaburi lake msikiti na huchora ndani yake picha hiyo. Hao ndio viumbe waovu kabisa mbele ya Allaah.”

⁷⁹ al-Bukhaariy (335) na Muslim (521).

⁸⁰ Ahmad (3844), Ibn Khuzaymah (789), Ibn Hibbaan (6847) na at-Twabaraaniy (10413). Swahiyyh kwa mujibu wa al-Albaaniy katika “ath-Thamar al-Mustatwab” (1/363).

Walipohama kwenda Habashah waliona kanisa likiadhimishwa kwa jina “Kanisa la Maria”. Ndani yake kulikuwa mapicha na mapambo. Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) amesema:

“Hao ndio wale ambao wanapofiwa na mtu mwema...”

Hapa kunabainishwa hali ya manaswara na kwamba ni wenye kuchupa mipaka kwa wafu wao. Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) amesema:

“... na huchora ndani yake picha hiyo.”

Wanachora picha ya mtu huyo mwema au hata wakati mwingine picha yake mwenyewe na wafuasi wake, kama ilivyokuwa kwa watu wa Nuuh. Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) amesema:

“Hao ndio viumbe waovu kabisa mbele ya Allaah.”

Bi maana hawa wanaofanya kitendo hichi ndio viumbe waovu kabisa, kwa sababu kitendo chao kinapelekea katika shirki. Kwa jumla ni kwamba wanafanya hivo kwa sababu ya I'tiqaad yao ya shirki. Wanayaadhimisha makaburi na kujenga juu yake ili waweze kuyaabudu na kuyaomba uokozi. Kwa ajili hiyo wakawa viumbe waovu kabisa. Mwenye kufanya hivo basi amejifananisha na manaswara na amefanya matendo yao. Yule mwenye kujifananisha na watu basi yeye ni katika wao. Makusudio kwa haya ni kutahadharisha juu ya matendo yao. Ummah umetumbukia katika hayo. Waovu zaidi waliofanya mambo kama hayo ni Raafidhwah waliopindukia kwa watu wa nyumbani kwa Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam). Wao ndio wa mwanzo waliojenga misikiti juu ya makaburi na wakayaabudu badala ya Allaah. Baada ya hapo katika miji mingi ya waislamu wakapatikana watu katika Ahl-us-Sunnah ambao wakawafuata kichwa mchungu. Matokeo yake Ummah ukawafuata makafiri hatua kwa hatua:

2- Watu hawa wamekusanya kati ya fitina mbili; fitina ya makaburi na fitina ya masanamu.

Wameyaadhimisha makaburi na wakatengeneza mapicha. Vivyo hivyo wako watu katika Ummah huu ambao wanajifananisha nao ambao wamefanya hivo. Wamejifananisha na manaswara na watu wa Nuuh.

3- al-Bukhaariy na Muslim kumepokelewa ya kwamba 'Aaishah (Radhiya Allaahu 'anhaa) amesema vilevile:

“Wakati Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) alipokuwa anataka kufa alikuwa akijifunika kitambara usoni mwake. Anapohisi joto hukifunua na anasema akiwa katika hali hiyo: “Laana ya Allaah iwe juu ya mayahudi na manaswara. Wameyafanya makaburi ya Mitume wao kuwa ni sehemu ya kuswalia.” Mtume akitahadharisha yale waliyokuwa wakiyafanya. Lau sikuchelea hilo basi kaburi lake lingewachwa nje, isipokuwa yeye alikhofia lisije kufanywa kuwa ni mahali pa kuswalia.”

Hapa kiumbe mtukufu zaidi anahisi maumivu ya kifo ili aweze kupanda ngazi zaidi na awe ni kiigizo kwa Ummah. Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Laana ya Allaah iwe juu ya mayahudi na manaswara.”

Ameyasema hayo katika hali nzito kama hii ili kuutahadharisha Ummah wake kutokamana na matendo yao. 'Aaishah amesema:

“Lau sikuchelea hilo basi kaburi lake lingewachwa nje...”

Bi maana al-Baqiy' pamoja na Maswahabah wake. Amesema:

“... isipokuwa yeye alikhofia lisije kufanywa kuwa ni mahali pa kuswalia.”

Alichelea wasije kuja watu na wakajenga msikiti juu yake baada ya kutoweka Maswahabah. Maswahabah wao hawakufanya hivo. Lakini jambo hilo linafaywa hii leo na baadhi ya watu wajinga. Wanautembelea msikiti na kumuomba Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) nyuma ya kuta. Hii ni shirki kubwa.

Hadiyth inaonyesha ghera waliokuwa nayo Maswahabah na pupa yao juu ya Ummah. Kwa ajili hiyo ndio maana wakawanukulia Ummah Hadiyth hizi.

4- Muslim amepokea kupitia kwa Jundub bin 'Abdillaah (Radhiya Allaahu 'anh) ambaye amesimulia kwamba amemsikia Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) kabla ya kufa kwake kwa siku tano akisema:

“Hakika mimi najitakasa kwa Allaah kuwa na kipenzi wa karibu katika nyinyi. Kwani hakika Allaah amenifanya kuwa kipenzi Wake wa karibu kama alivyomfanya Ibraahiyim kuwa kipenzi Wake wa karibu. Na lau ningemchukua yeyote katika Ummah wangu kuwa kipenzi wangu wa karibu, basi ningelimfanya Abu Bakr kuwa kipenzi wangu wa karibu. Tanabahini! Hakika wale waliokuwa kabla yenu walikuwa wakiyafanya makaburi ya Mitume wao kuwa mahali pa kuswalia. Tanabahini! Msiyafanye makaburi kuwa mahali pa kuswalia. Hakika mimi nawakatazeni na hilo.”

Mapenzi haya ni aina ya juu kabisa ya mapenzi. Hadiyth inathibitisha fadhilah za Abu Bakr as-Swiddiyq (Radhiya Allaahu 'anh) na kwamba yeye ndiye Swahabah bora kwa maafikiano. Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Na lau ningemchukua yeyote katika Ummah wangu kuwa kipenzi wangu wa karibu, basi ningelimfanya Abu Bakr kuwa kipenzi wangu wa karibu.”

Lakini hakufanya hivo kwa sababu mapenzi yake kumpenda yasije kuchanganyikana na mapenzi ya kumpenda Allaah ('Azza wa Jall). Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Tanabahini! Hakika wale waliokuwa kabla yenu walikuwa wakiyafanya makaburi ya Mitume wao kuwa mahali pa kuswalia.”

Katika upokezi wa Muslim imekuja:

“Tanabahini! Hakika wale waliokuwa kabla yenu walikuwa wakiyafanya makaburi ya Mitume wao na waja wao wema kuwa ni mahali pa kuswalia.”

Tamko limeanguka kwa sababu mtunzi wa kitabu amelinukuu kutoka katika kitabu “Iqtidhwaa’-us-Swiraat al-Mustaqiym” ambapo linakosekana. Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) amekataza kitendo hicho kwa njia tatu:

1- Ameyakemea wayafanyayo.

2- Amesema:

“Msiyafanye...”

3- Amesema:

“Hakika mimi nawakatazeni na hilo.”

Huku ni kutilia mkazo kwa yale anayoyakataza kwa sababu kitendo hicho kinapelekea katika shirki, kama ilivyotokea hii leo. ‘Aaishah amesema:

“... isipokuwa yeye alikhofia lisije kufanywa kuwa ni mahali pa kuswalia.”

Kwa sababu kuswali kwenye makaburi ni kuyafanya msikiti. Kila sehemu ambayo kunaweza kuswaliwa ni msikiti. Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) amesema:

“Nimefanyiwa ardhi yote kuwa msikiti na safi.”

Mtu akiswali kwenye makaburi basi ameyafanya kuwa msikiti hata kama haukujengwa. Mtu asemeje ikiwa kumejengwa kitu? Ni njia inayopelekea katika shirki.

5- Ahmad amepokea kwa cheni ya wapokezi nzuri kupitia kwa Ibn Mas'ud (Radhiya Allaahu 'anh) kutoka kwa Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) ambaye amesema:

“Hakika waovu katika watu ni wale ambao Qiyaamah kitawakuta nao wako hai na wale wenye kuyafanya makaburi kuwa ni mahali pa kuswalia.”

Ameipokea Abu Haatim katika “as-Swahiyyh” yake.

Kwa sababu Qiyaamah hakitowasimamia isipokuwa viumbe waovu kabisa. Kuhusu waumini watakufa kabla ya hapo ambapo kutakuja upepo uzichukue roho zao. Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“... na wale wenye kuyafanya makaburi kuwa ni mahali pa kuswalia.”

Hawa pia ni katika viumbe waovu kabisa. Kwa sababu wamesababisha watu kutumbukia katika shirki, Bid'ah na batili. Kwa sababu watu wanapoona kaburi limejengwa wanaanza kufikiria kuwa linatakiwa kuombwa na kutakwa msaada.

Hakuna neno kukiwepo msikiti karibu na makaburi. Pamoja na hivyo ukitenganishwa kwa kuwekwa barabara ndio bora zaidi.

21. Mlango kuhusu kuchupa mipaka katika makaburi ya watu wema hupelekea huyafanya kama masanamu yaabudiwayo badala ya Allaah

Shaykh-ul-Islaam Muhammad bin 'Abdil-Wahhaab (Rahimahu Allaah) amesema:

1- Maalik amepokea katika "al-Muwattwa" yake ya kwamba Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

"Ee Allaah! Nakuomba usilifanye kaburi langu kuwa sanamu lenye kuabudiwa. Ghadhabu za Allaah huwa kali kwa watu ambao wameyafanya makaburi ya Mitume wao kuwa ni mahali pa kuswalia."⁸¹

Ibn Jariyr amepokea kwa cheni ya wapokezi wake kutoka kwa Sufyaan, kutoka kwa Mansuur, kutoka kwa Mujaahid ambaye amesema kuhusiana na maneno ya Allaah:

أَفَرَأَيْتُمُ اللَّاتَ وَالْعُزَّىٰ وَمَنَاةَ الثَّالِثَةَ الْأُخْرَىٰ أَلَكُمُ الذَّكَرُ وَلَهُ الْأُنثَىٰ

"Je, mmeona al-Laat na al-'Uzzaa na Manaata, mwengine wa tatu [mliokuwa mkiwaabudu]? Je, nyinyi mna wana wa kiume Naye ana wana wa kike?" (**an-Najm 53:19-21**)

"al-Laat alikuwa akiwapikia uji [mahujaji]. Alipokufa ndipo watu wakawa wakikusanyika kwa muda mrefu kwenye kaburi lake."

⁸¹ Maalik (414), 'Abdur-Razzaaq katika "al-Muswannaf" (1587) na Ibn Abiy Shaybah (7544). Swahihi kwa mujibu wa al-Albaani katika "Mishkaat-ul-Maswaabiyh" (750).

Namna hii ndivyo alivyosema Abul-Jawzaa' kutoka kwa Ibn 'Abbaas (Radhiya Allaahu 'anhumaa) ambaye amesema:

“Alikuwa akitengeneza uji kwa ajili ya mahujaji.”

2- Ibn 'Abbaas (Radhiya Allaahu 'anhumaa) amesema:

“Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amewalaani wanawake wenye kuyatembelea makaburi, wenye kuyafanya ni mahali pa kuswalia na wanaoyatilia mataa.”⁸²

Wameipokea watunzi wa Sunan.

MAELEZO

Haya ni kweli kama ilivyotangulia. Kuchupa mipaka kunamfanya yule mwenye kufanyiwa upetukaji kuwa ni mwabudiwa badala ya Allaah. Kwa ajili hii wakati baadhi ya watu walipoanza kuchupa mipaka kwa baadhi ya watu wema wakawaabudu badala ya Allaah. Kama mfano wa makaburi ya waja wema kama mfano wa kaburi la al-Hasan, al-Husayn na la Faatwimah. Kadhalika Ummah huu umechupa mipaka kwa Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) na matokeo yake wakamuabudu, wakamuomba uokozi na kumuomba badala ya Allaah. Pindi watu wa Nuuh walipopetuka mipaka kwa watu wema wakawaabudu, kama ilivyokwishatangulia.

1- Maalik amepokea katika “al-Muwattwa” yake ya kwamba Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Ee Allaah! Nakuomba usilifanye kaburi langu kuwa sanamu lenye kuabudiwa. Ghadhabu za Allaah huwa kali kwa watu ambao wameyafanya makaburi ya Mitume wao kuwa ni mahali pa kuswalia.”

⁸² Abu Daawuud (3236), at-Tirmidhiy (320), an-Nasaa'iy (2043) na Ahmad (2030). Dhaifu kwa mujibu wa al-Albaaniy katika “Silsilat-ul-Ahaadiyth adh-Dhwa'iyfah” (225).

Upokezi huu umepokelewa vilevile na 'Atwaa' bin Yasaar na Zayd bin Aslam bila ya Swahabah katika cheni ya wapokezi kama vile Abu Sa'iyd al-Khudriy (Radhiya Allaahu 'anh) kutoka kwa Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam). Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Ghadhabu za Allaah huwa kali...”

Kwa sababu wanapojenga misikiti juu yake wanakuwa wamefanya ni waungu wanaoabudiwa badala ya Allaah. Wanaanza kuwaadhimisha, kuyazunguka, kuwaomba msaada na kuyawekea nadhiri. Pindi watu wa at-Twaaif walipochupa mipaka kwa al-Laah wakawa ni wenye kumuabudu badala ya Allaah. Huu ni mwenendo wa wakale na wa waliokuja nyuma. Kuyajengea makaburi na kuyaadhimisha kunayafanya kuwa ni waungu wanaoabudiwa badala ya Allaah. Njia inapelekea katika lengo.

2- Ibn 'Abbaas (Radhiya Allaahu 'anhumaa) amesema:

“Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amewalaani wanawake wenye kuyatembelea makaburi, wenye kuyafanya ni mahali pa kuswalia na wanaoyatilia mataa.”

Hadiyth inafahamisha juu ya kwamba ni haramu kwa wanawake kuyatembelea makaburi. Haya ndio maoni sahihi kwa mujibu wa dalili. Kadhalika Hadiyth imepokelewa na Hassaan bin Thaabit na Abu Hurayrah. Kuyatembelea makaburi ni jambo linalowahusu wanaume tu.

Kama tulivyotangulia kusema kwamba kuyafanya makaburi ni mahali pa kuswali ni kujifananisha na mayahudi na manaswara na vilevile ni njia miongoni mwa njia zinazopelekea katika shirki.

Haijuzu kwa wanawake kuyatembelea makaburi hata kaburi la Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) vilevile. Haya ndio maoni sahihi kwa sababu Hadiyth

ni zenye kuenea. Imepokelewa vilevile kwa tamko “wanawake wenye kuyatembelea makaburi sana”.

Inajuzu kuapa kwa Qur-aan kwa sababu ni maneno ya Allaah.

22. Himaya ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) kuihami Tawhiyd na kufunga kila njia inayopelekea katika shirki

Shaykh-ul-Islaam Muhammad bin 'Abdil-Wahhaab (Rahimahu Allaah) amesema:

1- Allaah (Ta'ala) amesema:

لَقَدْ جَاءَكُمْ رَسُولٌ مِّنْ أَنْفُسِكُمْ عَزِيزٌ عَلَيْهِ مَا عَنِتُّمْ حَرِيصٌ عَلَيْكُمْ بِالْمُؤْمِنِينَ رَءُوفٌ رَّحِيمٌ

“Hakika amekujieni Mtume anayetokana na nyinyi wenyewe. Yanamuhuzunisha yanayokutaabisheni, anakuhangaikieni na kwa waliomuamini ni mpole na mwenye huruma.” (at-Tawbah 09:128)

2- Abu Hurayrah (Radhiya Allaahu 'anh) ameeleza kwamba Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Msizifanye nyumba zenu kuwa makaburi na wala msilifanye kaburi langu kuwa ni lenye kutembelewa mara kwa mara. Niswalieni; kwani hakika swalah zenu hunifikia popote mlipo.”⁸³

Ameipokea Abu Daawuud kwa cheni ya wapokezi nzuri na wapokezi wake ni waaminifu.

3- 'Aliy bin al-Husayn alimuona mtu anaenda kwenye kijitundu kilichokuwa mahali pa kaburi la Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) ili apate kuingia na kuomba ambapo akamkataza na akasema:

⁸³ Abu Daawuud (2042), Ahmad (8790), at-Twabaraaniy katika "al-Awsatw" (8030) na al-Bayhaqiy katika "Shu'ab-ul-Ilymaan" (4162). Swahiyh kwa mujibu wa al-Albaaniy katika "Swahiyh-ul-Jaami'" (7226).

“Hivi nikuhadithie Hadiyth niliyoisikia kutoka kwa baba yangu ambaye na yeye kaisikia kutoka kwa babu yangu Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) wa Allaah ambaye amesema: “Msilifanye kaburi langu kuwa ni lenye kutembelewa mara kwa mara wala nyumba zenu kuwa makaburi. Niswalieni; kwani hakika swalah zenu hunifikia popote mlipo.”⁸⁴

Imepokelewa katika “al-Mukhtaarah”.

MAELEZO

Katika mlango huu mwandishi wa kitabu amebainisha namna ambavyo Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) alivyoihami Tawhiyd dhidi ya maneno na matendo ya kishirki. Mlango huu unazungumzia kuihami Tawhiyd na kuziba njia zote zinazopelekea katika shirki. Ndani yake kuna utetezi wa kimaneno na matahadharisho ya shirki na yale yote maneno na matendo yote yanayopelekea huko.

1- Allaah (Ta‘ala) amesema:

لَقَدْ جَاءَكُمْ رَسُولٌ مِّنْ أَنْفُسِكُمْ عَزِيزٌ عَلَيْهِ مَا عَنِتُّمْ حَرِيصٌ عَلَيْكُمْ بِالْمُؤْمِنِينَ رَءُوفٌ رَّحِيمٌ

“Hakika amekujieni Mtume anayetokana na nyinyi wenyewe. Yanamuhuzunisha yanayokutaabisheni, anakuhangaikieni na kwa waliomuamini ni mpole na mwenye huruma.”

Huu ni wasifu wake na Ummah wote ndio wanaozungumzishwa na khaswakhaswa Quraysh kwa sababu wao wanamjua na wanajua ukoo wake na kwamba anatokamana na wao. Kuna kisomo kingine kisichokuwa cha kawaida kiko namna hii:

⁸⁴ Abu Ya‘laa (469), ‘Abdur-Razzaaq (7826) na Ibn Abiy Shaybah (7542). Ni yenye nguvu kwa mujibu wa al-Albaaniy katika “Tahdhiyr-us-Saajid” (9).

مَنْ أَنْفَسِكُمْ

“... anayetokamana na watukufu wenu...”⁸⁵

Allaah (Ta'ala) amesema:

عَزِيزٌ عَلَيْهِ مَا عَنِتُّمْ

“Yanamuhuzunisha yanayokutaabisheni.”

Bi maana anaudhiwa na jambo lolote linalokudhuruni na linalokutaabisheni. Haya ni kwa sababu ya kukuhurumieni na kukupendeni na kupupia kwake juu ya kuongoka kwenu na kukutahadharisheni na Moto kwa matendo na maneno yake. Ni mpole kwa waumini. Alikuwa na hisia juu yao. Lakini hata hivyo alikuwa ni mkali kwa maadui wa Allaah kwa sababu ya ukafirin na upotevu wao. Mtu aliye na sifa hizi ni wajibu kumfuata na kumpenda, lakini walipindua mambo chini juu na wakamchukia kufikia kiasi cha kwamba wakataka kumuua.

Mtu aliye na sifa hizi hauachi Ummah wake pasi na kuwatakia kheri. Ndio maana kawaamrisha Tawhiyd, akawahimiza watu kuwa na msimamo na kutahadhari kutokamana na shirki na sababu zote zinazopelekea huko. Miongoni mwa aliyoyasema:

“Msipindukie kwangu kama walivyopindukia manaswara kwa 'Iysaa mwana wa Maryam.”

“Nakutahadharisheni na kupetuka mipaka.”

2- Abu Hurayrah (Radhiya Allaahu 'anh) ameeleza kwamba Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

⁸⁵ al-Haakim (02/240).

“Msizifanye nyumba zenu kuwa makaburi na wala msilifanye kaburi langu kuwa ni lenye kutembelewa mara kwa mara. Niswalieni; kwani hakika swalah zenu hunifikia popote mlipo.”

Sehemu inayotembelewa mara kwa mara ni mahali ambapo kunaendewa mara kwa mara na kuomba mtu akiwa mahali hapo, akaswali, akaomba msaada na mfano wa hayo. Hakuingii katika haya kutembelea kaburi la Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) pasi na kulifungia safari, kuchupa mipaka au kuabudu kwenye kaburi hilo.

(Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Msizifanye nyumba zenu kuwa makaburi...”

Bi maana msizifanye kama makaburi ambapo hokuswaliwi wala kusomwa Qur-aan makaburini. Bali kinyume chake swalini na someni Qur-aan katika nyumba zenu. Imekuja katika Hadiyth:

“Zifanyeni baadhi ya swalah zenu katika nyumba zenu na wala msiyafanye kuwa makaburi.”⁸⁶

Ni dalili inayothibitisha kuwa makaburini hokuswaliwi na wala hokusomwi Qur-aan. Swalah zinazoswali nyumbani ni swalah za sunnah.

(Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Niswalieni...”

Amesitiza (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) kumswalia.

3- 'Aliy bin al-Husayn alimuona mtu anaenda kwenye kijitundu kilichokuwa mahali pa kaburi la Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) ili apate kuingia na kuomba ambapo akamkataza na akasema:

⁸⁶ al-Bukhaariy (432) na Muslim (777).

“Hivi nikuhadithie Hadiyth niliyoisikia kutoka kwa baba yangu ambaye na yeye kaisikia kutoka kwa babu yangu Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) wa Allaah ambaye amesema: “Msilifanye kaburi langu kuwa ni lenye kutembelewa mara kwa mara wala nyumba zenu kuwa makaburi. Niswalieni; kwani hakika swalah zenu hunifikia popote mlipo.”

Imepokelewa katika “al-Mukhtaarah”.

‘Aliy bin al-Husayn ni Zayn-ul-‘Aabidiyn.

Kumswalia Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) kunakuwa kila mahali. Anaweza kuswaliwa mtu akiwa nyumbani, sokoni na njiani. Kumswalia sio kwenye kaburi peke yake. Kwa ajili hii ndio maana ‘Aliy bin al-Husayn alimkemea mtu yul. Alimbainishia kwamba kitendo chake hakikuwekwa katika Shari‘ah na kwamba anachotakiwa ni yeye kumswalia pasi na kukaa kwenye kaburi lake na kuomba.

Sunnah hii imepokelewa na watu wa nyumbani kwa Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam). Wote wamebainisha kwamba kuyatembelea makaburi mara kwa mara ni jambo linalopelekea katika shirki. Ikiwa yule aliyelitembelea atasimama hapo kwa muda mrefu, akaswali na akaomba kwenye kaburi hilo basi hilo litampelekea katika shirki na kuchua mipaka. Haya yamekatazwa na Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam). Wale wenye kuyafanya makaburi kuwa ni mahali pa kuswalia, wakayajengea, wakayaweka chokaa, wayavisha vitambara na nguo ni mambo yanayopelekea kuwafanya wale wasiokuwa na elimu kufikiria kuwa ni yenye kuadhimishwa na kwamba yananufaisha. Yote haya yametokea pamoja na kuwa Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) amehami Tawhiyd na akatahadharisha kutokamana na shirki.

23. Baadhi ya watu katika Ummah huu wataabudu masanamu

1- Allaah (Ta'ala) amesema:

أَلَمْ تَرَ إِلَى الَّذِينَ أُوتُوا نَصِيحًا مِّنَ الْكِتَابِ يُؤْمِنُونَ بِالْجَنَّةِ وَالطَّاعُوتِ

“Je, huzingatii wale ambao wamepewa sehemu ya Kitabu [hapo kale] wanaamini mazimwi na Twaaghuut?” (an-Nisaa’ 04:51)

2-

قُلْ هَلْ أُنَبِّئُكُمْ بِشَرِّ مِّنْ ذَلِكَ مَثُوبَةً عِنْدَ اللَّهِ ۗ مَنْ لَعَنَهُ اللَّهُ وَغَضِبَ عَلَيْهِ وَجَعَلَ مِنْهُمْ الْفِرْدَ وَالْحَنَازِيرَ
وَعَبَدَ الطَّاعُوتِ

“Sema: “Je, nikujulisheni yule ambaye ni mwenye malipo mabaya zaidi kuliko haya mbele ya Allaah? Yule ambaye Allaah amemlaani na akamghadhibikia na akawafanya miongoni mwao manyani na nguruwe na wakaabudu twaaghuut.” (al-Maaidah 05:60)

3-

قَالَ الَّذِينَ غَلَبُوا عَلَىٰ أَمْرِهِمْ لَنَتَّخِذَنَّ عَلَيْهِم مَّسْجِدًا

“Wakasema wale walioshinda katika shauri lao: “Bila shaka tutajenga msikiti juu yao [kama kumbukumbu]!” (al-Kahf 18:21)

4- Abu Sa’iyd al-Khudriy (Radhiya Allaahu ‘anh) ameeleza kwamba Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) amesema:

“Mtafuata nyayo za wale waliokuwa kabla yenu hatua kwa hatua, shibiri kwa shibiri, mpaka wakiingia shimo la mburukenge nanyi mtaingia. Wakasema: “E

Mtume wa Allaah! Unamaanisha mayahudi na manaswara?" Akasema: "Kina nani wengine?"⁸⁷

Ameipokea al-Bukhaariy na Muslim.

5- Muslim amepokea kupitia kwa at-Thawbaan (Radhiya Allaahu 'anh) ya kwamba Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

"Hakika Allaah amenikusanyia ardhi nikaona mashariki na magharibi yake. Hakika ufalme wa Ummah wangu utafikia kiasi na vile nilivyokusanyiwa. Nimepewa hazina mbili; nyekundu na nyeupe. Mimi nimemuomba Mola wangu asiuangamize Ummah wangu kwa njaa kubwa yenye kuenea na wala asiwatumie adui akawatawalia ardhi zao isipokuwa kutokamana na wao wenyewe. Mola wangu akanambia: "Ee Muhammad! Mimi ninapotoa amri hakika hairudi wala kurejeshwa. Mimi Nimekupa wewe kwa ajili ya Ummah wako ya kwamba sintowahilikisha kwa njaa kubwa yenye kuenea na kwamba sintowatumia adui, isipokuwa kutokamana na wao wenyewe, watawalie nguvu zao wenyewe kwa wenyewe, hata kama watajikusanya watu wa pande zote za dunia wasingeliwapata, mpaka itakuwa baadhi yao wakiwaangamiza wengine na wakidhulumiana wao kwa wao."⁸⁸

6- al-Barqaaniy ameipokea Hadiyth hii katika "as-Swahiyh" yake na kaongezea:

"Kubwa ninalolikhofia juu ya Ummah wangu ni viongozi wenye kupoteza. Watapoanza kusimamishiana panga hazitosimamishwa mpaka siku ya Qiyaamah. Hakitosimama Qiyaamah mpaka kikundi katika Ummah wangu kiwafuate washirikina na mpaka kikundi katika Ummah wangu kiabudu masanamu. Hakika kutakuwa katika Ummah wangu waongo thelathini na kila mmoja wao atadai ya kwamba yeye ni Mtume ilihali mimi ndiye Mtume wa mwisho. Hakuna Mtume mwingine baada yangu. Hakitoacha kikundi katika

⁸⁷ al-Bukhaariy (4356) na Muslim (2669).

⁸⁸ Muslim (2889).

Ummah wangu kuwa juu ya haki hali ya kuwa ni chenye kushinda; hakitodhurika na wale wenye kuwakosesha nusura mpaka itapofika amri ya Allaah (Tabaarak wa Ta'ala)."⁸⁹

MAELEZO

Mlango unazungumzia kuhusu Hadiyth na Aayah zinazofahamisha juu ya hilo na kwamba Ummah huu haukukingwa na kutumbukia katika shirki. Kama ambavyo watu waliingia katika dini makundi kwa makundi wamekuwa pia ni wenye kutoka kwa wingi. Tayari wakati wa Abu Bakr as-Swiddiyq walikuwepo watu walioritadi kutoka katika Uislamu.

1- Allaah (Ta'ala) amesema:

أَلَمْ تَرَ إِلَى الَّذِينَ أُوتُوا نَصِيحًا مِّنَ الْكِتَابِ يُؤْمِنُونَ بِالْجِبْتِ وَالطَّاغُوتِ

“Je, huzingatii wale ambao wamepewa sehemu ya Kitabu [hapo kale] wanaamini mazimwi na Twaaghuut?”

Allaah ameeleza kwamba kuna watu katika Ahl-ul-Kitaab ambao wanaamini mazimwi, Twaaghuut na shaytwaan:

وَيَقُولُونَ لِلَّذِينَ كَفَرُوا هَؤُلَاءِ أَهْدَىٰ مِنَ الَّذِينَ آمَنُوا سَبِيلًا

“Wanasema juu ya wale ambao wamekufuru kuwa: “Hawa wameongoka zaidi katika njia kuliko wale ambao wameamini.”

Haya yalisemwa na mayahudi kama vile Ka'b bin al-Ashraf na Huyayy bin Akhtwab. Walisema kwamba Quraysh ni wenye kuongoka zaidi kuliko Muhammad na Maswahabah wake pamoja na kuwa wanatambua kuwa yuko katika haki. Walisema hivo kwa sababu ya ukaidi, hasadi, chuki na kumpinga.

⁸⁹ Ahmad (22448). Swahiyh kwa mujibu wa al-Albaaniy katika "Swahiyh-ul-Jaami" (1773).

Wamepewa sehemu ya Kitabu lakini hata hivyo hawakuifanyia kazi. Bali wameenda kinyume nayo na wakaamini uchawi na twaaghuut na wakasema kuwa Quraysh ni wenye kuongoka njia zaidi. Ikiwa haya yaliwatokea mayahudi basi Ummah huu pia utaanguka katika hayo kutokana na Hadiyth:

“Mtafuata nyayo za wale waliokuwa kabla yenu hatua kwa hatua, shibiri kwa shibiri, mpaka wakiingia shimo la mburukenge nanyi mtaingia. Wakasema: “E Mtume wa Allaah! Unamaanisha mayahudi na manaswara?” Akasema: “Kina nani wengine?”

Ni dalili inayofahamisha kuwa haya ya ukafiri yatatokea katika Ummah wa Muhammad (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam). Watapatikana wataokufuru na wenye kusema kuwa makafiri ni wenye kuongoka zaidi kuliko wafuasi wa Muhammad (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam). Haya yametokea hapo kale na bado ni yenye kuendelea kutokea wanapatikana watu ambao wanawafadhilisha mayahudi na manaswara mbele ya Ummah huu.

2-

قُلْ هَلْ أَنْبِئُكُمْ بِشَرِّ مِّنْ ذَلِكَ مَثُوبَةً عِنْدَ اللَّهِ ۚ مَن لَّعَنَهُ اللَّهُ وَعَظِمَ عَلَيْهِ وَجَعَلَ مِنْهُمْ الْفِرْدَةَ وَالْحَنَازِيرَ
وَعَبَدَ الطَّاغُوتِ

“Sema: “Je, nikujulisheni yule ambaye ni mwenye malipo mabaya zaidi kuliko haya mbele ya Allaah? Yule ambaye Allaah amemlaani na akamghadhibikia na akawafanya miongoni mwao manyani na nguruwe na wakaabudu twaaghuut.”

Ikiwa wale wa kabla yetu waliabudu waungu wa batili kama vile shaytwaan na kila chenye kuabudiwa badala ya Allaah basi kadhalika watapatikana katika Ummah huu watu watakaoabudia waungu wa batili na mizimu kutokana na Hadiyth:

“Mtafuata nyayo za wale waliokuwa kabla yenu hatua kwa hatua, shibiri kwa shibiri, mpaka wakiingia shimo la mburukenge nanyi mtaingia. Wakasema: “E Mtume wa Allaah! Unamaanisha mayahudi na manaswara?” Akasema: “Kina nani wengine?”

3-

قَالَ الَّذِينَ غَلَبُوا عَلَىٰ أَمْرِهِمْ لَنَتَّخِذَنَّ عَلَيْهِم مَّسْجِدًا

“Wakasema wale walioshinda katika shauri lao: “Bila shaka tutajenga msikiti juu yao [kama kumbukumbu]!”

Ikiwa katika nyumati zilizotangulia walipatikana watu waliojenga misikiti juu ya makaburi na wakaiadhimisha basi vivyo hivyo Ummah huu utakuja kufanya hivo. Haya yalitokea mwishoni mwa miaka mia moja ya mwanzo ambapo Raafidhwah wakajenga misikiti juu ya makaburi na wakaiadhimisha. Halafu kitendo chao kikaigwa na watu wanaojinasibisha na Uislamu. Hali ya waislamu ni kama ilivyotajwa katika Hadiyih:

4- Abu Sa'iyd al-Khudriy (Radhiya Allaahu 'anh) ameeleza kwamba Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Mtafuata nyayo za wale waliokuwa kabla yenu hatua kwa hatua, shibiri kwa shibiri, mpaka wakiingia shimo la mburukenge nanyi mtaingia. Wakasema: “E Mtume wa Allaah! Unamaanisha mayahudi na manaswara?” Akasema: “Kina nani wengine?”

Ameipokea al-Bukhaariy na Muslim.

Kama jinsi wanavofanana watajifananisha makafiri kutoka katika Ummah huu na wale makafiri waliotangulia katika kumshirikisha Allaah na kuabudu mizimu na masanamu. Kama ambavyo watu wa mwanzo waliwatukana wafuasi wa Mitume vivyo hivyo watapatikana watu katika Ummah huu kama vile

Raafidhwa na Khawaarij wenye kuwatukana Maswahabah. Kila maasi na kufuru iliojitokeza kwa wale wa kale itajitokeza vilevile katika Ummah huu. Katika hayo kunaingia vilevile Hadiyth ya al-Bukhaariy kutoka kwa Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam):

“Hakitosimama Qiyaamah mpaka wanawake wasongamane kulizunguka Dhul-Khilswah.”⁹⁰

Daws ni kabila kusini mwa Ghaamid na Zahraan. Hayo yalipitika muda si mrefu sana kabla ya kutangazwa kwa nchi hii. Walikuwepo watu wanaoliabudu sanamu hili, wanalizunguka na hilo litatokea mara nyingine. Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Hakitosimama Qiyaamah mpaka wajiunge watu katika Ummah wangu na washirikina na mpaka kundi katika Ummah wangu waabudu masanamu.”⁹¹

Haya pia yametokea. 'Aaishah (Radhiya Allaahu 'anhaa) ameeleza kwamba Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Hazitoenda nyusiku na michana mpaka aabudiwe al-Laah na al-'Uzzaa.”⁹²

Yote haya yatatokea.

Kuna Hadiyth inayosema:

“Shaytwaan amekata tamaa ya kuabudiwa katika kisiwa cha kiarabu.”⁹³

Wajinga wanatumia hoja kwa Hadiyth hii. Lakini aliyekata tamaa amekingwa na makosa? Yeye hakuingwa na makosa. Anaweza kukata tamaa juu ya kitu lakini kikatokea huko katika mustakabali. Alikata tamaa wakati alipoona dini

⁹⁰ al-Bukhaariy (7116) na Muslim (2906).

⁹¹ Abu Daawuud (42529, Ahmad (22448) na Abu Nu'aym katika "al-Hilyah" (2/289). Swahiyh kwa mujibu wa al-Albaaniy katika "Swahiyh-ul-Jaami'" (1773).

⁹² Muslim (2907).

⁹³ Muslim (2812).

imeshinda. Hata hivyo shirki imetokea. Kadhalika anaweza kuwa na matarajio ya kitu na kisitokee. Imesemekana vilevile kwamba amekata tamaa hali za waislamu kuwa kama zilivyokuwa hapo kabla kwa sababu kutaendelea siku zote kuwepo kundi katika Ummah huu likiwa juu ya haki. Imesemekana vilevile kwamba walengwa ni Maswahabah kutokana na upokezi “waswaliji”, bi maana Maswahabah wenye kuswali kwa sababu Allaah aliwawafikisha na akawaruzuku elimu. Maoni yote matatu ni sahihi.

5- Muslim amepokea kupitia kwa at-Thawbaan (Radhiya Allaahu 'anh) ya kwamba Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Hakika Allaah amenikusanyia ardhi nikaona mashariki na magharibi yake. Hakika ufalme wa Ummah wangu utafikia kiasi na vile nilivyokusanyiwa. Nimepewa hazina mbili; nyekundu na nyeupe. Mimi nimemuomba Mola wangu asiuangamize Ummah wangu kwa njaa kubwa yenye kuenea na wala asiwatumie adui akawatawalia ardhi zao isipokuwa kutokamana na wao wenyewe. Mola wangu akanambia: “Ee Muhammad! Mimi ninapotoa amri hakika hairudi wala kurejeshwa. Mimi Nimekupa wewe kwa ajili ya Ummah wako ya kwamba sintowahilikisha kwa njaa kubwa yenye kuenea na kwamba sintowatumia adui, isipokuwa kutokamana na wao wenyewe, watawalie nguvu zao wenyewe kwa wenyewe, hata kama watajikusanya watu wa pande zote za dunia wasingeliwapata, mpaka itakuwa baadhi yao wakiwaangamiza wengine na wakidhulumiana wao kwa wao.”

Hii ni alama katika alama za utume. Ufalme wa Ummah wake ulisambaa mpaka mashariki China na mpaka magharibi kama vile Tangiee, Morocco. Lakini hata hivyo mambo hayajakuwa hivo kuhusiana na kaskazini na kusini. Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Nimepewa hazina mbili... “

Ni hazina ya kirumi na hazina ya kifursi. Walitawala nchi mbili kubwa; nchi ya kinaswara na nchi ya kishirikina. Haya ndio yanayotokea katika Ummah huu.

Hazina zao zilitolewa katika njia ya Allaah, kama alivyokhabarisha Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) hayo, wakati wa ukhaliyfah wa 'Umar na 'Uthmaan. Hii ni alama nyingine ya utume. Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Mimi nimemuomba Mola wangu asiuangamize Ummah wangu kwa njaa kubwa yenye kuenea...”

Bi maana asiwaangamize kwa mara moja kama ilivyotokea kwa watu wa Nuuh, Swaalih na wengineo. Kwa sababu huu ndio Ummah wa mwisho. Vilevile kwa sababu ya ile kheri na baraka inayoptikana kwa Mtume wake (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) utabaki mpaka Qiyaamah kisimame.

Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“... na wala asiwatumie adui akawatawalia ardhi zao isipokuwa kutokamana na wao wenyewe.”

Pindi watapoanza kutawaliana na kupigana vita wao kwa wao ndipo Allaah atawatawalishia adui wao. Haya yatatokea pindi waislamu watapofarikiana na kutofautiana. Hapo ndipo adui atatumia fursa hiyo na kuchukua yale yaliyoko mikononi mwa waislamu kwa muda mrefu.

Allaah (Ta'ala) akasema:

“Ee Muhammad! Mimi ninapotoa amri hakika hairudi wala kurejeshwa.”

Allaah anapopanga na kukadiria jambo hakuna yeyote anaweza kulizuia. Kumeshatangulia katika elimu ya Allaah ya kwamba Ummah huu kutatokea tofauti na mipasuko na kwamba du'aa yake (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) kuwaombea juu ya kwamba wasipigane vita na wasifarikiane baina yao haitoitikiwa. Bali amekataza du'aa hii. Kwa ajili hiyo ndio maana kumetokea mipasuko tokea wakati wa zama za kwanza na baadaye ikatokea kwa wamongoli na baadaye maadui wengine ambao walitawalia jambo la waislamu

ili wasishikamane barabara na dini yao sahihi. Allaah habadilishi hali za watu mpaka wao wenyewe kwanza wazibadili hali zao. Hapa inapata kufahamika kwamba iwapo Ummah utakusanyika juu ya haki, wakanyooka kisawasawa na na wakasaidizana basi adui wao hatoweza kuwashinda. Matokeo yake Allaah atakusanyia kheri zote. Pindi watapofarikiana na wakatofautiana basi adui wao atatumia fursa hiyo na kuwashambulia.

6- al-Barqaaniy ameipokea Hadiyth hii katika “as-Swahiyyh” yake na kaongezea:

“Kubwa ninalolikhofia juu ya Ummah wangu ni viongozi wenye kupoteza. Watapoanza kusimamishiana panga hazitosimamishwa mpaka siku ya Qiyaamah. Hakitosimama Qiyaamah mpaka kikundi katika Ummah wangu kiwafuate washirikina na mpaka kikundi katika Ummah wangu kiabudu masanamu. Hakika kutakuwa katika Ummah wangu waongo thelathini na kila mmoja wao atadai ya kwamba yeye ni Mtume ilihali mimi ndiye Mtume wa mwisho. Hakuna Mtume mwingine baada yangu. Hakitoacha kikundi katika Ummah wangu kuwa juu ya haki hali ya kuwa ni chenye kushinda; hakitodhurika na wale wenye kuwakosesha nusura mpaka itapofika amri ya Allaah (Tabaarak wa Ta’ala).”

Hili linafidisha ukhatari wa viongozi wenye kupotosha. Nao ni wale watawala waovu. Wanafuatwa na watu wanaathirika nao na wanachukua msaada kutoka kwao katika kuyaendea mambo ya batili. Ndio maana (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) alichelea juu yao. Hili linajumuisha viongozi na mahakimu wapotevu.

Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) amesema:

“Watapoanza kusimamishiana panga hazitosimamishwa mpaka siku ya Qiyaamah.”

Haya pia yametokea. Hii ni alama nyingine miongoni mwa alama za utume wake. Mlango wa fitina ulifunguka wakati alipouawa ‘Umar. Baada ya hapo ikazidi kwa kuuawa kwa ‘Uthmaan. Baada ya hapo shari ikazidi na kuzidi.

Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Hakitosimama Qiyaamah mpaka kikundi katika Ummah wangu kiwafuate washirikina na mpaka kikundi katika Ummah wangu kiabudu masanamu.”

Hii ni dalili inayothibitisha kuwa shirki itatokea katika Ummah huu, jambo ambalo limekwishatokea. Shirki imetokea katika kisiwa cha kiarabu na kwenginepo.

Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Hakika kutakuwa katika Ummah wangu waongo thelathini na kila mmoja wao atadai ya kwamba yeye ni Mtume ilihali mimi ndiye Mtume wa mwisho.”

Hii ni alama nyingine tena ya utume. Haya pia yametokea. Mmoja wapo ni Musaylamah ambaye alidai kuwa ni Mtume na akauawa na Maswahabah. Vilevile al-Aswad al-'Ansiy mbye naye alidai utume na akauawa wakati wa uhai wa Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam). Pia Sajaah at-Tamiymiyyah alifanya hivo lakini baadaye akatubia. Twulaykhah al-Asdiy alifanya hali kadhalika lakini baadaye akatubia. Wa mwisho wao atakuwa ad-Dajjal ambaye kwanza atadai kuwa ni Mtume na hatimaye adai kuwa yeye ndiye Mola wa walimwengu. Hawa waliotajwa ndio wataokuwa na nguvu, mamlaka na utata. Vinginevyo wako wengi wanaodai kuwa ni Mitume. Hata hivyo baadhi yao wanasema hivo kwa sababu ya wendawazimu, upunguani na mengineyo.

Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Hakitoacha kikundi katika Ummah wangu kuwa juu ya haki hali ya kuwa ni chenye kushinda; hakitodhurika na wale wenye kuwakosesha nusura mpaka itapofika amri ya Allaah (Tabaarak wa Ta'ala).”

Hii ni alama nyingine ya utume na ni bishara njema. Kundi hili lipo mpaka hii leo. Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“... mpaka itapofika amri ya Allaah (Tabaarak wa Ta’ala).”

Bi maana mpaka pale kutapokuja upepo mzuri utaozichukua roho za waumini na mwishowe Qiyaamah kiwasimamie wale viumbe waovu kabisa. Imekuja katika baadhi ya mapokezi kwamba kikundi hicho kitakuwepo Shaam. Ikiwa mapokezi haya yamesihi basi hiyo ina maana kwamba baadhi ya nyakati na si kwamba ni daima. Lakini mapokezi yake mengi ni dhaifu. Kundi hilo halina sehemu maalum. Linaweza kuwa sehemu moja kama ambavo linaweza kuwa sehemu mbalimbali. Hakuna Hadiyth Swahiyh inayoonyesha kwamba litakuwa sehemu maalum.

24. Mlango kuhusu uchawi

1- Allaah (Ta'ala) amesema:

وَلَقَدْ عَلِمُوا لَمَنِ اشْتَرَاهُ مَا لَهُ فِي الْآخِرَةِ مِنْ خَلَاقٍ

“Kwa hakika wamekwishaelewa kwamba atakayenunua [kwa kujipatia elimu ya uchawi huo] hatopata katika Aakhirah fungu lolote.” (al-Baqarah 02:102)

2-

أَمْ تَرَى إِلَى الَّذِينَ أُوتُوا نَصِيحًا مِّنَ الْكِتَابِ يُؤْمِنُونَ بِالْجِبْتِ وَالطَّاغُوتِ

“Je, huzingatii wale ambao wamepewa sehemu ya Kitabu [hapo kale] wanaamini mazimwi na Twaaghuut?” (an-Nisaa' 04:51)

'Umar (Radhiya Allaahu 'anh) amesema:

“Jibt ni uchawi na Twaaghuut ni shaytwaan.”⁹⁴

2- Jaabir (Radhiya Allaahu 'anh) amesema:

“Twaaghuut ni makuhani walikuwa wakiteremkiwa na mashaytwaan. Katika kila kabila kuna mmoja.”

3- Abu Hurayrah (Radhiya Allaahu 'anh) amesimulia kwamba Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Jiepusheni na dhambi saba zenye kuangamiza.” Wakasema: “Ee Mtume wa Allaah! Ni yepi hayo?” Akasema: “Ni kumshirikisha Allaah, uchawi, kuiua nafsi ambayo Allaah kaiharamisha kuuliwa isipokuwa kwa haki, kula ribaa, kula mali

⁹⁴ al-Bukhaariy (8/252).

ya mayatima, kukimbia siku ya vita na kuwazulia uongo wa kuzini wanawake waumini waliohifadhika.”⁹⁵

4- Jundub (Radhiya Allaahu ‘anh) ameeleza kwamba Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) amesema:

“Adhabu ya mchawi ni kuuawa kwa upanga.”⁹⁶

Ameipokea at-Tirmidhiy ambaye amesema:

“Sahihi ni kwamba ni maneno ya Swahabah.”

5- al-Bukhaariy amepokea katika “as-Swahiyyh” yake kupitia kwa Bajaalah bin ‘Abadah aliyesimulia:

“‘Umar bin al-Khattwaab (Radhiya Allaahu ‘anh) aliandika barua ambapo ndani yake kulikuwemo:

“Muueni kila mchawi mwanaume na mchawi mwanamke.”

Tukawaua wachawi watatu.”

6- Imesihi kutoka kwa Hafswah (Radhiya Allaahu ‘anhaa) ya kwamba yeye aliamrisha auawe kijakazi wake ambaye alikuwa kamfanyia uchawi ambapo akauawa⁹⁷. Vivyo hivyo kitendo hicho kimesihi kutoka kwa Jundub (Radhiya Allaahu ‘anh) pia⁹⁸.

Ahmad amesema:

“Imesihi kupokelewa kutoka kwa Maswahabah watatu wa Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam).

⁹⁵ al-Bukhaariy (2767) na Muslim (89).

⁹⁶ at-Tirmidhiy (1460), al-Haakim (8073), ad-Daaraqutwniy (112) na wengineo. Dhaifu kwa mujibu wa al-Albaaniy katika “Jaami’-us-Swaghiyyr” (2699).

⁹⁷ Maalik (1526) na wengineo.

⁹⁸ ad-Daaraqutwniy (113) na al-Bayhaqiyy (16278).

MAELEZO

Uchawi ni mambo yanayofanywa na mchawi ambapo anafunga vifundo, madawa na kupulizia katika vifundo hivyo na mambo mengine ambayo wanayapokea kutoka kwa majini na mashaytwaan. Uchawi ni yale yanayowaroga watu. Uchawi umeitwa kuwa ni uchawi kwa sababu unafanywa kwa njia ya kujificha.

Uchawi ni uovu na shirki. Kwa sababu mtu hawezi kufikia uchawi isipokuwa kwa kupata msaada kutoka kwa mashaytwaan na mtu huyo akajikurubisha kwao na akawaabudu badala ya Allaah:

وَمَا يُعَلِّمَانِ مِنْ أَحَدٍ حَتَّى يَقُولَا إِنَّمَا نَحْنُ فِتْنَةٌ فَلَا تَكْفُرْ

“Nao wawili hawamfundishi yeyote mpaka waseme [kumwambia mtu huyo]:
“Hakika sisi ni mtihani, basi usikufuru.” (al-Baqarah 02:102)

Ni dalili inayothibitisha kwamba kujifunza uchawi ni kufuru. Kisha akasema (Ta'ala):

1-

وَلَقَدْ عَلِمُوا لَمَنِ اشْتَرَاهُ مَا لَهُ فِي الْآخِرَةِ مِنْ خَلَاقٍ

“Kwa hakika wamekwishaelewa kwamba atakayenunua [kwa kujipatia elimu ya uchawi huo] hatopata katika Aakhirah fungu lolote.”

Kuununua maana yake kuufanya. Mtu kama huyo hana fungu lolote mbele ya Allaah. Hii ni dalili inayoonyesha kwamba uchawi ni uovu na ni haramu:

وَلَوْ أَنَّهُمْ آمَنُوا وَاتَّقَوْا لَمَثُوبَةٌ مِّنْ عِنْدِ اللَّهِ خَيْرٌ ۖ لَّو كَانُوا يَعْلَمُونَ

“Na lau wangeliamini na wakawa na wakamcha Allaah, basi malipo kutoka kwa Allaah yangekuwa ni kheri lau wangekuwa wanajua.” (al-Baqarah 02:103)

Ni dalili inayofahamisha kwamba uchawi ni kinyume na imani na kumcha Allaah. Kwa ajili hiyo wamesema wanachuoni kwamba uchawi ni kufuru na upotevu kwa sababu hakuna njia ya mtu kufikia uchawi isipokuwa mpaka awaabudu majini na mashaytwaan. Imesemekana vilevile kwamba inatakiwa kupambanua; uchawi wenye maana ya kuwaabudu majini na mashaytwaan ni kumkufuru na kumshirikisha Allaah, na uchawi wenye maana ya madawa ambayo hayana mahusiano yoyote na mashaytwaan na kuwaabudu – basi ni haramu, dhambi na uovu mkubwa na vilevile ni kuwadhulumu na kuwashambulia viumbe. Kwa sababu watu wenye kufanya mambo hayo wanaharibu na kuzibadilisha akili za watu.

Allaah (‘Azza wa Jall) amesema:

أَلَمْ تَرَ إِلَى الَّذِينَ أُوتُوا نَصِيحًا مِّنَ الْكِتَابِ يُؤْمِنُونَ بِالْجِبْتِ وَالطَّاغُوتِ

“Je, huzingatii wale ambao wamepewa sehemu ya Kitabu [hapo kale] wanaamini mazimwi na Twaaghuut?”

Aayah hii imeteremka kuhusu mayahudi. Allaah amekhabarisha kwamba wanaamini mazimwi na shaytwaan. Wajuzi wa lugha wamesema kuwa Jibt ni kitu kisichokuwa na kheri ndani yake kama mfano wa uchawi, sanamu na mfano wake. Twaaghuut ni kila chenye kuvukiwa mipaka. Msemo huo unatumiwa kwa mashaytwaan katika majini na watu kwa sababu wamevuka mipaka kwa kufuru na upotevu wao.

2- Jaabir (Radhiya Allaahu ‘anh) amesema:

“Twaaghuut ni makuhani walikuwa wakiteremkiwa na mashaytwaan. Katika kila kabila kuna mmoja.”

Hii ina maana kwamba kuhani ni katika Twaaghuut. Ibn-ul-Qayyim amesema:

“Twaaghuut ni kila chenye kuabudiwa, kufuatwa na kutiwa ambacho mja anachupa kwacho mipaka.”

Bi maana anayefuatwa katika batili na kutiwa katika isiyokuwa Shari'ah ya Allaah. Viongozi wake ni watano:

- 1- Ibliys.
- 2- Mtu anayewaita wengine wamwabudu, kama vile Fir'wan.
- 3- Anayeabudiwa na wakati huohuo akaridhia hilo.
- 4- Anayedai kujua mambo yaliyofichikana.
- 5- Anayehukumu kinyume na yale aliyoteremsha Allaah kwa kukusudia.

Wachawi na makuhani wanaingia katika sampuli hizo kwa sababu wameiacha njia iliyonyooka na kuwakera watu kwa matendo yao.

3- Abu Hurayrah (Radhiya Allaahu 'anh) amesimulia kwamba Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Jiepusheni na dhambi saba zenye kuangamiza.” Wakasema: “Ee Mtume wa Allaah! Ni yepi hayo?” Akasema: “Ni kumshirikisha Allaah, uchawi, kuiua nafsi ambayo Allaah kaiharamisha kuuliwa isipokuwa kwa haki, kula ribaa, kula mali ya mayatima, kukimbia siku ya vita na kuwazulia uongo wa kuzini wanawake waumini waghafilikaji na waliohifadhika.”

Kubwa katika hayo ni shirki. Kisha kunafuata uchawi kwa sababu mara nyingi unatokamana na shirki. Kwani uchawi una maana ya kuwaabudu majini na kuwaomba msaada na kujikurubisha kwao. Baada ya hapo kunafuatia kuiua nafsi ambayo imeharamishwa na Allaah isipokuwa kwa haki, riba, kukimbia siku ya vita ambapo yamekutana makundi mawili katika safu ana kwa ana ambapo mtu akalikimbia kundi lake na kuwatuhumu machafu wanawake waumini wenye kujihifadhi. Tuhuma hapa inahusiana na uchafu wa uzinzi.

Wameitwa waghafilikaji kwa sababu mara nyingi huwa hawatambui waliowatuhumu. Hukumu hiyohiyo inahusiana na wanaume wenye kujihifadhi. Hii ni dhambi kubwa. Mtuhumu anastahiki kusimamishiwa adhabu. Lakini hili mara nyingi linakuwa kwa wanawake. Ndio maana yule mwenye kuwatuhumu anatakiwa kuadhibiwa.

Haijuzu kwenda kwa wachawi kwa ajili ya matibabu hata kama itahusiana na kujitibu. Haijalishi kitu hata kama mtu hayuko radhi na uchawi. Kwa sababu mtu akienda kwa wachawi anaita na kushaji'isha katika shirki na katika yale aliyoharamisha Allaah. Yule mwenye kufanyiwa uchawi ajitibu kwa madawa yenye kuafikiana na Shari'ah. Haya ndio maoni sahihi ya wanachuoni.

4- Jundub (Radhiya Allaahu 'anh) ameeleza kwamba Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Adhabu ya mchawi ni kuuawa kwa upanga.”

Ameipokea at-Tirmidhiy ambaye amesema:

“Sahihi ni kwamba ni maneno ya Swahabah.”

Alisema hivo wakati kulikuwepo mchawi katika kikao cha al-Waliyd bin Yaziyd. Mchawi huyu alikuwa eti anakikata kichwa chake kisha anakirudisha. al-Waliyd akamwendea pasi na yule mchawi kujua kitu na akampiga upanga. Halafu akasema: “Kama ni mkweli basi akirudishe kichwa chake hivi sasa.” Hapo ndipo Jundub akasema hivo. Ni maneno yake aliyoyafikia kutoka katika dalili za Shari'ah. Malengo yake ni kwamba mchawi anatakiwa kuuawa pasi na kumtaka atubie. Kutubia kwake hakuzuii kuuawa. Huenda akawa ni mwenye kudanganya na akadhihirisha kuwa ametubia na madhara yake yakabaki kwa watu. Yule ambaye itathibiti kama kweli ni mchawi basi ni wajibu kumuua ili asije kuwadhuru watu.

5- al-Bukhaariy amepokea katika “as-Swahiyh” yake kupitia kwa Bajaalah bin 'Abadah aliyesimulia:

“'Umar bin al-Khattwaab (Radhiya Allaahu 'anh) aliandika barua ambapo ndani yake kulikuwemo:

“Muueni kila mchawi mwanaume na mchawi mwanamke.”

Tukawaua wachawi watatu.”

Aliwaandikia wakubwa wa majeshi Shaam. Wanatakiwa kuuawa kutokana na yale madhara ambayo hayawezi kutokomea isipokuwa kwa kuuawa. Wao ni waongo, kama wanafiki, wanaweza kujionyesha kwa uinje tu kuwa wametubia. Mchawi anauawa kwa ukafiri na tawbah yake haikubaliwi. Haya ndio maoni sahihi.

6- Imesihi kutoka kwa Hafswah (Radhiya Allaahu 'anhaa) ya kwamba yeye aliamrisha auawe kijakazi wake ambaye alikuwa kamfanyia uchawi ambapo akauawa.” Vivyo hivyo kitendo hicho kimesihi kutoka kwa Jundub (Radhiya Allaahu 'anh) pia.

Ahmad amesema:

“Imesihi kupokelewa kutoka kwa Maswahabah watatu wa Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam).

Bi maana imesihi kupokelewa kutoka kwa Maswahabah watatu wa Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam). Nao ni 'Umar, Jundub na Hafswah (Radhiya Allaahu 'anhum). Haya ndio maoni ya sawa.

Faida

Baadhi ya wanachuoni akiwemo ash-Shaafi'iy wamesema ikiwa uchawi wa mchawi unatokamana na mambo yanayotambulika yanayoudhi/yanayokera na yanasababisha maradhi pasi na kuzigeuza akili na pasi na ndani yake kuna kudai kujua mambo yaliyofichikana na pasi na kuwatumia na kuwataka msaada mashaytwaan na kutumia vyengine alivyoharamisha Allaah, basi asiuawe. Hoja yao ni kwamba haya sio uchawi, bali ni maudhi tu na dhuluma. Mtu huyu

anatakiwa kupigwa na kutiwa adabu. Maswahabah walichokuwa wanalenga kuhusu kuuawa kwa wachawi ni wale wanaowatumia majini na kuwaabudu na kudai kwamba wanajua mambo yaliyofichikana. Hali kama hii ndio hutokea mara nyingi kwa wachawi. Hawa wanatakiwa kuuawa. Haya ndio maoni ya sawa.

Imethibiti kwamba Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) alifanyiwa uchawi. Lakini hata hivyo ni jambo halikuathiri kitu katika mambo ya ujumbe. Yaligusa tu katika mambo yanayohusiana kati yake yeye na familia yake, kama alivyopokea al-Bukhaariy na Muslim⁹⁹.

⁹⁹ al-Bukhaariy (5763) na Muslim (2189).

25. Mfano wa aina za uchawi

Shaykh-ul-Islaam Muhammad bin 'Abdil-Wahhaab (Rahimahu Allaah) amesema:

1- Ahmad amesema: "Muhammad bin Ja'far ametuhadithia: 'Awf ametuhadithia, kutoka kwa Hayyaan bin al-'Alaa': Qutwn bin Qabiyswah ametuhadithia, kutoka kwa baba yake ambaye amemsikia Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) akisema:

"'Iyaafah, Twarq na at-Twiyarah ni katika Jibt."

'Awf amesema:

"'Iyaafah ni kumshtua ndege aruke, Twarq ni misitari inayochorwa katika ardhi na Jibt, al-Hasan amesema, ni nyimbo ya shaytwaan."¹⁰⁰

Cheni ya wapokezi wake ni nzuri.

Abu Daawuud, an-Nasaa'iy na Ibn Hibbaan katika "as-Swahiyyh" yake pia ana upokezi wenye cheni ya wapokezi ilioungana kutoka kwa Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam).

2- Ibn 'Abbaas (Radhiya Allaahu 'anhumaa) ameeleza kwamba Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

"Yeyote atakayejifunza sehemu ya elimu ya nyota basi atakuwa amejifunza sehemu katika uchawi. Vile anavyojizidishia hujizidishia."¹⁰¹

Ameipokea Abu Daawuud na cheni ya wapokezi wake ni Swahiyyh.

¹⁰⁰ Abu Daawuud (3907), Ahmad (20623), at-Twabaraaniy (941) na al-Bayhaqiy (16292). Dhaifu kwa mujibu wa al-Albaaniy katika "Dhwa'iyf-ul-Jaami'" (8336).

¹⁰¹ Abu Daawuud (3905), Ibn Maajah (3726), Ahmad (2841) na al-Bayhaqiy (16290). Swahiyyh kwa mujibu wa al-Albaaniy katika "Swahiyyh-ul-Jaami'" (11019).

3- an-Nasaa'iy amepokea kutoka katika Hadiyth ya Abu Hurayrah (Radhiya Allaahu 'anh) isemayo:

“Atakayefunga fundo kisha akalipuliza, basi atakuwa amefanya uchawi. Mwenye kufanya uchawi atakuwa ameshirikisha. Atakayejifungamanisha na kitu basi huwakilishwa kwacho.”¹⁰²

4- Ibn Mas'uud (Radhiya Allaahu 'anh) amesimulia kwamba Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Je, nisikwambieni ni nini 'Adhwh? Ni kueneza uvumi baina ya watu.”

Ameipokea Muslim.

5- al-Bukhaariy na Muslim wamepokea kupitia kwa Ibn 'Umar (Radhiya Allaahu 'anhuma) ambaye ameeleza kwamba Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Hakika katika ufasaha kuna uchawi.”¹⁰³

MAELEZO

Mwandishi anachotaka ni kutoa baadhi ya mifano ya uchawi ili kumzindua muumini, ajiepushe nao na kujiweka nao mbali. Uchawi unaweza kuitwa kwa njia fulani kwa sababu unadhuru na kukera ijapokuwa uhalisia wa mambo sio uchawi wa aina ya kuwatumia na kuwaabudu mashaytwaan. Hili la pili ni uchawi safi kabisa na lile la kwanza lina athari ya uchawi.

1- Ahmad amesema: “Muhammad bin Ja'far ametuhadithia: 'Awf ametuhadithia, kutoka kwa Hayyaan bin al-'Alaa': Qutwn bin Qabiyswah ametuhadithia,

¹⁰² an-Nasaa'iy (4079) na at-Twabaraaniy katika "al-Awsatw" (1469). Dhaifu kwa mujibu wa al-Albaaniy katika "Ghayaat-ul-Maraam" (288).

¹⁰³ Muslim (2606).

kutoka kwa baba yake ambaye amemsikia Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) akisema:

“'Iyaafah, Twarq na at-Twiyarah ni katika Jibt.”

'Awf amesema:

“'Iyaafah ni kumshtua ndege aruke, Twarq ni misitari inayochorwa katika ardhi na Jibt, al-Hasan amesema, ni nyimbo ya shaytwaan.”

Jibt ni uchawi, kama alivosema 'Umar (Radhiya Allaahu 'anh).

Mambo haya yanaitwa kuwa ni uchawi kwa sababu ya ile shari na ufisadi unaopatikana ndani yake na kwa sababu wafanyayo hayo wakati mwingine wanaweza kudai kujua mambo yaliyofichikana.

'Iyaafah ni kumshtua ndege akaruka, kama alivosema 'Awf. Wanamshtua na wanadai kwamba atawaelekeza juu ya kitu. Wakati fulani huamini mkosi na wakati mwingine wanakuwa na matumaini. Haya ni katika matendo ya kipindi cha kikafiri. Ndege hana kheri wala shari. Haya yanaonyesha ujinga waliokuwa nao watu hawa. Walikuwa wakiamini mkosi kwa jogoo, bundi na wanyama wengine wabaya na wanakuwa na matumaini na kuamini bahati nzuri wanapowaona wanyama wazuri na wanaona kuwa kuna matokeo mazuri.

Twarq ni msitari unachorwa ardhini. Baada ya kuchora wanasema kuwa ni dalili yenye kuonyesha kuwa jambo fulani litatokea. Wakati fulani jambo hilo linaweza kuhusiana na mchezo na wakati mwingine yanaweza kuwa ni mambo ya kiini-macho/mazingaombwe. Uhalisia wa mambo ni kuwatumikia mashaytwaan na kuwatii. Aidha wanadai kwamba wanajua mambo yaliyofichikana. Yote hayo ni uongo usiofidisha kitu.

Jibt ni nyimbo ya shaytwaan.

Twiyarah ni kuamini nuksi kwa kitu cha kuonywa au cha kusikiwa. Kuamini mkosi na nuksi ni haramu na ni shirki ndogo. Inaweza vilevile ikawa shirki

kubwa ikiwa mtu ataamini kuwa ndege huyo anaendesha ulimwengu au uwezo wa kuendesha kitu. Lakini mara nyingi watu huamini mkosi wake tu.

Yote haya ni katika mambo ya kipindi cha kikafiri na ni katika mazimwi. Imesemekana vilevile kwamba ni katika sanamu au kitu kisichokuwa na kheri ndani yake. Kinachokusudiwa ni kwamba kuwashtua ndege kwa njia kama hii imekatazwa kwa sababu ni kujifananisha na matendo ya watu wa kipindi cha kikafiri.

Maneno “Cheni ya wapokezi wake ni nzuri. Abu Daawuud, an-Nasaa’iy na Ibn Hibbaan katika “as-Swahiyyh” yake pia ana upokezi wenye cheni ya wapokezi ilioungana kutoka kwa Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) kunamaanishwa Hadiyyth:

“Iyaafah, Twarq na at-Twiyarah ni katika Jibt.”

Yaliyo baada yake yako kwa Ahmad peke yake.

2- Ibn ‘Abbaas (Radhiya Allaahu ‘anhumaa) ameeleza kwamba Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) amesema:

“Yeyote atakayejifunza sehemu ya elimu ya nyota basi atakuwa amejifunza sehemu katika uchawi. Vile anavyojizidishia hujizidishia.”

Ni dalili inayothibitisha kwamba elimu ya unajimu unaohusiana na kuathiri katika ulimwengu ni batili. Inahusiana na mtu kuamini tafaasiri juu ya nyota zinamaanisha kufa kwa mtu, kuwa hai kwa mtu, kuondoka utawala wa mtu fulani na mfano wa hayo.

Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) amesema:

“Vile anavyojizidishia hujizidishia.”

Bi maana kila anavyojizidishia kujifunza elimu ya unajimu ndivo pia anavyojizidishia uchawi na shari. Kinachokusudiwa hapa ni kwamba nyota zina

taathira katika ulimwengu. Ni dhambi kuamini hivo. Hata hivyo ni sawa kufaidika na nyota na sayari ili mtu kujua ni wapi Qiblah kipo na hali ya hewa. Elimu kama hiyo ni katika neema za Allaah.

Miongoni mwa aina za kuamini mikosi za leo ni kutochinja, kutonunua na kutokuoa katika Swafar. Ni kitendo cha kipindi cha kikafiri.

3- an-Nasaa'iy amepokea kutoka katika Hadiyth ya Abu Hurayrah (Radhiya Allaahu 'anh) isemayo:

“Atakayefunga fundo kisha akalipuliza, basi atakuwa amefanya uchawi. Mwenye kufanya uchawi atakuwa ameshirikisha. Atakayejifungamanisha na kitu basi huwakilishwa kwacho.”

Mwandishi wa kitabu anachotaka ni kutoa baadhi ya mifano ya uchawi kukiwemo kupuliza kwenye fundo. Wachawi hufunga vifundo kisha wanapuliza ndani yake kwa pumzi zao mbaya. Aidha wanashirikiana na na kuwatumikia mashaytwaan. Halafu yanatokea baadhi ya malengo yao kwa idhini ya Allaah. Amesema (Subhaanah):

وَمَا هُمْ بِضَارِّينَ بِهِ مِنْ أَحَدٍ إِلَّا بِإِذْنِ اللَّهِ

“Wao hawawezi kumdhuru yeyote kwayo isipokuwa kwa idhini ya Allaah.” (al-Baqarah 02:102)

Bi maana kwa idhini Yake ya kilimwengu. Ametaja uchawi pale aliposema:

وَمِنْ شَرِّ النَّفَّاثَاتِ فِي الْعُقَدِ

“Na kutokana na uchawi wa wanaopuliza vifundoni.” (al-Falaq 113:04)

Ni wachawi.

Uchawi umegawanyika aina mbili:

- 1- Uchawi unaokuwa kwa vifundo, kupuliza na madawa ya kudhuru. Haya yapo.
- 2- Uchawi unaokuwa kiini-macho na talbisi. Allaah amesema kuhusu wachawi wa Fir'awn:

فَإِذَا حِبَاهُمْ وَعَصِيئُهُمْ يُجَيَّلُ إِلَيْهِ مِنْ سِحْرِهِمْ أَنَّهَا تَسْعَىٰ

“Tahamaki kamba zao na fimbo zao zikaonekana kwake kutokana na uchawi wao kwamba zinakwenda kwa haraka.” (Twaahaa 20:66)

فَلَمَّا أَلْقَوْا سَحَرُوا أَعْيُنَ النَّاسِ وَاسْتَرْهَبُوهُمْ وَجَاءُوا بِسِحْرٍ عَظِيمٍ

“Basi walipotupa [fimbo zao] wakayasihiri macho ya watu na wakawatia woga na wakaja na uchawi mkubwa.” (al-A'raaf 07:116)

Allaah amesema kuwa uchawi wao ulikuwa mkubwa kutokana na vile ulivyowababaisha watu na kuwachanganya machoni mwao.

Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Mwenye kufanya uchawi atakuwa ameshirikisha.”

Kwa sababu kufanya uchawi kunakuwa kwa kuwaabudu mashaytaan na kuwaomba. Kwa ajili hiyo ndio maana amesema:

وَمَا كَفَرَ سُلَيْمَانُ وَلَكِنَّ الشَّيَاطِينَ كَفَرُوا يُعَلِّمُونَ النَّاسَ السِّحْرَ وَمَا أُنزِلَ عَلَى الْمَلَائِكَةِ بِبَابِلَ هَارُوتَ
وَمَارُوتَ ۚ وَمَا يُعَلِّمَانِ مِنْ أَحَدٍ حَتَّى يَقُولَا إِنَّمَا نَحْنُ فِتْنَةٌ فَلَا تَكْفُرْ

“Sulaymaan hakukufuru lakini mashaytaan ndio waliokufuru, wanafundisha watu uchawi na yaliyoteremshwa kwa Malaika wawili katika [mji wa] Baabil, Haaruut na Maaruu. Nao wawili hawamfundishi yeyote mpaka waseme [kumwambia mtu huyo]: “Hakika sisi ni mthani, basi usikufuru.” (al-Baqarah 02:102)

Ni dalili inayothibitisha kwamba kujifunza uchawi ni ukafiri.

Cheni ya wapokezi wa Hadiyth hii ni dhaifu kwa sababu al-Hasan ameipokea kutoka kwa Abu Hurayrah. Kundi la wanachuoni wamesema kuwa al-Hasan hakuisikia kutoka kwa Abu Hurayrah. Kwa hivyo Hadityh inakuwa yenye kukatika. Imepokelewa kupitia kwa 'Ubaadah bin Maysarah na ndani yake kuna udhaifu. Lakini Hadiyth ina yenye kuyatia nguvu kwa upande wa maana.

Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Atakayejifungamanisha na kitu basi huwakilishwa kwacho.”

Mwenye kujifungamanisha na Allaah basi huwakilishwa kwa Allaah kwa msemomwingine Allaah humtosheleza kutokamana na dhiki zake:

أَلَيْسَ اللَّهُ بِكَافٍ عَبْدَهُ

“Je, kwani Allaah si Mwenye kumtosheleza mja Wake?” (az-Zumar 39:36)

وَمَنْ يَتَوَكَّلْ عَلَى اللَّهِ فَهُوَ حَسْبُهُ

“Yeyote anayemtegemea Allaah, basi Yeye humtosheleza.” (at-Twalaq 65:03)

Na yule mwenye kujifungamanisha na kuutegemea uchawi, hirizi na mashaytaan basi Allaah humfungamanishia mambo hayo. Yule atakayemtegemea mwengine asiyekuwa Allaah basi amekhasirika na kuangamia.

4- Ibn Mas'ud (Radhiya Allaahu 'anh) amesimulia kwamba Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Je, nisikwambieni ni nini 'Adhwh? Ni kueneza uvumi baina ya watu.”

Ameipokea Muslim.

Mtunzi wa “al-Qaamus” amesema:

“'Adwh ni uchawi, uongo na uvumi.”

Ameutaja katika mazingira haya kwa sababu uchawi unapelekea katika uzushi, uongo, talbisi na kughushi kati ya watu.

(Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Ni kueneza uvumi baina ya watu.”

Uvumi umeitwa hivo kwa sababu unawadhuru watu na unapelekea katika uongo, uzushi na kuharibu kati ya watu. Kwa ajili hii amesema Yahyaa bin Abiy Kathiy:

“Mvumi na mwongo wanaweza kuharibu kwa saa moja mengi kuliko yale yanayoweza kuharibiwa na mchawi kwa mwaka mmoja.”

Hivo ndivo alivyopokea Ibn 'Abdil-Barr kutoka kwake. Shari yao ni kubwa. Ndio maana Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) akasema:

“Hatoingia Peponi mvumi.”¹⁰⁴

5- al-Bukhaariy na Muslim wamepokea kupitia kwa Ibn 'Umar (Radhiya Allaahu 'anhumaa) ambaye ameeleza kwamba Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

¹⁰⁴ Muslim (105).

“Hakika katika ufasaha kuna uchawi.”

Kwa sababu mtu mwenye ufasaha anaweza kuwaroga watu kwa usulubu na ufasaha wake. Huenda akawababaisha. Huenda akawahadaa na wasibainikiwe na ukweli wa mambo. Wengi wanasema kuwa Hadiyth inasifia ufasaha ikiwa inahusiana na haki. Wengine wanasema kuwa ufasaha unasemwa vibaya, kama alivosema Ibn 'Abdil-Barr kutoka kwa baadhi ya wanachuoni. Lakini hata hivyo ufasaha ikiwa unahusiana na haki na kulingania katika Qur-aan na Sunnah basi ni wenye kusifiwa kama ambavyo ni wenye kusemwa vibaya ikiwa utatumiwa katika kuhadaa na kuwababaisha watu. Hadiyth inaweza kuwa na maana zote mbili. Qur-aan na Sunnah vimekuja kwa ubainisho wa wazi na ufasaha katika kubainisha haki na kuwaita watu katika haki hiyo. Kuna mtu aliyekhutubu kwa ufasaha kabisa mbele na wakati wa 'Umar bin 'Abdil-'Aziyz ambapo akasema:

“Huu ni uchawi halali.”

26. Kuhusu makuhani na mfano wao

Shaykh-ul-Islaam Muhammad bin 'Abdil-Wahhaab (Rahimahu Allaah) amesema:

1- Muslim amepokea katika "as-Swahiyyh" kutoka kwa baadhi ya wakeze Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) ya kwamba Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

"Atakayemwendea mpiga ramli, akamuuliza juu ya kitu na akamsadikisha, basi hazitokubaliwa swalah zake kwa siku arubaini."¹⁰⁵

2- Abu Hurayrah (Radhiya Allaahu 'anh) amesimulia kuwa Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

"Atakayemwendea kunahi na akamsadikisha kwa aliyoyasema, basi amekufuru yale yaliyoteremshwa kwa Muhammad (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam)."¹⁰⁶

Ameipokea Abu Daawuud.

3- Maimamu wane na al-Haakim wamepokea kupitia kwa Abu Hurayrah (Radhiya Allaahu 'anh):

"Atakayemwendea kunahi na akamsadikisha kwa aliyoyasema, basi amekufuru yale yaliyoteremshwa kwa Muhammad (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam)."¹⁰⁷

al-Haakim amesema:

"Hadiyth ni Swahiyyh kwa mujibu wa masharti ya al-Bukhaariy na Muslim.

¹⁰⁵ Muslim (2230).

¹⁰⁶ Abu Daawuud (3904), Ibn Maajah (639) na ad-Daarimiy (1136). Swahiyyh kwa mujibu wa al-Albaaniy katika "as-Silsilah as-Swahiyyah" (3387).

¹⁰⁷ Ahmad (9532), al-Hakim (15) na al-Bayhaqiyy (16273). Swahiyyh kwa mujibu wa al-Albaaniy katika "Swahiyyh-ul-Jaami" (5939).

4- Abu Ya'laa amepokea kwa cheni ya wapokezi nzuri ya kwamba Ibn Mas'uud vilevile amesema hivo.

5- 'Imraan bin Huswayn (Radhiya Allaahu 'anh) amesimulia kuwa Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Si katika sisi yule atakayetafuta au akaomba kubashiriwa mikosi ya ndege, akafanya ukuhani au akafanyiwa ukuhani, akafanya uchawi au akafanyiwa uchawi. Atakayemwendea kuhani na akamsadikisha kwa aliyoyasema, basi amekufuru yale aliyoteremshiwa Muhammad (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam).”

Ameipokea al-Bazaar kwa cheni ya wapokezi nzuri na at-Twabaraaniy amepokea katika “al-Awsatw” kwa cheni ya wapokezi nzuri kupitia kwa Ibn 'Abbaas bila ya ziada ya neno:

“Na atakayemwendea kuhani...”

6- al-Baghawiy amesema: “Mpiga ramli ni yule anayedai kuvijua vitu vilivyoibiwa na vitu vilivyopotea na kama hayo kwa vitangulizi. Imesemekana vilevile kwamba ni kuhani. Kuhani ni yule anayeelezea juu ya vitu vilivyofichikana katika mustakabli. Imesemekana vilevile kwamba ni yule anayeelezea juu ya vitu vilivyomo katika dhamira ya mtu.”

7- Abul-'Abbaas bin Taymiyyah amesema:

“Mpiga ramli ni jina la kuhani, mtabiri wa nyota, mwaguzi na mfano wao katika wanaoongelea kuyajua mambo kwa kutumia njia hizi.”

8- Ibn 'Abbaas amesema kuhusu watu wanaoandika “Abaa Jaad” na wanatazama nyota:

“Sioni wanaofanya hivyo kuwa wana sehemu yoyote mbele ya Allaah.”

MAELEZO

Mlango unaowazungumzia wapiga ramli, waguzi na wengineo wanaodai kuyajua mambo yaliyofichikana.

Makuhani ni wale wanaoshirikiana na majini. Watu kama hawa wanatakiwa kutokomezwa, kuwaaziri, kuwakadhibisha na kutowauliza kitu.

1- Muslim amepokea katika “as-Swahiyyh” kutoka kwa baadhi ya wakeze Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) ya kwamba Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) amesema:

“Atakayemwendea mpiga ramli, akamuuliza juu ya kitu na akamsadikisha, basi hazitokubaliwa swalah zake kwa siku arubaini.”

Wanachuoni wanasema kuwa wakeze ni Hafswah (Radhiya Allaahu ‘anhaa).

Sentesi “na akamsadikisha” haiko katika Muslim. Ima mwandishi ameteleza au amenukuu kutoka katika nusukha ambayo iko na maneno haya. Sentesi “na akamsadikisha” iko kwa Ahmad.

Upokezi kwa Muslim unathibitisha kuwa kule kuwauliza tu haijuzu kwa sababu kunawakweza wapiga ramli na kunapelekea uchawi wao kusadikishwa na kuadhimishwa huko mbeleni. Kwa ajili hiyo inapaswa kuachana nao na kuwapuuza. Muslim amepokea kupitia kwa Mu’aawiyah bin al-Hakam ya kwamba Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) amesema:

“Wao si lolote si chochote. Usiwaendee.”

Hivi ndivo wanavotakiwa kutaamiliwa ili wao na mfano wao watwezwe, wapuuzwe na kutokomezwa.

2- Abu Hurayrah (Radhiya Allaahu ‘anh) amesimulia kuwa Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) amesema:

“Atakayemwendea kunahi na akamsadikisha kwa aliyoyasema, basi amekufuru yale yaliyoteremshwa kwa Muhammad (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam).”

Ameipokea Abu Daawuud.

3- Maimamu wane na al-Haakim wamepokea kupitia kwa Abu Hurayrah (Radhiya Allaahu 'anh):

“Atakayemwendea kunahi na akamsadikisha kwa aliyoyasema, basi amekufuru yale yaliyoteremshwa kwa Muhammad (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam).”

Hadiyth inafahamisha kwamba kuwaendea haijuzu na kuwasadikisha katika mambo yanayohusiana na kudai mambo yaliyofichikana ni kufuru. Kwa sababu hakuna ajuaye mambo yaliyofichikana isipokuwa Allaah pekee. Watu hawa sio Mitume. Kuhani ni kafiri akisema kuwa yeye anajua mambo yaliyofichikana. Mwenye kumsadikisha pia kwamba anajua mambo yaliyofichikana ni kafiri kwa sababu hakuamini maneno Yake (Ta'ala):

قُلْ لَا يَعْلَمُ مَنْ فِي السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ الْغَيْبَ إِلَّا اللَّهُ

“Sema: “Hakuna katika mbingu na ardhi ajuaye yaliyofichikana isipokuwa Allaah.” (an-Naml 27:65)

Kwa ajili hiyo ni wajibu kutahadhari nao.

4- Abu Ya'laa amepokea kwa cheni ya wapokezi nzuri ya kwamba Ibn Mas'uud vilevile amesema hivo.

5- 'Imraan bin Huswayn (Radhiya Allaahu 'anh) amesimulia kuwa Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Si katika sisi yule atakayetafuta au akaomba kubashiriwa mikosi ya ndege, akafanya ukuhani au akafanyiwa ukuhani, akafanya uchawi au akafanyiwa uchawi. Atakayemwendea kuhani na akamsadikisha kwa aliyoyasema, basi amekufuru yale aliyoteremshiwa Muhammad (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam).”

Ameipokea al-Bazaar kwa cheni ya wapokezi nzuri na at-Twabaraaniy amepokea katika “al-Awsatw” kwa cheni ya wapokezi nzuri kupitia kwa Ibn 'Abbaas bila ya ziada ya neno:

“Na atakayemwendea kuhani...”

Haya ni makemeo na ni matishio kwa yule anayefanya mambo kama haya. Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“... si katika sisi.”

Bi maana si katika wale wanaofuata Sunnah ya Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam). Ama kuhusu Takfiyr, japokuwa udhahiri wake unafahamisha Takfiyr, inachukuliwa kutoka katika dalili zengine zilizopambanua suala hili. Haijalishi kitu mtu ameamini mkosi wa ndege juu ya nafsi yake mwenyewe au amewaomba wengine wambashirie mkosi wa ndege, amejifanyia ukuhani mwenyewe au amewaomba wengine wamfanyie ukuhani kwa kuridhia kwake. Kuhusu Takfiyr inatakiwa kupambanuliwa kama tulivyotangulia kusema. Kuwasadikisha ni kufuru kubwa. Mwenye kudai kujua mambo yaliyofichikana basi anatakiwa kuambiwa kutubia. Ima atubie au auawe. Ikiwa atasema kuwa hajui mambo yaliyofichikana, basi atatakiwa kuaziriwa ili asije kurudi tena katika mambo hayo.

6- al-Baghawiy amesema: “Mpiga ramli ni yule anayedai kuvijua vitu vilivyoibiwa na vitu vilivyopotea na kama hayo kwa vitangulizi. Imesemekana vilevile kwamba ni kuhani. Kuhani ni yule anayeelezea juu ya vitu vilivyofichikana katika mustakabli. Imesemekana vilevile kwamba ni yule anayeelezea juu ya vitu vilivyomo katika dhamira ya mtu.”

Vitangulizi inahusiana na vitu anavyopanga na baadaye vinamjulisha mahali kulipoibiwa kitu fulani. Kwa mfano anaweza kujua kwa nyayo za mnyama na nyasi zake. Haya ni mambo yanaweza kutokea, lakini mpiga ramli anakuwa ni

mwenye kusemwa vibaya pindi anapodai kutambua mambo yaliyofichikamana. Ama kuhusu mambo yenye kuhisiwa hayaingii katika mlango huu.

Mpiga ramli anasema vile vilivyomo katika dhamira ya mtu. Hayafikii hayo isipokuwa kwa kuwauliza mashaytwaan na majini.

Faida

Haijuzu kujifunza uchawi kwa hali yoyote ile hata kama lengo la mtu ni kutaka kuzingua uchawi. Kwa sababu mtu hawezi kulifikia hilo isipokuwa kwa kumuabudu asiyekuwa Allaah, kufanya yale aliyoharamisha Allaah au kuacha yale Allaah aliyowajibisha.

7- Abul-'Abbaas bin Taymiyyah amesema:

“Mpiga ramli ni jina la kuhani, mtabiri wa nyota, mwaguzi na mfano wao katika wanaoongelea kuyajua mambo kwa kutumia njia hizi.”

Maandiko yote haya yanafahamisha ya kwamba kuhani, mchawi, mtabiri wa nyota, mwaguzi na mfano wao ni wenye kusemwa vibaya na kwamba wanadai kuyajua mambo yaliyofichikana.

8- Ibn 'Abbaas amesema kuhusu watu wanaoandika “Abaa Jaad” na wanatazama nyota:

“Sioni wanaofanya hivyo kuwa wana sehemu yoyote mbele ya Allaah.”

Bi maana zile herufi za alfabeti a, b, j, d. Wanaziandika herufi hizo, wanaziweka baadhi juu ya zengine na wanasema kwamba kutatokea kitu fulani na fulani. Kusema kwamba hawana sehemu yoyote mbele ya Allaah ni kwamba hawana fungu lolote kwa sababu ni wenye kudai kuyajua mambo yaliyofichikana.

27. Mlango kuhusu kuagua na kuondosha uchawi

Shaykh-ul-Islaam Muhammad bin 'Abdil-Wahhaab (Rahimahu Allaah) amesema:

1- Jaabir (Radhiya Allaahu 'anh) ameeleza kwamba Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) aliulizwa kuhusu kuagua uchawi kwa uchawi ambapo akasema:

“Ni katika matendo ya shaytwaan.”¹⁰⁸

Ameipokea Ahmad kwa cheni ya wapokezi nzuri na Abu Daawuud ambaye amesema:

“Ahmad aliulizwa kuhusiana na hilo ambapo akasema:

“Ibn Mas' uud anachukia yote haya.”

2- al-Bukhaariy amepokea kwamba Qataadah amesema:

“Nilimwambia Ibn al-Musayyab kuhusu mtu ambaye karogwa au anasumbuliwa juu ya mke wake, je, ni halali kwake kuaguliwa?” Akajibu: “Hakuna neno. Hakika wamechokusudia ni kutengeneza. Kuhusu yanayonufaisha hayakukatazwa.”

3- Imepokelewa kwamba al-Hasan amesema:

“Haufungui uchawi isipokuwa mchawi.”

4- Ibn al-Qayyim (Rahimahu Allaah) amesema:

¹⁰⁸ Abu Daawuud (3868), Ahmad (141667), al-Haakim (8292) na al-Bayhaqiy (19397). Swahiyh kwa mujibu wa al-Albaaniy katika “Mishkaat-ul-Maswaabiyh” (4553).

“an-Nushrah ni kuondosha uchawi kwa yule aliyefanyiwa uchawi. Kuna aina mbili:

1- Kuuondosha uchawi kwa kutumia uchawi mwingine. Hili ndio katika matendo ya shaytwaan na ndivyo yanavyotakiwa kufahamika maneno ya al-Hasan. Mchawi na anayefanyiwa uchawi wote wawili wanajikurubisha kwa shaytwaan kwa wanayoyataka. Hivyo shaytwaan anamuondoshea aliyerogwa athari za uchawi.

2- Kuuondosha uchawi kwa Ruqyah, du'aa za kinga na dawa zilizoruhusiwa. Hili linajuzu.

MAELEZO

1- Jaabir (Radhiya Allaahu 'anh) ameeleza kwamba Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) aliulizwa kuhusu kuagua uchawi kwa uchawi ambapo akasema:

“Ni katika matendo ya shaytwaan.”

Ni dalili inayothibitisha kwamba uondoshaji au uaguaji wa uchawi unaotambulika katika kipindi cha kikafiri umekatazwa kwa sababu imetajwa katika fomu ya uhakika. Katika kipindi hicho walikuwa wakiondosha na kuagua uchawi kwa kutumia uchawi mwingine. Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Ni katika matendo ya shaytwaan.”

Kwa sababu mchawi anajikurubisha kwa mashaytwaan kwa yale wanayoyataka kama kuwaabudu na kuwawekea nadhiri. Matokeo yake ndipo wanawaitikia maombi yao kuhusu matendo ya mchawi na yale aliyomfanyia yule aliyerogwa ambayo yamefichikana kwao. Ni katika matendo ya shaytwaan. Ahmad aliulizwa kuhusiana na hilo ambapo akasema:

“Ibn Mas'uud anachukia yote haya.”

Bi maana uaguzi ambao ni katika matendo ya shaytwaan na ambao ndani yake kuna kujikurubisha kwao.

2- al-Bukhaariy amepokea kwamba Qataadah amesema:

“Nilimwambia Ibn al-Musayyab kuhusu mtu ambaye karogwa au anasumbuliwa juu ya mke wake, je, ni halali kwake kuaguliwa?” Akajibu: “Hakuna neno. Hakika wamechokusudia ni kutengeneza. Kuhusu yanayonufaisha hayakukatazwa.”

Maneno haya yanatakiwa kusafiriwa kwamba ni kule kuondosha na kuagua uchawi kwa njia iliyoruhusiwa kwa kutumia Ruqyah, du'aa za kinga na dawa zilizoruhusiwa. Kwa sababu huku ni katika kutengeneza na kutengeneza ni jambo limeamrishwa na maovu yamekatazwa.

3- Imepokelewa kwamba al-Hasan amesema:

“Haufungui uchawi isipokuwa mchawi.”

Hakuna aondoshaye uchawi kwa njia ya kishaytwaan isipokuwa mchawi. Ama kuhusu kuondosha na kuagua uchawi kwa njia inayokubalika katika Shari'ah ni jambo linaloruhusiwa na wanachuoni, wenye uoni wa mbali na wenye uzowefu. Kwa mfano mtu anaweza kusoma al-Faatihah, Aayah ya al-Kursiy au zote mbili pamoja vilevile na kusoma zile Aayah za uchawi katika Suurah “al-A'raaf”, “Twaahaa”, “Yuunus”, “al-Kaafiruun”, “al-Falaq” na “an-Naas” kwa kurudiarudia akasomewa yule aliyerogwa na mke wake na kuwatemea cheche za mate wakati wa kisomo. Ruqyah hii imetumiwa na wanachuoni na Allaah amenufaisha kwayo.

Hapo kale walikuwa wakichukua majani kutoka katika mti wa kijani wa mkunazi, wakayakunjakunja na kuyaweka ndani ya maji. Baadaye Aayah hizi zikasomwa ndani ya maji hayo na baadaye akayanywa yule aliyefanyiwa uchawi mara tatu halafu akayaoga yale ya kubaki. Matokeo yake akapona yule aliyerogwa. Uaguaji na uondoshaji wa uchawi wa sampuli hii ni wenye

kukubalika Kishari'ah na ni dawa zilizoruhusiwa na zilizojaribiwa ambazo hazina makatazo yoyote, si za najisi, ndani yake hakuna kuwakata msaada mashaytwaan wala mambo mengine aliyoharamisha Allaah. Hii ni haki na ni sawa.

4- Ibn al-Qayyim (Rahimahu Allaah) amesema:

“an-Nushrah ni kuondosha uchawi kwa yule aliyefanyiwa uchawi. Kuna aina mbili:

1- Kuuondosha uchawi kwa kutumia uchawi mwingine. Hili ndio katika matendo ya shaytwaan na ndivyo yanavyotakiwa kufahamika maneno ya al-Hasan. Mchawi na anayefanyiwa uchawi wote wawili wanajikurubisha kwa shaytwaan kwa wanayoyataka. Hivyo shaytwaan anamuondoshea aliyerogwa athari za uchawi.

2- Kuuondosha uchawi kwa Ruqyah, du'aa za kinga na dawa zilizoruhusiwa. Hili linajuzu.

Haya yamekwishatangulia.

28. Mlango kuhusu kuamini mkosi na nuksi

Shaykh-ul-Islaam Muhammad bin 'Abdil-Wahhaab (Rahimahu Allaah) amesema:

1- Allaah (Ta'ala) amesema:

فَإِذَا جَاءَتْهُمْ الْحُسْنَةُ قَالُوا لَنَا هَذَا ۗ وَإِنْ تُصِبْهُمْ سَيِّئَةٌ يَطَّيَّرُوا بِمُوسَىٰ وَمَنْ مَّعَهُ ۗ أَلَا إِنَّمَا طَائِرُهُمْ عِنْدَ اللَّهِ وَلَكِنَّ أَكْثَرَهُمْ لَا يَعْلَمُونَ

“Basi yalipowajia mazuri husema: “Hili letu” na pindi likiwapata ovu hunasibisha nuksi kwa Muusa na walio pamoja naye. Tanabahi! Hakika nuksi yao iko kwa Allaah lakini wengi wao hawatambui.” (al-A'raaf 07:131)

2- Allaah (Ta'ala) amesema vilevile:

قَالُوا طَائِرُكُمْ مَعَكُمْ أَئِنْ ذُكِّرْتُمْ بَلْ أَنْتُمْ قَوْمٌ مُّسْرِفُونَ

“Wakasema: “Mkosi wenu uko pamoja nanyi. Je, [mnatutisha] kwa vile mnakumbushwa? Bali nyinyi ni watu wapindukao mipaka!” (Yaasin 36:19)

3- Abu Hurayrah (Radhiya Allaahu 'anh) amesimulia kwamba Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Hakuna maambukizi, kuamini mkosi wa ndege, bundi wala Swafar.”¹⁰⁹

Ameipokea na al-Bukhaariy na Muslim ambaye ameipokea kwa nyongeza:

“... na wala hakuna imani fulani kwa kuchomoza kwa nyota au sayari¹¹⁰ na wala mzimu.”¹¹¹

¹⁰⁹ al-Bukhaariy (5757) na Muslim (2220).

4- al-Bukhaariy na Muslim wamepokea kutoka kwa Anas ambaye amesimulia kwamba amemsikia Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) akisema:

“Hakuna maambukizi wala kuamini mkosi wa ndege. Inanipendeza al-Fa'1.” Akaulizwa: “Na ni nini al-Fa'1?” Akasema: “Ni neno zuri.”¹¹²

5- Abu Daawuud amepokea kwa cheni ya wapokezi nzuri ya kwamba 'Uqbah bin 'Aamir (Radhiya Allaahu 'anh) amesema:

“Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) alitajiwa mkosi wa ndege kisha akasema: “Nzuri yake ni al-Fa'1. [Ndege] isimrudishe nyuma muislamu. Mmoja wenu anapoona yanayomchukiza basi na aseme:

اللهم لا يأتي بالحسنات إلا أنت ، ولا يدفع السيئات إلا أنت ، ولا حول ولا قوة إلا بك

“Ee Allaah! Nakuna awezaye kuleta mambo mema isipokuwa Wewe na hakuna awezaye kuzuia mambo mabaya isipokuwa Wewe na wala hakuna njia na namna wala nguvu isipokuwa zitokane Nawe.”¹¹³

6- Ibn Mas'uud (Radhiya Allaahu 'anh) ameeleza kwamba Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Kuamini mkosi wa ndege ni shirki, kuamini mkosi wa ndege ni shirki. **Wala hakuna yeyote miongoni mwetu asiyehisi hilo, lakini Allaah huuondosha kwa utegemezi.**”¹¹⁴

Ameipokea Abu Daawuud na at-Tirmidhiy ambaye ameisahihisha na kwamba kipande cha maneno ya mwisho ni ya Ibn Mas'uud (Radhiya Allaahu 'anh).

¹¹⁰ Muslim (2220).

¹¹¹ Muslim (2222).

¹¹² al-Bukhaariy (5776) na Muslim (2224).

¹¹³ Abu Daawuud (3919), Ibn Abiy Shaybah (26392) na al-Bayhaqi (16298). Dhaifu kwa mujibu wa al-Albaaniy katika “Dhwa'iyf Sunan Abiy Daawuud” (843).

¹¹⁴ Abu Daawuud (3910), at-Tirmidhiy (1614), Ibn Maajah (3538) na Ahmad (3687). Swahiyh kwa mujibu wa al-Albaaniy katika “Swahiyh Sunan Ibn Maajah” (2850).

7- Ahmad amepokea kupitia kwa Ibn 'Amr:

“Yule ambaye kutokana na kuamini mkosi wa ndege kukamfanya akarudi nyuma na asiifanye haja yake basi ameshirikisha.” Wakasema: “Ni ipi kafara ya hilo?” Akasema: “Ni kusema:

اللهم لا خير إلا خيرك و لا طير إلا طيرك و لا إله غيرك

“Ee Allaah! Hakuna kheri isipokuwa ile inayotokamana na kheri Yako, wala hakuna kuamini mkosi isipokuwa kume kumetokamana Nawe na wala hapana mwabudiwa wa haki isipokuwa Wewe.”¹¹⁵

8- Amepokea vilevile kupitia kwa al-Fadhwl bin 'Abbaas (Radhiya Allaahu 'anhumaa):

“Kuamini mkosi ni kule kukufanyako ufanye kitu fulani au kukurudishe nyuma [usifanye kitu fulani].”¹¹⁶

MAELEZO

Maelezo hayakuja katika kitabu.

¹¹⁵ Ahmad (7045). Swahiyh kwa mujibu wa al-Albaaniy katika "Iswwlaah-ul-Masaajid" (1/116).

¹¹⁶ Ahmad (1824). Cheni ya wapokezi wake ni dhaifu kwa mujibu wa Shu'ayb al-Arnaa'ut.

29. Mlango kuhusu unajimu

Shaykh-ul-Islaam Muhammad bin 'Abdil-Wahhaab (Rahimahu Allaah) amesema:

1- al-Bukhaariy amepokea katika "as-Swahiyyh" yake ya kwamba Qadaatah amesema:

"Allaah ameumba nyota hizi kwa ajili ya mambo mtatu; mapambo ya mbingu, vimondo dhidi ya mashaytwaan na alama za kuongozwa njia. Yeyote atakayefasiri vinginevyo kakosea na kupoteza fungu lake na kajikalifisha kwa kitu asichokuwa na ujuzi nacho."

2- Qadaatah amechukizwa kujifunza elimu ya vituo vya mwezi kama ambavyo Ibn 'Uyaynah pia hakuruhusu hilo. Hayo yamepokelewa na Harb kutoka kwa hao wawili. Ahmad na Ishaq wameruhusu kujifunza elimu ya vituo vya mwezi.

3- Abu Muusa amesimulia ya kwamba Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

"Watu sampuli tatu hawatoingia Peponi; chapombe, mwenye kukata udugu na mwenye kusadikisha uchawi."¹¹⁷

Ameipokea Ahmad na Ibn Hibbaan katika "as-Swahiyyh" yake.

MAELEZO

Mwandishi ametaja unajimu kwa sababu ni kitu kilichoenea. Unajimu ni kule kubahatisha tafaasiri za nyota. Unajimu unahusiana na kujulisha kutokana na hali za nyota yale yatayotendeka ardhini. Matokeo yake wanatazama nyota na namna zilivyokusanyika na zilivyoachana, kuzama kwake na kutua kwake,

¹¹⁷ Ahmad (19587), Ibn Hibbaan (5346) na al-Haakim (7234). Nzuri kupitia zengine kwa mujibu wa Shu'ayb al-Arnaa'uut.

kuwa kwake karibu na kuwa kwake mbali. Kupitia mambo hayo wanajulisha kwamba ardhini kutatokea mambo kadhaa. Jambo hili ni la batili na ni katika kudai kujua mambo yaliyofichikana ambayo yamebatilishwa na Allaah pale aliposema:

قُلْ لَا يَعْلَمُ مَنْ فِي السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ الْغَيْبَ إِلَّا اللَّهُ ۗ وَمَا يَشْعُرُونَ أَيَّانَ يُبْعَثُونَ

“Sema: “Hakuna katika mbingu na ardhi ajuaye yaliyofichikana isipokuwa Allaah na wala hawajui lini watafufuliwa.” (an-Naml 27:65)

Ama kutazama nyota kwa ajili ya kujua mashukio ya mwezi, nyakati za swalah na kujua ni wapi Qiblah kipo ni sawa na hakuna ubaya. Kama alivosema Ahmad na Ishaq bin Raahuyah.

1- al-Bukhaariy amepokea katika “as-Swahiyyh” yake ya kwamba Qadaatah amesema:

“Allaah ameumba nyota hizi kwa ajili ya mambo mtatu; mapambo ya mbingu, vimondo dhidi ya mashaytwaan na alama za kuongozwa njia. Yeyote atakayefasiri vinginevyo kakosea na kupoteza fungu lake na kajikalifisha kwa kitu asichokuwa na ujuzi nacho.”

Allaah (Ta’ala) amesema:

لَقَدْ زَيَّنَّا السَّمَاءَ الدُّنْيَا بِمَصَابِيحَ وَجَعَلْنَاهَا رُجُومًا لِلشَّيَاطِينِ

“Hakika Tumeipamba mbingu ya dunia kwa mataa na tukazifanya kuwa ni makombora kwa mashaytwaan.” (al-Mulk 67:05)

وَعَلَامَاتٍ ۗ وَبِالنَّجْمِ هُمْ يَهْتَدُونَ

“... na [zinawapeni] alama za kutambulisha - na kwa nyota [watu] wanaojiongoza njia.” (an-Nahl 16:16)

Qataadah amesema:

“Yeyote atakayefasiri vinginevyo kakosea na kupoteza fungu lake na kajikalifisha kwa kitu asichokuwa na ujuzi nacho.”

Bi maana mwenye kusema kuwa zinafahamisha jambo fulani katika mambo yaliyofichikana basi amekosea, amepoteza fungu lake na amezungumza asichokuwa nacho ujuzi. Maneno Yake:

وَعَلَامَاتٍ ۚ وَبِالنَّجْمِ هُمْ يَهْتَدُونَ

“... na [zinawapeni] alama za kutambulisha - na kwa nyota [watu] wanaojiongoza njia.”

Hii ni elimu ya mashukio na upepo.

2- Qadaatah amechukizwa kujifunza elimu ya vituo vya mwezi kama ambavyo Ibn 'Uyaynah pia hakuruhusu hilo. Hayo yamepokelewa na Harb kutoka kwa hao wawili. Ahmad na Ishaq wameruhusu kujifunza elimu ya vituo vya mwezi.

Haya ni maoni yasiyokuwa na nguvu. Ahmad na Ishaq wote wawili wameliruhusu hilo na ndio maoni ya sawa.

3- Abu Muusa amesimulia ya kwamba Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Watu sampuli tatu hawatoingia Peponi; chapombe, mwenye kukata udugu na mwenye kusadikisha uchawi.”

Kuhusu chapombe ameambiwa kwa minajili ya kumtishia kwa sababu ni dhambi kubwa. Chapombe anaingia katika utashi wa Allaah muda wa kuwa hajatubia. Lakini ikiwa anaonelea kuwa ni halali anakufuru. Kadhalika kukata udugu ni katika madhambi makubwa.

Ama kuhusu mwenye kuamini uchawi, ikiwa anaona kuwa uchawi ni haki na kwamba unayageuza mambo na kwamba mchawi yuko katika haki na kwamba anajua mambo yaliyofichikana, huyu ni kafiri. Ama ikiwa anaamini kuwa uchawi upo na kwamba una athari lakini pamoja na hivyo akakubali kuwa ni haramu na ni dhambi, huyu hakuna neno juu yake kwa sababu Allaah ameeleza kuhusu kuwepo kwa uchawi:

وَيَتَعَلَّمُونَ مَا يَضُرُّهُمْ وَلَا يَنْفَعُهُمْ

“Wanajifunza yanayowadhuru na wala hayawanufaishi.” (al-Baqarah 02:102)

30. Mlango kuhusu kuomba kunyeshewa mvua kwa sayari

Shaykh-ul-Islaam Muhammad bin 'Abdil-Wahhaab (Rahimahu Allaah) amesema:

1- Allaah (Ta'ala) amesema:

وَجَعَلُونَ رِزْقَكُمْ أَنْكُمْ تُكَذِّبُونَ

“... na mnafanya shukurani za riziki yenu kuwa nyinyi mnakadhibisha.” (al-Waaqi'ah 56:82)

2- Abu Maalik al-Ash'ariy (Radhiya Allaahu 'anhu) ameeleza kwamba Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Mambo mane katika Ummah wangu ni miongoni mwa mambo ya kipindi cha kikafiri na hawatoyaacha; kujifakhari kwa unasabu, kutukaniana nasabu, kuinasibisha mvua kwa nyota na kuomboleza.”

Vilevile amesema:

“Mwanamke mwenye kuomboleza ikiwa hakutubia kabla ya kufa kwake, basi atafufuliwa siku ya Qiyaamah na huku akiwa amevishwa nguo ya shaba iliyoyeyuka na kanzu ya ukoma.”¹¹⁸

Ameipokea Muslim.

3- al-Bukhaariy na Muslim wamepokea kupitia kwa Zayd bin Khaalid (Radhiya Allaahu 'anh) ambaye ameeleza:

“Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) alituswalisha swalah ya Fajr Hudaybiyah baada ya mvua iliyonyesha usiku. Alipomaliza kuswali akawaelekea watu na akasema: “Je, mnajua nini Kasema Mola wenu?” Wakasema: “Allaah na Mtume wake ndio wanajua zaidi.” Akasema: “Katika asubuhi hii kuna baadhi ya waja Wangu wamepambaukia wakiwa ni wenye kuniamini na wengine wamekufuru. Ama yule aliyesema kwamba: “Tumenyeshewa mvua kwa fadhila na rehema ya Allaah”, basi huyo ndiye aliyeniamini Mimi na amekufuru sayari. Ama yule aliyesema ya kwamba tumenyeshewa mvua kutokana na sayari fulani na fulani, basi huyo amenikufuru Mimi na ameamini sayari.”¹¹⁹

Imepokelewa na al-Bukhaariy na Muslim.

4- al-Bukhaariy na Muslim wamepokea kupitia kwa Ibn 'Abbaas upokezi wenye maana kama hio na ndani yake imekuja:

¹¹⁸ Muslim (934).

¹¹⁹ al-Bukhaariy (1038) na Muslim (71).

“Baadhi yao wamesema: “Sayari fulani imesema kweli.” Ndipo Allaah akateremsha Aayah ifuatayo:

فَلَا أُفْسِمُ بِمَوَاقِعِ النُّجُومِ وَإِنَّهُ لَقَسَمٌ لَّوْ تَعْلَمُونَ عَظِيمٌ إِنَّهُ لَقُرْآنٌ كَرِيمٌ فِي كِتَابٍ مَّكْنُونٍ لَا يَمَسُّهُ إِلَّا
الْمُطَهَّرُونَ تَنْزِيلٌ مِّن رَّبِّ الْعَالَمِينَ أَفَبِهَذَا الْحَدِيثِ أَنْتُمْ مُذْهِبُونَ وَتَجْعَلُونَ رِزْقَكُمْ أَنْكُمْ تُكَذِّبُونَ

“Basi Naapa kwa maangukio ya nyota – na hakika hicho ni kiapo kikubwa mno, lau mngelielewa! – hakika hii bila shaka ni Qur-aan karimu, katika Kitabu kilichohifadhiwa, hakuna akigusaye isipokuwa waliotakaswa, ni uteremsho kutoka kwa Mola wa walimwengu! Je, kwa maneno haya nyinyi ni wenye kuitweza na kuikanusha na mnafanya shukurani za riziki yenu kuwa nyinyi mnakadhibisha... ” (al-Waaqi’ah 56:75-82)

MAELEZO

Allaah ameweka katika Shari’ah kuomba kunyeshewa mvua. Kuomba kunyeshewa mvua maana yake ni kunyenyekea mbele ya Allaah wakati wa ukame. Washirikina wao hawafanyi hivo ambao wanaziomba nyota kuwanyeshea mvua, kufungamana nazo na kuziomba msaada. Walikuwa wakiziomba nyota kuwateremshia mvua. Nyota ndio sayari. Mwezi na jua vinaizunguka. Mwezi unaenda kwa mwezi na jua linaenda kwa mwaka. Wakati wa kipindi cha kikafiri walikuwa wakifungamana navyo na wakiviomba msaada. Hili ni kutokana na shirki na upotevu wao.

1- Allaah (Ta’ala) amesema:

وَتَجْعَلُونَ رِزْقَكُمْ أَنْكُمْ تُكَذِّبُونَ

“... na mnafanya shukurani za riziki yenu kuwa nyinyi mnakadhibisha.”

Wanakadhibisha kwamba ni Allaah ndiye ameteremsha mvua na kukunyweshelezeni. Badala yake mnaziomba nyota na kuzitaka msaada. Ndipo

Allaah akawakadhibisha, kwa sababu nyota hizi hazinufaishi, hazidhuru na wala hazimiliki kitu katika mambo hayo. Kwa hivyo ni wajibu kwa waumini kuamini yale aliyoeleza Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam), kushikamana nayo na kujiepusha na matendo ya kipindi cha kikafiri. Mfano miongoni mwa matendo yao ni:

2- Abu Maalik al-Ash'ariy (Radhiya Allaahu 'anhu) ameeleza kwamba Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Mambo mane katika Ummah wangu ni miongoni mwa mambo ya kipindi cha kikafiri na hawatoyaacha; kujifakhari kwa unasabu, kutukaniana nasabu, kuinasibisha mvua kwa nyota na kuomboleza.”

Watu wataendelea kuyafanya mambo haya na kuwaiga makafiri ikiwa ni pamoja na:

1- Kujifakhari kwa unasabu. Ina maana kwamba mtu akajifakhari kwamba baba yake ni fulani, akajikweza kwa hilo na akatumia hoja juu ya batili yake na kujifakharisha kwa wengine. Unasabu ni yale waliokuwa nayo mababu kama vile athari, ushujaa, wingi wa kutoa na ukarimu. Hii ni sifa ya wakati wa kipindi cha kikafiri. Mtu anakuwa juu kutokamana na matendo yake na si kwa matendo ya wengine.

2- Kutukaniana nasabu. Ina maana kwamba mtu akamtukana mwengine kwa sababu ni fundi seremala, mshumaji, anazungumza kwa njia ya kumtweza. Ama akizungumza kwa njia ya kuelezea hakuna neno.

3- Kuinasibisha mvua kwa nyota. Ima anasema kuwa tumepata mvua kwa sababu ya nyota fulani au mtu anaiomba moja kwa moja.

4- Kuomboleza. Pindi maiti anapokufa basi wanapiga ukelele, wanachana nguo, wanakokota nywele zao na kujirushia udongo usoni. Haya yote yanafanywa na baadhi ya waislamu. Ni wajibu kutahadhari nayo na kukipiga vita kitendo hichi. Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Si katika sisi yule mwenye kujipiga mashavu, akachana nguo au akaita kwa wito wa kipindi cha kikafiri.”¹²⁰

Amesema vilevile:

“Mimi niko mbali kabisa na mwanamke anayenyanyua sauti yake, mwenye kuzinyoa nywele zake na mwenye kuzipasua nguo zake wakati wa msiba.”¹²¹

Vilevile amesema (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam):

“Mwanamke mwenye kuomboleza ikiwa hatotubia kabla ya kufa kwake, basi atafufuliwa siku ya Qiyaamah na huku akiwa amevishwa nguo ya shaba iliyoyeyuka na kanzu ya ukoma.”

Mara nyingi wanawake ndio wenye kuomboleza. Ndio maana (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amentaja mwanamke. Inawezekana vilevile mwanaume akaomboleza. Kuomboleza kumeharamishwa kwa wanaume na kwa wanawake wote wawili. Imetajwa nguo ya shaba iliyoyeyuka kwa sababu apate adhabu yenye kuumiza kwelikweli. Kadhalika kanzu ya ukoma kwa sababu ya maudhi. Haya yanaonyesha ubaya wa mwisho wake ikiwa hatotubia.

Masuala: Ni sawa kwa mtu kumuoa mwanamke mwenye dini asiyetokamana na familia yenye kabila tukufu ikiwa mwanaume huyo anachelea watu wake wasije kumuudhi. Kwa sharti asiwe amewaacha kwa sababu ya kuwatweza na kuwadharau.

Faida: Baadhi ya vijiji wanachinja vichinjwa juu kwenye vilele vya milima ili waweze kupata mvua. Hii ni shirki kubwa kwa sababu ni kuwachinjia majini, mawe na masanamu. Huenda kweli wakanyeshewa na mvua, inakuwa ni majaribio kwao.

¹²⁰ al-Bukhaariy (1294) na Muslim (103).

¹²¹ al-Bukhaariy kwa cheni ya wapokezi iliopungua na Muslim (104).

3- al-Bukhaariy na Muslim wamepokea kupitia kwa Zayd bin Khaalid (Radhiya Allaahu 'anh) ambaye ameeleza:

“Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) alituswalisha swalah ya Fajr Hudaibiyah baada ya mvua iliyonyesha usiku. Alipomaliza kuswali akawaelekea watu na akasema: “Je, mnajua nini Kasema Mola wenu?” Wakasema: “Allaah na Mtume wake ndio wanajua zaidi.” Akasema: “Katika asubuhi hii kuna baadhi ya waja Wangu wamepambaukia wakiwa ni wenye kuniamini na wengine wamekufuru. Ama yule aliyesema kwamba: “Tumenyeshewa mvua kwa fadhila na rehema ya Allaah”, basi huyo ndiye aliyeniamini Mimi na amekufuru sayari. Ama yule aliyesema ya kwamba tumenyeshewa mvua kutokana na sayari fulani na fulani, basi huyo amenikufuru Mimi na ameamini sayari.”

Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) anapomaliza kuswali alikuwa na mazoweza ya kumuomba Allaah msamaha mara tatu kisha anasema:

اللَّهُمَّ أَنْتَ السَّلَامُ وَمِنْكَ السَّلَامُ تَبَارَكْتَ يَا ذَا الْجَلَالِ وَالْإِكْرَامِ

“Ee Allaah! Hakika Wewe ni mkamilifu usiyokuwa na mapungufu na amani inatoka Kwako. Umetukuka, ee Mwenye utukufu na ukarimu.”

Halafu anawaelekea watu na anasoma adhkaar zilizobaki.

Watu wakasema:

“Allaah na Mtume wake ndio wanajua zaidi.”

Hii ilikuwa ni katika adabu waliokuwa nayo Maswahabah (Radhiya Allaahu 'anhum). Baada ya kufa kwa Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) inatakiwa kusema “Allaah ndiye anajua zaidi” peke yake. Kwa sababu Wahy umekatika. Yeye (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) hajui yanayoendelea baada ya kufa kwake. Dalili ya hilo ni Hadiyth ya hodhi. Isipokuwa tu yale

anayoonyeshwa na Allaah kama pale anaposwaliwa (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam).

Allaah ('Azza wa Jall) amesema:

“... basi huyo ndiye aliyeniamini Mimi na amekufuru sayari.”

Kwa sababu ametambua kuwa Allaah ndiye kateremsha mvua. Mvua hii inatokamana na rehema na fadhilah za Allaah.

Allaah ('Azza wa Jall) amesema:

“Ama yule aliyesema ya kwamba tumenyeshewa mvua kutokana na sayari fulani na fulani, basi huyo amenikufuru Mimi na ameamini sayari.”

Ni aina ya kufuru. Haitakiwi kusema sayari fulani ilisema kweli au kwamba tumepata mvua kwa sababu ya sayari fulani. Bali kinachotakiwa kusema ni:

“Tumenyeshewa mvua kwa fadhila na rehema ya Allaah.”

Mwenye kusema kuwa tumepata mvua kwa sababu ya sayari fulani na wakati huohuo anamaanisha kwamba sayari ndio imeumba mvua na kuiendesha, basi hiyo ni kufuru kubwa. Ama ikiwa anamaanisha kuwa sayari hiyo ni sababu iliopelekea katika kupata mvua, basi hiyo ni kufuru ndogo kwa sababu anaona kuwa Allaah (Ta'ala) ndiye kaumba mvua na sio sayari. Nyota hutokea kwa matukio kama vile michana na nyusiku vinavyotokea kwa matukio. Hata hivyo mtu akisema kwa mfano kwamba wakati wa kipwa tulipata mvua hakuna neno kwa sababu huku ni kueleza tu yaliyotokea katika wakati. Kwa hivyo ni wajibu kutahadhari na tabia hizi za kipindi cha kikafiri na kuzitambua neema za Allaah (Subhaanah) kwa moyo.

31. Mlango kuhusu maneno Yake (Ta'ala) “Miongoni mwa watu wako wenye kuchukua asiyekuwa Allaah kuwa ni mungu mshirika ambapo wanawapenda kama mapenzi wanavyompenda Allaah... “

Shaykh-ul-Islaam Muhammad bin 'Abdil-Wahhaab (Rahimahu Allaah)
amesema:

1- Allaah (Ta'ala) amesema:

وَمِنَ النَّاسِ مَن يَتَّخِذُ مِن دُونِ اللَّهِ أَنَدَادًا يُحِبُّونَهُمْ كَحُبِّ اللَّهِ

“Miongoni mwa watu wako wenye kuchukua asiyekuwa Allaah kuwa ni mungu mshirika ambapo wanawapenda kama mapenzi wanavyompenda Allaah... “ (al-Baqarah 02:165)

2-

قُلْ إِن كَانَ آبَاؤُكُمْ وَأَبْنَاؤُكُمْ وَإِخْوَانُكُمْ وَأَزْوَاجُكُمْ وَعَشِيرَتُكُمْ وَأَمْوَالٌ اقْتَرَفْتُمُوهَا وَتِجَارَةٌ تَخْشَوْنَ كَسَادَهَا
وَمَسَاكِينُ تَرْضَوْنَهَا أَحَبَّ إِلَيْكُمْ مِّنَ اللَّهِ وَرَسُولِهِ وَجِهَادٍ فِي سَبِيلِهِ فَتَرَبَّصُوا حَتَّى يَأْتِيَ اللَّهُ بِأَمْرِهِ وَاللَّهُ لَا
يَهْدِي الْقَوْمَ الْفَاسِقِينَ

“Sema: “Ikiwa baba zenu na watoto wenu na ndugu zenu na wake zenu na jamaa zenu na mali mliyoichuma na biashara mnayoikhofia kuharibika kwake na majumba mnayoridhika nayo - [ikiwa vyote hivi] ni vipenzi zaidi kwenu kuliko Allaah na Mtume Wake na kupambana jihaad katika njia Yake, basi ngojeeni

mpaka Allaah alete Amri Yake; hakika Allaah hawaongoi watu mafasiki.” (**at-Tawbah 09:24**)

3- Anas (Radhiya Allaahu ‘anh) ameeleza kwamba Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) amesema:

“Hatoamini mmoja wenu mpaka mimi niwe kwake ni mpendwa zaidi kuliko baba yake, mtoto wake na watu wote.”¹²²

Ameipokea al-Bukhaariy na Muslim.

4- al-Bukhaariy na Muslim wamepokea kwamba Anas (Radhiya Allaahu ‘anh) amesimulia kuwa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) amesema:

“Mambo matatu yakipatikana kwa mtu hupata utamu wa imani; Allaah na Mtume Wake wawe ni wenye kupendwa zaidi kwake kuliko yeyote yule, ampende mtu na asimpendei jengine isipokuwa iwe ni kwa ajili ya Allaah na achukie kurudi katika ukafiri baada ya Allaah kumwokoia nao kama anavyochukia kutupwa ndani ya Moto.”¹²³

Katika upokezi mwingine imekuja:

“Hatopata mmoja wenu utamu wa imani mpaka...”¹²⁴

5- Ibn ‘Abbaas (Radhiya Allaahu ‘anhuma) amesema:

“Mwenye kupenda kwa ajili ya Allaah na akachukia kwa ajili ya Allaah, kufanya urafiki kwa ajili ya Allaah na kujenga uadui kwa ajili ya Allaah, hakika hupatikana urafiki wa Allaah kwa hayo. Na wala mja hatohisi utamu wa imani - hata kama zitakuwa nyingi swalah na swawm zake - mpaka awe hivo. Leo watu

¹²² al-Bukhaariy (15) na Muslim (44).

¹²³ al-Bukhaariy (16) na Muslim (43).

¹²⁴ al-Bukhaariy (6041).

wengi wamekuwa ni wenye kujenga udugu kwa ajili ya mambo ya kidunia, hilo haliwasaidii wenye nalo kitu.”

Ameipokea Ibn Jariyr.

6- Ibn 'Abbaas amesema kuhusu maneno Yake Allaah (Ta'ala):

إِذْ تَبَرَّأَ الَّذِينَ اتَّبَعُوا مِنَ الَّذِينَ اتَّبَعُوا وَرَأُوا الْعَذَابَ وَتَقَطَّتْ بِهِمُ الْأَسْبَابُ

“Wale waliofuatwa watakapojitenga mbali na wale waliowafuata wakiwa wameshaiona adhabu [mbele yao] na yatawakatika mafungamano yao.”

“Bi maana mapenzi.”

MAELEZO

1- Allaah (Ta'ala) amesema:

وَمِنَ النَّاسِ مَن يَتَّخِذُ مِن دُونِ اللَّهِ أَنْدَادًا يُحِبُّونَهُمْ كَحُبِّ اللَّهِ

“Miongoni mwa watu wako wenye kuchukua asiye kuwa Allaah kuwa ni mungu mshirika ambapo wanawapenda kama mapenzi wanavyompenda Allaah...”

Mlango huu unazungumzia mapenzi kwa Allaah na kwamba ni miongoni mwa 'ibaadah muhimu na bora zaidi na msingi wa dini. Kwa sababu kumpenda Allaah kunapelekea kumtakasia Yeye 'ibaadah, kutekeleza maamrisha Yake na kujiepusha na makatazo Yake.

Aayah inathibitisha kwamba wapo watu ambao wanamfanyia Allaah washirika katika masanamu, watu na mawe. Wanawaabudu kwa mapenzi anayostahiki kupendwa Allaah pekee. Wanawapenda washirika hawa kama mapenzi wanavyompenda Allaah au kama waumini wanavyompenda Allaah. Watu hawa wamepotea kwa vile wamewapenda wengine pamoja na Allaah, wamewawekea nadhiri, wamewanyenyekea na kuwaomba. Mapenzi ya kuwapenda wengine

yanatakiwa kuwa ni yenye kuafikiana na mapenzi ya Allaah. Kwa mfano tunawapenda Mitume wa Allaah kwa sababu ni Mitume wa Allaah, hatuwaabudu kwa mapenzi haya. Kadhalika tunawapenda waumini; tunawapenda kwa sababu wamemtii Allaah na hivyo tunawasapoti. Ama kuhusu mapenzi ya kujidhalilisha na mapenzi ya 'ibaadah anatakiwa kutekelezewa Allaah pekee. Hayawi kwa mwengine. Washirikina wanawatekelezea mapenzi haya washirika. Bali baadhi yao wanathubutu kuapa kwa jina la Allaah kwa kusema uongo na wala hawawezi kuthubutu kufanya hivo kwa washirika wao na wanachuoni wao kwa sababu wanaona kuwa washirika hawa wanalipiza kisasi vibaya sana na kwa haraka kuliko Allaah.

Allaah (Ta'ala) amesema:

وَالَّذِينَ آمَنُوا أَشَدُّ حُبًّا لِلَّهِ

“Lakini wale walioamini wana mapenzi zaidi kwa Allaah.”

Ni mapenzi yenye nguvu na zaidi kabisa kuliko mapenzi ya washirikina hawa kwa waungu wao kwa sababu wanamwabudu Allaah kwa kumpwekesha na wanatambua haki Yake ('Azza wa Jall).

Allaah (Ta'ala) amesema:

وَلَوْ يَرَى الَّذِينَ ظَلَمُوا إِذْ يَرُونَ الْعَذَابَ أَنَّ الْقُوَّةَ لِلَّهِ جَمِيعًا وَأَنَّ اللَّهَ شَدِيدُ الْعَذَابِ

“Lau wale waliodhulumu wanaijua [adhabu inayowasubiri] watakapoona adhabu [mbele yao siku hiyo] kwamba nguvu zote ni za Allaah na kwamba hakika Allaah ni mkali wa kuadhibu.” (al-Baqarah 02:165)

Lau wangeliyaona hayo basi wangelimpenda Allaah zaidi, wakamuadhimisha na wangelimtakasia Yeye 'ibaadah. Lakini kwa sababu ya ujinga wao na uchache wa uoni wao kumewafanya kutumbukia katika shirki. Allaah (Ta'ala) amesema:

إِذْ تَبَرَّأَ الَّذِينَ اتَّبَعُوا مِنَ الَّذِينَ اتَّبَعُوا وَرَأَوْا الْعَذَابَ وَتَقَطَّتْ بِهِمُ الْأَسْبَابُ

“Wale waliofuatwa watakapojitenga mbali na wale waliowafuata wakiwa wameshaiona adhabu [mbele yao] na yatawakatika mafungamano yao.”

Wakati wale mawalii wa Allaah waliokuwa wakiabudiwa watakapoona adhabu ndipo watajiweka mbali kabisa na wale waliokuwa wakiwaabudu. Watasema:

رَبَّنَا هَؤُلَاءِ الَّذِينَ أَعْوَيْنَا كَمَا عَوَيْنَا ۖ تَبَرَّأْنَا إِلَيْكَ ۖ مَا كَانُوا إِيَّانَا يَعْبُدُونَ

“Mola wetu! Hawa ndio wale tuliowapotoa. Tumewapotoa kama tulivyopotoka. Tumejivua jukumu mbele Yako - hawakuwa wakituabudu sisi.” (al-Qaswasw 28:63)

Ama kuhusu mapenzi ya kimaumbile kama kupenda chakula, wanawake na watoto, mapenzi haya hayapunguzi mapenzi ya kumpenda Allaah midhali mtu hayatangulizi mbele kabla ya mapenzi ya kumpenda Yeye. Ikiwa yatapitiliza na kuwa na nguvu kiasi cha kwamba kwa mfano mtu akawa anamtii mke wake katika maasi, basi mapenzi haya yanapunguza imani kwa kiasi cha vile mtu atavyoyatanguliza mbele ya mapenzi ya Allaah. Ni lazima mapenzi haya yafungamanishwe na Shari'ah ya Allaah.

3- Anas (Radhiya Allaahu 'anh) ameeleza kwamba Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Hatoamini mmoja wenu mpaka mimi niwe kwake ni mpendwa zaidi kuliko baba yake, mtoto wake na watu wote.”

Ameipokea al-Bukhaariy na Muslim.

Hii ni dalili inayothibitisha kwamba ni wajibu kumpenda Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) yanayolingana naye yanayopelekea kumfuata na kutii maamrishi yake na kujiepusha na makatazo yake. Haihusiani na

mapenzi ya kumwabudu (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam); ni lazima yawe ni yenye kuafikiana na mapenzi ya kumpenda Allaah.

4- al-Bukhaariy na Muslim wamepokea kwamba Anas (Radhiya Allaahu 'anh) amesimulia kuwa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Mambo matatu yakipatikana kwa mtu hupata utamu wa imani; Allaah na Mtume Wake wawe ni wenye kupendwa zaidi kwake kuliko yeyote yule, ampende mtu na asimpendei jengine isipokuwa iwe ni kwa ajili ya Allaah na achukie kurudi katika ukafiri baada ya Allaah kumwokoia nao kama anavyochukia kutupwa ndani ya Moto.”

Katika upokezi mwingine imekuja:

“Hatopata mmoja wenu utamu wa imani mpaka...”

Ni dalili inayothibitisha kwamba mapenzi ya kumpenda Allaah na Mtume Wake (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) yanatakiwa kutangulizwa mbele ya mapenzi ya kuwapenda mababa, watoto, mali na vyenginevyo. Hivyo mtu anatakiwa kumtii Allaah na kujiepusha na makatazo Yake japokuwa yatakuwa ni yenye kupingana na matamania ya mtoto wake, mke wake au wengineo. Allaah amesema:

قُلْ إِنْ كَانَ آبَاؤُكُمْ وَأَبْنَاؤُكُمْ وَإِخْوَانُكُمْ وَأَزْوَاجُكُمْ وَعَشِيرَتُكُمْ وَأَمْوَالٌ اقْتَرَفْتُمُوهَا وَتِجَارَةٌ تَخْشَوْنَ كَسَادَهَا
وَمَسَاكِينُ تَرْضَوْنَهَا أَحَبَّ إِلَيْكُمْ مِّنَ اللَّهِ وَرَسُولِهِ وَجِهَادٍ فِي سَبِيلِهِ فَتَرَبَّصُوا حَتَّى يَأْتِيَ اللَّهُ بِأَمْرِهِ وَاللَّهُ لَا
يَهْدِي الْقَوْمَ الْفَاسِقِينَ

“Sema: “Ikiwa baba zenu na watoto wenu na ndugu zenu na wake zenu na jamaa zenu na mali mliyoichuma na biashara mnayoikhofia kuharibika kwake na majumba mnayoridhika nayo - [ikiwa vyote hivi] ni vipenzi zaidi kwenu kuliko

Allaah na Mtume Wake na kupambana jihaad katika njia Yake, basi ngojeeni mpaka Allaah alete Amri Yake; hakika Allaah hawaongoi watu mafasiki.”

Ni dalili inayothibitisha kwamba Jihaad katika njia ya Allaah inatakiwa kutangulizwa mbele kabla ya matamanio ya nafsi na ya jamaa wa karibu. Vinginevyo mtu anakuwa ni mwenye kuingia katika makemeo:

فَتَرْتَضُوا حَتَّى يَأْتِيَ اللَّهُ بِأَمْرِهِ وَاللَّهُ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الْفَاسِقِينَ

“... basi ngojeeni mpaka Allaah alete Amri Yake; hakika Allaah hawaongoi watu mafasiki.”

Hizi ni miongoni mwa sababu za ukamilifu wa imani. Ni wajibu kuchukua ukafiri na makafiri na kuitakidi ubatilifu wake.

Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) amesema:

“Watu saba Allaah atawafunika katika kivuli siku ambayo kutakuwa hakuna kivuli isipokuwa kivuli Chake; kiongozi mwadilifu, kijana ambaye amekulia katika kumuabudu Allaah, mtu ambaye moyo wake umefungamana na misikiti, watu wawili ambao wamependana kwa ajili ya Allaah na hivyo wakakusanyika kwa ajili Yake na wakatengana kwa ajili Yake, mtu ambaye ameitwa na mwanamke mwenye cheo na akasema “Mimi namuogopa Allaah, Mola wa walimwengu”, mtu ambaye ametoa swadaqah kisiri kabisa mpaka mkono wake wa kushoto haujui kile kilichotolewa na mkono wake wa kulia na mtu ambaye amemkumbuka Allaah akiwa peke yake na akaanza kutitikwa na machozi.”

Zingatia “watu wawili ambao wamependana kwa ajili ya Allaah na hivyo wakakusanyika kwa ajili Yake na wakatengana kwa ajili Yake”.

5- Ibn ‘Abbaas (Radhiya Allaahu ‘anhumaa) amesema:

“Mwenye kupenda kwa ajili ya Allaah na akachukua kwa ajili ya Allaah, kufanya urafiki kwa ajili ya Allaah na kujenga uadui kwa ajili ya Allaah, hakika

hupatikana urafiki wa Allaah kwa hayo. Na wala mja hatopata utamu yawa imani - hata kama zitakuwa nyingi swalah na swawm zake - mpaka awe hivo. Leo watu wengi wamekuwa ni wenye kujenga udugu kwa ajili ya mambo ya kidunia, hilo haliwasaidii wenye nalo kitu.”

Ameipokea Ibn Jariyr.

Utamu wa imani ni ladha ya imani. Ni dalili inayoonyesha kuwa urafiki wa Allah unapatikana kwa kupenda na kuchukia kwa ajili ya Allaah. Ibn 'Abbaas (Radhiya Allaahu 'anhumaa) amesema:

“Na wala mja hatohisi utamu wa imani - hata kama zitakuwa nyingi swalah na swawm zake - mpaka awe hivo.”

Bi maana mpaka apende na kuchukia kwa ajili ya Allaah. Amesema:

“Leo watu wengi wamekuwa ni wenye kujenga udugu kwa ajili ya mambo ya kidunia, hilo haliwasaidii wenye nalo kitu.”

Haya yalikuwa katika wakati wake (Radhiya Allaahu 'anhumaa). Watu wengi walikuwa ni wenye kupendana na ni wenye kuchukiana kwa ajili ya dunia. Hili ni jambo khatari. Halisaidii kitu. Bali ni jambo linawadhuru ikiwa linawazuia kutokamana na haki na kwenda kinyume na Shari'ah ya Allaah. Hata hivyo hakuna neno ikiwa watafanya kazi kwa ajili ya dunia katika biashara na kutafuta riziki ili waweze kumtii Allaah midhali mambo hayo hayadhuru imani yao na wala hayawapelekei kuingia katika madhambi.

6- Ibn 'Abbaas amesema kuhusu maneno Yake Allaah (Ta'ala):

إِذْ تَبَرَّأَ الَّذِينَ اتَّبَعُوا مِنَ الَّذِينَ اتَّبَعُوا وَرَأَوْا الْعَذَابَ وَتَقَطَّعَتْ بِهِمُ الْأَسْبَابُ

“Wale waliofuatwa watakapojitenga mbali na wale waliowafuata wakiwa wameshaiona adhabu [mbele yao] na yatawakatika mafungamano yao.”

“Bi maana mapenzi.”

Bi maana mapenzi yaliokuwa baina yao yasiyoafikiana na dini ya Allaah. Yatakatika siku ya Qiyaamah, watafanyiana khiyana na yatakuwa uadui.

32. Mlango kuhusu maneno Yake (Ta'ala) ”Hakika huyo ni shaytwaan anawakhofisha marafiki zake. Basi msiwakhofu - na nikhofuni Mimi - mkiwa ni waumini!”

Shaykh-ul-Islaam Muhammad bin 'Abdil-Wahhaab (Rahimahu Allaah) amesema:

1- Allaah (Ta'ala) amesema:

إِنَّمَا دُلِّكُمُ الشَّيْطَانُ يُخَوِّفُ أَوْلِيَاءَهُ فَلَا تَخَافُوهُمْ وَخَافُوا إِن كُنْتُمْ مُؤْمِنِينَ

”Hakika huyo ni shaytwaan anawakhofisha marafiki zake. Basi msiwakhofu - na nikhofuni Mimi - mkiwa ni waumini!” (Aal 'Imraan 03:175)

2-

إِنَّمَا يَعْمُرُ مَسَاجِدَ اللَّهِ مِنْ آمَنَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ وَأَقَامَ الصَّلَاةَ وَآتَى الزَّكَاةَ وَلَمْ يَخْشَ إِلَّا اللَّهَ

”Hakika wanaoamirisha misikiti ya Allaah ni wale wanaomwamini Allaah na siku ya Mwisho na wakasimamisha swalah na wakatoa zakaah na hawamkhofu yeyote isipokuwa Allaah.” (at-Tawbah 09:18)

3-

وَمَنْ النَّاسِ مَنْ يَقُولُ آمَنَّا بِاللَّهِ فَإِذَا أُوذِيَ فِي اللَّهِ جَعَلَ فِتْنَةَ النَّاسِ كَعَذَابِ

”Miongoni mwa watu wako wasemao “Tumemwamini Allaah”; lakini wanapofanyiwa maudhi kwa ajili ya Allaah, hufanya mitihani ya watu kama kwamba ni adhabu ya Allaah.” (an-'Ankabuut 29:10)

4- Abu Sa'iyd (Radhiya Allaahu 'anh) ameeleza kwamba Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Hakika katika udhaifu wa yakini ni kuwaridhisha watu kwa yanayomkasirisha Allaah, kuwasifu kutokana na riziki iliyoruzuku Allaah na kuwasema vibaya kwa kitu ambacho Allaah hakukuruzuku. Hakika riziki ya Allaah hailetwi kwa mbio za mwenye kuipupia na wala haizuiwi kwa chuki za mwenye kuchukia.”¹²⁵

5- 'Aaishah (Radhiya Allaahu 'anhaa) amesimulia kwamba Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Yule mwenye kutaka radhi za Allaah kwa yanayowachukiza watu, basi Allaah atamridhia na pia watu watamridhia. Na yule mwenye kutaka radhi za watu kwa yanayomchukiza Allaah, basi Allaah atamkasirikia na watu pia watamkasirikia.”¹²⁶

Ameipokea Ibn Hibbaan katika “as-Swahiyyh” yake.

MAELLEZO

1- Allaah (Ta'ala) amesema:

إِنَّمَا دُلِّكُمُ الشَّيْطَانُ يُخَوِّفُ أَوْلِيَاءَهُ فَلَا تَخَافُوهُمْ وَخَافُوا مِنِّي إِن كُنْتُمْ مُؤْمِنِينَ

“Hakika huyo ni shaytwaan anawakhofisha marafiki zake. Basi msiwakhofu - na nikhofuni Mimi - mkiwa ni waumini!” (Aal 'Imraan 03:175)

Anachokusudia mwandishi ni kwamba ni wajibu kumuogopa Allaah (Ta'ala) khofu ambayo itamfanya kumtakasia Yeye 'ibaadah, kutekeleza maamrisho aliyomfaradhishia na kusimama katika mipaka Yake. Khofu imegawanyika aina tatu:

¹²⁵ at-Twabaraaniy (10514). Imezuliwa kwa mujibu wa al-Albaaniy katika “adh-Dhwa'iyfah” (1482).

¹²⁶ at-Tirmidhiy (2414) na Ibn Hibbaan (276). Swahiyyh kwa mujibu wa al-Albaaniy katika “Swahiyyh-ul-Jaami” (6097).

1- Kumuogopa Allaah. Hii ndio kubwa na muhimu zaidi. Inamfanya mtu kumtakasia 'ibaadah Yeye pekee. Ni shirki kumtekelezea khofu kama hii mwingine asiyekuwa Allaah. Ni shirki kumuogoa mwingine asije kukudhuru.

2- Khofu inayomfanya mtu kuacha mambo ya wajibu au kufanya mambo ya haramu. Kuwaogopa viumbe. Khofu hii ndio ambayo kwa ajili yake kumeteremshwa maneno Yake (Ta'ala):

فَلَا تَخَافُوهُمْ وَخَافُونِ إِنْ كُنْتُمْ مُؤْمِنِينَ

“Basi msiwakhofu - na nikhofuni Mimi - mkiwa ni waumini!”

Khofu hii inamfanya mtu kutotoka kwenda katika Jihaad. Ni wajibu kwa mtu asimwogope kiumbe mwenzake. Khofu inayoruhusiwa tu ni ile ambayo inamfanya mtu kuyafanya yale yaliyowekwa na Shari'ah na Allaah na akayaruhusu. Isiwe ni khofu yenye kumfanya akatenda madhambi. Hata hivyo hakuna neno mtu akamwogopa kiumbe katika mambo ya kimaumbile. Hii ni khofu ya kimaumbile. Imewekwa katika Shari'ah mtu akaogopa vitu vyenye kushtua kama kwa mfano akafunga milango ili wezi wasiingie, akabeba silaha dhidi ya mashambulizi ya wanyama wakali au akajitibu dhidi ya maradhi. Mlango huu unahusiana na aina hii ya pili ya khofu. Nayo ndio shaytwaan aliyowafanya waislamu kuwaogopa makafiri katika Uhud na wakabweteka kutotaka kutoka kwenda katika Jihaad. Ndipo Allaah akawakataza na akawaamrisha kuwa imara ambapo Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) akawafuata makafiri moja kwa moja baada ya vita vya Uhud, lakini hakukutokea vita kwa sababu walikimbia.

3- Khofu ya kimaumbile kama kwa mfano kuwaogopa wanyama wakali, maradhi na mfano wake.

2-

إِنَّمَا يَعْمُرُ مَسَاجِدَ اللَّهِ مِنْ آمَنَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ وَأَقَامَ الصَّلَاةَ وَآتَى الزَّكَاةَ وَمِمَّا يَخْشَى إِلَّا اللَّهَ

“Hakika wanaoamirisha misikiti ya Allaah ni wale wanaomwamini Allaah na siku ya Mwisho na wakasimamisha swalah na wakatoa zakaah na hawamkhofu yeyote isipokuwa Allaah.”

Hii ndio khofu aliyowajibisha Allaah. Vilevile khofu ya kimaumbile na ya kawaida inafaa kama tulivyotangulia kusema.

3-

وَمِنَ النَّاسِ مَنْ يَقُولُ آمَنَّا بِاللَّهِ فَإِذَا أُوذِيَ فِي اللَّهِ جَعَلَ فِتْنَةَ النَّاسِ كَعَذَابِ

“Miongoni mwa watu wako wasemao “Tumemwamini Allaah”; lakini wanapofanyiwa maudhi kwa ajili ya Allaah, hufanya mitihani ya watu kama kwamba ni adhabu ya Allaah.”

Hapa wanasemwa vibaya. Baadhi ya watu wanapoudhiwa basi hawawezi kusubiri. Kinyume chake khofu hiyo inawafanya kutendea kazi yale aliyoharamisha Allaah na kuacha kumtii na yale aliyoyaamrisha. Huku ni kusemwa vibaya kwa sababu ni wajibu kumuogopa Allaah. Pindi mtu anapoudhiwa kwa ajili ya Allaah, basi afanye zile sababu zinazoafikiana na Shari’ah na kwenda mahakamani, kumshtakia mtawala na mfano wa hayo.

4- Abu Sa’iyd (Radhiya Allaahu ‘anh) ameeleza kwamba Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) amesema:

“Hakika katika udhaifu wa yakini ni kuwaridhisha watu kwa yanayomkasirisha Allaah, kuwasifu kutokana na riziki iliyoruzuku Allaah na kuwasema vibaya kwa kitu ambacho Allaah hakukuruzuku. Hakika riziki ya Allaah hailetwi kwa mbio za mwenye kuipupia na wala haizuiwi kwa chuki za mwenye kuchukia.”

Ni dalili inayoonyesha udhaifu wa imani kumkasirisha Allaah katika mambo yanayowaridhisha watu na kuwashukuru watu juu ya neema uliyotunukiwa na

Allaah kupitia wao. Kilicho cha wajibu ni kumshukuru Allaah. Watu wakikufanyia wema washukuru na uwalipe, lakini shukurani zote njema anastahiki Allaah pekee ambaye ndiye kawafanya wakutendee wema. Kwa hivyo ni wajibu kumshukuru Allaah kwanza halafu ndio baadaye uwashukuru viumbe kwa kiasi cha wema wao. Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Asiyewashukuru watu hamshukuru Allaah.”

Lakini hata hivyo shukurani kwa Allaah ndio zinatakiwa kuwa kubwa zaidi kwa sababu Yeye ndiye kasababisha na ndiye kawafanya watu kukutendea wema. Hadiyth inasema:

“... na kuwasema vibaya kwa kitu ambacho Allaah hakukuruzuku.”

Kuwasema vibaya kwa sababu hawakukufanyia kitu ambacho Allaah amekuwa amekuandikia. Ni wajibu kwako kumuomba Allaah katika fadhilah Zake. Ikiwa watu wako na haki yako basi tambua kuwa Allaah hatopoteza. Utaipata siku ya Qiyaamah. Lakini hata hivyo hii haina maana kwamba hili linazuia mtu kutoomba haki yake, kama vile haki yake ya zakaah ikiwa ni katika wenye kuistahiki kupewa, lakini usiwaseme vibaya kwa sababu hawakukupa kitu. Bali unatakiwa kumsema vibaya yule aliyesemwa vibaya na Allaah na kumsifu yule aliyesifiwa na Allaah. Waseme vibaya kwa sababu hawakutekeleza haki ya Allaah na wanafanya mambo ya haramu, lakini sio kwa sababu hawakukupa. Usiwe ni mwenye kulipiza kisasi juu ya nafsi yako. Hadiyth inasema:

“Hakika riziki ya Allaah hailetwi kwa mbio za mwenye kuipupia na wala haizuiwi kwa chuki za mwenye kuchukia.”

Kile ambacho hukuandikiwa hakipatikani kwa mbio za kukipupia. Bali unachotakiwa wewe ni kufanya sababu. Usipopata kile unachotafuta basi usivunjike moyo. Kadhalika hakuna yeyote awezaye kuzuia kile ambacho Allaah amekwishakuandikia japokuwa watu watachukia.

5- 'Aaishah (Radhiya Allaahu 'anhaa) amesimulia kwamba Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Yule mwenye kutaka radhi za Allaah kwa yanayowachukiza watu, basi Allaah atamridhia na pia watu watamridhia. Na yule mwenye kutaka radhi za watu kwa yanayomchukiza Allaah, basi Allaah atamkasirikia na watu pia watamkasirikia.”

Ameipokea Ibn Hibbaan katika “as-Swahiyyh” yake.

Ni dalili inayoonyesha kuwa ni wajibu kwa muislamu kutafuta radhi za Allaah na kufanya sababu kuzipata. Kwa sababu ukiridhiwa na Allaah basi umepata kheri zote na akikukasirikia basi umepata shari zote. Kumridhisha Allaah haina maana kwamba mtu asifanye zile sababu zitazofanya watu kutomkasirikia. Lakini hayo yasifanywe kwa kumkasirisha Allaah. Lakini kama kuna kitu kinachomkasirisha Allaah basi usikifanye. Katika hali kama hiyo usiwaogope watu, bali mtegemee Allaah. Katika upokezi mwingine kutoka kwa 'Aaishah imekuja:

“Yule mwenye kutaka radhi za Allaah kwa yanayowachukiza watu, basi Allaah atamtosheleza. Na yule mwenye kutaka radhi za watu kwa yanayomchukiza Allaah hatotoshelezwa nao dhidi ya Allaah – yule asiyemsifu atakuja kumsema vibaya.”

33. Mlango kuhusu maneno Yake (Ta'ala) “Kwa Allaah pekee tegemeeni ikiwa nyinyi ni waumini!”

Shaykh-ul-Islaam Muhammad bin 'Abdil-Wahhaab (Rahimahu Allaah)
amesema:

1- Allaah (Ta'ala) amesema:

وَعَلَى اللَّهِ فَتَوَكَّلُوا إِن كُنْتُمْ مُؤْمِنِينَ

“Kwa Allaah pekee tegemeeni ikiwa nyinyi ni waumini!” (al-Maaidah 05:23)

2-

إِنَّمَا الْمُؤْمِنُونَ الَّذِينَ إِذَا ذُكِرَ اللَّهُ وَجِلَتْ قُلُوبُهُمْ وَإِذَا تُلِيَتْ عَلَيْهِمْ آيَاتُهُ زَادَتْهُمْ إِيمَانًا وَعَلَىٰ رَبِّهِمْ يَتَوَكَّلُونَ

“Hakika waumini ni wale ambao anapotajwa Allaah nyoyo zao zinajaa khofu, na wanaposomewa Aayah Zake huwazidishia imani na kwa Mola wao wanategemea.” (al-Anfaal 08:02)

3-

يَا أَيُّهَا النَّبِيُّ حَسْبُكَ اللَّهُ وَمَنِ اتَّبَعَكَ مِنَ الْمُؤْمِنِينَ

“Ee Nabii! Anakutoshele za Allaah na anayekufuata miongoni wa waumini.” (al-Anfaal 08:64)

4-

وَمَنْ يَتَوَكَّلْ عَلَى اللَّهِ فَهُوَ حَسْبُهُ

“Na yeyote yule atakayemtegemea Allaah, basi Yeye humtosheleza.” (at-Twalaq 65:03)

5- Ibn 'Abbaas (Radhiya Allaahu 'anhumaa) amesema:

حَسْبُنَا اللَّهُ وَنِعْمَ الْوَكِيلُ

“Allaah pekee anatutosheleza na Yeye ndiye mbora wa kutegemewa.”

neni hili lilisemwa na Ibraahiym ('alayhis-Salaam) alipotupwa ndani ya moto na alilisema Muhammad (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) wakati alipoambiwa:

الَّذِينَ قَالَ لَهُمُ النَّاسُ إِنَّ النَّاسَ قَدْ جَمَعُوا لَكُمْ فَاخْشَوْهُمْ فَزَادَهُمْ إِيمَانًا

“Wale ambao waliambiwa na watu: “Hakika watu wamekusanyika dhidi yenu hivyo basi waogopeni”; yakawazidishia imani... ¹²⁷ (Aal 'Imraan 03:173)

Ameipokea al-Bukhaariy na an-Nasaa'iy.

MAELEZO

1- Allaah (Ta'ala) amesema:

وَعَلَى اللَّهِ فَتَوَكَّلُوا إِن كُنْتُمْ مُؤْمِنِينَ

“Kwa Allaah pekee tegemeeni ikiwa nyinyi ni waumini!”

Alichokusudia mwandishi (Rahimahu Allaah) kwa mlango huu ni kwamba lililo la wajibu ni kumtegemea Allaah na kuegemea Kwake katika mambo yote ya dini na ya dunia. Kutegemea maana yake ni kumwachia kila kitu Allaah, kumwamini, kuamini kwamba Yeye ndiye anasababisha sababu na kwamba kila kitu kiko mikononi Mwake; kwamba Anachotaka huwa na Asichotaka hakiwi. Aidha

¹²⁷ al-Bukhaariy (4563).

anatakiwa kutambua kuwa tayari kumeshapangwa kila kitu na kwamba mja hana uwezo wa chochote anachotaka ikiwa Allaah (Subhaanahu wa Ta'ala) hakukikadiria. Vilevile kutegemea kunahusiana na mtu kufanya sababu.

2-

إِنَّمَا الْمُؤْمِنُونَ الَّذِينَ إِذَا ذُكِرَ اللَّهُ وَجِلَتْ قُلُوبُهُمْ وَإِذَا تُلِيَتْ عَلَيْهِمْ آيَاتُهُ زَادَتْهُمْ إِيمَانًا وَعَلَىٰ رَبِّهِمْ يَتَوَكَّلُونَ

“Hakika waumini ni wale ambao anapotajwa Allaah nyoyo zao zinajaa khofu, na wanaposomewa Aayah Zake huwazidishia imani na kwa Mola wao wanategemea.”

3-

يَا أَيُّهَا النَّبِيُّ حَسْبُكَ اللَّهُ وَمَنِ اتَّبَعَكَ مِنَ الْمُؤْمِنِينَ

“Ee Nabii! Anakutoshele za Allaah na anayekufuata miongoni wa waumini.”

4-

وَمَنْ يَتَوَكَّلْ عَلَى اللَّهِ فَهُوَ حَسْبُهُ

“Na yeyote yule atakayemtegemea Allaah, basi Yeye humtosheleza.”

Allaah atakutosheleza wewe na wafuasi wako na msiwahitajie wengine. Yule ambaye yuko na Allaah hamuhitajii mwingine. Ni wajibu kwa muumini kumtegemea Allaah pamoja vilevile na kufanya sababu zinazonufaisha duniani na Aakhirah na aziepuke sababu zinazomdhuru duniani na Aakhirah. Anapaswa kufanya matendo mema na kujiepusha na maasi ili aweze kupata Pepo. Anatakiwa kula na kunywa na kujiepusha na yale yote yenye kumdhuru. Kwa sababu haya ni sababu ya [kuendelea] kuishi kwake. Haya hayapingani na kutegemea. Kutegemea kumekusanya mambo mawili:

1- Kumwamini Allaah na kwamba Yey ndiye anayesababisha sababu na anayeyaendesha mambo.

2- Kufanya sababu.

Kutegemea haina maana kwamba mtu aache kufanya sababu, kama wanavosema Suufiyyah. Bali mja anatakiwa kukusanya yote mawili na wakati huohuo amwombe Allaah msaada.

5- Ibn 'Abbaas (Radhiya Allaahu 'anhumaa) amesema:

حَسْبُنَا اللَّهُ وَنِعْمَ الْوَكِيلُ

“Allaah pekee anatutosheleza na Yeye ndiye mbora wa kutegemewa.”

neni hili lilisemwa na Ibraahiym ('alayhis-Salaam) alipotupwa ndani ya moto na alilisema Muhammad (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) wakati alipoambiwa:

الَّذِينَ قَالَ لَهُمُ النَّاسُ إِنَّ النَّاسَ قَدِ جَمَعُوا لَكُمْ فَآخِشُوهُمْ فَرَادَهُمْ إِيمَانًا

“Wale ambao waliambiwa na watu: “Hakika watu wamekusanyika dhidi yenu hivyo basi waogopeni”; yakawazidishia imani...”

Ameipokea al-Bukhaariy na an-Nasaa'iy.

Ibraahiym ('alayhis-Salaam) alisema hivo wakati Namruud alipomtuma ndani ya moto. Allaah akamwokoia kutokamana na moto huo na:

قُلْنَا يَا نَارُ كُونِي بَرْدًا وَسَلَامًا عَلَىٰ إِبْرَاهِيمَ

“Tukasema: “Ee moto! Kuwa baridi na salama kwa Ibraahiym!” (al-Anbiyaa' 21:69)

Allaah akamlinda kutokamana na shari yake na shari zao na akamwoko ya yeye na akawa ni ishara na miujiza inayofahamisha juu ya ukweli wa ujumbe wake. Kadhalika yalisemwa na Muhammad (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) wakati alipoambiwa kwamba washirikika wamekusanyika kwa ajili ya kuwashambulia kwa mara nyingine. Ndipo Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) akasema:

حَسْبُنَا اللَّهُ وَنِعْمَ الْوَكِيلُ

“Allaah pekee anatutosheleza na Yeye ndiye mbora wa kutegemewa.”

Ndipo Allaah akamlinda.

Hivi ndivyo anvyotakiwa muislamu kusema wakati wa matatizo. Lakini haina maana kwamba asifanye sababu. Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) alisema hivo na akafanya maandalizi ya vita, akabeba silaha na akavaa kofia maalum kwa ajili ya vita. Vivyo hivyo wakafanya Maswahabah. Wakati wa vita vya Ahzaab walichimba handaki. Allaah (Ta'ala) amesema:

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا خُذُوا حِذْرَكُمْ فَانفِرُوا تُبَاتٍ أَوْ انفِرُوا جَمِيعًا

“Enyi mlioamini! Shikeni hadhari yenu; tokeni makundi moja moja au tokeni kwa pamoja.” (an-Nisaa' 04:71)

34. Mlango kuhusu maneno Yake (Ta'ala) “Je, wameaminisha na mipango ya Allaah? Basi hawaaminishi mipango ya Allaah isipokuwa watu wenye kukhasirika.”

Shaykh-ul-Islaam Muhammad bin 'Abdil-Wahhaab (Rahimahu Allaah) amesema:

1-

Allaah (Ta'ala) amesema:

أَفَأَمِنُوا مَكْرَ اللَّهِ ۗ فَلَا يَأْمَنُ مَكْرَ اللَّهِ إِلَّا الْقَوْمُ الْخَاسِرُونَ

“Je, wameaminisha na mipango ya Allaah? Basi hawaaminishi mipango ya Allaah isipokuwa watu wenye kukhasirika.” (al-A'raaf 07:99)

2-

وَمَنْ يَغْنَطُ مِنْ رَحْمَةِ رَبِّهِ إِلَّا الضَّالُّونَ

“Na nani anayekata tamaa na rehema ya Mola wake isipokuwa waliopotea.” (al-Hijr 15:56)

3- Ibn 'Abbaas (Radhiya Allaahu 'anhumaa) amesimulia kwamb Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) aliulizwa kuhusiana na madhambi makubwa halafu ambapo akajibu:

“Kumshirikisha Allaah, kukata tamaa na rehema ya Allaah na kujiaminisha na mipango/njama za Allaah.”¹²⁸

4- Ibn Mas'ud (Radhiya Allaahu 'anh) ameeleza kwamba kwamba Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Madhambi makubwa kabisa ni kumshirikisha Allaah, kujiaminisha mipango/njama za Allaah, kukata tamaa na rehema ya Allaah na kukata tamaa na rafaja ya Allaah.”¹²⁹

Ameipokea 'Abdur-Razzaaq.

MAELEZO

1-

Allaah (Ta'ala) amesema:

أَفَأَمِنُوا مَكْرَ اللَّهِ ۗ فَلَا يَأْمَنُ مَكْرَ اللَّهِ إِلَّا الْقَوْمُ الْخَاسِرُونَ

“Je, wameaminisha na mipango ya Allaah? Basi hawaaminishi mipango ya Allaah isipokuwa watu wenye kukhasirika.”

2-

وَمَنْ يَغْتَبِطْ مِنْ رَحْمَةِ رَبِّهِ إِلَّا الضَّالُّونَ

“Na nani anayekata tamaa na rehema ya Mola wake isipokuwa waliopotea.”

Mlango huu unazumgumzia kwamba ni haramu kujiaminisha na njama za Allaah, kukatika moyo na rehema ya Allaah na baadhi ya madhambi mengine makubwa. Kujiaminisha na njama za Allaah ni dhambi kubwa na ni jambo

¹²⁸ Majma'-uz-Zawaa-id (1/104).

¹²⁹ Majma'-uz-Zawaa-id (1/104).

linapelekea mtu kuchukulia wepesi na maharamisho ya Allaah. Kwa sababu yule ambaye atajiaminisha na njama za Allaah basi matendo yake, tabia yake na mienendo yake itakuwa miovu na hatomcha Allaah.

Kukata tamaa na faraja ya Allaah ndio kukata tamaa na rehema ya Allaah. Kutaka tamaa na faraja ya Allaah ni kumdhania vibaya Allaah na kuvunjika moyo. Muislamu anapaswa awe kati na kati; anatakiwa kutarajia rehema ya Allaah na kuogopa kwa sababu ya madhambi yake. Asizame katika maasi na akajiaminisha na njama za Allaah. Vilevile hatakiwi kukata tamaa na rehema ya Allaah. Anatakiwa awe kama ndege na mbawa mbili. Baadhi ya wanachuoni wamependekeza kuwa na khofu zaidi wakati mtu yuko na afya njema, kwa sababu ambaye ana afya njema ana uwezo mkubwa wa kutendea kazi maasi, na kuwa na matarajio zaidi wakati wa ugonjwa, kwa sababu mgonjwa ni mdhaifu wa kufanya matendo mema. Msingi ni kwamba anatakiwa awe kati na kati kwa hayo mawili.

3- Ibn 'Abbaas (Radhiya Allaahu 'anhumaa) amesimulia kwamb Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) aliulizwa kuhusiana na madhambi makubwa halafu ambapo akajibu:

“Kumshirikisha Allaah, kukata tamaa na rehema ya Allaah na kujiaminisha na mipango/njama za Allaah.”

Haya yamepokelewa kutoka kwa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) na kutoka kwa Swahabah. Hata kama yamesemwa na Swahabah, yana hukumu moja kama maneno ya Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) kwa sababu hawezi kusema hivo kutoka kichwani mwake mwenyewe. Inawezekana vilevile kayasema Ibn 'Abbaas kutoka kichwani mwake mwenyewe kwa kutegemea dalili kutoka katika Qur-aan na Sunnah. Kwa hali yoyote ile ni maneno sahihi.

4- Ibn Mas'uud (Radhiya Allaahu 'anh) ameeleza kwamba kwamba Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Madhambi makubwa kabisa ni kumshirikisha Allaah, kujiaminisha mipango/njama za Allaah, kukata tamaa na rehema ya Allaah na kukata tamaa na rafaja ya Allaah.”

Ameipokea 'Abdur-Razzaaq.

Shirki ndio dhambi kubwa kabisa kwa sababu inaporomoshha matendo mengine yote. Vilevile kuvunjika moyo na faraja ya Allaah, ambako ni kule kukata tamaa kwa kiasi kikubwa, ni dhambi kubwa. Allaah (Ta'ala) amesema:

وَمَنْ يَفْتِنُ مِنْ رَحْمَةِ رَبِّهِ إِلَّا الضَّالُّونَ

“Na nani anayekata tamaa na rehema ya Mola wake isipokuwa waliopotea.”

Hili ni swali limeulizwa kwa njia ya makanusho. Bi maana hii ni sifa ya wapotevu peke yao.

Ama kuhusu madhambi makubwa mengine yote, hayaporomoshi matendo mema.

35. Kuwa na subira kwa makadirio ya Allaah ni katika kumuamini Allaah

Shaykh-ul-Islaam Muhammad bin 'Abdil-Wahhaab (Rahimahu Allaah) amesema:

1- Allaah (Ta'ala) amesema:

مَا أَصَابَ مِنْ مُصِيبَةٍ إِلَّا بِإِذْنِ اللَّهِ ۗ وَمَنْ يُؤْمِن بِاللَّهِ يَهْدِ اللَّهُ قَلْبَهُ ۚ وَاللَّهُ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمٌ

“Hausibu msiba wowote [kukupateni] isipokuwa kwa idhini ya Allaah. Yeyote anayemuamini Allaah, basi huuongoza moyo wake. - Allaah kwa kila kitu ni mjuzi.” (at-Taghaabuun 64:11)

'Alqamah amesema:

“Huyo ni yule mtu ambaye anapofikwa na msiba anajua kuwa umetoka kwa Allaah, basi akaridhika na akajisalimisha.”

2- Muslim amepokea katika “as-Swahiyyh” yake kupitia kwa Abu Hurayrah (Radhiya Allaahu 'anh) ya kwamba Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Mambo mawili kwa watu ni kufuru; kutukaniana nasabu na kuomboleza juu ya maiti.”¹³⁰

3- al-Bukhaariy na Muslim wamepokea kupitia kwa Ibn Mas'uud (Radhiya Allaahu 'anh) kutoka kwa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) kwamba amesema:

¹³⁰ Muslim (67).

“Si katika sisi yule mwenye kujipiga kwenye mashavu, akachana nguo na akaita kwa mayowe ya kipindi cha kikafiri.”¹³¹

4- Anas (Radhiya Allaahu ‘anh) amesimulia ya kwamba Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) amesema:

“Allaah anapomtakia mja Wake kheri, basi humharakishia adhabu duniani, na anapomtakia mja Wake shari, humcheleweshea adhabu ya dhambi yake mpaka siku ya Qiyaamah.”¹³²

5- Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) amesema:

“Ukubwa wa malipo ni pamoja na ukubwa wa mitihani. Hakika Allaah (Ta’ala) anapowapenda watu basi huwapa huwajaribu. Yule mwenye kuridhia basi hupara radhi Zake na yule mwenye kuchukia basi hupata hasira Zake.”¹³³

Ni nzuri kwa mujibu wa at-Tirmidhiy.

MAELEZO

Mwandishi alichotaka ni kubainisha kwamba kuwa na subira juu ya makadirio ya Allaah ni katika imani na kwamba ni wajibu kwa muumini kutokata tamaa wakati anapofikwa na msiba kwake mwenyewe, mwana wake, mali yake au familia yake. Anachotakiwa ni yeye kuvuta subira. Allaah (Ta’ala) amesema:

وَلَنْبَلُوْكُمْ بِشَيْءٍ مِّنَ الْخَوْفِ وَالْجُوعِ وَنَقْصٍ مِّنَ الْأَمْوَالِ وَالْأَنْفُسِ وَالثَّمَرَاتِ ۗ وَبَشِّرِ الصَّابِرِينَ الَّذِينَ إِذَا
أَصَابَتْهُمْ مُصِيبَةٌ قَالُوا إِنَّا لِلَّهِ وَإِنَّا إِلَيْهِ رَاجِعُونَ

¹³¹ al-Bukhaariy (1294) na Muslim (103).

¹³² at-Tirmidhiy (2396), al-Haakim (8799) na Abu Ya’laa (4254). Swahiyh kwa mujibu wa al-Albaaniy katika “Swahiyh-ul-Jaami” (308).

¹³³ at-Tirmidhiy (2396) na Ibn Maajah (4031). Nzuri kwa mujibu wa al-Albaaniy katika “Swahiyh-ul-Jaami” (2110).

“Bila shaka Tutakujaribuni kwa kitu kidogo katika khofu na njaa na upungufu wa mali na nafsi na mazao [ya kazi zenu]. Wabashirie wenye kusubiri ambao unapowafika msiba basi husema: “Hakika sisi ni wa Allaah na hakika sisi Kwake ni wenye kurejea.” (al-Baqarah 02:155-156)

وَاصْبِرُوا ۚ إِنَّ اللَّهَ مَعَ الصَّابِرِينَ

“Subirini! Hakika Allaah yupamoja na wenye kusubiri.” (al-Anfaal 08:46)

إِنَّمَا يُوفَّى الصَّابِرُونَ أَجْرَهُمْ بِغَيْرِ حِسَابٍ

“Hakika wale wenye kusubiri watalipwa kikamilifu ujira wao pasi na hesabu.” (az-Zumar 39:10)

Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

“Yule ambaye atafanya subira basi Allaah atamsubirisha. Hakuna yeyote aliyepewa zawadi bora na pana kama subira.”¹³⁴

1- Allaah (Ta´ala) amesema:

مَا أَصَابَ مِنْ مُصِيبَةٍ إِلَّا بِإِذْنِ اللَّهِ ۗ وَمَنْ يُؤْمِنْ بِاللَّهِ يَهْدِ اللَّهُ قَلْبَهُ ۗ وَاللَّهُ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمٌ

“Hausibu msiba wowote [kukupateni] isipokuwa kwa idhini ya Allaah. Yeyote anayemuamini Allaah, basi huuongoza moyo wake. - Allaah kwa kila kitu ni mjuzi.”

´Alqamah amesema:

¹³⁴ al-Bukhaariy (1469) na Muslim (1053).

“Huyo ni yule mtu ambaye anapofikwa na msiba anajua kuwa umetoka kwa Allaah, basi akaridhika na akajisalimisha.”

Bi maana anaamini kwamba Allaah ndiye kapanga na ndiye kakadiria msiba huu ambapo akavuta subira pasi na kukata tamaa. Kwa sababu ya kitendo chake kizuri Allaah anauongoza moyo wake katika kheri, anamtuliza na kumfanya imara. 'Alqamah amesema:

“Huyo ni yule mtu ambaye anapofikwa na msiba anajua kuwa umetoka kwa Allaah, basi akaridhika na akajisalimisha.”

2- Muslim amepokea katika “as-Swahiyh” yake kupitia kwa Abu Hurayrah (Radhiya Allaahu 'anh) ya kwamba Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Mambo mawili kwa watu ni kufuru; kutukaniana nasabu na kuomboleza juu ya maiti.”

Bi maana kuzitweza koo [za watu] kwa sababu ya kiburi, jeuri kwa watu na kuwadharau. Ni aina fulani ya kufuru, lakini ni aina ya kufuru ndogo na sio kubwa. Kitendo hichi ni miongoni mwa mambo ya kipindi cha kikafiri. Katika ile Hadiyth iliotangulia imekuja:

“Mambo mane katika Ummah wangu ni miongoni mwa mambo ya kipindi cha kikafiri na hawatoyaacha; kujifakhari kwa unasabu, kutukaniana nasabu, kuinasibisha mvua kwa nyota na kuomboleza.”

Ama ikiwa makusudio ni kuwatambulisha watu fulani, hakuna neno na hakuingii katika Hadiyth.

Kuomboleza juu ya maiti kunafahamisha kukata tamaa na ndani yake kuna kunyanyua sauti juu. Haijuzu. Ama kutiririkwa na machozi, kwa msemu mwingine kulia, hakuna neno. Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Macho yanatokwa na machozi na moyo unahuzunika na hatusemi isipokuwa yale yenye kumridhisha Mola wetu. Hakika ni wenye kuhuzunika kwa kutengana na wewe Ibraahiym.”¹³⁵

3- al-Bukhaariy na Muslim wamepokea kupitia kwa Ibn Mas'ud (Radhiya Allaahu 'anh) kutoka kwa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) kwamba amesema:

“Si katika sisi yule mwenye kujipiga kwenye mashavu, akachana nguo na akaita kwa mayowe ya kipindi cha kikafiri.”¹³⁶

Haya yanafahamisha kukata tamaa na ni katika matendo ya kipindi cha kikafiri. Ni wajibu kuwa na subira na kutambua kuwa Allaah ndiye kayakadiria makadirio haya. Pamoja na kuwa kifo hakiepukiki mtu anatakiwa kufanya zile sababu zinazokubaliana na Shari'ah. Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Mimi niko mbali kabisa na mwanamke anayenyanyua sauti yake, mwenye kuzinyoa nywele zake na mwenye kuzipasua nguo zake wakati wa msiba.”¹³⁷

4- Anas (Radhiya Allaahu 'anh) amesimulia ya kwamba Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Allaah anapomtakia mja Wake kheri, basi humharakishia adhabu duniani, na anapomtakia mja Wake shari, humcheleweshea adhabu ya dhambi yake mpaka siku ya Qiyaamah.”

Akitaka kumfutia mja madhambi yake basi humharakishia adhabu hapa duniani ima kwa kumpa ufakiri, kumpa magonjwa, kuharibika kw mali yake na mfano wake. Kwa njia hiyo Allaah anamfutia madhambi yake na mambo yake mabaya.

¹³⁵ al-Bukhaariy (1303) na Muslim (2315).

¹³⁶ al-Bukhaariy (1294) na Muslim (103).

¹³⁷ al-Bukhaariy kwa cheni ya wapokezi iliopungua na Muslim (104).

Anapomtikia shari basi humwacha akatenda madhambi na akamcheleweshea adhabu ya madhambi yake mpaka siku ya Qiyaamah. Adhabu ya Aakhirah ni mbaya zaidi kuliko ya duniani. Mitihani mingi ya duniani kuna uwezekano ikawa ni sababu ya kusamehewa na kufutiwa madhambi. Kwa ajili hiyo ndio maana mtu anatakiwa kuwa na subira.

5- Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Ukubwa wa malipo ni pamoja na ukubwa wa mitihani. Hakika Allaah (Ta'ala) anapowapenda watu basi huwapa huwajaribu. Yule mwenye kuridhia basi hupara radhi Zake na yule mwenye kuchukia basi hupata hasira Zake.”

Ni nzuri kwa mujibu wa at-Tirmidhiy.

Jinsi mtihani utakuwa mkubwa ndivo malipo yanavyokuwa makubwa zaidi. Jinsi maradhi yanavyokuwa makali ndivo mtu anavyosamehewa zaidi. Jinsi msiba katika mali ya mtu ni mkubwa au vyenginevyo ndivo malipo na thawabu zinavyokuwa nyingi zaidi. Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Hakika Allaah (Ta'ala) anapowapenda watu basi huwapa huwajaribu.”

Anawajaribu watu ili awafuatie madhambi yao na kuwaondoshea mambo yao maovu hadi pale wanapokutana Naye wanakuwa safi na matokeo yake wanaingia Peponi pale mwanzoni mwanzoni. Mfano wa Hadiyth kama hiyo ni maneno yake Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam):

“Watu wenye mitihani mizito kabisa ni Mitume, kisha wenye kufanana nao, kisha wenye kufanana nao. Mtu anapewa majaribio kwa kiasi cha dini yake.”¹³⁸

Katika upokezi mwingine imekuja:

¹³⁸ at-Tirmidhiy (2398), Ibn Hibbaan (2900), al-Haakim (121) na al-Bayhaqi (6326). Swahiyh kwa mujibu wa al-Albaaniy katika “Swahyih-ul-Jaami” (994).

“Watu wenye mitihani mizito kabisa ni Mitume, kisha watu wema, kisha wenye kufanana nao, kisha wenye kufanana nao. Mtu anapewa majaribio kwa kiasi cha dini yake.”¹³⁹

Dini ya mtu ikiwa na nguvu ndivo anavyopewa majaribio zaidi.

¹³⁹ Ahmad (1481). Nzuri kwa mujibu wa Shu'ayb al-Arnaa'uut.

36. Kujionyesha

Shaykh-ul-Islaam Muhammad bin 'Abdil-Wahhaab (Rahimahu Allaah) amesema:

1- Allaah (Ta'ala):

قُلْ إِنَّمَا أَنَا بَشَرٌ مِّثْلُكُمْ يُوحَىٰ إِلَيَّ أَنَّمَا إِلَهُكُمُ إِلَهٌ وَاحِدٌ فَمَن كَانَ يَرْجُوا لِقَاءَ رَبِّهِ فَلْيَعْمَلْ عَمَلًا صَالِحًا وَلَا يُشْرِكْ بِعِبَادَةِ رَبِّهِ أَحَدًا

"Sema: "Hakika mimi ni mtu [wa kawaida] kama nyinyi. Nafunuliwa Wahy kwamba hakika mwabudiwa wenu wa haki ni Mungu mmoja pekee. Hivyo yule anayetaraji kukutana na Mola wake basi na atende matendo mema na wala asimshirikishe katika 'ibaadah za Mola wake yeyote!" (al-Kahf 18:110)

2- Abu Hurayrah (Radhiya Allaahu 'anh) ameeleza kwamba Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

"Allaah (Ta'ala) amesema: "Hakika Mimi ni Mwenye kujitosheleza kutohitajia washirika. Hivyo basi yule atakayefanya kitendo akanishirikisha Mimi pamoja na mwingine, basi nitamwacha yeye na shirki yake."¹⁴⁰

Ameipokea Muslim.

3- Abu Sa'iyd al-Khudriy (Radhiya Allaahu 'anh) amesimulia kwamba Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

"Je, nisikwambieni kile ninachokukhofieni kuliko hata huyo al-Masiyh ad-Dajjaal?" Wakasema: "Ndio." Akasema: "Ni shirki iliyojificha; anasimama mtu kuswali na akaipamba swalah yake kwa kuwa anaona watu wanamwangalia."¹⁴¹

¹⁴⁰ Muslim (2985).

Ameipokea Ahmad.

MAELEZO

Mtunzi wa kitabu ameweka mlango huu ili kutahadharisho kujionyesha. Kujionyesha maana yake ni mtu kufanya kitendo ili wengine wapate kumuona au kumsifu au ili aweze kufikia kitu cha kimanufaa cha kidunia. Inaweza vilevile kutaka kuwafanya wengine wamsikie namna anavyosoma Qur-aan, namna anavyomsabihi Allaah, namna anavyoamrisha mema na kukataza maovu. Kwa ajili hiyo imekuja katika Hadiyth:

“Yule anayetaka kujionyesha basi Allaah atamfanya kuonekana na yule anayetaka kusikika basi Allaah atamfanya kusikika.”¹⁴²

Katika upokezi mwingine imekuja:

“Yule anayetaka kujionyesha basi Allaah atamuonyesha na yule anayetaka kusikika basi Allaah atamfanya kusikika.”

Bi maana atamfedhehesha na atamlipa kwa mujibu wa kitendo chake. Ni wajibu kwa muislamu kumtakasia matendo yake Allaah na kutarajia thawabu kutoka kwa Allaah.

1- Allaah (Ta'ala):

قُلْ إِنَّمَا أَنَا بَشَرٌ مِّثْلُكُمْ يُوحَىٰ إِلَيَّ أَنَّمَا إِلَهُكُمْ إِلَهٌ وَاحِدٌ فَمَن كَانَ يَرْجُوا لِقَاءَ رَبِّهِ فَلْيَعْمَلْ عَمَلًا صَالِحًا وَلَا يُشْرِكْ بِعِبَادَةِ رَبِّهِ أَحَدًا

”Sema: “Hakika mimi ni mtu [wa kawaida] kama nyinyi. Nafunuliwa Wahy kwamba hakika mwabudiwa wenu wa haki ni Mungu mmoja pekee.

¹⁴¹ Ahmad (11270) na Ibn Maajah (4203). Nzuri kwa mujibu wa al-Albaaniy katika “Swahiyh Sunan Ibn Maajah” (3389).

¹⁴² al-Bukhaariy (6499) na Muslim (93).

Hivyo yule anayetaraji kukutana na Mola wake basi na atende matendo mema na wala asimshirikishe katika 'ibaadah za Mola wake yeyote!"

Tendo jema ni lile lililotimiza masharti mawili:

1- Kumtakasia nia Allaah katika 'ibaadah zote.

2- Kiwe kimeafikiana na Shari'ah na kisiwe kimezuliwa.

Yule ambaye kweli anataraji kukutana na Mola wake basi afanye matendo mema yenye kuafikiana na Shari'ah na asimshirikishe katika 'ibaadah za Mola wake yeyote.

2- Abu Hurayrah (Radhiya Allaahu 'anh) ameeleza kwamba Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

"Allaah (Ta'ala) amesema: "Hakika Mimi ni Mwenye kujitosheleza kutohitajia washirika. Hivyo basi yule atakayefanya kitendo akanishirikisha Mimi pamoja na mwingine, basi nitamwacha yeye na shirki yake."

Ameipokea Muslim.

Haya yanafahamisha kwamba Allaah anajitenga mbali na kitendo ambacho ndani yake kina shirki na kwamba hayakubali. Katika upokezi mwingine imekuja:

"Mimi ni Mwenye kujitenga nayo mbali. Bali ni ya yule aliyemshirikisha."

Hii ni dalili inayofahamisha juu ya uwajibu wa kumtakasia matendo Allaah.

3- Abu Sa'iyd al-Khudriy (Radhiya Allaahu 'anh) amesimulia kwamba Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

"Je, nisikwambieni kile ninachokukhofieni kuliko hata huyo al-Masiyh ad-Dajjal?" Wakasema: "Ndio." Akasema: "Ni shirki iliyojificha; anasimama mtu kuswali na akaipamba swalah yake kwa kuwa anaona watu wanamwangalia."

Siku ya Qiyaamah Allaah atawaambia wale waliojionyesha:

“Allaah atawaambia wale waliojionyesha: “Nendeni kwa wale mliokuwa mkiwaonyesha duniani na muone kama watakulipeni.”

Haya yanaonyesha ukhatari wa kujionyesha na khaswakhaswa kwa wale wafanya 'ibaadah. Yeye (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) aliwakhofia Maswahabah ilihali ndio watu bora kabisa. Kwa sababu jambo la kujionyesha linawatokea wema. Wanapewa majaribio ya kujionyesha kama wanavyopewa majaribio wengine na wanalichukulia hilo wepesi. ad-Dajjaal mtu anaweza kumtambua kutokana na zile alama. Shirki iliyojificha ni khatari kwa sababu imefichikana moyoni mwa mwanadamu. Lakini ina baadhi ya ishara ambazo zinaweza kuonekana kwa mwenye nayo. Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema kama ilivyosihhi kutoka kwake:

“Kikubwa ninachokikhofieni juu yenu ni shirki ndogo.” Alipoulizwa juu yake akasema: "Kujionyesha."¹⁴³

¹⁴³ Ahmad (23680). Swahiyh kwa mujibu wa al-Albaaniy katika "Swahiyh-ul-Jaami" (1555).

37. Mtu kufanya kitendo kwa ajili ya dunia ni katika shirki

Shaykh-ul-Islaam Muhammad bin 'Abdil-Wahhaab (Rahimahu Allaah) amesema:

1- Allaah (Ta'ala) amesema:

مَنْ كَانَ يُرِيدُ الْحَيَاةَ الدُّنْيَا وَزِينَتَهَا نُوَفِّ إِلَيْهِمْ أَعْمَالَهُمْ فِيهَا وَهُمْ فِيهَا لَا يُبْخَسُونَ أُولَئِكَ الَّذِينَ لَيْسَ لَهُمْ فِي الْآخِرَةِ إِلَّا النَّارُ وَحَبِطَ مَا صَنَعُوا فِيهَا وَبَاطِلٌ مَّا كَانُوا يَعْمَلُونَ

"Anayetaka maisha ya dunia na mapambo yake, basi Tutawalipa kikamilifu matendo yao humo nao hawatopunjwa humo; [lakini] hao ndio wale ambao hawatokuwa na chochote katika Aakhirah isipokuwa Moto. Yataharibika yale yote waliyoyafanya humo [hapa duniani] na yatabatilika yale waliyokuwa wakiyatenda." (Hud 11:15-16)

2- Imepokelewa kutoka kwa Abu Hurayrah (Radhiya Allaahu 'anh) ya kwamba Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

"Ameangamia mja wa dinari! Ameangamia mja wa dirhamu! Ameangamia mja wa Khamiyswah! Ameangamia mja wa Khamiylah! Akipewa huridhia na kama hakupewa hukasirika. Ameangamia na amehiliki mtu huyo! Kama mwiba ukimchoma basi asipate mtu wa kumchomoa! Twuubaa kwa mja ambaye amechukua khitamu za farasi wake kwa ajili ya kupigana Jihaad katika njia ya Allaah; niywele zake ziko timentim na miguu yake imejaa vumbi. Anapowekwa kuchunga [kikosi cha jeshi] basi huchunga kikwelikweli na anapowekwa nyuma

kuchunga basi anachunga kikwelikweli. Akiomba idhini asingeliidhinishwa na akiombea basi maombi yake yasingekubaliwa.”¹⁴⁴

MAELEZO

Shirki imegawanyika katika mafungu mawili; shirki kubwa na shirki ndogo. Shirki iliokusudiwa katika mlango huu wakati fulani inaweza kuwa shirki kubwa na wakati mwingine inaweza kuwa shirki ndogo. Yule mwenye kuingia katika Uislamu kwa sababu ya kutaka manufaa ya kidunia hii ni shirki kubwa kama wafanyavyo wanafiki ambao watakuwa katika tabaka ya chini kabisa Motoni. Wakati mwingine inakuwa shirki ndogo kama mfano wa yule mwenye kusoma Qur-aan, anaamrisha mema na kukataza maovu kwa kujionyesha. Kadhalika anapigana Jihaad kwa sababu ya ngawira na sio kwa sababu ya Allaah. Huyu ni muumini na muislamu, lakini mambo haya yamemtokea.

1- Allaah (Ta'ala) amesema:

مَنْ كَانَ يُرِيدُ الْحَيَاةَ الدُّنْيَا وَزِينَتَهَا نُوفَّ إِلَيْهِمْ أَعْمَالَهُمْ فِيهَا وَهُمْ فِيهَا لَا يُبْخَسُونَ أُولَئِكَ الَّذِينَ لَيْسَ لَهُمْ فِي الْآخِرَةِ إِلَّا النَّارُ وَحَبِطَ مَا صَنَعُوا فِيهَا وَبَاطِلٌ مَّا كَانُوا يَعْمَلُونَ

”Anayetaka maisha ya dunia na mapambo yake, basi Tutawalipa kikamilifu matendo yao humo nao hawatopunjwa humo; [lakini] hao ndio wale ambao hawatokuwa na chochote katika Aakhirah isipokuwa Moto. Yataharibika yale yote waliyoyafanya humo [hapa duniani] na yatabatilika yale waliyokuwa wakiyatenda.”

Haya ni matishio makali. Aayah hii inawahusu makafiri ambao walikuwa wakimwabudu Allaah kwa sababu ya mambo ya kidunia, kama walivokuwa wakifanya wanafiki. Kuenea kwa Aayah kunapelekea kumfanya mtu

¹⁴⁴ al-Bukhaariy (2887).

kutahadhari kufanya 'ibaadah kwa sababu ya manufaa ya kidunia japokuwa hayo yatakuwa katika baadhi ya mambo. Kadhalika Allaah (Ta'ala) amesema:

مَنْ كَانَ يُرِيدُ حَرْثَ الْآخِرَةِ نَزِدْ لَهُ فِي حَرْثِهِ وَمَنْ كَانَ يُرِيدُ حَرْثَ الدُّنْيَا نُؤْتِهِ مِنْهَا وَمَا لَهُ فِي الْآخِرَةِ مِنْ نَصِيبٍ

“Yeyote mwenye kutaka jaza ya Aakhirah basi Tunamzidishia katika jaza yake na yeyote mwenye kutaka jaza ya dunia, tutampa humo, lakini Aakhirah hatokuwa na fungu lolote.” (ash-Shuuraa 42:20)

مَنْ كَانَ يُرِيدُ الْعَاجِلَةَ عَجَّلْنَا لَهُ فِيهَا مَا نَشَاءُ لِمَنْ نُرِيدُ ثُمَّ جَعَلْنَا لَهُ جَهَنَّمَ يَصْلَاهَا

“Yeyote anayetaka [starehe za dunia] ipitayo upesi, basi Tunamharakizia humo tuyatakayo na kwa tumtakaye - halafu tutamjaalia Jahannam aingie na kuungua hali ya kuwa ni mwenye kutwezwa na ni mwenye kufukuziliwa mbali.” (al-Israa' 17:18)

Aayah hii imesema kwa kufungamanisha ile iliotangulia kwa sababu sio kila ambaye anaikimbilia dunia huipata. Mtu anaweza kufikia tu baadhi ya yale mambo aliokuwa anatafuta. Allaah (Ta'ala) amesema:

وَمَنْ أَرَادَ الْآخِرَةَ وَسَعَىٰ لَهَا سَعْيَهَا وَهُوَ مُؤْمِنٌ فَأُولَٰئِكَ كَانَ سَعْيُهُمْ مَشْكُورًا

“Na anayetaka Aakhirah na akaifanyia jitihada vitendo vyake, ilihali ni muumini, basi hao jitihada zao ni za kushukuriwa.” (al-Israa' 17:19)

Kutaka peke yake hakutoshi pasi na kufanya bidii na imani. Ni lazima kufanya bidii, kumwamini na kumpwekesha Allaah. Bidii ya mtu kama huyu ndio yenye kupendwa na Allaah na waumini. Ni dalili inayofahamisha juu ya uwajibu wa kumtakasia nia Allaah na kwamba kitendo kinabatilika kikichanganyikana pamoja na shirki.

2- Imepokelewa kutoka kwa Abu Hurayrah (Radhiya Allaahu 'anh) ya kwamba Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Ameangamia mja wa dinari! Ameangamia mja wa dirhamu! Ameangamia mja wa Khamiyswah! Ameangamia mja wa Khamiylah! Akipewa huridhia na kama hakupewa hukasirika. Ameangamia na amehiliki mtu huyo! Kama mwiba ukimchoma basi asipate mtu wa kumchomoa! Twuubaa kwa mja ambaye amechukua khitamu za farasi wake kwa ajili ya kupigana Jihaad katika njia ya Allaah; niywele zake ziko timentim na miguu yake imejaa vumbi. Anapowekwa kuchunga [kikosi cha jeshi] basi huchunga kikwelikweli na anapowekwa nyuma kuchunga basi anachunga kikwelikweli. Akiomba idhini asingeliidhinishwa na akiombea basi maombi yake yasingekubaliwa.”

Khamiyswah ni kitambara kilicho na michoromichoro na Khamiylah ni kitambara kilichoshonywa vya watu maarufu na hakina michoromichoro.

Aangamie yule ambaye ameingia katika Uislamu, au anajidhihisha kwa kufanya matendo ya Kiislamu, kwa lengo hili. Aangamie yule ambaye anaabudu kwa ajili ya pesa au mambo ya kidunia. Hivyo ndivo wanavofanya wanafiki na wengineo. Mtu kama huyu anapoteza thawabu zake na badala yake anapata dhambi. Ndio maana (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amemuomba du'aa ya maangamivu na kuhiliki. Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Kama mwiba ukimchoma basi asipate mtu wa kumchomoa!”

Huku ni kuomba du'aa dhidi yake asipate mtu wa kumchomoa ili kumfanyia mambo yake mazito na apate mwisho mbaya. Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Twuubaa kwa mja ambaye amechukua khitamu za farasi wake kwa ajili ya kupigana Jihaad katika njia ya Allaah; niywele zake ziko timentim na miguu yake imejaa vumbi.”

Kutokana na vile anavyoitilia umuhimu na kujishughulisha sana na Jihaad anakosa hata muda wa kuzichanua nywele zake na kuusafisha mwili wake. Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Anapowekwa kuchunga [kikosi cha jeshi] basi huchunga kikwelikweli na anapowekwa nyuma kuchunga basi anachunga kikwelikweli. Akiomba idhini asingeliidhinishwa na akiombea basi maombi yake yasingekubaliwa.”

Ni mmoja kati ya watu wengi na hatambuliki. Haya ni kutokana na ukamilifu wa kumtakasia kwake nia Allaah na ukamilifu wa ukweli wake. Hajali nafasi za juu na wala kwenda kwa wafalme, viongozi na nafasi nyenginezo za juu. Ndio maana hawamtambui. Huyu ndiye ana Pepo na karama tofauti na mnafiki na yule mwenye kufanya matendo kwa ajili ya jambo la kidunia wakati anapoamrisha, anapokataza, anapopambana na pindi anapofanya mambo mengine ya kidini; mtu kama huyu matendo yake ni yenye kuporomoka.

38. Mwenye kuwatii wanachuoni na viongozi katika kuharamisha aliyohalalisha au kuhalalisha aliyoharamisha Allaah amewafanya ni waungu badala ya Allaah

Shaykh-ul-Islaam Muhammad bin 'Abdil-Wahhaab (Rahimahu Allaah) amesema:

1- Ibn 'Abbaas amesema:

“Kumekurubia kukushukieni mawe kutoka mbinguni; nawaambieni: “Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema na nyinyi mnanambia Abu Bakr na 'Umar wamesema.”¹⁴⁵

2- Imaam Ahmad bin Hanbal amesema:

“Nashangazwa na watu ambao wanajua cheni ya wapokezi na usahihi wake wanaiacha na kufuata maoni ya Suftaan. Allaah (Ta'ala) amesema:

فَلْيَحْذَرِ الَّذِينَ يُخَالِفُونَ عَنْ أَمْرِهِ أَنْ تُصِيبَهُمْ فِتْنَةٌ أَوْ يُصِيبَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ

“Basi watahadhari wale wanaokhalifu amri yake; isije kuwapata fitina au ikawapata adhabu iumizayo.” (an-Nuur 24:63)

Unajua ni nini fitina? Fitina ni shirki. Pengine ataporudisha baadhi ya maneno yake (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) akaingiwa moyoni mwake na kitu kama mashaka na upotevu na matokeo yake akaangamia.”

¹⁴⁵ Ahmad (3121).

3- 'Adiy bin Haatiym amesimulia kwamba amemsikia Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) akisoma Aayah hii:

اتَّخَذُوا أَحْبَابَهُمْ وَرُءْبَانَهُمْ أَرْبَابًا مِّن دُونِ اللَّهِ

“Wamewafanya marabi wao na watawa wao kuwa ni waungu badala ya Allaah.”
(at-Tawbah 09:31)

Nikamwambia: “Sisi hatukuwa tukiwaabudu.” Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) akasema: “Je, hawakuwa wakiharamisha aliyoyahalalisha Allaah nanyi mkayaharamisha na wakihalalisha aliyoyaharamisha Allaah nanyi mkayahalalisha?” Nikajibu: “Ndio.” Ndipo akasema (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam): “Huko ndio kuwaabudu.”¹⁴⁶

Ameipokea Ahmad na at-Tirmidhiy ambaye ameifanya kuwa ni nzuri.

MAELEZO

Amechokusudia mwandishi kwa mlango huu ni kuhakikisha Tawhiyd na kutendewa kazi Shari'ah. Kadhalika kuadhimisha maamrisho na makatazo ya Allaah na vilevile kutahadhari kuwafuata kichwa mchungu wanachuoni na viongozi katika mambo yanayopingana na Shari'ah ya Allaah. Huku ni kufuata kwa kipofu.

Ni wajibu kwa wanachuoni na waumini kuadhimisha maamrisho na makatazo ya Allaah, wahalalishe aliyohalalisha Allaah na waharamishe aliyoharamisha Allaah na Mtume Wake (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam). Wasimtii yeyote katika kwenda kinyume na hayo. Wengine wanatiiwa tu katika mema. Ni haramu kumtii yeyote katika jambo linalopingana na Shari'ah. Haifai kumtii kiumbe katika jambo la kumuasi Muumba. Haijuzu hata kwa mtu kuwatii

¹⁴⁶ at-Tirmidhiy (3095), at-Twabaraaniy katika "al-Mu'jam al-Kabiy" (218), al-Bayhaqi katika "as-Sunan al-Kubraa" (20137). Nzuri kwa mujibu wa al-Albaani katika "Ghaayat-ul-Maraam" (6).

wazazi wake, mtoto wake au mke wake katika jambo linalopingana na Shari'ah katika ya halali na ya haramu.

1- Ibn 'Abbaas amesema:

“Kumekurubia kukushukieni mawe kutoka mbinguni; nawaambieni: “Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema na nyinyi mnanambia Abu Bakr na 'Umar wamesema.”

Haya ni matishio ya adhabu. Anachotaka kusema ni kwamba anatumia hoja kwao kwa amri ya Allaah na Mtume Wake (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) ambapo mnakwenda kinyume na kurudisha amri ya Allaah na Mtume Wake (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) kwa maneno ya Abu Bakr na 'Umar. Hii ina maana kwamba haijuzu kwenda kinyume na amri ya Allaah na Mtume Wake (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) japokuwa maoni yatakuwa ni yenye kutoka kwa Abu Bakr na 'Umar ambao ndio watu bora kabisa baada ya Mitume - mtu asemeje yakiwa ni maoni ya wengine? Hapa Ibn 'Abbaas anashaji'isha kufuata Shari'ah na kutahadharisha kuwaadhimisha watu katika mambo yanayopingana na Shari'ah.

2- Imaam Ahmad bin Hanbal amesema:

“Nashangazwa na watu ambao wanajua cheni ya wapokezi na usahihi wake wanaiacha na kufuata maoni ya Suftaan. Allaah (Ta'ala) amesema:

فَلْيَحْذَرِ الَّذِينَ يُخَالِفُونَ عَنْ أَمْرِهِ أَنْ تُصِيبَهُمْ فِتْنَةٌ أَوْ يُصِيبَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ

“Basi watahadhari wale wanaokhalifu amri yake; isije kuwapata fitina au ikawapata adhabu iumizayo.” (an-Nuur 24:63)

Unajua ni nini fitina? Fitina ni shirki. Pengine ataporudisha baadhi ya maneno yake (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) akaingiwa moyoni mwake na kitu kama mashaka na upotevu na matokeo yake akaangamia.”

Bi maana wamejua cheni ya wapokezi kuwa ni sahihi kwenda kwa Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) na Maswahabah. Imaam Ahmad anamkaripia yule mwenye kufanya hivo na kwamba haimstahikii. Halafu akasoma:

فَلْيَحْذَرِ الَّذِينَ يُخَالِفُونَ عَنْ أَمْرِهِ أَنْ تُصِيبَهُمْ فِتْنَةٌ أَوْ يُصِيبَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ

“Basi watahadhari wale wanaokhalifu amri yake; isije kuwapata fitina au ikawapata adhabu iumizayo.”

Yule mwenye kurudisha kitu kutoka kwa Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) kuna khatari kwake akapewa mtihani na akaingia katika shirki na kuritadi. Katika haya pia kuna maonyo ya kwenda kinyume na Shari'ah. Haijalishi kitu hata kama yule aliyefanya hivo ni mwanachuoni mkubwa. Maswahabah na wale waliokuja baada yao wamesema wazi kwamba haijuzu kuwatii katika jambo linalopingana na amri ya Allaah na Mtume Wake (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam). Matishio haya yanamuhusu yule mtu ambaye anajua kuwa maoni ya mtu fulani yanapingana na Shari'ah pamoja na hivyo akahalalisha kitu ambacho ni haramu.

3- 'Adiy bin Haatiym amesimulia kwamba amemsikia Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) akisoma Aayah hii:

اتَّخَذُوا أَحْبَابَهُمْ وَرُهْبَانَهُمْ أَرْبَابًا مِّنْ دُونِ اللَّهِ

“Wamewafanya marabi wao na watawa wao kuwa ni waungu badala ya Allaah.”
(at-Tawbah 09:31)

Nikamwambia: “Sisi hatukuwa tukiwaabudu.” Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) akasema: “Je, hawakuwa wakiharamisha aliyoyahalalisha Allaah nanyi mkayaharamisha na wakihalalisha aliyoyaharamisha Allaah nanyi mkayahalalisha?” Nikajibu: “Ndio.” Ndipo akasema (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam): “Huko ndio kuwaabudu.”

Ameipokea Ahmad na at-Tirmidhiy ambaye ameifanya kuwa ni nzuri.

Hii ina maana kwamba yule mwenye kuwatii wanachuoni na viongozi katika kuharamisha kitu cha halali au kuhalalisha kitu cha haramu na wakati huohuo akaonelea kuwa kufanya hivo kuna faa na yeye anajua kuwa kunaenda kinyume na Shari'ah ya Allaah, huku ni kuwaabudu na amekufuru. Ama ikiwa anawafuata kwa sababu ya ujinga na Ijtihad, sio kuwaabudu na wala haingii katika matishio. Kwa sababu mtu anatakiwa kuwauliza wanachuoni na kuchukua fatwa zao maadamu hajui kuwa jambo hilo linapingana na Shari'ah ya Allaah.

39. Mlango maneno Yake (Ta'ala) “Je, huoni wale ambao wanadai kwamba wao wameamini yaliyoteremshwa kwako na yale yaliyoteremshwa kabla yako, wanataka wahukumiane kwa Twaaghuut na hali wameamrisha wakanushe hiyo, na shaytwaan anataka awapoteze upotofu wa mbali kabisa”

Shaykh-ul-Islaam Muhammad bin 'Abdil-Wahhaab (Rahimahu Allaah) amesema:

1- Allaah (Ta'ala) amesema:

أَلَمْ تَرَ إِلَى الَّذِينَ يَزْعُمُونَ أَنَّهُمْ آمَنُوا بِمَا نُزِّلَ إِلَيْكَ وَمَا نُزِّلَ مِنْ قَبْلِكَ يُرِيدُونَ أَنْ يَتَحَاكَمُوا إِلَى الطَّاغُوتِ
وَقَدْ أُمِرُوا أَنْ يَكْفُرُوا بِهِ وَيُرِيدُ الشَّيْطَانُ أَنْ يُضِلَّهُمْ ضَلَالًا بَعِيدًا

“Je, huoni wale ambao wanadai kwamba wao wameamini yaliyoteremshwa kwako na yale yaliyoteremshwa kabla yako, wanataka wahukumiane kwa Twaaghuut na hali wameamrisha wakanushe hiyo, na shaytwaan anataka awapoteze upotofu wa mbali kabisa.” (an-Nisaa' 04:60)

2-

وَإِذَا قِيلَ لَهُمْ لَا تُفْسِدُوا فِي الْأَرْضِ قَالُوا إِنَّمَا نَحْنُ مُصْلِحُونَ

"Na wanapoambiwa: "Msifanye uharibifu katika ardhi." Husema: "Hakika sisi ni watengenezaji." (al-Baqarah 02:11)

3-

وَلَا تُفْسِدُوا فِي الْأَرْضِ بَعْدَ إِصْلَاحِهَا

"Na wala msifanye ufisadi katika ardhi baada ya kutengenea kwake." (al-A'raaf 07:56)

4-

أَفْحُكْمِ الْجَاهِلِيَّةِ يَبْغُونَ

"Je, wanataka [uwahukumu kwa] hukumu ya kipindi cha makafiri?" (al-Maaidah 05:50)

5- 'Abdullaah bin 'Amr (Radhiya Allaahu 'anhumaa) ameeleza kwamba Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

"Hatoamini mmoja wenu mpaka matamanio yake yawe ni yenye kufuata yale niliyokuja nayo."¹⁴⁷

an-Nawawiy amesema:

"Hadiyth ni Swahiyh. Nimeipokea katika "Kitaab-ul-Hujjah" kwa cheni ya wapokezi Swahiyh.

6- ash-Sha'biy amesema:

"Kulikuwa ugomvi baina ya mtu mmoja mnafiki na mwingine myahudi. Yule myahudi akasema: "Twende kwa Muhammad atuhukumu." Mnafiki yule alijua kuwa hachukui rushwa. Mnafiki yule akasema: "Twende kwa mayahudi

¹⁴⁷ Dhaifu kwa mujibu wa al-Albaaniy katika "Dhwilaal-ul-Jannah" (15) na "Mishkaat-ul-Maswaabih" (167).

watuhukumu.” Kwa kujua kwake kuwa wao wanachukua rushwa. Hivyo wote wawili wakakubaliana kumwendea kuhani Juhaynah ili awahukumu. Ndipo kukateremka:

أَلَمْ تَرَ إِلَى الَّذِينَ يَزْعُمُونَ أَنَّهُمْ آمَنُوا بِمَا أُنزِلَ إِلَيْكَ وَمَا أُنزِلَ مِنْ قَبْلِكَ يُرِيدُونَ أَنْ يَتَحَاكَمُوا إِلَى الطَّاغُوتِ
وَقَدْ أُمِرُوا أَنْ يَكْفُرُوا بِهِ وَيُرِيدُ الشَّيْطَانُ أَنْ يُضِلَّهُمْ ضَلَالًا بَعِيدًا

”Je, huoni wale ambao wanadai kwamba wao wameamini yaliyoteremshwa kwako na yale yaliyoteremshwa kabla yako, wanataka wahukumiane kwa Twaaghuut na hali wameamrisha wakanushe hiyo, na shaytwaan anataka awapoteze upotofu wa mbali kabisa.” (an-Nisaa’ 04:60)

Kuna maoni mengine yanayosema kwamba iliteremka juu ya watu wawili waliogombana ambapo mmoja wao akasema:

”Hebu tumpelekee kesi yetu Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) aihukumu.” Yule mwengine akasema: “Wacha tumpelekee Ka’b bin al-Ashraf.” Mwishowe wakampelekea nayo ‘Umar mmoja wao akamueleza kisa kilivyokuwa. Akamuuliza yule ambaye hakuridhia ipelekwe kesi kwa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam): “Mambo ni hivyo?” Mtu yule akasema: “Ndio.” ‘Umar akampiga kwa upanga na akamuua.”

MAELEZO

1- Allaah (Ta’ala) amesema:

أَلَمْ تَرَ إِلَى الَّذِينَ يَزْعُمُونَ أَنَّهُمْ آمَنُوا بِمَا أُنزِلَ إِلَيْكَ وَمَا أُنزِلَ مِنْ قَبْلِكَ يُرِيدُونَ أَنْ يَتَحَاكَمُوا إِلَى الطَّاغُوتِ
وَقَدْ أُمِرُوا أَنْ يَكْفُرُوا بِهِ وَيُرِيدُ الشَّيْطَانُ أَنْ يُضِلَّهُمْ ضَلَالًا بَعِيدًا

”Je, huoni wale ambao wanadai kwamba wao wameamini yaliyoteremshwa kwako na yale yaliyoteremshwa kabla yako, wanataka wahukumiane

kwa Twaaghuut na hali wameamrishwa wakanushe hiyo, na shaytwaan anataka awapoteze upotofu wa mbali kabisa.”

Anachotaka mwandishi ni kuwatahadharisha watu kuhukumiana kinyume na Shari’ah ya Allaah. Lililo la wajibu ni kuhukumian na Shari’ah ya Allaah katika mambo yote. Allaah (Ta’ala) amesema:

فَلَا وَرَبِّكَ لَا يُؤْمِنُونَ حَتَّىٰ يُحَكِّمُوكَ فِيمَا شَجَرَ بَيْنَهُمْ ثُمَّ لَا يَجِدُوا فِي أَنفُسِهِمْ حَرَجًا مِّمَّا قَضَيْتَ وَيُسَلِّمُوا
تَسْلِيمًا

“Naapa kwa Mola wako! Hawatoamini mpaka wakufanye wewe ni hakimu katika yale wanayozozana kati yao kisha wasipate katika nyoyo zao uzito katika yale uliyohukumu na wajisalimishe kwa kujisalimisha” (an-Nisaa’ 04:65)

وَأَنِ احْكُم بَيْنَهُم بِمَا أَنزَلَ اللَّهُ

“Wahukumu baina yao kwa yale aliyoyateremsha Allaah.” (al-Maaidah 05:49)

وَمَنْ لَّمْ يَحْكَمْ بِمَا أَنزَلَ اللَّهُ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْكَافِرُونَ

“Yeyote asiyehukumu kwa yale aliyoyateremsha Allaah, basi hao ndio makafiri.” (al-Maaidah 05:44)

وَمَنْ لَّمْ يَحْكَمْ بِمَا أَنزَلَ اللَّهُ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الظَّالِمُونَ

“Yeyote asiyehukumu kwa yale aliyoyateremsha Allaah, basi hao ndio madhalimu.” (al-Maaidah 05:45)

وَمَنْ لَّمْ يَحْكَمْ بِمَا أَنزَلَ اللَّهُ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ

“Yeyote asiyehukumu kwa yale aliyoyateremsha Allaah, basi hao ndio mafasiki.”
(al-Maaidah 05:47)

Haya yote yanafahamisha juu ya uwajibu wa kuhukumiana na Shari’ah ya Allaah na kwamba haijuzu kuhukumiana na kitu kingine. Huu ni msingi ambao kuna maafikiano juu yake.

Aayah inabainisha vilevile kwamba wapo watu wanaodai imani na Uislamu ilihali ukweli wa mambo sivo hivyo; bali ni wanafiki. Kunapotokea kitu basi wanataka wahukumiwe kinyume na Shari’ah ya Allaah na Twaaghuut. Twaaghuut ni kila chenye kuabudiwa badala ya Allaah na mwenye kuhukumu kinyume na Shari’ah ya Allaah kwa kukusudia na kwa matamano. Wanafiki wanataka wahukumiwe na yule ambaye anaafikiana na matamano yao na ambaye anapokea rushwa ili aweze kuwapatia haki wao. Hii ni dalili juu ya unafiki wao. Wanafiki kazi yao ni kuipa mgongo haki. Allaah (Ta’ala) amesema:

وَدَا قَيْلٌ هُمْ تَعَالَوْا إِلَىٰ مَا أَنْزَلَ اللَّهُ وَإِلَى الرَّسُولِ رَأَيْتَ الْمُنافِقِينَ يَصُدُّونَ عَنْكَ صُدُودًا

“Wanapoambiwa: “Njooi kwenye yale aliyoyateremsha Allaah na kwa Mtume”, basi utawaona wanafiki wanakugeukilia mbali kwa mkengeuko.” **(an-Nisaa’ 04:61)**

Kwa hivyo ni wajibu kwa mtu kutahadhari nao na tabia zao mbaya.

2-

وَإِذَا قِيلَ لَهُمْ لَا تُفْسِدُوا فِي الْأَرْضِ قَالُوا إِنَّمَا نَحْنُ مُصْلِحُونَ

“Na wanapoambiwa: “Msifanye uharibifu katika ardhi.” Husema: “Hakika sisi ni watengenezaji.”

Wanadai kwamba ni wenye kutengeneza, lakini uhakika wa mambo ni wenye kuharibu kwa sababu ya ujinga wao, upotevu wao na unafiki wao. Akili zao

zimepinduliwa chini juu na ndio maana wakachukulia ufigadi kuwa ni matengenezo. Kwa ajili hii Allaah (Ta'ala) akasema:

أَلَا إِنَّهُمْ هُمُ الْمُفْسِدُونَ وَلَكِن لَّا يَشْعُرُونَ

“Tanabahi! Hakika wao ndio mafisadi lakini hawahisi.” (al-Baqarah 02:12)

3-

وَلَا تُفْسِدُوا فِي الْأَرْضِ بَعْدَ إِصْلَاحِهَا

“Na wala msifanye ufigadi katika ardhi baada ya kutengenea kwake.”

Kutengenea kwa ardhi kunakuwa kwa kufuata na kuhukumiana kwa Shari'ah. Inaharibiwa kwa kwenda kinyume na amri ya Allaah na kuhukumiana na sheria zengine.

4-

أَفَحُكْمَ الْجَاهِلِيَّةِ يَبْغُونَ

“Je, wanataka [uwahukumu kwa] hukumu ya kipindi cha makafiri?”

Watu hawa wanataka kuhukumiwa na mayahudi na Twaaghuut sampuli zengine kwa hukumu za kipindi cha kikafiri. Hivi kuna hukumu ilio bora kuliko hukumu ya Allaah? Yeye ndiye anajua bora manufaa ya waja Wake. Anajua namna mambo yatavyomalizika. Yeye ndiye mjuzi wa kila kitu.

5- 'Abdullaah bin 'Amr (Radhiya Allaahu 'anhumaa) ameeleza kwamba Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Hatoamini mmoja wenu mpaka matamano yake yawe ni yenye kufuata yale niliyokuja nayo.”

Bi maana hatoamini imani kamilifu na ya wajibu mpaka matamanio yake, utashi wake, makusudio yake na matakwa yake yawe ni yenye kufuata yale aliyokuja nayo yeye (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam). Ni wajibu makusudio ya muumini yawe ni yenye kujisalimisha na hukumu ya Allaah. Baadhi ya wanachuoni wamesema kuwa Hadiyth hii ni dhaifu, lakini hata hivyo maana yake ni sahihi.

6- ash-Sha'biy amesema:

“Kulikuwa ugomvi baina ya mtu mmoja mnafiki na mwingine myahudi. Yule myahudi akasema: “Twende kwa Muhammad atuhukumu.” Mnafiki yule alijua kuwa hachukui rushwa. Mnafiki yule akasema: “Twende kwa mayahudi watuhukumu.” Kwa kujua kwake kuwa wao wanachukua rushwa. Hivyo wote wawili wakakubaliana kumwendea kuhani Juhaynah ili awahukumu. Ndipo kukateremka:

أَمْ تَرَى إِلَى الَّذِينَ يَزْعُمُونَ أَنَّهُمْ آمَنُوا بِمَا أَنْزَلَ إِلَيْكَ وَمَا أَنْزَلَ مِنْ قَبْلِكَ يُرِيدُونَ أَنْ يَتَحَاكَمُوا إِلَى الطَّاغُوتِ
وَقَدْ أُمرُوا أَنْ يَكْفُرُوا بِهِ وَيُرِيدُ الشَّيْطَانُ أَنْ يُضِلَّهُمْ ضَلَالًا بَعِيدًا

“Je, huoni wale ambao wanadai kwamba wao wameamini yaliyoteremshwa kwako na yale yaliyoteremshwa kabla yako, wanataka wahukumiane kwa Twaaghuut na hali wameamrisha wakanushe hiyo, na shaytwaan anataka awapoteze upotofu wa mbali kabisa.”

Hii ni dalili inayoonyesha kuwa mnafiki ana shari zaidi kuliko myahudi. Kwa sababu wanawababaisha watu na kusababisha upotevu. Kwa ajili hio ndio maana wakawa katika tabala ya chini kabisa Motoni.

Ni wajibu kuhukumiana na Shari'ah ya Allaah na kutoridhia nyengine. Kisa cha 'Umar kinathibitisha kwamba kuhukumu kinyume na Shari'ah ni kufuru na kuritadi. Vilevile yule mwenye kuchukua hukumu ya Allaah ni kafiri. Usahihi wa visa vyote viwili unahitajia kutazamwa vizuri, lakini maana zake ni sahihi.

ash-Sha'biy ni 'Aamir bin Sharaahil.

Faida:

Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Allaah amemuumba Aadam kwa sura Yake.”¹⁴⁸

Ina maana kwamba Allaah alimuumba Aadam kwa usikizi, uoni, akizungumza, uso, mikono, nyayo na mengineyo. Allaah anasikia na Aadam pia alikuwa akisikia. Allaah anazungumza na Aadam pia alikuwa akizungumza na kadhalika. Lakini hafanani na Allaah inapokuja katika dhati na sifa za Allaah:

لَيْسَ كَمِثْلِهِ شَيْءٌ ۖ وَهُوَ السَّمِيعُ الْبَصِيرُ

“Hakuna chochote kinachofanana Naye - Naye ni Mwenye kusikia, Mwenye kuona.” (ash-Shuuraa 42:11)

Kuhusiana na ambaye amesema kuwa dhamiri inarudi kwa Aadam, ni kosa. Aliyesema hivo lengo lake ilikuwa kukimbia kufananisha.

¹⁴⁸ al-Bukhaariy (6227) na Muslim (2841).

40. Anayepinga kitu katika majina na sifa za Allaah

Shaykh-ul-Islaam Muhammad bin 'Abdil-Wahhaab (Rahimahu Allaah) amesema:

1- Maneno ya Allaah (Ta'ala):

وَهُمْ يَكْفُرُونَ بِالرَّحْمَنِ

“... ilihali wao wanamkanusha Mwingi wa rehema.” (ar-Ra'd 13:30)

2- al-Bukhaariy amepokea katika “as-Swahiyyh” yake kwamba 'Aliy (Radhiya Allaahu 'anh) amesema:

“Waelezeni watu kwa wanayoyajua. Je, mnataka akadhibishwe Allaah na Mtume Wake (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam)?”¹⁴⁹

3- 'Abdur-Razzaaq amepokea kutoka kwa Ma'mar, kutoka kwa Ibn Twaawuus, kutoka kwa baba yake, kutoka kwa Ibn 'Abbaas ambaye alimuona mtu akisisimka wakati aliposikia Hadiyth kutoka kwa Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) iliotaja sifa za Allaah akiwa ni mwenye kulipinga hilo ambapo akasema:

“Ni kitu gani kinachowatia woga watu hawa? Wanafanya woga kwa Aayah zilizo wazi ilihali wanaegemea Aayah sizizokuwa waz.”¹⁵⁰

Pindi Quraysh walipomsikia Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) akitaja Mwingi wa rehema wakapinga hilo. Ndipo Allaah akateremsha juu yao:

¹⁴⁹ al-Bukhaariy (129).

¹⁵⁰ al-Muswannaf (20895). Swahiyyh kwa mujibu wa al-Albaaniy katika “Dhwilaal-ul-Jannah” (485).

وَهُمْ يَكْفُرُونَ بِالرَّحْمَنِ

“... ilihali wao wanamkanusha Mwingi wa rehema.”

MAELEZO

Mlango huu mwandishi ameutunga kwa ajili ya kubainisha uwajibu wa kuthibitisha majina na sifa za Allaah kwa njia inayolingana Naye (Subhaanahu wa Ta'ala) pasi na kupotosha, kukanusha, kuzifanyia namna, kuzifananisha wala kuzigeuza. Mtu hatakiwi kudhanganyika na maoni ya Mu'tazilah na watu wa batili wengine. Ni wajibu kwake kuchukua yale yaliyosemwa na Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa'ah katika Maswahabah na wale waliofuata mwenendo wao. Hii ndio 'Aqiydah iliofikishwa na Mitume. Wote walikuwa ni wenye kuthibitisha majina na sifa za Allaah kwa njia inayolingana Naye. Maswahabah na wale wote waliowafuata kwa wema walizipitisha Aayah na Hadiyth zinazozungumzia sifa kama zilivyokuja na wakathibitisha zile dalili za majina na sifa. Yote hayo kwa ajili ya kutendea kazi maneno Yake Allaah:

قُلْ هُوَ اللَّهُ أَحَدٌ اللَّهُ الصَّمَدُ لَمْ يَلِدْ وَلَمْ يُولَدْ وَلَمْ يَكُنْ لَهُ كُفُوًا أَحَدٌ

“Sema: “Yeye ni Allaah - Mmoja pekee, Allaah aliyekamilika, mkusudiwa wa haja zote. Hakuzaa na wala hakuzaliwa, na wala hakuna yeyote anayefanana na kulingana Naye.” (al-Ikhlaasw 112:01-04)

فَلَا تَضْرِبُوا لِلَّهِ الْأَمْثَالَ ۚ إِنَّ اللَّهَ يَعْلَمُ وَأَنْتُمْ لَا تَعْلَمُونَ

“Basi msimpigie Allaah mifano! Hakika Allaah anajua nanyi hamjui.” (al-Israa' 16:74)

لَيْسَ كَمِثْلِهِ شَيْءٌ ۖ وَهُوَ السَّمِيعُ الْبَصِيرُ

“Hakuna chochote kinachofanana Naye - Naye ni Mwenye kusikia, Mwenye kuona.” **(ash-Shuuraa 42:11)**

هَلْ تَعْلَمُ لَهُ سَمِيًّا

“Je, unamjua yeyote mwenye jina kama Lake?” **(Maryam 19:65)**

Allaah (Subhaanahu wa Ta'ala) hana Mwenye jina kama Lake wala anayelingana Naye.

Kuhusu Jahmiyyah wao wamekanusha majina na sifa za Allaah na wakayapindisha majina. Maoni yao yanapelekea kukanusha kabisa kabisa uwepo wa Allaah. Kwa ajili hiyo ndio maana Ahl-us-Sunnah wamewakufurisha. Ni wajibu kuwaua ikiwa hawakutubia. Wanatakiwa kuambiwa kutubia kwa sababu ya kupinga kwao yale yaliyotajwa katika Qur-aan na Sunnah na maafikiano. Mwandishi ametaja kichwa cha khabari kwa kutokufungamanisha pasi na kumhukumu yule mwenye kukanusha majina na sifa za Allaah. Hata hivyo hukumu yake ni kwamba ni kafiri.

1- Kauli ya Allaah (Ta'ala):

وَهُمْ يَكْفُرُونَ بِالرَّحْمَنِ

“... ilihali wao wanamkanusha Mwingi wa rehema.”

Allaah (Ta'ala) amebainisha kwamba Mwingi wa rehema ndio Mola na Mungu wetu na kwamba yule mwenye kumkufuru Mwingi wa rehema basi amemkufuru Allaah. Kwa hivyo ni wajibu kwa muumini kutahadhari na sifa za wapotevu hawa na afuate mwenendo wa wanachuoni na waumini. Allaah ameonelea kule kukanusha kwao sifa hii ni kumkufuru Mwingi wa huruma na ni dalili inayofahamisha kwamba mwenye kukanusha sifa amekufuru.

2- al-Bukhaariy amepokea katika “as-Swahiyyh” yake kwamba ‘Aliy (Radhiya Allaahu ‘anh) amesema:

“Waelezeni watu kwa wanayoyajua. Je, mnataka akadhibishwe Allaah na Mtume Wake (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam)?”

Mtu ambaye anawawaidhi na kuwakumbusha wengine basi anatakiwa kutumia matamshi na usulubu wanaoutambua ili waweze kustafidi na kufaidika. Kila watu wana usulubu wao. Ukiwazungumzisha watu kwa njia wasiyoitambua basi kuna khataru wakaja kukufahamu vibaya. Haijalishi kitu maudhui yanahusiana na majina, sifa au hukumu za Allaah. Haijalishi kitu lugha unayozungumza ni kiarabu, kingereza, urdu au lugha nyingine. Hata waarabu wenyewe wanaelewa tofauti. Zungumza na watu wote kwa njia waliyozowea ili waweze kukifahamu kile unachokisema na ili wasije kumkadhibisha Allaah na Mtume Wake (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam).

Wale wanaomkadhibisha Allaah na Mtume Wake (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) katika sifa za Allaah wako katika khataru kubwa. Kwa sababu wamezipindisha sifa za Allaah kinyume na tafsiri zake na wamezizungumzia kwa njia isiyostahiki mpaka mwishowe wakazikanusha. Wengi wao kuna uwezekano wakawa wamezifahamu kimakosa kwa sababu sio waarabu. Baadhi ya Salaf wamesema kuwa ‘Amr bin ‘Ubayd amesema kuwa watenda madhambi watadumishwa Motoni milele kwa sababu Allaah kawaahidi hilo. Ndipo Salaf wakamwambia kwamba Allaah anaweza kuvunja ahadi ya adhabu na hawezi kuvunja ahadi ya thawabu. Kuvunja ahadi ya adhabu ni utukufu na kuvunja ahadi ya thawabu ni kusemwa vibaya. Ndipo wakamwambia:

“Umetumbukia katika hayo kwa sababu sio mwarabu.”

Bi maana unadhani kuwa ni jambo baya kuvunja ahadi ya adhabu. Si kweli. Mshairi amesema:

Mimi nikiyahidi kumuadhibu au kumlipa

nitaiwunja ahadi yangu ya kumuadhibu na kutimiza ahadi yangu ya kumlipa

Hii ni sifa.

3- 'Abdur-Razzaaq amepokea kutoka kwa Ma'mar, kutoka kwa Ibn Twaawuus, kutoka kwa baba yake, kutoka kwa Ibn 'Abbaas ambaye alimuona mtu akisisimka wakati aliposikia Hadiyth kutoka kwa Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) iliotaja sifa za Allaah akiwa ni mwenye kulipinga hilo ambapo akasema:

“Ni kitu gani kinachowatia woga watu hawa? Wanafanya woga kwa Aayah zilizo wazi ilihali wanaegemea Aayah sizizokuwa waz.”

Pindi Quraysh walipomsikia Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) akitaja Mwingi wa rehema wakapinga hilo. Ndipo Allaah akawateremshia juu yao:

وَهُمْ يَكْفُرُونَ بِالرَّحْمَنِ

“... ilihali wao wanamkanusha Mwingi wa rehema.”

Wakati wanaposikia Aayah za wazi na Hadiyth wanasikia woga na wanakuwa na unyenyekevu. Wanaposikia Aayah kuhusu sifa za Allaah zinawatatiza na wanaangamia kwa sababu ya kutatizika na kukanusha. Hii ni dalili inayoonyesha kuwa jambo hili ni la tokea hapo kale na kwamba kitu kama hicho kilikuwepo tokea hapo wakati wa Maswahabah. Wanaangamia kwa sababu ya Aayah za Qur-aan na Hadiyth ambazo wanaona kuwa haziko wazi na wanazitilia mashaka. Ni dalili inayofahamisha kwamba kupinga na kutilia mashaka yale Allaah aliyowabainishia waja Wake ni maangamivu.

Haki ni kuamini yale yote yaliyokhabarishwa na Allaah na Mtume Wake (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam). Ukifahamu kilichosemwa, ni jambo zuri na himdi zote ni za Allaah, na kama bado hujafahamu, basi unachotakiwa kusema ni kwamba Allaah ndiye mjuzi zaidi na uwaulize wanachuoni. Ahl-us-Sunnah wal-

Jamaa'ah wanaamini yale yote yaliyotajwa katika Qur-aan na Sunnah. Wameridhishwa nayo na wanayatendea kazi. Pindi wanapokutana na kitu ambacho kimewatatiza basi wanakirudisha katika zile Aayah ambazo ziko wazi na bainifu na kwa njia hiyo wanakifahamu. Hawaifanyi Qur-aan wala Sunnah kuwa ni vyenye kugongana. Hawatili mashaka. Wanatambua kuwa yale maandiko ambayo hayako wazi hayapingani na yale yaliyo wazi. Bali uhakika wa mambo yale maandiko yasiyokuwa wazi ni sehemu ya yale yaliyo wazi. Yale yote ambayo hawakuyafahamu wanamwacha Yeye ambaye anayajua yaliyofichikana ayashughulikie ambaye ni Allaah (Subhaanah). Kuhusu maana yake ni yenye kufahamika katika lugha ya kiarabu ambayo Allaah amewazungumzisha watu kwayo. Kwa ajili hiyo Imaam Maalik (Rahimahu Allaah) amesema wakati alipoulizwa swali kuhusu kulingana kwa Allaah:

“Kulingana kunatambulika. Namna haijulikani. Kuuliza juu ya hilo ni Bid'ah.”

Bi maana ni Bid'ah kuuliza kuhusu namna. Amebainisha (Rahimahu Allaah) kwamba kulingana kunatambulika na kwamba namna haitambuliki.

Faida:

Mwenye kusema kwamba Pepo na Moto vitatokomea/vitakwisha ni kafiri. Allaah (Tabaarak wa Ta'ala) amesema:

وَأَمَّا الَّذِينَ سُعِدُوا ففِي الْجَنَّةِ خَالِدِينَ فِيهَا مَا دَامَتِ السَّمَاوَاتُ وَالْأَرْضُ إِلَّا مَا شَاءَ رَبُّكَ ۗ عَطَاءٌ غَيْرَ

مُجْدُودٍ

“Ama wale walio furahani, basi watakuwa katika mabustani, ni wenye kudumu ndani yake zitakavyodumu mbingu na ardhi isipokuwa atakavyo Mola wako - ni hiba isiyokatizwa.” (Hud 11:108)

لَا يَمَسُّهُمْ فِيهَا نَصَبٌ وَمَا هُمْ مِنْهَا بِمُخْرَجِينَ

“Hautowapata ndani yake uchovu nao humo hawatotolewa.” (al-Hijr 15:48)

Kadhhalika ni kosa kusema kwamba Moto utakwisha. Maoni sahihi walionayo Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa'ah ni kwamba Moto hautakwisha.

Faida:

Waislamu wamekubaliana juu ya kwamba ardhi imetulizana na jua ndio linalozunguka. Wale wanaosema kwamba ardhi ndio inayolizunguka jua wanachomaanisha ni kwamba ardhi ndio iliyotulizana, jambo ambalo ni kufuru:

وَالشَّمْسُ تَجْرِي لِمُسْتَقَرٍّ هَآءَ ۚ ذَٰلِكَ تَقْدِيرُ الْعَزِيزِ الْعَلِيمِ

“Na jua linatembea hadi matulio yake, hayo ni matengenezo ya Mwenye nguvu kabisa, mjuzi.” (Yaa Siyn 36:38)

41. Mlango kuhusu maneno Yake (Ta'ala) “Wanazitambua vyema neema za Allaah, kisha wanazikanusha - na wengi wao ni makafiri”

Shaykh-ul-Islaam Muhammad bin 'Abdil-Wahhaab (Rahimahu Allaah) amesema:

1- Allaah (Ta'ala) amesema:

يَعْرِفُونَ نِعْمَتَ اللَّهِ ثُمَّ يُنْكِرُونَهَا وَأَكْثَرُهُمُ الْكَافِرُونَ

“Wanazitambua vyema neema za Allaah, kisha wanazikanusha - na wengi wao ni makafiri.” (an-Nahl 16:83)

2- Mujaahid amesema kuhusu maana yake:

“Ni mtu kusema: “Hii ni mali yangu. Nimeirithi kutoka kwa mababu zangu.”

3- 'Awn bin 'Abdillaah amesema:

Wanasema: “Lau kama si fulani nisingelikuwa hivi na hivi.”

4- Ibn Qutaybah amesema:

“Wanasema: “Haya ni kutokana na uombezi wa waungu wetu.”

5- Abul-'Abbaas amesema baada ya Hadiyth ya Zayd bin al-Haarith:

“Katika asubuhi hii kuna baadhi ya waja Wangu wamepambaukia wakiwa ni wenye kuniamini na wengine wamekufuru. Ama yule aliyesema kwamba: “Tumenyeshewa mvua kwa fadhila na rehema ya Allaah”, basi huyo ndiye aliyeniamini Mimi na amekufuru sayari. Ama yule aliyesema ya kwamba

tumenyeshewa mvua kutokana na sayari fulani na fulani, basi huyo amenikufuru Mimi na ameamini sayari.”

“Haya yamekuja sehemu nyingi katika Qur-aan na Sunnah; Allaah (Subhaanah) anawasema vibaya wale ambao wanazinasibisha neema Zake kwa asiyekuwa Yeye na wanamshirikisha.”

6- Baadhi ya Salaf wamesema:

“Aayah inawazungumzia wale wenye kusema: “Upepo ulikuwa mzuri na baharia huyu alikuwa hodari” na mfano wa maneno kama hayo ambayo hupitika katika ndimi za watu wengi.”

MAELEZO

1- Allaah (Ta’ala) amesema:

يَعْرِفُونَ نِعْمَتَ اللَّهِ ثُمَّ يُنْكِرُونَهَا وَأَكْثَرُهُمُ الْكَافِرُونَ

“Wanazitambua vyema neema za Allaah, kisha wanazikanusha - na wengi wao ni makafiri.”

Mwandishi amechokusudia ni watu wazitambue neema za Allaah (Subhaanah) na wamshukuru Yeye kwa ajili yazo kwa sababu watu wengi wanaghafilika juu ya hilo. Wanastareheka na neema za Allaah lakini pamoja na hivyo hawamshukuru. Bali wanazinasibisha neema hizo kwa sababu yazo na kwa nguvu zao wenyewe na matendo yao na wakati huohuo wanaghafilika Naye ambaye kihakika ndiye kawatunukia neema hizi. Lau Allaah angelitaka basi angelitokomeza sababu na nguvu ya neema hizo. Allaah ndiye ambaye kamtunukia mtu huyo usikizi, uoni, akili, werevu na mengineyo. Hii ni moja katika tabia za makafiri ambao husema kuwa wamepata mali kwa sababu ya mirathi na mengineyo. Allaah (Ta’ala) amesema:

ثُمَّ يُكْرِمُونَهَا

“... kisha wanazikanusha...”

Wanastareheka nazo na wanazitambua vyema, halafu pamoja na yote haya wanazinasibisha kwa waungu na masanamu yao. Hawataki kuzikiri.

2- Mujaahid amesema kuhusu maana yake:

“Ni mtu kusema: “Hii ni mali yangu. Nimeirithi kutoka kwa mababu zangu.”

Anasema hivo kwa kujisifu na kujiona juu ya jambo hili pasi na kuzikiri neema za Allaah na anaghafilika na hilo. Hasemi hivo kwa njia ya kuelezea, bali anasema hivo kwa kughafilika na kusahau kwamba ni Allaah kweli ndiye kamtunukia neema hiyo. Hata hivyo ni jambo linalofaa mtu akaelezea sababu ya neema fulani.

3- 'Awn bin 'Abdillaah amesema:

Wanasema: “Lau kama si fulani nisingelikuwa hivi na hivi.”

Hili pia ni kosa. Mtu anatakiwa kusema:

“Lau kama si Allaah *kisha* hivi na hivi...”

Neema inatakiwa kunasibishwa kwa Alallah. Allaah (Subhaanahu wa Ta'ala) ndiye mwenye kutoa na kutunuku.

4- Ibn Qutaybah amesema:

“Wanasema: “Haya ni kutokana na uombezi wa waungu wetu.”

Haya ni maneno ya makafiri. Ni wajibu kwa muislamu kujitofautisha nao na kuzinasibiha neema kwa Allaah. Allaah ndiye Mwenye kusababisha sababu. Kwa ajili hiyo ni wajibu kwa muislamu kumshukuru Allaah na kuyatendea kazi maamrishi Yake. Allaah (Ta'ala) amesema:

وَمَا بِكُمْ مِّنْ نُّعْمَةٍ فَمِنَ اللَّهِ ۖ ثُمَّ إِذَا مَسَّكُمُ الضُّرُّ فَإِلَيْهِ تَجْأَرُونَ

“Neema yoyote mliyo nayo, basi ni kutoka kwa Allaah. Kisha inapokuguseni dhara Kwake mnamlilia msaada.”¹⁵¹

5- Abul-'Abbaas amesema baada ya Hadiyih ya Zayd bin al-Haarith:

“Katika asubuhi hii kuna baadhi ya waja Wangu wamepambaukia wakiwa ni wenye kuniamini na wengine wamekufuru. Ama yule aliyesema kwamba: “Tumenyeshewa mvua kwa fadhila na rehema ya Allaah”, basi huyo ndiye aliyeniamini Mimi na amekufuru sayari. Ama yule aliyesema ya kwamba tumenyeshewa mvua kutokana na sayari fulani na fulani, basi huyo amenikufuru Mimi na ameamini sayari.”

“Haya yamekuja sehemu nyingi katika Qur-aan na Sunnah; Allaah (Subhaanah) anawasema vibaya wale ambao wanazinasibisha neema Zake kwa asiye kuwa Yeye na wanamshirikisha.”

Wanasema hivo kwa kujisifu na kujitapa mbele za wengine.

6- Baadhi ya Salaf wamesema:

“Aayah inawazungumzia wale wenye kusema: “Upepo ulikuwa mzuri na baharia huyu alikuwa hodari” na mfano wa maneno kama hayo ambayo hupitika katika ndimi za watu wengi.”

Wanasema hivo pindi safina inaporudi salama salimina. Wanamsahau Allaah kwamba ndiye ambaye aliwapa upepo huo na ndiye ambaye kamfunza baharia huyo. Kwa hivo ni wajibu kuzinasibisha neema kwa Allaah (Ta'ala) pamoja na kuzitambua sababu kama vile kusema kwamba Allaah katusahalishia upepo mzuri. Hili linafaa. Hii ni dalili inayoonyesha namna ambavo Salaf walikuwa

¹⁵¹ 16:53

wakitilia bidii na kupupia juu ya kumshukuru Allaah na kuzitambua neema Zake (Subhaanahu wa Ta'ala).

42. Mlango kuhusu maneno Yake (Ta'ala) “Hivyo basi msimfanyie Allaah washirika, na hali ya kuwa nyinyi mnajua.”

Shaykh-ul-Islaam Muhammad bin 'Abdil-Wahhaab (Rahimahu Allaah) amesema:

1- Allaah (Ta'ala) amesema:

الَّذِي جَعَلَ لَكُمُ الْأَرْضَ فِرَاشًا وَالسَّمَاءَ بِنَاءً وَأَنْزَلَ مِنَ السَّمَاءِ مَاءً فَأَخْرَجَ بِهِ مِنَ الثَّمَرَاتِ رِزْقًا لَّكُمْ ۗ فَلَا
تَجْعَلُوا لِلَّهِ أَنْدَادًا وَأَنْتُمْ تَعْلَمُونَ

“Ambaye amewafanyieni ardhi kuwa kama tandiko na mbingu kuwa kama paa na akateremsha kutoka mbinguni maji akawatolea kwayo matunda kuwa ni riziki kwenu. Hivyo basi msimfanyie Allaah washirika, na hali ya kuwa nyinyi mnajua.” (al-Baqarah 02:22)

2- Ibn 'Abbaas (Radhiya Allaahu 'anhuma) amesema:

“Washirika ni shirki ambayo imejificha zaidi kuliko mdudu mchungu apitae juu ya jiwe jeusi katika usiku wenye giza. Nako ni kusema: “Naapa kwa jina la Allaah na kwa uhai wako fulani na uhai wangu”, “Lau ama si kijibwa hiki mwizi angelituingilia”, “Lau kama si bata ya nyumbani wezi wangelituingilia” na mtu kumwambia mwenzake: “Akitaka Allaah na wewe” na mtu kusema pia: “Lau kama si Allaah na fulani”. Usimchanganye Allaah na mwingine yeyote. Yote haya ni kumshirikisha Allaah.

Ameipokea Ibn Abiy Haaatim.

3- 'Umar bin al-Khattwaab (Radhiya Allaahu 'anh) amesimulia ya kwamba Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Mwenye kuapa kwa asiyekuwa Allaah amekufuru au ameshirikisha.”¹⁵²

Ameipokea at-Tirmidhiy ambaye ameisahihisha na al-Haakim pia ameisahihisha.

4- Ibn Mas'ud (Radhiya Allaahu 'anh) amesema:

“Kuapa kwa Allaah hali ya kuwa ni mwenye kusema uongo inapendeza zaidi kwangu kuliko kuapa kwa asiyekuwa Allaah hali ya kuwa ni mwenye kusema ukweli.”

5- Hudhayfah (Radhiya Allaahu 'anh) ameeleza kwamba Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Msisemi “Akitaka Allaah na fulani”. Lakini semeni: “Akitaka Allaah kisha akataka fulani”.”¹⁵³

Ameipokea Abu Daawuud kwa cheni ya wapokezi Swahiyh.

6- Imekuja kutoka kwa Ibraahim an-Nakha-iy ya kwamba alikuwa akichukia mtu kusema: “Najilinda kwa Allaah na kwako”, lakini alikuwa anajuzisha kusema: “Najilinda kwa Allaah kisha kwako”. Pia akijuzisha mtu kusema: “Lau kama si kwa ajili ya Allaah kisha fulani” na wala usisemi: “Lau kama si kwa ajili ya Allaah na fulani”.

MAELEZO

1- Allaah (Ta'ala) amesema:

¹⁵² Abu Daawuud (3251), at-Tirmidhiy (1535) na Ahmad (6072). Swahiyh kwa mujibu wa al-Albaaniy katika “al-Irwaa” (2561).

¹⁵³ Abu Daawuud (4980), Ahmad (23313) na Ibn Abiy Shaybah (2669). Swahiyh kwa mujibu wa al-Albaaniy katika “as-Silsilah as-Swahiyah” (137).

الَّذِي جَعَلَ لَكُمُ الْأَرْضَ فِرَاشًا وَالسَّمَاءَ بِنَاءً وَأَنْزَلَ مِنَ السَّمَاءِ مَاءً فَأَخْرَجَ بِهِ مِنَ الثَّمَرَاتِ رِزْقًا لَّكُمْ ۖ فَلَا
تَجْعَلُوا لِلَّهِ أَنْدَادًا وَأَنْتُمْ تَعْلَمُونَ

“Ambaye amewafanyieni ardhi kuwa kama tandiko na mbingu kuwa kama paa na akateremsha kutoka mbinguni maji akawatolea kwayo matunda kuwa ni riziki kwenu. Hivyo basi msimfanyie Allaah washirika, na hali ya kuwa nyinyi mnajua.”

Katika mlango huu mtunzi wa kitabu anachotaka ni kuwatahadharisha watu kumfanyia Allaah washirika. Washirika ni wingi wa mshirika na walinganizi. Allaah amewaita waungu kama makaburi, miti na sayari kuwa ni “washirika” kwa sababu watu wanawaabudu pamoja na Allaah. Kama mtu anakiomba kitu, anakiomba uokozi, anakiomba mambo mengine na anaamini kuwa kinanufaisha na kudhuru kinaitwa “mshirika”. Allaah (Ta’ala) amesema:

وَأَنْتُمْ تَعْلَمُونَ

“... na hali ya kuwa nyinyi mnajua.”

Bi maana na nyinyi mnatambua kuwa Yeye ndiye Muumbaji, Mruzukaji na Mungu wa haki (Subhaanahu wa Ta’ala). Amesema wakati alipokuwa akiwasema vibaya baadhi ya watu:

وَمَنْ النَّاسِ مَنْ يَتَّخِذُ مِنْ دُونِ اللَّهِ أَنْدَادًا يُحِبُّونَهُمْ كَحُبِّ اللَّهِ

“Miongoni mwa watu wako wenye kuchukua asiyekuwa Allaah kuwa ni mungu mshirika ambapo wanawapenda kama mapenzi wanavyompenda Allaah... ” (**al-Baqarah 02:165**)

Lengo kwa haya ni kuwaita watu kumtakasia ‘ibaadah Allaah (Ta’ala) pekee. Yeye ndiye awe Mungu wa haki wa kuabudiwa pekee. Amesema (Ta’ala):

وَإِلَهُكُمْ إِلَهٌ وَاحِدٌ ۖ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ الرَّحْمَنُ الرَّحِيمُ

“Mungu wenu ni Mungu mmoja pekee; hapana mwabudiwa wa haki isipokuwa Yeye, Mwingi wa huruma, Mwenye kurehemu.” (al-Baqarah 02:163)

وَمَنْ يَدْعُ مَعَ اللَّهِ إِلَهًا آخَرَ لَا بُرْهَانَ لَهُ بِهِ فَإِنَّمَا حِسَابُهُ عِنْدَ رَبِّهِ ۗ إِنَّهُ لَا يُفْلِحُ الْكَافِرُونَ

“Yeyote yule anayeomba pamoja na Allaah mungu mwingine - hana ushahidi wa wazi juu ya hilo - basi hakika hesabu yake iko kwa Mola wake. Hakika hawafaulu makafiri.” (al-Mu’minuun 23:117)

2- Ibn ‘Abbaas (Radhiya Allaahu ‘anhuma) amesema:

“Washirika ni shirki ambayo imejificha zaidi kuliko mdudu mchungu apitae juu ya jiwe jeusi katika usiku wenye giza. Nako ni kusema: “Naapa kwa jina la Allaah na kwa uhai wako fulani na uhai wangu”, “Lau ama si kijibwa hiki mwizi angelituingilia”, “Lau kama si bata ya nyumbani wezi wangelituingilia” na mtu kumwambia mwenzake: “Akitaka Allaah na wewe” na mtu kusema pia: “Lau kama si Allaah na fulani”. Usimchanganye Allaah na mwingine yeyote. Yote haya ni kumshirikisha Allaah.

Ameipokea Ibn Abiy Haaatim.

Ibn ‘Abbaas ameyafasiri yote hayo kuwa ni shirki. Anamaanisha kuwa ni shirki ndogo iliyofichikana. Kwa sababu shirki ndogo ndani yake kunaingia kufanya washirika. Lakini baya na khatari zaidi ni kuyaomba masanamu na mawe. Hii ni shirki kubwa. Mtu anatakiwa kutia akilini kwamba shirki iliyofichikana (yaani shirki ndogo) inapelekea katika shirki kubwa. Kwa ajili hiyo ndio maana akazindua juu ya hilo ili watu waweze kujitenga mbali na yote mawili. Wakati Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) alipoambiwa “Akitaka Allaah na wewe” akasema (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam):

“Je, umenifanya kuwa mshirika wa Allaah? Sema: “Akitaka Allaah pekee.”¹⁵⁴

Hivyo Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) akaonelea kusema “Akitaka Allaah na wewe” ni katika kumfanyia Allaah washirika. Kwa ajili hiyo ndio maana inatakiwa kwa mtu kujiepusha na mambo kama hayo na misemo kama hiyo, kwa sababu “wa” inafahamisha ushirikiano na usawazishaji. Kadhalika inahusiana na msemu “Lau kama si bata au mbwa nyumbani basi watu wa nyumbani wasingeliwatambua wageni”. Ni kosa. Badala yake unatakiwa kusema “Lau kama si Allaah kisha bata”. Allaah ndiye Mwenye kusababisha sababu. Mtu hatakiwi kutegemea sababu; anatakiwa amtegemea Allaah pekee. Kwa ajili hiyo zile sababu hazitakiwi kutajwa peke yake au kuambatanishwa pamoja na “na”, isipokuwa ziambatanishwe na “kisha/halafu”. Mfano wa usemi mwingine ni “Lau kama si mtu yule basi alikuwa azame.” Ni kosa. Bali inatakiwa kusemwa “Lau kama si Allaah kisha fulani basi angelizama”.

3- 'Umar bin al-Khattwaab (Radhiya Allaahu 'anh) amesimulia ya kwamba Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Mwenye kuapa kwa asiyekuwa Allaah amekufuru au ameshirikisha.”¹⁵⁵

Ameipokea at-Tirmidhiy ambaye ameisahihisha na al-Haakim pia ameisahihisha.

Ukweli wa mambo ni kwamba Ibn 'Umar (Radhiya Allaahu 'anhuma) ndiye kasimulia haya. Mashaka katika Hadiyth inawezekana yanatokamana na Ibn 'Umar au mpokezi mwingine. Lakini maana yake ni moja. Kuapa kwa jina la mwingine asiyekuwa Allaah ni kumuadhimisha na kuona kuwa mtu/kitu hicho ni chenye kustahiki kiapo hicho. Kwa ajili hiyo inatakiwa kuapa kwa jina la Allaah pekee kwa sababu Yeye ndiye Mwenye kujua siri na mambo yaliyofichikana.

¹⁵⁴ Ahmad (1839), al-Bukhaariy katika “al-Adab al-Mufrad” (783) na at-Twabaraaniy (13005). Swahiyh kwa mujibu wa al-Albaaniy katika “as-Silsilah as-Swahiyhah” (139).

¹⁵⁵ Abu Daawuud (3251), at-Tirmidhiy (1535) na Ahmad (6072). Swahiyh kwa mujibu wa al-Albaaniy katika “al-Irwaa” (2561).

Hapo kabla waarabu walikuwa wakiapa kwa baba zao na kwa watu wakuu. Ni jambo lililokuwa linafaa mwanzoni mwa Uislamu. Kisha baadaye Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) akalikataza na kulitahadharisha. Amesema (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam):

“Msiape kwa baba zenu, mama zenu wala washirika.”¹⁵⁶

Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Mwenye kutaka kuapa basi aape kwa Allaah au anyamaze.”¹⁵⁷

Imaam Ahmad amepokea kupitia kwa 'Umar kwamba Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Mwenye kutaka kuapa basi aape kwa Allaah au anyamaze. Mwenye kuapa kwa kitu kingine badala ya Allaah ameshirikisha.”

Haya ni matamshi ya 'Umar kama tulivosema.

Kitendo hichi ni shirki ndogo. Kuna uwezekano vilevile ikawa ni shirki kubwa ikiwa yule muapaji anaonelea kuwa mtu huyo anayemuapia ana hadhi, anaendesha ulimwengu au anastahiki kuabudiwa badala ya Allaah. Vinginevyo ni shirki ndogo. Kwa ajili hiyo imepokelewa kwamba Salaf walikuwa wakiapa kwa baba zao mwanzoni mwa Uislamu. Lakini kwa ajili ya kukamilisha Tawhiyd, kumuadhimisha Allaah na kufunga njia zote zinazopelekea katika shirki wakayakataza hayo.

4- Ibn Mas'uud (Radhiya Allaahu 'anh) amesema:

¹⁵⁶ Abû Daawuud (3248) na an-Nasaa'iy (3769). Swahiyh kwa mujibu wa al-Albaaniy katika "Swahiyh-ul-Jaami'" (7249).

¹⁵⁷ al-Bukhaariy (2679) na Muslim (1646).

“Kuapa kwa Allaah hali ya kuwa ni mwenye kusema uongo inapendeza zaidi kwangu kuliko kuapa kwa asiyekuwa Allaah hali ya kuwa ni mwenye kusema ukweli.”

Kwa sababu kuapa kwa asiyekuwa Allaah ni shirki na kuapa kwa kuapa kwa Allaah kwa kusema uongo ni dhambi. Shirki ni jambo la khatari kuliko dhambi. Sampuli ya shirki ni khatari kuliko sampuli ya maasi. Pamoja na hivyo uongo pia ni haramu.

5- Hudhayfah (Radhiya Allaahu 'anh) ameeleza kwamba Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Msisemi “Akitaka Allaah na fulani”. Lakini semeni: “Akitaka Allaah kisha akataka fulani”.”¹⁵⁸

Ameipokea Abu Daawuud kwa cheni ya wapokezi Swahiyh.

Kwa sababu “na” inafahamisha ushirika na usawazishaji. Kwa ajili hiyo haijuzu kusema hivo. Hata hivyo inafaa kusema “kisha/halafu” kwa sababu inaonyesha tofauti. Hata hivyo bora zaidi ni kusema “Lau kama si Allaah pekee.”

6- Imekuja kutoka kwa Ibraahiym an-Nakha-iy ya kwamba alikuwa akichukia mtu kusema: “Najilinda kwa Allaah na kwako”, lakini alikuwa anajuzisha kusema: “Najilinda kwa Allaah kisha kwako”. Pia akijuzisha mtu kusema: “Lau kama si kwa ajili ya Allaah kisha fulani” na wala usisemi: “Lau kama si kwa ajili ya Allaah na fulani”.

Haijuzu kusema “Najilida kwa fulani na fulani” au “Najilinda kwa Allaah na fulani na fulani”. Badala yake sema “Najilinda kwa Allaah”. Huu ndio ukamilifu wa Tawhiyd. Ni wajibu kwa muislamu kutilia bidii juu ya ukamilifu wa Tawhiyd na imani na kujiepusha na aina zote za shirki. Ni wajibu vilevile kujiepusha na

¹⁵⁸ Abu Daawuud (4980), Ahmad (23313) na Ibn Abiy Shaybah (2669). Swahiyh kwa mujibu wa al-Albaaniy katika “as-Silsilah as-Swahiyhah” (137).

sampuli zote za maasi kwa sababu ni mambo yanaipunguza Tawhiyd, imani na yakini.

Faida:

Hadiyth inayosema “Naapa kwa baba yangu atafaulu”¹⁵⁹ ni jambo lilitokea mwanzoni mwa Uislamu na kabla ya kukatazwa kusema hivo.

Haijuzu kusema “Lau kama si Allaah kisha Mtume wake basi tusingeongoka.”

Hadiyth inayosema “Hamwogopi isipokuwa Allaah na mbwa mwitu”¹⁶⁰ ni jambo haliingii katika maudhui haya. Inajuzu.

Haijuzu kusema “Nakuuliza kwa dhimma yako” au “Nakuuliza kwa amana” ikiwa mtu amekusudia kuapa kwa vitu hivyo. Vinginevyo inajuzu.

Inajuzu kusema “Naomba ulinzi kwa Allaah kutokamana na wewe”. Pindi mwanamke alipomwambia hivo Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) akamwambia mwanamke yule:

“Umeomba ulinzi kwa aliye Mtukufu.”¹⁶¹

Baada ya hapo akamwacha.

Mtu akitendewa wema na mwengine na akamwambia kwamba yeye ni mwokozi mkubwa, yote haya yanategemea nia. Bora ni kusema “Lau kama isingelikuwa Allaah kisha wewe”. Kusema “Wewe ni mwokozi mkubwa” ni jambo linaweza kuleta mashaka.

¹⁵⁹ Muslim (11).

¹⁶⁰ al-Bukhaariy (3852).

¹⁶¹ al-Bukhaariy (5254).

43. Mlangu kuhusu ambaye hakuridhika kuapiwa kwa Allaah

Shaykh-ul-Islaam Muhammad bin 'Abdil-Wahhaab (Rahimahu Allaah) amesema:

1- Ibn 'Umar (Radhiya Allaahu 'anhumaa) amesimulia kwamba Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Msiape kwa baba zenu. Atakayeapa kwa Allaah basi na aseme ukweli. Yule mwenye kuapiwa kwa Allaah basi aridhie. Yule ambaye hakuridhia sio katika Allaah.”¹⁶²

Ameipokea Ibn Maajah kwa cheni ya wapokezi nzuri.

MAELEZO

Mwandishi anakusudia kwa kichwa cha khabari hiki kubainisha uwajibu wa kuridhika kwa kiapo japokuwa mtu atakuwa ni mwenye kutilia mashaka ukweli wa yule mwenye kuapa au pengine hata akawa anajua kuwa anasema uongo au kwamba ni mwenye kutuhumiwa uongo. Pamoja na hivyo anatakiwa kuridhia hukumu ya Kishari'ah na kuridhika na hilo. Kwa sababu watu hawana ya kutazama isipokuwa yale ya dhahiri. Kadhalika hakimu hana jengine analoweza kufanya kunapokosekana ushahidi isipokuwa kusikiliza ule ushahidi wa mashahidi au kiapo cha mtuhumiwa.

1- Ibn 'Umar (Radhiya Allaahu 'anhumaa) amesimulia kwamba Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

¹⁶² Ibn Maajah (2101) na al-Bayhaqiy (20512). Swahiyh kwa mujibu wa al-Albaaniy katika "Swahiyh Ibn Maajah" (1708).

“Msiape kwa baba zenu. Atakayeapa kwa Allaah basi na aseme ukweli. Yule mwenye kuapiwa kwa Allaah basi aridhie. Yule ambaye hakuridhia sio katika Allaah.”

Ameipokea Ibn Maajah kwa cheni ya wapokezi nzuri.

Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) amekataza kuapa kwa baba, mama wala viumbe wengineo. Mwanzoni mwa Uislamu na wakati walipohajiri kwa mara ya kwanza kwenda al-Madiynah walikuwa wakifanya hivo. Ndipo wakakatazwa kufanya hivo. Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) akasema:

“Atakayeapa kwa Allaah basi na aseme ukweli.”

Ni wajibu kwa ambaye anaapa kwa Allaah aseme ukweli na asidanganye. Ndio maana Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) amesema:

“Mwenye kuapa kiapo ilihali ni mwongo basi atakutana na Allaah hali ya kuwa amemkasirikia.”¹⁶³

Ni wajibu kutahadhari kuapa kwa Allaah hali ya kudanganya na khaswakhaswa katika magomvi na wakati inapohusiana na kupokonya haki ya muislamu. Kwa ajili hiyo imekuja katika Hadiyth nyingine:

“Yule mwenye kupokonya haki ya muislamu kwa kiapo chake basi amejijawajibishia kwa Allaah Moto na ameharamishiwa Moto.” Wakauliza: “Hata kama inahusiana na kitu kidogo?” Akajibu: “Hata kama inahusiana na kokwa ya tende.”¹⁶⁴

Ameipokea Muslim.

¹⁶³ al-Bukhaariy (2357) na Muslim (138).

¹⁶⁴ Muslim (137).

Ni wajibu kwa mtu kuyaepuka yote hayo na asichukue haki ya nduguye muislamu isipokuwa kwa dalili za Kishari'ah au kwa mtazamo wa Kishari'ah. Mtu akimtaka kuapa basi atahadhari asiseme uongo.

Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Yule mwenye kuapiwa kwa Allaah basi aridhie.”

Haya ndio makusudio. Anatakiwa kuridhia na kukinaika. Hana jengine la kufanya kwa sababu yeye ndiye ambaye kazembea kwa sababu hakushuhudisha, hakuandika na wala hakutoa hoja. Ailaumu nafsi yake mwenyewe na aridhie kiapo cha Kishari'ah. Allaah atampa haki yake siku ya Qiyaamah.

Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Yule ambaye hakuridhia sio katika Allaah.”

Haya ni matishio makali juu ya yule asiyeridhia na asiyekinaika na hukumu ya Allaah.

Faida:

Kafara kwa mwenye kuapa kwa kusema uongo atubie na arudishe haki kwa wenye nayo.

44. Mlango kuhusu kusema “Akitaka Allaah na wewe”

Shaykh-ul-Islaam Muhammad bin 'Abdil-Wahhaab (Rahimahu Allaah) amesema:

1- Qutaylah amesema:

“Kuna myahudi alikuja kwa Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) na akasema: “Hakika nyinyi mnafanya shirki. Mnasema: “Akitaka Allaah na ukataka wewe” na mnasema: “Naapa kwa Ka'bah.” Ndipo Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) akawa amewaamrisha wanapotaka kuapa basi waseme: “Naapa kwa Mola wa Ka'bah” na waseme: “Akitaka Allaah kisha wewe”.”¹⁶⁵

Ameipokea an-Nasaa'iy na ameisahihisha.

2- an-Nasaa'iy amepokea vilevile Hadiyth kutoka kwa Ibn 'Abbaas (Radhiya Allaahu 'anhumaa) ambaye amesema:

“Kuna mtu alimwambia Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam): “Akitaka Allaah na ukataka wewe”. Ndipo akasema: “Je, umenifanya mimi kuwa mshirika wa Allaah?” Watakiwa kusema: “Akitaka Allaah pekee.”¹⁶⁶

3- Ibn Maajah amepokea kutoka kwa at-Twufayl ambaye ni kaka wa 'Aaishah (Radhiya Allaahu 'anhaa) kwa upande wa mama yake, amesema:

“Nimeona ndotoni ambapo niliwapitia kundi la mayahudi na kuwaambia: “Nyinyi ni watu wazuri lau msingelisema kwamba 'Uzayr ni mwana wa Allaah.” Wakasema: “Nanyi ni watu wazuri pia lau msingelisema: “Akitaka

¹⁶⁵ an-Nasaa'iy (3773) na at-Twabaraaniy (7). Swahiyh kwa mujibu wa al-Albaaniy katika “Silsilat-ul-Ahaadiyth as-Swahiyhah” (136).

¹⁶⁶ al-Bukhaariy katika “al-Adab al-Mufrad” (783) na at-Twabaraaniy (13005).

Allaah na akataka Muhammad". Baada ya hapo nikawapitia kundi katika manaswara na nikawaambia: "Nyinyi ni watu wazuri lau msingelisema kwamba al-Masiyh ni mwana wa Allaah". Nao wakasema: "Nanyi ni watu wazuri pia lau msingelisema: "Akitaka Allaah na akataka Muhammad". Kulipopambazuka nikamweleza niliyemweleza kisha nikamwendea Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) na nikamweleza. Akasema: "Je, umemweleza haya yeyote?" Nikasema: "Ndio." Akamhimidi Allaah na kumsifu kisha akasema "Ama baada ya hayo; hakika Twufayl ameona ndoto na kishamweleza aliyemweleza katika nyinyi. Hakika nyinyi mlikuwa mkisema maneno kadhaa na kadhaa ambayo yalikuwa yakinitatiza nikawa nashindwa kuwakataza nayo. Hivyo msisemi: "Akitaka Allaah na akataka Muhammad". Lakini semeni: "Akitaka Allaah pekee"."¹⁶⁷

MAELEZO

Anachotaka mwandishi ni kubainisha hukumu ya kusema "Akitaka Allaah na akataka fulani" na mfano wa maneno kama hayo na kwamba kilicho cha wajibu ni kusema "Akitaka Allaah kisha fulani". Haya ndio yanayopelekewa na Tawhiyd na Ikhlaasw. Ndani yake kuna ukamilifu wa Tawhiyd na kujitenga mbali na aina zote za shirki. Hukumu ya kusema namna hiyo ni kwamba haifai. Makusudio ya mlango huu kwa msemu mwingine ni kwamba hukumu ya kutamka namna hiyo.

Kamilifu zaidi ni kusema "Akitaka Allaah pekee". Hata hivyo inafaa kusema "Akitaka Allaah kisha akataka fulani". Ama kusema "Akitaka Allaah na akataka fulani" haijuzu. Ni aina ya shirki ndogo na linaipunguza Tawhiyd. Vilevile inahusiana na matamshi mfano wa hayo.

1- Qutaylah amesema:

¹⁶⁷ Ibn Maajah (2118), Ahmad (20713), Ibn Hibbaan (5725), al-Haakim (5945) na at-Twabaraaniy (8214). Swahiyh kwa mujibu wa al-Albaaniy katika "Swahiyh Ibn Maajah" (1721).

“Kuna myahudi alikuja kwa Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) na akasema: “Hakika nyinyi mnafanya shirki. Mnasema: “Akitaka Allaah na ukataka wewe” na mnasema: “Naapa kwa Ka’bah.” Ndipo Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) akawa amewaamrisha wanapotaka kuapa basi waseme: “Naapa kwa Mola wa Ka’bah” na waseme: “Akitaka Allaah kisha wewe”.”

Ameipokea an-Nasaa’iy na ameisahihisha.

Hapa kuna dalili inayoonyesha kwamba watu wapotevu wanaweza kuyafahamu baadhi ya mambo japokuwa wao wenyewe ni wenye kutumbukia katika dhambi na kufuru mbaya zaidi. Kwa ajili hiyo mayahudi waliwakaripia waislamu kwa sababu ya matamshi hayo yote haya kwa sababu tu ya chuki na vifundo walivyo navyo dhidi ya Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam). Hata hivyo walipatia katika haya. Ndio maana Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) akawaamrisha waseme “Akitaka Allaah kisha akataka fulani” na waape kwa Mola wa Ka’bah.

2- an-Nasaa’iy amepokea vilevile Hadiyih kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (Radhiya Allaahu ‘anhumaa) ambaye amesema:

“Kuna mtu alimwambia Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam): “Akitaka Allaah na ukataka wewe”. Ndipo akasema: “Je, umenifanya mimi kuwa mshirika wa Allaah?” Watakiwa kusema: “Akitaka Allaah pekee.”

Katika upokezi mwingine imekuja:

“Je, umenifanya kuwa ni mwenye kulingana na Allaah?”

3- Ibn Maajah amepokea kutoka kwa at-Twufayl ambaye ni kaka wa ‘Aaishah (Radhiya Allaahu ‘anhaa) kwa upande wa mama yake, amesema:

“Nimeona ndotoni ambapo niliwapitia kundi la mayahudi na kuwaambia: “Nyinyi ni watu wazuri lau msingelisema kwamba ‘Uzayr ni mwana wa

Allaah.” Wakasema: “Nanyi ni watu wazuri pia lau msingelisema: “Akitaka Allaah na akataka Muhammad”. Baada ya hapo nikawapitia kundi katika manaswara na nikawaambia: “Nyinyi ni watu wazuri lau msingelisema kwamba al-Masiyh ni mwana wa Allaah”. Nao wakasema: “Nanyi ni watu wazuri pia lau msingelisema: “Akitaka Allaah na akataka Muhammad”. Kulipopambazuka nikamweleza niliyemweleza kisha nikamwendea Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) na nikamweleza. Akasema: “Je, umemweleza haya yeyote?” Nikasema: “Ndio.” Akamhimidi Allaah na kumsifu kisha akasema “Ama baada ya hayo; hakika Twufayl ameona ndoto na kishamweleza aliyemweleza katika nyinyi. Hakika nyinyi mlikuwa mkisema maneno kadhaa na kadhaa ambayo yalikuwa yakinitatiza nikawa nashindwa kuwakataza nayo. Hivyo msisemi: “Akitaka Allaah na akataka Muhammad”. Lakini semeni: “Akitaka Allaah pekee”.”

Bi maana mlikuwa ni wenye kustahiki kusifiwa msingelisema hivo.

Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) akasema:

“Hakika nyinyi mlikuwa mkisema maneno kadhaa na kadhaa ambayo yalikuwa yakinitatiza nikawa nashindwa kuwakataza nayo.”

Kwa sababu kulikuwa hakujakuja kitu kutoka kwa Allaah. Wakati ndoto ilipokuja ndipo kukaja sababu ya kuwakataza. Vivyo hivyo kumekuja Wahy wa makatazo juu ya kusema hivo na badala yake maamrishi ya kusema:

“Akitaka Allaah pekee.”

Katika Hadiyth iliopokelewa na al-Bukhaariy na Muslim kuhusu kipofu, mwenye ukoma na mwenye upara imekuja:

“Hakuna yeyote awezaye kunifikisha hii leo isipokuwa Allaah kisha wewe.”¹⁶⁸

¹⁶⁸ al-Bukhaariy (3464) na Muslim (2964).

Hili ndilo la wajibu.

Ni kama tulivosema kwamba kusema “Akitaka Allaah na wewe” ni shirki ndogo. Inaweza vilevile kuwa shirki kubwa ikiwa anamaanisha kwamba mtu huyo yeye ndiye anayeyaendesha mambo kwa kutaka kwake mwenyewe.

45. Mwenye kutukana wakati amemuudhi Allaah

Shaykh-ul-Islaam Muhammad bin 'Abdil-Wahhaab (Rahimahu Allaah) amesema:

1- Allaah (Ta'ala) amesema:

وَقَالُوا مَا هِيَ إِلَّا حَيَاتُنَا الدُّنْيَا نَمُوتُ وَنَحْيَا وَمَا يُهْلِكُنَا إِلَّا الدَّهْرُ

“Wakasema: “Haya sisi chochote isipokuwa ni maisha yetu dunia. Tunakufa na tunahuika na hakuna cha kutuangamiza isipokuwa zama tu.” (al-Jaathiyah 45:24)

2- Imesihi kupokelewa kupitia kwa Abu Hurayrah (Radhiya Allaahu 'anh) kwamba Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Allaah (Ta'ala) amesema: “Mwanadamu ananiudhi. Anatukana wakati – ilihali Mimi ni wakati; Nageuza usiku na mchana.”¹⁶⁹

Katika upokezi mwingine imekuja:

“Msitukane wakati. Kwani hakika ya Allaah ndiye wakati.”¹⁷⁰

MAELEZO

Alichokusudia mwandishi kwa kichwa cha khabari hiki ni kubainisha kwamba kutukana wakati na madhambi mengine ni miongoni mwa mambo yanayopunguza na kudhoofisha Tawhiyd na kupunguza ukamilifu wake. Kwa hivyo ni wajibu kutahadhari na madhambi yote yanayoidhoofisha imani

¹⁶⁹ al-Bukhaariy (4826) na Muslim (2246).

¹⁷⁰ Muslim (2246).

kukiwemo vilevile kutukana wakati, upepo na vyengine vyote visivyostahiki kutukanwa. Ni wajibu kutahadhari na yale yote yanayomkasirisha Allaah.

Wakati umeumbwa na unaendeshwa. Hauwezi kufanya kitu peke yake. Allaah (Ta'ala) ndiye mwenye kuuendesha. Wakati ndani yake kuna nyusiku na michana. Mwenye kutukana wakati anamuudhi Allaah. Hakuna chochote kiwezacho kumdhuru Allaah, lakini maasi yanamuudhi kwa sababu yanamughadhibisha. Allaah (Ta'ala) amesema:

إِنَّ الَّذِينَ يُؤْذُونَ اللَّهَ وَرَسُولَهُ لَعَنَهُمُ اللَّهُ فِي الدُّنْيَا وَالْآخِرَةِ وَأَعَدَّ لَهُمْ عَذَابًا مُّهِينًا

“Hakika wale wanaomuudhi Allaah na Mtume wake, Allaah amewalaani duniani na Aakhirah na amewaandalia adhabu ya kutweza.” (al-Ahzaab 33:57)

Kutukana wakati maana yake ni kutukana zama kutokana na yale yanayopitika ndani ya usiku na mchana. Mfano wa hayo ni kama mtu kumuomba Allaah alaani saa au akamuomba Allaah alaani siku fulani au akamuomba Allaah asiibariki siku fulani na mfano wa hayo. Kutukana wakati maana yake ni kuuapiza, kuulani au kuomba du'aa dhidi yake.

Hata hivyo sio matusi kuelezea kwamba wakati ni mzito. Mfano wa hilo ni kama mtu kusema kwamba siku hii ni nzito, ngumu, yenye huzuni, yenye baridi au yenye joto kali.

2- Imesihi kupokelewa kupitia kwa Abu Hurayrah (Radhiya Allaahu 'anh) kwamba Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Allaah (Ta'ala) amesema: “Mwanadamu ananiudhi. Anatukana wakati – ilihali Mimi ni wakati; Nageuza usiku na mchana.”

Katika upokezi mwingine imekuja:

“Msitukane wakati. Kwani hakika ya Allaah ndiye wakati.”

Hapa kumbainishwa maana ya wakati na kwamba ni usiku na mchana. Allaah ndiye mwenye kugeuza usiku na mchana. Mwenye kutukana wakati anamtukana Yule aliyeuumba na kuugeuza. Jambo hilo halijuzu.

Amekosea yule aliyesema kuwa ad-Dahr, wakati, ni katika majina ya Allaah. Mmoja katika wao ni Ibn Hazm. Hadiyth inafahamisha kwamba Allaah ndiye ambaye kaumba wakati na kuutunuku yale yote yanayotokea. Miongoni mwa hayo ni maneno yake Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam):

“Msitukane upepo.”¹⁷¹

Vivyo hivyo kumtukana ngamia, mbuzi, kondoo, ng'ombe na vyengine vyote visivyostahiki kutukanwa. Kutukana huku kunaipunguza imani na Tawhiyd ya mtu.

¹⁷¹ at-Tirmidhiy (2252), Ibn Maajah (3727), Ahmad (7407), al-Haakim (3075) na al-Bukhaariy katika "al-Adab al-Mufrad" (719). Swahiyh kwa mujibu wa al-Albaaniy katika "Swahiyh Ibn Maajah" (3003).

46. Kuitwa “qaadhi wa maqaadhi” na mfano wake

Shaykh-ul-Islaam Muhammad bin 'Abdil-Wahhaab (Rahimahu Allaah) amesema:

1- Imesihi kupokelewa kupita kwa Abu Hurayrah (Radhiya Allaahu 'anh) ya kwamba Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Jina twevu na lenye kuchukiza mbele ya Allaah ni mtu kujiita “mfalme wa wafalme”. Hakika hakuna mfalme isipokuwa Allaah.”¹⁷²

Sufyaan amesema:

“Mfano mwingine ni kama mtu kujiita “Shaahaan Shaah”.”

Katika upokezi mwingine imekuja:

“Mtu anayechukiwa zaidi na Allaah siku ya Qiyaamah na mbaya zaidi... ”¹⁷³

Mtwevu bi maana mbaya.

MAELEZO

Alichokusudia mwandishi kwa kichwa cha khabari hiki ni makatazo juu ya majina yanayoweza kufanana na majina ya Allaah. Kwa sababu Yeye (Subhaanah) ana majina ambayo amepwekeka nayo. Baadhi ya majina hayo ni “ar-Rahmaan”, “Maalik-ul-Mulk”, “al-Khallaq”, “Rabb-ul-'Aalamiyn”, “Haakim-ul-Hukkaam” na “Sultwaan-us-Salaatwiyn”. Katika kuikamilisha na kuitimiliza Tawhiyd ni kujiepusha kujiita majina kama haya. Kujiita majina kama hayo ni jambo linaipunguza Tawhiyd na imani. Haijuzu.

¹⁷² al-Bukhaariy (6205) na Muslim (2143).

¹⁷³ Muslim (2143).

Kadhalika inahusiana na “qaadhiy wa maqaadhiy”. Hili ni jambo lipo katika baadhi ya miji. Hata kama wanamaanisha kwamba mtu huyo ndiye hakimumu wa mahakimu katika nchi hiyo lakini hata hivyo ni jina lisilosilihi na lisilofaa.

Ama ikiwa jina hilo litafungamanishwa na nchi fulani kama kwa mfano “qaadhiy wa maqaadhiy wa Misri au Makkah” ni jambo linakuwa na wepesi fulani, lakini pamoja na hivyo kuacha kufanya hivo ndio bora zaidi. Badala yake mtu anaweza kutumia jina “kiongozi wa maqaadhiy” au “amiri wa maqaadhiy” ili mtu awe ameeepuka majina haya yanayotajwa kwa kutokufungamanisha.

1- Imesihi kupokelewa kupita kwa Abu Hurayrah (Radhiya Allaahu ‘anh) ya kwamba Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) amesema:

“Jina twevu na lenye kuchukiza mbele ya Allaah ni mtu kujiita “mfalme wa wafalme”. Hakika hakuna mfalme isipokuwa Allaah.”

Bi maana jina dhalili na lenye kuchukiwa zaidi.

Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) amekataza jina hilo kwa sababu linamfanya mtu kufikiria sifa isiyoendana naye. Sifa kama hiyo ni ya Allaah (Ta’ala) peke yake. Mtu sio mfalme wa wafalme. Si jina lenye kusilihi kwake. Vivyo hivyo inahusiana na majina mengine yote.

Shaahaan Shaah ni jina la wasiokuwa waarabu na maana yake ni “mfalme wa wafalme”.

47. Kuyaheshimu majina ya Allaah na kubadilisha jina kwa ajili aa hilo

Shaykh-ul-Islaam Muhammad bin 'Abdil-Wahhaab (Rahimahu Allaah) amesema:

1- Abu Shurayh ameeleza ya kwamba alikuwa akiitwa "Abul-Hakam", baba wa wahakimu, Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) akamwambia: "Allaah ndiye Hakimu na hukumu ni Yake." Kisha Abu Shurayh akasema: "Hakika watu wangu wanapotofautiana katika kitu basi hunijia na nikahukumu baina yao na matokeo yake pande zote mbili huridhika." Akasema (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam): "Ni uzuri ulioje wa jambo hilo! Kwani wewe huna mtoto?" Nikasema: "Shurayh, Muslim na 'Abdullaah." Akasema (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam): "Ni nani mkubwa wao?" Nikasema: "Shurayh." Ndipo akasema (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam): "Basi wewe ni Abu Shurayh."¹⁷⁴

Ameipokea Abu Daawuud na wengineo.

MAELEZO

Anachotaka kubainisha mwandishi ni kwamba ni wajibu kuyaheshimu majina ya Allaah na kutahadhari juu ya kuyatweza, kuyadharau au kumwita nayo mwengine yale majina ambayo ni maalum Kwake Yeye. Kwa ajili hiyo ni jambo limesuniwa kuyabadilisha kwa ajili ya kuyaheshimu na kuyaadhimisha.

Majina yamegawanyika sehemu mbili:

1- Majina ambayo haifai kuwa nayo isipokuwa Allaah peke yake. Mfano wa majina hayo ni ar-Rahmaan, al-Khaaliq na Rabb-ul-'Aalamiyn.

¹⁷⁴ Abu Daawuud (4955), an-Nasaa'iy (5387) na Ibn Hibbaan (504). Nzuri kwa mujibu wa al-Albaaniy katika "Mishkaat-ul-Maswaabiyh" (4766).

2- Majina ambayo sio maalum kwa Allaah (Subhaanah) pekee. Katika hali hii majina haya ya Allaah yanalingana na utukufu na ukubwa wa Allaah na majina ya viumbe yanalingana na maumbile yao. Makusudio ya mlango huu ni hayo majina ya kwanza.

1- Abu Shurayh ameeleza ya kwamba alikuwa akiitwa “Abul-Hakam”, baba wa wahakimu, Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) akamwambia: “Allaah ndiye Hakimu na hukumu ni Yake.” Kisha Abu Shurayh akasema: “Hakika watu wangu wanapotofautiana katika kitu basi hunijia na nikahukumu baina yao na matokeo yake pande zote mbili huridhika.” Akasema (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam): “Ni uzuri ulioje wa jambo hilo! Kwani wewe huna mtoto?” Nikasema: “Shurayh, Muslim na ‘Abdullaah.” Akasema (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam): “Ni nani mkubwa wao?” Nikasema: “Shurayh.” Ndipo akasema (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam): “Basi wewe ni Abu Shurayh.”

Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) alisema:

“Ni uzuri ulioje wa jambo hilo!”

Bi maana ni uzuri ulioje wa jambo hili wa kusuluhisha kati yao na kuwaombea hadi wakaridhika na wakaacha kuzozana. Hivi ndivo inavyotakikana kuwa.

Faida mbalimbali:

Ni wajibu kuyaheshimu majina ya Allaah na kubadilisha jina kwa ajili ya hilo. Ndio maana akambadilisha jina lake la Abul-Hakam na kumpa Abu Shurayh. Hadiyth inaonyesha pia kwamba kun-ya ya mtu inapaswa iwe ya yule mtoto wake mkubwa.

Hadiyth inatupa dalili nyingine kwamba imesuniwa kusuluhisha hali za watu na kwamba ni jambo linalotakikana na inapaswa kwa wale wakuu kuwaombea baina ya watu wakati wa magomvi ili wasiendeleo kugombana na kufanyiana vifundo na chuki. Kusuluhisha kati ya watu ni bora kuliko kuwahukumu. Hukumu inapelekea katika mizozo. Wakipatana kwa kuridhiana na ikaondoka

ile chuki yote iliyomo vifuani mwao na mapenzi na mahaba yakafunguka inakuwa bora.

Mwandishi amesema:

“Ameipokea Abu Daawuud na wengineo.”

Udhahiri ni kwamba mtunzi wa kitabu anaona kuwa Hadiyth ni hoja. Ndio maana ametosheka nayo. Ameitumia kama dalili kuonyesha kuwa haifai kuitwa kwa majina kama “al-Hakam” na “Abul-Hakam”. Kwa sababu hizi ni sifa za Allaah (Ta’ala). Yeye ndiye mwenye kuhukumu kati ya waja Wake. Katika dunia hii anahukumu kwa Shari’ah Yake na Aakhirah atahukumu Mwenyewe.

Lakini hata hivyo imekuja katika Hadiyth nyingi Swahiyh ambazo zinaonyesha kuwa kuna majina kama al-Hakam na al-Hakiym ambayo Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) hakuyabadilisha. Hadiyth hizo ni Swahiyh zaidi kuliko Hadiyth hii katika mlango huu. Ni dalili inayoonyesha kuwa usahihi wa Hadiyth hii unahitaji kuangaliwa vizuri. Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) aliyakubali majina kama Hakiym bin Hizaam, al-Hakam bin ‘Amr al-Ghifaariy na majina mengineyo. Hakuyabadilisha. Lau ingelikuwa ni dhambi basi angeliyabadilisha. Jina “al-Hakam” kunalengwa yule anayewahukumu watu kwa Shari’ah ya Allaah. Ni jina lisilokuwa na neno. Vivyo hivyo inahusiana na jina “al-Haakim”, “al-Qaadhwiy” na mengineyo.

48. Mlango kuhusu anayekifanyia mzaha kitu kilichotajwa ndani yake jina la Allaah, Qur-aan au Mtume

Shaykh-ul-Islaam Muhammad bin 'Abdil-Wahhaab (Rahimahu Allaah) amesema:

1- Allaah (Ta'ala) amesema:

وَلَيْن سَأَلْتَهُمْ لَيَقُولُنَّ إِنَّمَا كُنَّا نَخُوضُ وَنَلْعَبُ

“Ukiwauliza bila shaka watasema: “Hakika sisi tulikuwa tunaporoja na tunacheza.” (at-Tawbah 09:65)

2- Ibn 'Umar, Muhammad bin Ka'b, Zayd bin Aslam na Qadaatah wamesimulia:

“Wakati wa vita vya Tabuk kuna mtu aliyesema: “Hatujapata kuona watu kama wasomi wetu hawa, matumbo yao yanapenda kula sana, ndimi zao zinasema uongo na ni waoga wakati wa mapambano”. Akimaanisha Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) na Maswahabah wake waliokuwa wasomi. 'Awf bin Maalik akamwambia: “Hakika umesema uongo, lakini wewe ni mnafiki! Nitamweleza Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam).” 'Awf akaenda kwa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) kumweleza ambapo akakuta Qur-aan imekwishamtangulia. Mtu yule akaja kwa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) ambapo akakuta Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) ndio anaanza kuondoka mahali hapo na kishampanda ngamia wake. Yule mtu akasema: “Ee Mtume wa Allaah! Hakika sisi tulikuwa tunafanya mzaha na tukipiga masoga ili muda uweze kwenda.”

Ibn 'Umar amesema:

“Kama kwamba hivi sasa namuona mtu huyo akining’inia kamba za ngamia wa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) na huku mawe yakikwaruza miguu yake na huku akisema: “Hakika tulikuwa tunaporoja na tunacheza.” Ndipo Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) akamwambia:

أَبِاللَّهِ وَآيَاتِهِ وَرَسُولِهِ كُنْتُمْ تَسْتَهْزِؤُونَ

“Je, mlikuwa mkimfanyia mzaha Allaah na Aayah Zake na Mtume wake?”

Hamgeukii na wala hazidishi jengine zaidi ya hayo.”¹⁷⁵

MAELEZO

Mlango huu unazungumzia kwamba wale waislamu ambao wanafanya istihzai na Allaah, Qur-aan na Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) wanaritadi. Mlango unazungumzia kwamba kufanya mzaha ni kuritadi na kufuru, kama inavyopata kufahamika kutoka katika kichwa cha mlango. Ni jambo linalotambulika kutokana na maneno ya Allaah (Ta’ala):

وَلَمَّا سَأَلْتَهُمْ لَيَقُولُنَّ إِنَّمَا كُنَّا نَخُوضُ وَنَلْعَبُ قُلْ أَبِاللَّهِ وَآيَاتِهِ وَرَسُولِهِ كُنْتُمْ تَسْتَهْزِؤُونَ

“Ukiwauliza bila shaka watasema: “Hakika sisi tulikuwa tunaporoja na tunacheza. Sema: “Je, mlikuwa mkimfanyia mzaha Allaah na Aayah Zake na Mtume wake?”

2- Ibn ‘Umar, Muhammad bin Ka’b, Zayd bin Aslam na Qadaatah wamesimulia:

“Wakati wa vita vya Tabuk kuna mtu aliyesema: “Hatujapata kuona watu kama wasomi wetu hawa, matumbo yao yanapenda kula sana, ndimi zao zinasema uongo na ni waoga wakati wa mapambano”. Akimaanisha Mtume wa Allaah

¹⁷⁵ Ibn Jariyr (10/172) na Ibn Abiy Haatim (10047). Nzuri kwa mujibu wa al-Waadi’iy katika “ as-Swahiyyh al-Musnad min Asbab-in-Nuzuul”, uk. 122.

(Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) na Maswahabah wake waliokuwa wasomi. 'Awf bin Maalik akamwambia: "Hakika umesema uongo, lakini wewe ni mnafiki! Nitamweleza Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam)." 'Awf akaenda kwa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) kumweleza ambapo akakuta Qur-aan imekwishamtangulia. Mtu yule akaja kwa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) ambapo akakuta Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) ndio anaanza kuondoka mahali hapo na kishampanda ngamia wake. Yule mtu akasema: "Ee Mtume wa Allaah! Hakika sisi tulikuwa tunafanya mzaha na tukipiga masoga ili muda uweze kwenda."

Mtu yule alisema:

"Matumbo yao yanapenda kula sana... "

Bi maana wanapenda kula sana.

Vilevile amesema:

"... na ni waoga wakati wa mapambano."

Bi maana sio mashujaa.

'Awf bin Maalik amesema:

"Hakika umesema uongo, lakini wewe ni mnafiki!"

Hapa ndani yake kuna kukemea maovu kwa yule aliyeyasikia. Ni wajibu kwa yule aliyeyasikia kuyakaripia na khaswakhaswa ikiwa inahusiana na maovu kama haya makubwa na ya khatari ambapo Allaah, Mtume Wake (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) na dini yake vinatukanwa.

Imekuja katika Hadiyth:

"... ambapo akakuta Qur-aan imekwishamtangulia."

Bi maana akakuta kumekwishateremshwa Aayah juu yao, nazo ni maneno Yake Allaah (Ta'ala):

وَلَيْنَ سَأَلْتَهُمْ لَيَقُولُنَّ إِنَّمَا كُنَّا نَخُوضُ وَنَلْعَبُ قُلْ أَبِاللَّهِ وَآيَاتِهِ وَرَسُولِهِ كُنْتُمْ تَسْتَهْزِؤُونَ

“Ukiwauliza bila shaka watasema: “Hakika sisi tulikuwa tunaporoja na tunacheza. Sema: “Je, mlikuwa mkimfanyia mzaha Allaah na Aayah Zake na Mtume wake?”

Hapa kuna dalili inayoonyesha kwamba yule mwenye kufanya istihzai na Qur-aan, Sunnah au Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) basi ni kafiri. Haijalishi kitu hata kama atasema kuwa anafanya hivo ili muda uweze kwenda haraka safarini na kwamba hakuwa ni mwenye kumaanisha hivo; ni kafiri kwa hali zote. Kwa sababu kufanya mzaha kama huu haufai safarini wala kwenginepo. Mwenendo kama huu unaonyesha unafiki uliyomo moyoni mwake, ubaya na chuki zake dhidi ya waislamu. Muislamu hawezi kusema maneno yaliyosemwa na mtu huyu na khaswa anapowatumu uongo. Huku ni kumkadhibisha Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) na Maswahabah wake. Amewatumu kwamba ni waoga na waroho, jambo ambalo linaonyesha kuipupia kwao dunia. Wakati alipokuja akitoa nyudhuru mbele ya Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) akampuuza. Hakuna jengine alichomwambia isipokuwa:

أَبِاللَّهِ وَآيَاتِهِ وَرَسُولِهِ كُنْتُمْ تَسْتَهْزِؤُونَ

“Je, mlikuwa mkimfanyia mzaha Allaah na Aayah Zake na Mtume wake?”

Ni dalili inayothibitisha kwamba (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) hakumkubalia udhuru wake huu na akambainishia kwamba ni kafiri kwa kitendo hichi. Hapa tunapata kubainikiwa kwamba yule mwenye kufanya mzaha na Shari'ah ni kafiri baada ya kuamini kwake. Kadhalika ikiwa atamponda Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) au akasema kuwa ni mwoga,

mwongo, kwamba hakufikisha ujumbe au mapungufu mengine kama hayo. Vivyo hivyo inahusiana na yule mwenye kusema kwamba Qur-aan ni yenye kujigonga, kwamba Qur-aan au Shari'ah si vyenye kukamilisha yale wanayohitajia watu au mfano wa ukosoaji au upungufu mwingine kama huo. Hata hivyo akisema kuwa Qur-aan imekuja kubainisha baadhi ya mambo ambayo hayakutajwa katika Qur-aan ni kweli. Ama ikiwa anazungumza hivo kwa njia ya kejeli na kwamba watu wanahitajia sheria zilizotungwa na watu na kwamba Qur-aan na Sunnah si venye kutosheleza ni kufuru kubwa na kuritadi. Kadhalika inahusiana na anayesema kwamba Pepo ni mambo ya ndoto tu na sio mambo ya kweli.

49. Mlango kuhusu maneno Yake (Ta'ala) “Tunapomuonjesha rehema kutoka Kwetu baada ya dhara iliyomgusa, bila shaka husema: “Haya nayastahiki mimi na sidhani kama Saa itatokea.”

Shaykh-ul-Islaam Muhammad bin 'Abdil-Wahhaab (Rahimahu Allaah) amesema:

1- Allaah (Ta'ala) amesema:

وَلَئِنْ أَذَقْنَاكَ رَحْمَةً مِّنَّا مِنْ بَعْدِ ضَرَاءٍ مَسَّتَهُ لَيَقُولَنَّ هَذَا لِي وَمَا أَظُنُّ السَّاعَةَ قَائِمَةً

“Tunapomuonjesha rehema kutoka Kwetu baada ya dhara iliyomgusa, bila shaka husema: “Haya nayastahiki mimi na sidhani kama Saa itatokea.” (Fuswswilat 41:50)

Mujaahid amesema:

“Hili ni kutokana na matendo yangu na mimi ndiye mwenye kuiistahiki.”

Ibn 'Abbaas amesema:

“Bi maana kilichokuwa kwangu.”

2-

قَالَ إِنَّمَا أُوتِيْتُهُ عَلَىٰ عِلْمٍ عِنْدِي

“Akasema: “Hakika [ninayomiliki] nimepewa haya kwa sababu ya elimu yangu.” (al-Qaswasw 28:78)

Qataadah amesema:

“Bi maana kutokana na elimu yangu kwa sababu ya uzoefu wa njia mbalimbali za kuchuma.”

Wengine wakasema:

“Ni kutokana na elimu ya Allaah kwa sababu mimi ndiye mwenye kuistahiki.”

Hii ndio maana ya maneno ya Mujaahid:

“Nimeipewa kwa sababu ya utukufu wangu.”

3- Abu Hurayrah (Radhiya Allaahu ‘anh) ameeleza ya kwamba amemsikia Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) akisema:

“Kuna watu watatu katika wana wa israaiyl, mwenye ukoma, kipara na kipofu. Allaah akataka kuwajaribu ambapo akawatumia Malaika. Malaika yule akamwendea yule aliyekuwa na ukoma na akamwambia: “Kitu gani unachokipenda sana?” Akajibu: “Rangi nzuri na ngozi nzuri na niondokwe na haya ambayo watu huniona ni mchafu kwayo.” Malaika yule akampapasa na uchafu wake ukaondoka na pia akapewa rangi nzuri na ngozi nzuri. Akamuuliza tena: “Mali ipi unayopenda sana?” Akajibu: “Ngamia (au ng’ombe, Ishaq ametilia shaka).” Akapewa ngamia kumi. Kisha Akamwambia: “Allaah akubarikie ngamia hawa.” Akamwendea yule wa kipara na kumuuliza: “Ni kitu gani unachokipenda sana?” Akajibu: “Kupata nywele nzuri na yaniondoke haya ambayo watu huniona mchafu kwayo.” Malaika akampapasa ambapo akaondokwa na uchafu wake na akapewa nywele nzuri. Akamuuliza tena: “Mali ipi unayopenda sana?” Akajibu: “Ng’ombe au ngamia.” Akapewa ng’ombe mwenye mimba na kumwambia: “Allaah akubarikie ng’ombe wako hawa.” Akamwendea kipofu na kumuuliza: “Ni kitu gani unachokipenda sana?” Akasema: “Allaah anirudishie macho yangu niweze kuwaona watu.” Akampapasa ambapo Allaah akamrudishia macho yake. Kisha akamuuliza tena: “Ni mali ipi unayopenda sana?” Akajibu: “Kondoo.” Akapewa kondoo wenye

mimba. Baadaye wale wanyama wote watatu wakashika mimba na kuzaana, huyu akawa na zizi la ngamia, huyu akawa na zizi la ng'ombe na huyu akawa na zizi la kondoo." Halafu Malaika yule akamwendea yule wa ukoma akiwa katika hali na umbo lake lilelile la mara ya kwanza na akamwambia: "Mimi ni mtu masikini na nimekatikiwa na nyenzo zangu katika safari yangu. Sina cha kunifikisha leo isipokuwa kwa msaada wa Allaah kisha msaada wako. Ninakuomba kwa Jina la yule Aliyekupa rangi nzuri, ngozi nzuri na mali unipe ngamia mmoja atakayenifikisha katika safari yangu." Akajibu: "Nina majukumu mengi." Malaika yule akamwambia: "Kana kwamba mimi nakujua, kwani wewe hukuwa na ukoma watu wanakuona mchafu tena fakiri kisha Allaah ndio akakupa mali?" Akajibu: "Mimi nimeirithi mali hii kutoka kwa mababu zangu." Malaika yule akasema: "Ikiwa umesema uongo, basi Allaah akurudishe katika hali uliokuwa nayo mwanzo!" Malaika yule akamwendea mtu wa kipara kwa hali yake na umbo lilelile na akamwambia kama alivyomwambia huyu wa kwanza ambapo akamjibu kama alivyomjibu yule wa kwanza. Akamwambia: "Ikiwa umesema uongo, basi Allaah akurudishe katika hali uliokuwa nayo mwanzo!" Akamwendea yule kipofu kwa hali yake na uombo lilelie na kumwambia: "Mimi ni mtu masikini na msafiri; nimekatikiwa na nyenzo zangu katika safari yangu. Sina cha kunifikisha leo isipokuwa kwa msaada wa Allaah kisha msaada wako. Ninakuomba kwa Jina la yule Aliyekurudishia macho yako unipe kondoo mmoja atakayenifikisha katika safari yangu." Akajibu: "Kwanza mimi nilikuwa kipofu ambapo Allaah akanirudishia macho yangu. Chukua unachokitaka na uache unachokitaka. Ninaapa kwa Allaah kwamba sintokuzuia kuchukua chochote unachokichukua kwa ajili ya Allaah." Malaika yule akamwambia: "Baki na mali yako. Hakika mmepewa majaribio na Allaah amekuridhia wewe na amewakasirikia wenzako wawili."¹⁷⁶

MAELEZO

¹⁷⁶ al-Bukhaariy (3464) na Muslim (2964).

Mwandishi ameandika mlango huu ili kuonyesha namna watu wengi wanavyokanusha neema na kutokukubali kwamba wametunukiwa nazo na Allaah (Subhaanahu wa Ta'ala).

1- Allaah (Ta'ala) amesema:

وَلَمَّا أَذَقْنَا رَحْمَةً مِّنَّا مِن بَعْدِ ضَرَاءٍ مَّسَّتْهُ لَيْفُوقَنَّ هَذَا لِي وَمَا أَظُنُّ السَّاعَةَ قَائِمَةً

“Tunapomuonjesha rehema kutoka Kwetu baada ya dhara iliyomgusa, bila shaka husema: “Haya nayastahiki mimi na sidhani kama Saa itatokea.”

Aayah inaonyesha haya ndio maumbile ya mwanadamu isipokuwa wale waliokingwa na Allaah. Anakanusha neema na kutokukubali kuwa zinatoka kwa Muumba wao ('Azza wa Jall). Namna hii ndivyo alivyo mwanadamu anakanusha neema na kusema kwamba inatokamana na matendo yake mwenyewe, bidii zake na kadhalika.

Malengo ya mlango huu ni kumuhimiza mwanadamu juu ya kumshukuru Allaah kwa neema na kuzinasibisha Kwake. Hata kama mwanadamu ndiye katenda lakini hata hivyo ni kutokana na fadhilah za Allaah. Yeye ndiye kamfanyia mimea kukuwa. Yeye ndiye kamfanyia wepesi biashara na kumfanya akaweza kufaidika. Hakuna neno akaelezea sababu zilizopelekea kumfikisha huko, lakini kwanza anatakiwa kubainisha kwamba neema hizo zinatokamana na Allaah na kumshukuru. Lakini kilichokatazwa ni kuziegemeza katika sababu na kumsahau Yule mneemeshaji.

3- Abu Hurayrah (Radhiya Allaahu 'anh) ameeleza ya kwamba amemsikia Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) akisema:

“Kuna watu watatu katika wana wa israaiyl, mwenye ukoma, kipara na kipofu...
“

Katika Hadiyth hii kuna faida kubwa. Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) ametusimulia nacho kutokana na mazingatio yake na ili tusitumbukie katika yale waliyotumbukia wana wa israaiyl.

Watu hawa watatu Allaah aliwajaribu kwanza kwa kuwapa madhara ya wakati mgumu kisha kwa kuwapa wakati wa raha. Wale wawili wakazikufuru neema za Allaah na yule mmoja akazishukuru. Haya yanatilia nguvu maneno Yake Allaah:

وَقَلِيلٌ مِّنْ عِبَادِيَ الشَّاكِرُونَ

“Wachache miongoni mwa waja Wangu wenye kushukuru.” (Saba' 34:13)

50. Mlango kuhusu maneno Yake (Ta'ala) “Lakini anapowapa [mtoto mzima na] mwema [waliyemuomba], wanamfanyia washirika katika kile alichowapa! Ametukuka Allaah kutokana na yale yote wanayoshirikisha!”

Shaykh-ul-Islaam Muhammad bin 'Abdil-Wahhaab (Rahimahu Allaah) amesema:

1- Allaah (Ta'ala) amesema:

فَلَمَّا آتَاهُمَا صَالِحًا جَعَلَا لَهُ شُرَكَاءَ فِيمَا آتَاهُمَا فَتَعَالَى اللَّهُ عَمَّا يُشْرِكُونَ

“Lakini anapowapa [mtoto mzima na] mwema [waliyemuomba], wanamfanyia washirika katika kile alichowapa! Ametukuka Allaah kutokana na yale yote wanayoshirikisha!” (al-A'raaf 07:190)

Ibn Hazm amesema:

“Wamekubaliana juu ya kuharamisha kila jina ambalo yule mwenye kuitwa hivyo ni mja wa mwingine badala ya Allaah. Kama mfano wa “'Abd-'Umar” na “'Abd al-Ka'bah”. “'Abdul-Muttwalib” limevuliwa katika hayo.”

2- Ibn 'Abbaas (Radhiya Allaahu 'anhumaa) amesema kuhusiana na Aayah hapo juu:

“Adam alipomwendea mkewe alishika ujauzito. Ndipo Ibliys akawajia na kuwaambia: “Mimi ndiye yule niliyesababisha mkatolewa Peponi. Ima nitiini au vinginevyo nitamfanya mtoto wenu aote pembe mbili kama swala tumboni mwa

mama yake ambazo zitapasua tumbo lake wakati wa kumzaa na ntafanya hivyo ntafanya hivyo.” Alisema hivo kwa ajili ya kuwatia khofu na akawaambia: “Mwiteni “‘Abdul-Haarith”.” Wakakataa kumtii na mtoto akazaliwa hali ya kuwa ameshakufa. Kisha akabeba ujauzito mwingine ambapo akawajia kwa mara nyingine na akawaambia kama alivyowaambia mara ya kwanza ambapo akawakuta ni wenye kumpenda mtoto huyo kwelikweli na wakamwita jina la “‘Abdul-Haarith”. Hiyo ndio tafsiri ya maneno Yake (Ta’ala):

فَلَمَّا آتَاهُمَا صَالِحًا جَعَلَا لَهُ شُرَكَاءَ فِيمَا آتَاهُمَا فَتَعَالَى اللَّهُ عَمَّا يُشْرِكُونَ

“Lakini anapowapa [mtoto mzima na] mwema [waliyemuomba], wanamfanyia washirika katika kile alichowapa! Ametukuka Allaah kutokana na yale yote wanayoshirikisha!”¹⁷⁷

Ameipokea Ibn Abiy Haatim.

3- Naye (Ibn Haatim) ameipokea kwa cheni ya wapokezi Swahiyh kutoka kwa Qataadah aliyesema:

“Washirika inahusiana na kumshirikisha Allaah katika utiifu na si katika kumwabudu.”

4- Naye (Ibn Haatim) amepokea kwa cheni ya wapokezi Swahiyh kutoka kwa Mujaahid aliyesema kuhusiana na maneno Yake:

لَعْنَةُ آتَيْنَا صَالِحًا لَنَكُونَنَّ مِنَ الشَّاكِرِينَ

“Ukitupa [mtoto mzima na] mwema basi kwa hakika tutakuwa katika wenye kushukuru.” (al-A’raaf 07:189)

Akasema:

¹⁷⁷ Ahmad (20129) na at-Tirmidhiy (3077). Dhaifu kwa mujibu wa al-Albaaniy katika “Dhwa’iyf-ul-Jaami” (4769).

“Walichelea mtoto asijekuwa si mtu.”

Maana kama hiyo imethibiti pia kwa al-Hasan, Sa'iyd na wengineo.

MAELEZO

Alichokusudia mwandishi kwa kichwa cha khabari hichi ni kwamba majina yenye kuashiria mtu ni mja wa mwingine asiyekuwa Allaah ni haramu. Kwa mfano haijuzu kwa mtu akaitwa 'Abdun-Nabiy, 'Abdul-Ka'bah au 'Abdul-Husayn. Majina yanayojuzu ni yale yenye kuashiria kuwa mtu ni mja wa Allaah pekee kama mfano wa 'Abdur-Rahmaan na 'Abdullaah. Kwa sababu Allaah amemsema vibaya yule mwenye kufanya hivo na akasema:

فَلَمَّا آتَاهُمَا صَالِحًا جَعَلَا لَهُ شُرَكَاءَ فِيمَا آتَاهُمَا فَتَعَالَى اللَّهُ عَمَّا يُشْرِكُونَ

“Lakini anapowapa [mtoto mzima na] mwema [waliyemuomba], wanamfanyia washirika katika kile alichowapa! Ametukuka Allaah kutokana na yale yote wanayoshirikisha!”

Hapa anasemwa vibaya na anakejeliwa yule mwenye kuitwa hivo. Mtiririko wa Aayah unamzungumzia Adam na Hawwaa' ambao walimtii shaytwaan na wakamwita mtoto wao jina la “'Abdul-Haarith”. Wako wengine waliosema kwamba Aayah inawazungumzia kundi la wana wa israaiyl. Lakini hata hivyo mtiririko wa Aayah unayakataa hayo. Bali ukweli wa mambo ni kama alivosema Ibn 'Abbaas na wengine katika Salaf. Wakatumbukia katika maasi. Mitume wanaweza kutumbukia katika maasi madogo, ndivo wasemavyo wanachuoni. Inawezekana vilevile kwamba pindi walipofanya hivo walikuwa wakidhani kuwa ni kitendo kinachofaa. Hawakujua kuwa ni kitendo cha madhambi. Kwanza walilichukia jambo hilo kisha baadaye wakategwa na wasiwasiwa wake. Miongoni mwa yale Allaah aliyomteremshia Mtume Wake akambainishia (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) kwamba kitendo hicho hakijuzu. Hukumu ni yenye kufungamana na Shari'ah ya Muhammad (Swalla Allaahu 'alayhi wa

sallam) iliyoenea. Shari'ah zilizotangulia ziko na mambo ambayo yanafaa na ziko na mambo yasiyofaa.

Ibn Hazm amesema:

“Wamekubaliana juu ya kuharamisha kila jina ambalo yule mwenye kuitwa hivyo ni mja wa mwingine badala ya Allaah. Kama mfano wa “‘Abd-‘Umar” na “‘Abd al-Ka‘bah”. “‘Abdul-Muttwalib” limevuliwa katika hayo.”

Sababu ya kuvuliwa jina hili ni kwa kuwa Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) alilikubali na hakulibadilisha. Yupo Swahabah mwingine akiitwa ‘Abdul-Muttwalib bin Rabiyy‘ah. Hili ni kwa sababu msingi wa jina hilo ni utumwa kwa mwanadamu. Walikuwa wakimwita Shaybah bin Hishaam “‘Abdul-Muttwalib” kwa kuwa wakidhani kuwa ni mtumwa wa al-Muttwalib pindi wanapoona uso wake unapiga weusi baada ya safari. Ukweli wa mambo ni kwamba al-Muttwalib alikuwa ami yake. Jina hilo linakubalika katika Uislamu kinyume na majina mengine yote mfano wake.

3- Naye (Ibn Haatim) ameipokea kwa cheni ya wapokezi Swahiyh kutoka kwa Qataadah aliyesema:

“Washirika inahusiana na kumshirikisha Allaah katika utiifu na si katika kumwabudu.”

Kwa sababu walimtii juu ya jina hili pasi na wao kujua. Yote haya ni kwa minajili ya kuikamilisha Tawhiyd na kunyenyekea mbele ya Allaah na kufunga njia zote zinazopelekea katika shirki.

Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) amesema:

“Mimi ni mwana wa ‘Abdul-Muttwalib.”

Huku ni kuelezea jina lililotangulia. Ni jambo halidhuru kwa sababu alikuwa akitambulika kwa jina hilo. Kadhalika inahusiana na majina kama “‘Abdu Manaaf” na “‘Abdu ‘Amr” ikiwa yatatajwa kwa njia ya kuelezea.

51. Mlango kuhusu maneno Yake (Ta'ala) “Allaah ana majina mazuri mno; hivyo basi muombeni kwayo”

Shaykh-ul-Islaam Muhammad bin 'Abdil-Wahhaab (Rahimahu Allaah) amesema:

1- Allaah (Ta'ala) amesema:

وَلِلّٰهِ الْأَسْمَاءُ الْحُسْنَىٰ فَادْعُوهُ بِهَا وَذَرُوا الَّذِينَ يُلْحِدُونَ فِي أَسْمَائِهِ سَيُجْزَوْنَ مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ

“Allaah ana majina mazuri mno; hivyo basi muombeni kwayo na waacheni wale wanaopotoa katika majina Yake. Watalipwa yale waliokuwa wakifanya.” (al-A'raaf 07:180)

Ibn Abiy Haatim amepokea kwamba Ibn 'Abbaas (Radhiya Allaahu 'anhumaa) amesema kuhusu:

وَذَرُوا الَّذِينَ يُلْحِدُونَ فِي أَسْمَائِهِ

“... na waacheni wale wanaopotoa katika majina Yake.”

“Wanashirikisha.”

Amesema vilevile:

“Wametoa jina la al-Laah kutoka katika al-Ilaah na al-'Uzzaa kutoka katika al-'Aziyz.”

2- al-A'mash amesema:

“Wameingiza ndani yake yasiyokuwemo.”

MAELEZO

1- Allaah (Ta'ala) amesema:

وَلِلَّهِ الْأَسْمَاءُ الْحُسْنَىٰ فَادْعُوهُ بِهَا وَذَرُوا الَّذِينَ يُلْحِدُونَ فِي أَسْمَائِهِ سَيُجْزَوْنَ مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ

“Allaah ana majina mazuri mno; basi muombeni kwayo na waacheni wale wanaopotoa katika majina Yake. Watalipwa yale waliokuwa wakifanya.”

Allaah (Ta'ala) amebainisha kwamba ana majina mazuri mno ambayo hayawezi kuingiwa na upungufu wowote. Yote ni majina kamilifu na ni yenye kujulisha maana tukufu. Allaah anasifika nayo kwa njia inayolingana Naye. Anatakiwa kuombwa kwayo kwa mfano kwa kusema “Ewe Mwingi wa huruma, ewe Mwenye nguvu kabisa, ewe Mwenye kughufuria, nisamehe” na kadhalika.

Kuyapotoa majina Yake maana yake ni kupondoka kutoka katika haki na kumshirikisha na kuyatumia kwa mwingine asiyekuwa Allaah. Kama ambavyo mtu anamwabudu mwingine asiyekuwa Allaah na hivyo akawa kafiri kwa ajili ya hilo. Kadhalika inahusiana na yule mwenye kuyapotoa majina Yake kwa kupondoka kutoka katika haki na akasema kuwa hayana maana. Kama walivofanya Jahmiyyah, ambao wamekanusha sifa na majina ya Allaah, na Mu'tazilah, ambao wamekanusha sifa Zake. Wameyapotoa majina na sifa Zake na kwa kukengeuka kutoka katika haki.

Kuna aina mbili za kuyapotoa:

Upotoshaji mkubwa: Ni jambo linawatumbukiza katika kufuru.

Upotoshaji mdogo: Ni jambo wanatumbukia ndani yake baadhi ya waislamu pale wanapokosa kujisalimisha katika haki kikamilifu. Kwa njia hiyo wanakuwa ni wenye kukosa Uislamu na imani kamilifu kwa kiasi cha upotoaji wao na kupondoka kwao kutokamana na haki.

2- al-A'mash amesema:

“Wameingiza ndani yake yasiyokuwemo.”

Hii ni aina fulani ya upotoaji, nako ni kule kumwita Allaah kwa majina ambayo hakuyateremshia dalili yoyote. Hii ni aina fulani ya upotoaji na batili.

Upotoaji mwingine ni kusema al-Laah kutoka katika al-Ilaah na al-'Uzzaa kutoka katika al-'Aziyz.

Kadhalika kuingia katika maasi ni aina fulani ya upotoaji mdogo. Mwenye kumkanusha Allaah au akamshirikisha Allaah na mwingine ametumbukia katika upotoaji mkubwa.

52. Hakusemwi “as-Salaam iwe juu ya Allaah”

Shaykh-ul-Islaam Muhammad bin 'Abdil-Wahhaab (Rahimahu Allaah) amesema:

1- Imesihi kupokelewa kutoka kwa Ibn Mas'uud (Radhiya Allaahu 'anh) ambaye amesema:

“Tulikuwa tunapokuwa pamoja na Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) katika swalah tunasema: “as-Salaam iwe juu ya Allaah kutoka kwa waja Wake. as-Salaam iwe juu ya fulani na fulani.” Ndipo Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) akasema: “Msisemi “as-Salaam iwe juu ya Allaah”. Kwani Allaah Yeye ndiye as-Salaam.”¹⁷⁸

MAELEZO

1- Imesihi kupokelewa kutoka kwa Ibn Mas'uud (Radhiya Allaahu 'anh) ambaye amesema:

“Tulikuwa tunapokuwa pamoja na Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) katika swalah tunasema: “as-Salaam iwe juu ya Allaah kutoka kwa waja Wake. as-Salaam iwe juu ya fulani na fulani.” Ndipo Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) akasema: “Msisemi “as-Salaam iwe juu ya Allaah”. Kwani Allaah Yeye ndiye as-Salaam.”

as-Salaam inaweza kuwa na maana mbili:

1- Amesalimika kutokamana na kila aina ya upungufu na aibu. Yeye ana ukamilifu usiokuwa na kikomo kwa njia zote katika dhati Yake, majina Yake, sifa Zake na matendo Yake.

¹⁷⁸ al-Bukhaariy (835) na Muslim (402).

2- Anawapa amani waja Wake. Kwa hivyo haitakiwi kusema “as-Salaam iwe juu ya Allaah”. Kwani hii ni du’aa na Allaah ni mkwasi asiyehitajia kitu. Hana haja ya maombi ya watu. Kilichowekwa katika Shari’ah ni kumuadhimisha na kumtakasa na kuamini kwamba ni Mwenye kusifiwa kwa sifa kamilifu na kwamba Yeye ni Mwenye kufanya vizuri na Mwenye kudhuru.

Hata hivyo ni sawa kusema “as-Salaam juu ya baadhi ya viumbe” kwa sababu ni wenye kuhitajia afya na du’aa.

Kusema kwamba lau kama si Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) basi tusingeongoka hakuna neno iwapo mtu anakusudia ulinganizi wake (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam). Vinginevyo bora zaidi ni kusema “lau kama si Allaah kisha ulinganizi wa Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) basi tusingeongoka”.

53. Mlango kuhusu msemu “Ee Allaah! Nisamehe Ukitaka”

Shaykh-ul-Islaam Muhammad bin 'Abdil-Wahhaab (Rahimahu Allaah) amesema:

1- Imesihi kupokelewa kutoka kwa Abu Hurayrah (Radhiya Allaahu 'anh) ya kwamba Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Asiseme mmoja wenu: “Ee Allaah! Nisamehe Ukitaka! Ee Allaah! Nirehemu Ukitaka!” Akate azimio la maombi. Kwani Allaah hakuna amtenzaye nguvu.”¹⁷⁹

2- Kwa Muslim imekuja kwa tamko lisemalo:

“Anatakiwa aifanye kubwa shauku yake. Kwani Allaah hakioni kikubwa kwa kile alichokitoa.”

MAELEZO

Mwandishi anachotaka hapa ni kubainisha kwamba katika ukamilifu wa Tawhiyd na imani ni kuomba kwa kukata na kutokuwa na mashaka. Pindi muumini anapomuomba Mola wake basi anaomba kwa kukata pasi na kuwa na mashaka. Kwani ukarimu wa Allaah ni mkubwa. Yeye ndiye Tajiri, Mwenye kuhimidiwa. Si sawa kwa muumini kuomba kwa kuvua. Kiumbe ndiye aombwaye kwa kubagua kwa sababu ima akawa si muweza au akawa si mwenye kutaka. Kuhusu Mola ni Tajiri na Muweza.

1- Imesihi kupokelewa kutoka kwa Abu Hurayrah (Radhiya Allaahu 'anh) ya kwamba Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

¹⁷⁹ al-Bukhaariy (6339) na Muslim (2679).

“Asiseme mmoja wenu: “Ee Allaah! Nisamehe Ukitaka! Ee Allaah! Nirehemu Ukitaka!” Akate azimio la maombi. Kwani Allaah hakuna amtenzaye nguvu.”

Haisilihi kwa mja kuomba kwa kubagua. Kwa sababu kuomba kwa kuvua ni kama kwamba si mwenye dhiki wala mwenye kuhitajia maombi haya. Kwa hivyo ni wajibu awe mwenye kukata. Kwani hakika Allaah hakuna awezaye kumtenza nguvu wala hakuna kimshindacho.

2- Kwa Muslim imekuja kwa tamko lisemalo:

“Anatakiwa aifanye kubwa shauku yake. Kwani Allaah hakioni kikubwa kwa kile alichokitoa.”

Allaah (Ta’ala) ni Mtukufu, Tajiri, Mwenye kuhimidiwa. Kila anachowapa waja Wake ni kidogo na ni chepesi Kwake japokuwa (Subhaanahu wa Ta’ala) atakuwa ni Mwenye kuwapa kitu kikubwa.

Muumini anapaswa awe ni mwenye shauku kubwa kwa vile vilivyoko kwa Allaah. Anatakiwa aufungamanishe moyo wake kwelikweli kwa Allaah, awe ni mwenye kurejea kwa Allaah kikwelikweli na asiwe ni mwenye kuvunjika moyo. Pindi anapomuomba basi amuombe hali ya kuwa ni mwenye shauku kubwa, muhitaji na asivue kitu. Kadhalika anapowaombea ndugu zake asiseme “Allaah akusamehe akitaka, Allaah akurehemu akitaka.” Bali anatakiwa awe ni mwenye kukata na asiseme “Allaah akitaka” hata kama anafanya hivo kwa ajili ya baraka. Asifanye kubagua. Wala hatakiwi vilevile kusema: “Ee Allaah! Nisamehe kwa kile unachokitaka.”

Faida:

Pete ya ndoa haina msingi wowote na ni miongoni mwa matendo ya manaswara.

Hadiyth zote zilizopokelewa kuhusu watu wa Pangoni ni dhaifu. Lakini kuna uwezekano zikawa zinapeana nguvu. Hata hivyo kuna matamshi yaliyosihi

kutoka kwa Maswahabah, jambo ambalo linaweza kuzitia nguvu Hadiyth kutoka kwa Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam).

Haijuzu kusema: "Ee Mtume wa Allaah! Lau ungeliona hali ya Ummah wako basi ungelihuzunikia na kuumbea... " Kwa sababu yeye (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) hasikii wala haoni. Kama ilivyokuja katika Hadiyth:

"Hakika wewe hujui waliyozusha baada yako."¹⁸⁰

¹⁸⁰ al-Bukhaariy (4625) na Muslim (247).

54. Mlango wa kutosema “Mja wangu, kijakazi wangu”

Shaykh-ul-Islaam Muhammad bin 'Abdil-Wahhaab (Rahimahu Allaah) amesema:

1- Imesihi kupokelewa kutoka kwa Abu Hurayrah (Radhiya Allaahu 'anh) ya kwamba Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Asiseme mmoja wenu: “Mlishe mola wako, mpe maji mola wako.” Bali badala yake aseme: “Bwana wangu, mlinzi/bosi wangu.” Wala asiseme mmoja wenu: “Mja wangu, mjakazi wangu.” Badala yake aseme: “Kijana changu, msichana wangu na mvulana wangu.”¹⁸¹

MAELEZO

Mlango huu unabainisha baadhi ya mambo yanayopingana na ukamilifu wa Tawhiyd. Wakati mtu anapomzungumzisha mvulana wake au mfanyakazi wake wa kike asiseme: “Mja wangu, kijakazi changu.” Huku ni kwa ajili ya kufanya adabu na Allaah (Ta'ala). Bali anatakiwa kusema kwa mfano: “Kijana changu, msichana wangu, mvulana wangu, mfanyakazi wangu”. Kwa sababu waja wote ni waja wa Allaah, wajakazi wote ni wajakazi wa Allaah. Haya ni kwa minajili ya ukamilifu wa Tawhiyd na kufanya adabu na Allaah ('Azza wa Jall) pamoja vilevile na kumtambua Allaah (Subhaanah) kwamba Yeye ndiye mfalme wa kila kitu na ndiye Mwenye kukiendesha kila kitu.

Hata hivyo mtu akisema mtumwa wa fulani au mjakazi wa fulani kwa njia ya kuelezea, ni jambo jepesi kidogo na si kwamba anajiegemezea kwake mwenyewe.

¹⁸¹ al-Bukhaariy (2552) na Muslim (2249).

1- Imesihi kupokelewa kutoka kwa Abu Hurayrah (Radhiya Allaahu 'anh) ya kwamba Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Asiseme mmoja wenu: “Mlishe mola wako, mpe maji mola wako.” Bali badala yake aseme: “Bwana wangu, mlinzi/bosi wangu.” Wala asiseme mmoja wenu: “Mja wangu, mjakazi wangu.” Badala yake aseme: “Kijana changu, msichana wangu na mvulana wangu.”

Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Asiseme mmoja wenu: “Mlishe mola wako, mpe maji mola wako.”

Haya ni kwa minajili ya kufanya adabu. Kwani Mola wa wote ni Allaah. Allaah (Ta'ala) halishwi. Yeye hamuhitajii yeyote. Haitakikani kusema hivo kwa njia ya moja kwa moja. Maneno yake Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam):

“Bwana wangu, mlinzi/bosi wangu.”

Msemo mwingine ni 'ami'. Kwa sababu msemo huu ni wenye kutambulika na haupingani na uola wa Allaah. Bwana ni yule mmiliki na raisi. Yeye ndiye mmiliki wa kijana huyu. Vilevile bosu au mlinzi ni neno lenye maana nyingi ikiwa ni pamoja na mmiliki, mtu aliye karibu na msaidizi.

Imekuja katika upokezi mwingine:

“Asiseme mmoja: “Mlinzi/bosi wangu.” Kwa sababu Mlinzi ni Allaah.”

Lakini kilichohifadhiwa kwa wanachuoni ni ule upokezi unaoruhusu kusema hivo. Neno 'mlinzi' wengine pia wanaweza kuitwa hivo. Allaah (Ta'ala) amesema:

ذَلِكَ بِأَنَّ اللَّهَ مَوْلَى الَّذِينَ آمَنُوا وَأَنَّ الْكَافِرِينَ لَا مَوْلَى لَهُمْ

“Hivyo ni kwa kuwa Allaah ndiye Mlinzi wa wale walioamini na kwamba makafiri hawana mlinzi.” **(Muhammad 47:11)**

Bi maana hawana mwenye kuwanusuru. Ni wenye kukoseshwa nusura inapokuja katika mlinzi juu ya hesabu ya Allaah. Kwa hiyo hakuna neno kutumia msemu wa 'bwana` na 'mlinzi/bosi`. Hii leo imekuwa ni jambo la kawaida watu kutumia msemu wa 'ami` na mfano wake badala ya 'mola`.

55. Mwenye kuomba kitu kwa jina la Allaah asirudishwe nyuma

Shaykh-ul-Islaam Muhammad bin 'Abdil-Wahhaab (Rahimahu Allaah) amesema:

1- Ibn 'Umar (Radhiya Allaahu 'anhumaa) amesimulia kwamba Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Mwenye kuomba kwa jina la Allaah mpeni, mwenye kujilinda kwa jina la Allaah mlindeni, mwenye kukuiteni muitikieni na anayekufanyieni wema mlipeni wema. Msipopata cha kumlipa muombeeni du'aa mpaka muone kweli kwamba mmemlipa wema.”¹⁸²

Ameipokea Abu Daawuud na an-Nasaa'iy kwa cheni ya wapokezi Swahiyh.

MAELEZO

Mwandishi ametaja mlango huu kwa sababu ndani yake kuna kumuadhimisha na kumtukua Allaah kwa kule kumpa yule mwenye kuomba kwa jina la Allaah. Hadiyth ya Ibn 'Umar ni mfano wa maneno ya Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) ambayo ni machache lakini yaliyobeba maana kubwa.

1- Ibn 'Umar (Radhiya Allaahu 'anhumaa) amesimulia kwamba Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Mwenye kuomba kwa jina la Allaah mpeni, mwenye kujilinda kwa jina la Allaah mlindeni, mwenye kukuiteni muitikieni na anayekufanyieni wema mlipeni wema. Msipopata cha kumlipa muombeeni du'aa mpaka muone kweli kwamba mmemlipa wema.”

¹⁸² Abu Daawuud (1672), an-Nasaa'iy (2567), Ahmad (5365), al-Bukhaariy katika "al-Adab al-Mufrad" (216) na at-Twabaraaniy katika "al-Mu'jam al-Kabiy" (13465). Swahiyh kwa mujibu wa al-Albaaniy katika "Swahiyh Sunan Abiy Daawuud" (1468).

Maneno ya Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam):

“Mwenye kuomba kwa jina la Allaah mpeni... “

Haya ni kwa ajili ya kumuadhimisha na kumtukuza Allaah. Hata hivyo kumekuja Hadiyth nyingi zinazoonyesha kuwa imechukizwa kuomba kwa jina la Allah kwa sababu ni kuwatia watu katika uzito. Lakini hata hivyo ni wajibu kumpa yule mwenye kuomba haki yake kama mfano wa zakaah au akaomba kutoka katika mfuko wa mali ya waislamu. Mbali na hayo bora ni kumpa. Pamoja na hivyo haitakikani kwake kuomba kwa jina la Allaah kwa sababu ya kutendea kazi zile Hadiyth zinazoonyesha kuwa kitendo hicho kimechukizwa.

Maneno ya Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam):

“Mwenye kujilinda kwa jina la Allaah mlinden... “

Mwenye kuomba ulinzi kwa jina la Allaah basi ni jambo limewekwa katika Shari'ah kumlinda. Kwa ajili hii wakati 'Amrah bint al-Juun alipomwomba Allaah ulinzi dhidi ya Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) akasema:

“Hakika umeomba ulinzi kwa aliye Mtukufu. Rudi kwa familia yako.”¹⁸³

Kama tulivosema ni jambo limewekwa katika Shari'ah kumlinda yule mwenye kuomba ulinzi kwa jina la Allaah midhali yuko katika haki. Ama akiomba ulinzi kwa jina la Allaah kwa ajili ya kukwepa haki yenye kumuwajibikia kama vile kuswali, kutoa zakaah, madeni au kafara mbalimbali, basi hatakiwi kulindwa na kusalimishwa.

Akiomba ulinzi kwa jina la Allaah kutohitajia kufanya kazi kama hakimu, kiongozi au kitu kingine miongoni mwa kazi ambazo ni khatari na wakati huohuo wakawepo wastahiki wengine wanaoweza kusimamia kazi hizo, basi imewekwa katika Shari'ah kumlinda na kumsalimisha. Kama ilivyopokelewa

¹⁸³ al-Bukhaariy (5254).

kwamba wakati 'Uthmaan alipomwamrisha Ibn 'Umar (Radhiya Allaahu 'anhum) kufanya kazi kama hakimu aliomba kinga kwa jina la Allaah kusimamia jambo hilo ambapo 'Uthmaan akamlinda. Haya ikiwa yamesihi basi ni pale ambapo wapo wengine wastahiki ambao wanaweza kusimamia kazi hizo. Wakati wa 'Uthmaan walikuwepo wengi ambao wanaweza kusimamia kazi hizo.

Maneno ya Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam):

“... mwenye kukuiteni muitikieni.”

Kuitikia mwaliko ni jambo ambalo ndani yake kuna manufaa, kuunga udugu, urafiki na ukaribu. Kwa ajili hiyo ndio maana imewekwa katika Shari'ah kuitikia mwaliko ni mamoja ni mwaliko wa harusi au mwaliko mwingine. Hata hivyo mwaliko muhimu zaidi ni ule wa harusi. Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Asiyeitikia mwaliko basi amemuasi Allaah na Mtume Wake.”¹⁸⁴

Ni wajibu kuitikia mwaliko isipokuwa kama kutakuwepo vipingamizi katika hali mbili:

- 1- Kukawepo kikwazo kama vile maradhi, ni mbali na kuna uzito kwake.
- 2- Kukawepo kikwazo kama mfano wa muziki, nyimbo na pombe.

Ama ikiwa mwaliko umesalimika basi ni wajibu au angalau tunaweza kusema kwamba imekokotezwa sana kuitikia. Hata hivyo haiwajibiki kuitikia mwaliko isipokuwa pale ambap mtu mwenyewe ataupokea.

Maneno ya Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam):

“Anayekufanyieni wema mlipeni wema. Msipopata cha kumlipa muombeeni du'aa mpaka muone kweli kwamba mmemlipa wema.”

¹⁸⁴ al-Bukhaariy (5177) na Muslim (1432).

Kumlipa mtu wema aliyokufanyia ni miongoni mwa tabia nzuri na ni miongoni mwa ukamilifu wa imani. Ikiwa mtu anaweza kulipa wema kwa pesa, afanye hivo. Kama haliwezi hilo basi afanye hivo kwa maneno mazuri na du'aa.

Haifai kuziomba sifa za Allaah kitu chochote kama mfano kuomba kwa uso Wake au ujuzi Wake. Hata hivyo inafaa kumuomba Allaah kwa majina na sifa Zake kama vile Mwingi wa huruma. Inafaa kufanya Tawassul kwa sifa za Allaah na sio kuziomba. Shaykh-ul-Islam amenukuu maafikiano juu ya hilo. Mtu anaweza kuzitumia sifa Zake wakati wa kufanya maombi kwa mfano akasema:

“Nakuomba kwa msamaha Wako na huruma Yako na nakuomba ulinzi kwa radhi Zako kutokamana na hasira Zako.”

56. Hakuombwi kwa Uso wa Allaah isipokuwa Pepo tu

Shaykh-ul-Islaam Muhammad bin 'Abdil-Wahhaab (Rahimahu Allaah) amesema:

1- Jaabir (Radhiya Allaahu 'anh) amesimulia kwamba Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Hakuna kinachombwa kwa uso wa Allaah isipokuwa Pepo.”¹⁸⁵

Ameipokea Abu Daawuud.

MAELEZO

1- Jaabir (Radhiya Allaahu 'anh) amesimulia kwamba Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Hakuna kinachombwa kwa uso wa Allaah isipokuwa Pepo.”

Haya kwa sababu Pepo ndio malengo makubwa. Ndani yake utaonekana uso wa Allaah (Subhaanah) na ndani yake kuna neema zisizokatika. Uso wa Allaah ni wenye utukufu mkubwa. Kwa hivyo haifai kuomba kwa uso wa Allaah isipokuwa Pepo.

Vivyo hivyo inahusiana na yale yote yanayopelekea katika Pepo kama vile Ikhlaasw, kuafikishwa juu ya kheri na kunyooka juu ya utiifu. Kila ambacho kinapelekea katika Pepo kinaingia katika kuomba Pepo.

Haya ni miongoni mwa ukamilifu wa Tawhiyd na imani mtu kutoomba kwa uso wa Allaah isipokuwa Pepo na yale yote yanayopelekea katika Pepo kama vile

¹⁸⁵ Abu Daawuud (368). Dhaifu kwa mujibu wa al-Albaaniy katika "Dhwa'iyf Sunan Abiy Daawuud" (368).

matendo mema, kunyooka na kusalimika kutokamana na upotevu na mitihani mbalimbali.

Katika cheni ya wapokezi kuna udhaifu, lakini unatiwa nguvu na mapokezi mengine yanayokataza kuomba kwa uso wa Allaah. Kwa njia hiyo Hadiyth hii inakuwa maalum na inajuzisha kuomba kwa uso wa Allaah mtukufu na yale yote yanayopelekea katika Pepo.

57. Mlango kuhusu 'lau`

Shaykh-ul-Islaam Muhammad bin 'Abdil-Wahhaab (Rahimahu Allaah) amesema:

1- Allaah (Ta'ala) amesema:

يَقُولُونَ لَوْ كَانَ لَنَا مِنَ الْأَمْرِ شَيْءٌ مَّا قُتِلْنَا هَاهُنَا

Wanasema: "Lau tungelikuwa tuna amri yoyote katika jambo basi tusingeliuliwa hapa." (Aal 'Imraan 03:154)

2-

الَّذِينَ قَالُوا لِإِخْوَانِهِمْ وَقَعَدُوا لَوْ أَطَاعُونَا مَا قُتِلُوا

"Wale ambao waliwaambia ndugu zao nao wakakaa [hawakwenda vitani]: "Lau wangelitutii basi wasingeliuawa." (Aal 'Imraan 03:168)

3- Imesihi kupokelewa kutoka kwa Abu Hurayrah (Radhiya Allaahu 'anh) ya kwamba Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

"Pupia juu ya yale yanayokunufaisha na mtake msaada Allaah na wala usivunjike moyo. Utapofikwa na jambo usiseme 'Lau ningelifanya hivi basi ingelikuwa kadhaa na kadhaa'. Lakini badala yake sema:

قَدَرَ اللَّهُ وَ مَا شَاءَ فَعَلَ

"Hivi ndivyo alivyokadiria Allaah na hufanya atakavyo."

Kwani hakika ya 'lau` hufungua matendo ya shaytwaan."¹⁸⁶

¹⁸⁶ Muslim (2664).

MAELEZO

Mlango huu unazungumzia kuhusu neno 'lau` na kama linafaa au halifai. Kinachokusudiwa ni kwamba haitakikani kulitumia kwa sababu linapingana na Qadar. Ni wajibu kujisalimisha na kusubiri. Pindi ndugu anapofariki, anapokuwa mgonjwa au anapopatwa na msiba basi haitakikani kupingana na kusema 'lau`.

1- Allaah (Ta'ala) amesema:

يَقُولُونَ لَوْ كَانَ لَنَا مِنَ الْأَمْرِ شَيْءٌ مَّا قُتِلْنَا هَاهُنَا

Wanasema: "Lau tungelikuwa tuna amri yoyote katika jambo basi tusingeliuliwa hapa."

Hapa wanasemwa vibaya na kukosolewa.

2-

الَّذِينَ قَالُوا لِإِخْوَانِهِمْ وَقَعَدُوا لَوْ أَطَاعُونَا مَا قُتِلُوا

"Wale ambao waliwaambia ndugu zao nao wakakaa [hawakwenda vitani]: "Lau wangelitutii basi wasingeliuawa."

Ni dalili inayoonyesha kuwa haijuzu kutumia neno hilo kwa ajili ya kupingana na Qadar wakati wa ugonjwa, maangamivu na mfano wake. Hivi ndivo walivyo wanafiki. Makadirio na mipango ya Allaah ni jambo ambalo halina budi kutokea. Ameweka katika Shari'ah kufanya sababu kwa sababu ya hekima kubwa. Ni wajibu kwa muislamu kufanya yale anayotakiwa kufanya na pindi Qadar itatokea basi haimpasi yeye kupingana na makadirio hayo.

3- Imesihi kupokelewa kutoka kwa Abu Hurayrah (Radhiya Allaahu 'anh) ya kwamba Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Pupia juu ya yale yanayokunufaisha na mtake msaada Allaah na wala usivunjike moyo. Utapofikwa na jambo usiseme ‘Lau ningelifanya hivi basi ingelikuwa kadhaa na kadhaa’. Lakini badala yake sema:

قَدَّرَ اللهُ وَ مَا شَاءَ فَعَلَ

“Hivi ndivyo alivyokadiria Allaah na hufanya atakavyo.”

Kwani hakika ya ‘lau` hufungua matendo ya shaytwaan.”

Kuna baadhi wameiandika namna hii:

قَدَّرَ اللهُ وَ مَا شَاءَ فَعَلَ

“Hivi ndivyo alivyokadiria Allaah na hufanya atakavyo.”

Hata hivyo hiyo ya kwanza ndio sahihi zaidi na maana yake ni kwamba haya kweli ni makadirio ya Allaah. Makadirio ya Allaah na hufanya atakavyo.

Maneno yake Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam):

“Kwani hakika ya ‘lau` hufungua matendo ya shaytwaan.”

Inamfungulia mja matendo ya shaytwaan, bi maana wasiwasi na kumtia mashaka. Ni wajibu kwa muumini kuliepuka ili asije kutumbukia katika mtego wa shaytwaan. Mambo yote haya yamepangwa na Allaah. Kwa ajili hii amesema (Ta’ala):

وَلَنَبْلُوَنَّكُمْ بِشَيْءٍ مِّنَ الْخَوْفِ وَالْجُوعِ وَنَقْصٍ مِّنَ الْأَمْوَالِ وَالْأَنْفُسِ وَالثَّمَرَاتِ ۗ وَبَشِّرِ الصَّابِرِينَ الَّذِينَ إِذَا أَصَابَتْهُمُ مُصِيبَةٌ قَالُوا إِنَّا لِلَّهِ وَإِنَّا إِلَيْهِ رَاجِعُونَ أُولَٰئِكَ عَلَيْهِمْ صَلَوَاتٌ مِّن رَّبِّهِمْ وَرَحْمَةٌ ۖ وَأُولَٰئِكَ هُمُ الْمُهْتَدُونَ

“Bila shaka Tutakujaribuni kwa kitu katika khofu na njaa na upungufu wa mali na nafsi na mazao [katika kazi zenu]. Wabashirie wale wenye kusubiri ambao unapowafika msiba basi husema: “Hakika sisi ni wa Allaah na hakika sisi Kwake ni wenye kurejea - hao zitakuwa juu yao baraka kutoka kwa Mola wao na rehema na hao ndio wenye kuongoka.” (al-Baqarah 02:155-157)

Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Hakuna muislamu yeyote anayepatwa na msiba na akasema ‘Hakika sisi ni wa Allaah na Kwake ndiko tutarejea. Ee Allaah! Nilipe kwa msiba wangu na Unipe badala yake kheri kuliko’ isipokuwa humlipa kwa msiba wake na humpa badala ilio bora kuliko.”¹⁸⁷

Kwa mfano mgonjwa ameenda kwa daktari kutafuta matibabu na akafa, wale wengine hawatakiwi kusema ‘Lau angelienda kutibiwa kwa daktari mwingine na akasafiri nje ya nchi`. Wanachotakiwa kusema ni:

قَدَّرَ اللهُ وَ مَا شَاءَ فَعَلَ إِنَّ لِلَّهِ وَإِنَّا إِلَيْهِ رَاجِعُونَ

“Hivi ndivyo alivyokadiria Allaah na hufanya atakavyo. Hakika sisi ni wa Allaah na hakika sisi Kwake ni wenye kurejea.”

Asipingane kwa neno ‘lau`.

Ama ‘lau` ikitumiwa kubainisha kitu kilichotakikana kufanyika, haihesabiki ni kupingana. Ni ubainifu wa kitu ambacho ni bora zaidi. Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) alisema:

“Hivi sasa ningefanya kitu nilichokiacha basi ninge...”¹⁸⁸

Kuzungumza namna hiyo ili kubainisha ambacho kingekuwa bora zaidi haina neno. Mfano wa hilo ni:

¹⁸⁷ Muslim (918).

¹⁸⁸ al-Bukhaariy (1651) na Muslim (1216).

“Ningelijua kuwa ni mgonjwa basi ningelimtembelea.”

Hapa mtu anabainisha juu ya kitendo bora zaidi kilichompita. Huku sio kwa njia ya kukinzana na ni jambo halihusiani na mlango huu. Kilichokatazwa ni kukinzana na Qadar.

58. Makatazo ya kutukana upepo

Shaykh-ul-Islaam Muhammad bin 'Abdil-Wahhaab (Rahimahu Allaah) amesema:

1- Ubayd bin Ka'b (Radhiya Allaahu 'anh) amesimulia kwamba Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

"Msitukane upepo. Mtapoona mnachokichukia basi semeni:

اللَّهُمَّ إِنَّا نَسْأَلُكَ خَيْرَهَا وَخَيْرَ مَا فِيهَا وَخَيْرَ مَا أُرْسِلَتْ بِهِ وَنَعُوذُ بِكَ مِنْ شَرِّهَا وَشَرِّ مَا فِيهَا وَشَرِّ مَا أُرْسِلَتْ بِهِ

"Ee Allaah! Tunakuomba kheri za upepo huu, kheri ya yale yaliyomo ndani yake na kheri ya yale yaliyoamrisha kuvileta. Na tunajilinda Kwako kutokamana na shari ya upepo huu, shari ya yaliyomo ndani yake na shari ya yale yaliyoamrisha kuvileta."¹⁸⁹

Ameisahihisha at-Tirmidhiy.

MAELEZO

Pale ilipokuwa kutukana upepo na viumbe vyenginevyo ni upungufu katika imani na kuiponda Tawhiyd, ndipo mwandishi akataka kulizindua hilo ili muumini ajue kuwa maasi mengine yote yanaipunguza na kuidhoofisha Tawhiyd na imani. Imani inapanda na inashuka. Tawhiyd inapanda na inashuka. Kutukana upepo kunaipunguza imani kwa sababu upepo umeumbwa na ni wenye kuendeshwa. Unatumwa kwa kheri na shari. Hivyo hautakiwi kutukanwa. Badala yake muumini anatakiwa kutendea kazi yale aliyofundisha Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) katika Hadiyth:

¹⁸⁹ at-Tirmidhiy (2252), Ahmad (21176) na al-Bukhaariy katika "al-Adab al-Mufrad" (719). Swahiyh kwa mujibu wa al-Albaaniy katika "as-Silsilah as-Swahiyhah" (2756).

1- Ubayd bin Ka'b (Radhiya Allaahu 'anh) amesimulia kwamba Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Msitukane upepo. Mtapoona mnachokichukia basi semeni:

اللَّهُمَّ إِنَّا نَسْأَلُكَ خَيْرَهَا وَخَيْرَ مَا فِيهَا وَخَيْرَ مَا أُرْسِلَتْ بِهِ وَنَعُوذُ بِكَ مِنْ شَرِّهَا وَشَرِّ مَا فِيهَا وَشَرِّ مَا أُرْسِلَتْ بِهِ

“Ee Allaah! Tunakuomba kheri za upepo huu, kheri ya yale yaliyomo ndani yake na kheri ya yale yaliyoamrisha kuvileta. Na tunajilinda Kwako kutokamana na shari ya upepo huu, shari ya yaliyomo ndani yake na shari ya yale yaliyoamrisha kuvileta.”

al-Bukhaariy na Muslim wamepokea kutoka kwa 'Aaishah (Radhiya Allaahu 'anhaa) ambaye kasimulia kwamba Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) alikuwa akisema wakati wa upepo:

اللَّهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ خَيْرَهَا وَخَيْرَ مَا فِيهَا وَخَيْرَ مَا أُرْسِلَتْ بِهِ وَأَعُوذُ بِكَ مِنْ شَرِّهَا وَشَرِّ مَا فِيهَا وَشَرِّ مَا أُرْسِلَتْ بِهِ

“Ee Allaah! Mimi nakuomba kheri za upepo huu, kheri ya yale yaliyomo ndani yake na kheri ya yale yaliyoamrisha kuvileta. Na najilinda Kwako kutokamana na shari ya upepo huu, shari ya yaliyomo ndani yake na shari ya yale yaliyoamrisha kuvileta.”¹⁹⁰

Kuhusiana na haya kumekuja du'aa vilevile inayosema:

اللهم لا تجعلها ريحا، و اجعلها رياحا، و اجعلها رحمة، و لا تجعلها عذابا

“Ee Allaah! Usiufanye upepo mmoja, zifanye pepo nyingi, na ufanye kuwa rehema na usiufanye kuwa adhabu.”¹⁹¹

¹⁹⁰ al-Bukhaariy (4829) na Muslim (899).

¹⁹¹ at-Twabaraaniy (11533) na Abu Ya'laa (2456). Dhaifu kwa mujibu wa al-Albaaniy katika "Dhwa'if-ul-Jaami'" (4461).

Haya ndio yaliyowekwa katika Shari'ah kwa muumini kuyafanya wakati wa upepo. Amuombe Allaah pepo nyingi na sio upepo mmoja. Kwa sababu Allaah alituma upepo mmoja kwa ajili ya kuwaangamiza watu wa Huud na akatuma pepo nyingi kwa ajili ya bishara na rehema:

وَمِنْ آيَاتِهِ أَنْ يُرْسِلَ الرِّيحَ مُبَشِّرَاتٍ وَلِيُذِيقَكُمْ مِّن رَّحْمَتِهِ وَلِتَجْرِيَ الْفُلُكُ بِأَمْرِهِ وَلِتَبْتَغُوا مِنْ فَضْلِهِ وَلَعَلَّكُمْ تَشْكُرُونَ

“Katika ishara Zake ni kwamba anapeleka pepo zenye bishara nzuri na ili akuonjesheni katika huruma Zake na ili vyende vyombo kwa amri Yake na ili watafute katika fadhila Zake na ili mpate kushukuru.” (ar-Ruum 30:46)

Ni miongoni mwa ukamilifu wa Tawhiyd na imani kutekeleza maamrishi ya Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) na mtu asiutukane upepo wala kiumbe mwingine yeyote ambaye Allaah hakuweka katika Shari'ah watukanwe.

59. Mlango kuhusu maneno Yake (Ta'ala) ”Wakamdhanja Allaah pasi na haki, dhana ya kipindi cha kikafiri”

Shaykh-ul-Islaam Muhammad bin 'Abdil-Wahhaab (Rahimahu Allaah) amesema:

1- Allaah (Ta'ala) amesema:

يَظُنُّونَ بِاللَّهِ غَيْرَ الْحَقِّ ظَنَّ الْجَاهِلِيَّةِ يَقُولُونَ هَل لَّنَا مِنَ الْأَمْرِ مِنْ شَيْءٍ قُلْ إِنَّ الْأَمْرَ كُلَّهُ لِلَّهِ

”Wakamdhanja Allaah pasi na haki, dhana ya kipindi cha kikafiri, wanasema [kujiuliza wenyewe]: “Je, tuna amri yoyote sisi katika jambo hili?” Sema: “Hakika amri yote ni ya Allaah.” (Aal 'Imraan 03:154)

2-

الظَّالِمِينَ بِاللَّهِ ظَنَّ السَّوْءِ عَلَيْهِمْ دَائِرَةُ السَّوْءِ

”... wanaomdhanja Allaah dhana ovu. Utawafikia mgeuko mbaya ... ” (al-Fath 48:06)

3- Ibn-ul-Qayyim (Rahimahu Allaah) amesema kuhusu Aayah ya kwanza:

”Imefasiri dhana hii kwamba Yeye (Subhaanah) hatomnusuru Mtume wake na kwamba amri yake itaangamizwa. Imefasiriwa pia ya kwamba yaliyomsibu haikuwa kwa Qadar ya Allaah na kwa hekima Yake. Imefasiriwa vilevile kwa kupinga hekima, kupinga Qadar na kukanusha kutimia kwa amri ya Mtume wake (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) na kwamba itazishinda dini zengine zote.

Hizi ndio dhana mbaya walizokuwa wakidhania wanafiki na washirikina katika Suurah “al-Fath”. Hizi zimekuwa ni dhana mbaya kwa sababu ni kumdhania kinyume na yale yanayomstahikia Yeye (Subhaanah). Bali hayalingani na hekima Yake, sifa Zake na ahadi Yake ya kweli. Yeyote mwenye kudhania ya kwamba ataifanya batili kuitokomeza haki kwa hali ya kuendelea, akapinga yaliyotokea ni kwa mipango na makadirio Yake, akapinga kwamba ameyakadiria kwa hekima Yake kubwa inayostahiki kuhimidiwa na kufikiria ya kwamba hayo hutendeka kwa matakwa ya kiholela – mwenye kudhania hivi basi ana dhana za wale waliokufuru. Basi adhabu kali itawapata wale waliokufuru ya Moto. Watu wengi ni wenye kumfikiria Allaah dhana mbaya kwa yanayowasibu na kwa anayowafanyia wengine. Hakuna anayesalimika na hayo isipokuwa yule aliyemjua Allaah kwa majina Yake na sifa Zake na akajua yale yanayopelekewa na hekima Yake na sifa Zake. Hebu yule mwenye akili mwenye kuitakia kheri nafsi yake atilie umuhimu juu ya jambo hili, atubie kwa Allaah na amuombe msamaha kwa kumdhania Mola wake dhana mbaya. Lau ungempeleleza mtu kama basi ungemuona namna anavyojikakama juu ya Qadar na kuilaumu na jinsi alivyo na mitazamo mbalimbali juu ya mambo yalivyotakiwa kuwa badala yake. Inapokuja katika dhana hii baadhi wana kiwango kidogo na wengine kikubwa. Ichunguze nafsi yako mwenyewe; je, wewe umesalimika?

*Ikiwa umesalimika kwayo, basi utakuwa umesalimika kwa jambo kubwa
vinginevyo mimi sivezi kukuthibitishia kwamba ni mwenye kuokoka*

MAELEZO

Ibn-ul-Qayyim amesema kuhusiana na Aayah ya kwanza:

“Malengo ya mlango huu ni kwamba watu wengi si wenye kujisalimisha juu ya hekima na makadirio ya Allaah. Hawajisalimishi juu ya mawaidha ya Allaah (Subhaanah) kwa waja kuhusiana na makosa yao. Hawawaidhiki na kuzindukana. Bali wanamdhanika Allaah vibaya na wanafanya hivo kwa njia nyingi:

- 1- Wako ambao wanafikiria kuwa yale yanayotokea ambayo hawayapendi yanatokea pasi na hekima na makadirio ya Allaah.
- 2- Wengine wanadhania kwamba yanatokea tu kwa matakwa na sio kwa hekima.
- 3- Wapo wengine wanaodhania kuwa Allaah ni mwenye kuwadhulumu viumbe na wakahoji ni kwa nini wametendewa hivi na vile.

Watu wengi ni wenye kufikiria hivi. Ndio maana Allaah ('Azza wa Jall) amesema kuhusu wanafiki:

وَطَائِفَةٌ قَدْ أَهَمَّتْهُمْ أَنْفُسُهُمْ يَظُنُّونَ بِاللَّهِ غَيْرَ الْحَقِّ

“Na kundi likawashughulisha nafsi zao wakamdhanja Allaah pasi na haki.” (Aal 'Imraan 03:154)

Haya yalitokea katika vita vya Uhud wakati waislamu waliposhindwa. Wengi walijeruhiwa na sabini wakauawa. Hapo ndipo wanafiki waliongea, wakamdhanja Allaah kinyume na haki na wakasema:

هَلْ لَنَا مِنَ الْأَمْرِ مِنْ شَيْءٍ

“Je, tuna amri yoyote sisi katika jambo hili?”

Je, tulikuwa na mamlaka juu ya jambo hili? Wakasema vilevile:

لَوْ كَانَ لَنَا مِنَ الْأَمْرِ شَيْءٌ مَّا قُتِلْنَا هَاهُنَا

“Lau tungelikuwa tuna amri yoyote katika jambo basi tusingeuawa hapa.” (Aal 'Imraan 03:154)

Bi maana sisi tumetenzwa nguvu na hatuna la kusema. Muhammad ndiye katuleta katika jambo hili mpaka yakatokea yaliyotokea.

Haya yote ni kwa sababu ya ujinga wao, upotevu wao, uchache wa maono yao na upofu wa nyoyo zao. Ndio maana wakamdhanika Allaah vibaya. Hawakufikiria kuwa yaliyotokea yalitokea kwa hekima kubwa. Hawakufikiria kuwa Allaah atamnusuru Mtume Wake (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam). Wakafikiria kuwa itatokomea misheni ya Mtume huyu (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam). Wakadhania kuwa yaliyokea hayakutokea isipokuwa kwa utashi peke yake. Dhana zao mbaya hizi zikawa zimekusanya kati ya kumdhania Allaah vibaya kwamba hatomnusuru Mtume Wake (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) na mawalii wake pamoja vilevile na kwamba hafanyi hivo kwa hekima isipokuwa ni kwa utashi peke yake. Yote haya ni batili. Kwa ajili hii ndio maana akabainisha (Subhaanah) katika Kitabu Chake kitukufu hekima na siri ya yale anayoyapanga, anayoyafanya na kuyaweka katika Shari'ah na kwamba anawajaribu waja Wake kwa kuwapa vipindi vya tabu na vya raha ili kusafisha ule uchafu uliyomo katika nyoyo za waumini na kuwatokomeza makafiri. Waumini wanapaswa kutubia kwa Allaah, wamuombe msamaha, wajiandae kukutana Naye (Subhaanah) na kutekeleza haki Zake. Amesema (Ta'ala):

أَوْلَمَّا أَصَابَتْكُمْ مُصِيبَةٌ قَدْ أَصَبْتُمْ مِثْلَيْهَا قُلْتُمْ أَنَّى هَذَا ۖ قُلْ هُوَ مِنْ عِنْدِ أَنْفُسِكُمْ ۗ إِنَّ اللَّهَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ وَمَا أَصَابَكُمْ يَوْمَ التَّتَى الْجُمُعَانَ فَبِإِذْنِ اللَّهِ وَلِيَعْلَمَ الْمُؤْمِنِينَ وَلِيَعْلَمَ الَّذِينَ نَافَقُوا

“Ulipokusibuni msiba, ingawa mliwasibu [maadui wenu] mara mbili yake, mlisema: “Umetoka wapi huu?” Sema: “Huo ni kutoka kwenu wenyewe.” Hakika Allaah juu ya kila jambo ni muweza. Na yale yaliyokusibuni siku yalipokutana makundi mawili, basi [yalitokea] ni kwa idhini ya Allaah na ili adhihirishe waumini, na ili adhihirishe wale waliofanya unafiki.” (Aal 'Imraan 03:165-167)

Allaah (Subhaanah) anawajaribu watu hawa kwa sababu ya hekima kubwa. Waumini wanapewa mitihani ili zisafishwe imani zao, madhambi yao yasamehewe na ili wajiandae kwa ajili ya kukutana na Mola wao. Makafiri wanafutiliwa mbali na wanafiki wanafedheheshwa na aibu zao na batili zao

zinafichuliwa. Nyoyo za wanafiki zimeharibika. Ni wenye kumdhania Allaah vibaya na ndio maana Allaah akawanusuru waumini kama alivyowaahidi:

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا إِن تَنْصُرُوا اللَّهَ يَنْصُرْكُمْ وَيُثَبِّتْ أَقْدَامَكُمْ

“Enyi mloamini! Mkisaidia kuinusuru dini ya Allaah, basi Atakunusuruni na ataithibitisha miguu yenu.” (Muhammad 47:07)

وَلَيَنْصُرَنَّ اللَّهُ مَنْ يَنْصُرُهُ ۗ إِنَّ اللَّهَ لَقَوِيٌّ عَزِيزٌ الَّذِينَ إِِنْ مَكَّنَّاهُمْ فِي الْأَرْضِ

“Bila shaka Allaah atamnusuru yule mwenye kuinusuru dini Yake - hakika Allaah ni Mwenye nguvu kabisa, Asiyeshindika - ambao Tukiwamakinisha katika ardhi...” (al-Hajj 22:40-41)

Ahadi hii inaweza kupatikana kwa njia ya kushindwa ambapo waumini wakafa wakiwa mashahidi na wengine wakauawa kwa hekima zilizotajwa.”

Iwapo watu wangukuwa ni wenye kushinda siku zote na hawapatwi na kitu katika majaribio, huenda wangeingiwa na mthani wa kujiona na kuwa na kiburi kwa Allaah na kutokutambua mapungufu na kasoro zao. Huenda vilevile wangefikiria kuwa mafanikio yao yanatokamana na mamlaka yao, nguvu zao na matendo yao. Wanapofikwa na jambo lenye kuchukiza wanakuwa ni wenye kunyenyekea na kurejea kwa Allaah. Ni wajibu kwa muislamu kuipeleleza nafsi yake ili aweze kusalimika kutokamana na mthani huu. Endapo mtu ataipeleleza nafsi yake basi ataona namna alivyo na mapungufu na kasoro nyingi na vipingamizi juu ya Qadar na jinsi anavyojiona nafsi yake na matendo yake. Isipokuwa yule aliyekingwa na Allaah.

Ni wajibu kwa muumini kuamini mipango na makadirio ya Allaah, kwamba Yeye ana hekima kubwa katika yale yote anayofanya na kwamba amekwishatangulia kupanga kila kitu. Anatakiwa kutambua kuwa yanatokamana na hekima ya Allaah na sababu zake kuu kwamba

Amewasahilishia waumini kwa yale yaliyo bora kwao, akawanyanyua daraja zao na ili wapate kurejea Kwake (Subhaanahu wa Ta'ala).

60. Mlango juu ya mwenye kupinga Qadar

Shaykh-ul-Islaam Muhammad bin 'Abdil-Wahhaab (Rahimahu Allaah) amesema:

1- Ibn 'Umar (Radhiya Allaahu 'anhumaa) amesema:

“Naapa kwa Yule ambaye nafsi ya Ibn 'Umar iko mikononi Mwake! Lau mtu mmoja atakuwa na dhahabu mfano wa mlima wa Uhud kisha akazitoa katika njia ya Allaah hatomkubalia Allaah kutoka kwake mpaka aamini Qadar.”

Kisha akatolea dalili kwa maneno ya Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam):

“Imani ni kumuamini Allaah, Malaika Wake, Vitabu Vyake, Mitume Wake, Siku ya Mwisho na kuamini Qadar kheri na shari yake.”¹⁹²

Ameipokea Muslim.

2- 'Ubaadah bin as-Swaamit (Radhiya Allaahu 'anhu) alisema kumwambia mwanawe:

“Ee mwanangu! Hakika hutopata ladha ya imani mpaka kwanza ujue kuwa yaliyokufika hayakuwa yakukukosa na yaliyokukosa hayakuwa yakukufika. Nimemsikia Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) akisema: “Kitu cha kwanza alichoumba Allaah ni kalamu. Akaiambia: “Andika.” Ikasema: “Ee Mola Wangu! Niandike nini?” Akasema: “Andika makadirio ya kila kitu mpaka kitaposimama Qiyaamah.” Ee mwanangu! Nimemsikia Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa salla) akisema: “Yule atakayekufa akiamini kinyume na hivi, basi huyo si katika mimi.”¹⁹³

Katika upokezi wa Ahmad imekuja:

¹⁹² Muslim (8).

¹⁹³ Abu Daawuud (4700). Swahiyh kwa mujibu wa al-Albaaniy katika “Dhwilaal-ul-Jannah” (111).

“Hakika kitu cha kwanza alichoumba Allaah (Ta’ala) ilikuwa ni kalamu. Akaiambia: “Andika.” Basi tokea hapo kukapangwa kila kitu kitachokuwepo mpaka siku ya Qiyaamah.”¹⁹⁴

Ibn Wahb amesema:

“Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) amesema: “Yeyote ambaye haamini Qadar, kheri na shari yake, Allaah atamchoma kwa Moto.”

Imepokelewa katika “al-Musnad” Ahmad na tungo za Sunan kutoka kwa Ibn-ud-Daylamiy ambaye amesema:

“Nilimwendea Ka’b-ul-Ahbaar na kumwambia: “Katika nafsi yangu kuna kitu kuhusu Qadar. Tafadhali nieleze juu ya kitu pengine Allaah akakiondosha moyoni mwangu.” Akasema: “Lau utatoa dhahabu mfano wa sawa na mlima wa Uhud, basi Allaah hatozikubali kutoka kwako mpaka uamini Qadar, ujue ya kwamba yaliyokupata hayakuwa yenye kukukosa na yaliyokukosa hayakuwa yenye kukupata. Iwapo utakufa ukiwa na imani kinyume na hii utakuwa mmoja katika watu wa Motoni.” Nikamwendea ‘Abdullaah bin Mas’uud, Hudhayfah bin al-Yamaan na Zayd bin Thaabit na wote wakanieleza kwa mfano wa hayo kutoka kwa Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam).”¹⁹⁵

Hadiyth ni Swahiyh kaipokea al-Haakim katika “as-Swahiyh” yake.

MAELEZO

Pale ilipokuwa kuamini Qadar ni miongoni mwa misingi ya imani ndipo mwandishi akaweka mlango huu. Kuamini Qadar ni miongoni mwa mambo yanayopelekea katika Tawhiyd na yanapinga kufuru. Mlango huu ndani yake

¹⁹⁴ Ahmad (22757) na at-Tirmidhiy (2155). Swahiyh kwa mujibu wa al-Albaaniy katika “Swahiyh-ul-Jaami” (2017).

¹⁹⁵ Abu Daawuud (4699), Ibn Maajah (77), Ahmad (21629) na at-Twabaraaniy katika “al-Mu’jam al-Kabiy” (4940). Swahiyh kwa mujibu wa al-Albaaniy katika “Swahiyh Sunan Ibn Maajah” (62).

kuna makemeo na matahadharisho makali kwa yule anayepinga na kukadhibisha Qadar.

Waislamu wakati wa Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) walikuwa ni wenye kuamini Qadar na ni wenye kujisalimisha kwa Allaah. Mwishoni mwa zama za Maswahabah ndipo kukazuka kikundi kinachopinga Qadar na wakasema kuwa Allaah hajui yanayopitika kabla ya kutokea kwake. Wakadai kwamba kuthibitisha Qadar kunapingana na uadilifu. Ni vipi mambo yatapangwa hapo kabla kisha aadhibiwe mtenda maasi na kafiri kwa waliyoyafanya? Fikira zao zinatokamana na ujinga, upotevu na kutatizika kwao na mambo.

Ahl-ul-Haqq katika Maswahabah wa Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) na Ahl-ul-Sunnah wal-Jamaa'ah waliofuata mwenendo wao waliamini na wakadhibitisha Qadar. Wanaonelea kuwa Allaah amekadiria mambo na akayaandika na kwamba hakuna kinachotokea isipokuwa kwa matakwa Yake. Kila kitu kimeshakadiriwa, kila kitu kimeshadhibitiwa na ni Mwenye kutambua kila kitu. Imaam ash-Shaafi'iy (Rahimahu Allaah) amesema:

“Jadiliana nao juu ya elimu. Wakiithibitisha, basi wameshindwa, na wakiikanusha, wanakufuru.”

Maana yake ni kwamba wanatakiwa kuulizwa kama Allaah anayajua mambo kabla ya kutokea kwake au hayajui. Wakikubali, basi hiyo ndio Qadar. Wakipinga na wakasema kuwa Allaah hayajui yatayotokea, wanakufuru kwa sababu katika hali hii watakuwa wamemsifu Allaah kuwa na ujinga na upotevu. Allaah (Ta'ala) amesema:

إِنَّ اللَّهَ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمٌ

“Hakika Allaah ni mjuzi wa kila kitu.” (al-Anfaal 08:75)

لَتَعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ وَأَنَّ اللَّهَ قَدْ أَحَاطَ بِكُلِّ شَيْءٍ عِلْمًا

”[Haya yote] ili mjue kwamba Allaah juu ya kila kitu ni muweza na kwamba Allaah amekwishakizunguka kila kitu kwa ujuzi.” (at-Twalaah 65:12)

Mwenye kumnasibishia Allaah ujinga na kwamba hayajui mambo basi kwa hakika atakuwa ametukana ishara za Allaah na amemponda kikwelikweli na kwa ajili hiyo anakuwa kafiri. Kwa ajili hiyo ndio maana wanachuoni wengi wa Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa’ah wameonelea kuwa Qadariyyah ni makafiri. Kwa sababu wamekadhibisha Qadar ya Allaah, wamepinga ujuzi Wake, wamezikadhibisha dalili zote hizi na wamemnasibishia Allaah ujinga. Imesihi kupitia kwa ‘Umar (Radhiya Allaahu ‘anh) ya kwamba Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) amesema:

”Imani ni kumuamini Allaah, Malaika Wake, Vitabu Vyake, Mitume Wake, Siku ya Mwisho na kuamini Qadar kheri na shari yake.”

Hayo yamefahamishwa pia na Qur-aan. Allaah (Subhaanah) amesema:

مَا أَصَابَ مِنْ مُصِيبَةٍ فِي الْأَرْضِ وَلَا فِي أَنْفُسِكُمْ إِلَّا فِي كِتَابٍ مِّن قَبْلِ أَنْ نَبْرَأَهَا ۚ إِنَّ ذَٰلِكَ عَلَى اللَّهِ
يَسِيرٌ

”Hausibu msiba wowote katika ardhi au katika nafsi zenu isipokuwa upo katika Kitabu, kabla hatujautokezesha. Hakika hayo kwa Allaah ni mepesi.” (al-Hadiyd 57:22)

Kwa ajili hii ndio maana Ibn ‘Umar (Radhiya Allaahu ‘anhuma) amesema:

”Naapa kwa Yule ambaye nafsi ya Ibn ‘Umar iko mikononi Mwake! Lau mtu mmoja atakuwa na dhahabu mfano wa mlima wa Uhud kisha akazitoa katika njia ya Allaah hatomkubalia Allaah kutoka kwake mpaka aamini Qadar.”

Vivyo hivyo yamesemwa na Zayd bin Thaabit, Ubayy bin Ka'b, 'Abdullaah bin Mas'uud na wengineo. Hivyo pia ndivo wanavosema Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa'ah. Ni wajibu kwa kila muislamu kuamini Qadar.

Kuamini Qadar kumekusanya mambo mane:

- 1- Allaah anakijua kila kitu.
- 2- Akakiandika.
- 3- Amekiumba kila kitu na amekadiria kila kitu.
- 4- Anachotaka Allaah huwa na asichotaka Allaah hakiwi.

Mwenye kuamini mambo haya mane basi anaamini Qadar. Mwenye kukadhibisha moja katika mambo hayo amekadhibisha kitu katika Qadar.

2- 'Ubaadah bin as-Swaamit (Radhiya Allaahu 'anhu) alisema kumwambia mwanawe:

“Ee mwanangu! Hakika hutopata ladha ya imani mpaka kwanza ujue kuwa yaliyokufika hayakuwa yakukukosa na yaliyokukosa hayakuwa yakukufika. Nimemsikia Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) akisema: “Kitu cha kwanza alichoumba Allaah ni kalamu. Akaiambia: “Andika.” Ikasema: “Ee Mola Wangu! Niandike nini?” Akasema: “Andika makadirio ya kila kitu mpaka kitaposimama Qiyaamah.” Ee mwanangu! Nimemsikia Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa salla) akisema: “Yule atakayekufa akiamini kinyume na hivi, basi huyo si katika mimi.”

Bi maana hutohisi utulivu, raha na utamu wa imani isipokuwa mpaka uamini kwamba yaliyokufika hayakuwa yakukukosa na yaliyokukosa hayakuwa yakukufika. Huku ndio kuamini Qadar. Akiamini namna hii basi moyo wake utakunjuka na atafanyia kazi Shari'ah ya Allaah. Mtu kama huyu afanye yale anayotakiwa kufanya na huku moyo wake umetulizana kwa sababu anatambua

hakuna kitachomfika isipokuwa kile alichomwandikia Allaah. Tafsiri hii ya baadhi ya mambo ya Qadar imekusanya Qadar nzima.

Kadhalika walisema Maswahabah kumwambia 'Abdullaah bin Fayruuz ad-Daylamiy ambaye ni Taabiy' anayetambulika. Alipowauliza walimwambia kwamba Allaah hakubali chochote kutoka kwake mpaka aamini Qadar. Vinginevyo matendo yake ni yenye kuporomoka. Ni dalili inayoonyesha kuwa walimaanisha kwamba anakufuru kwa hilo. Kwa sababu Allaah amesema:

وَلَوْ أَشْرَكُوا لَحَبِطَ عَنْهُمْ مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ

“Lau wangemshirikisha basi pasi na shaka yangeporomoka yale waliyokuwa wakitenda.” (al-An'aam 06:88)

Ambaye matendo yake na swadaqah zake hazikubaliwi ni kafiri ambaye imani yake haijahakikika. Mwenye kukanusha Qadar basi amepinga moja ya nguzo za imani na kwa hivyo matendo yake yote yanaporomoka. Muslim amepokea kupitia kwa 'Abdullaah bin 'Awf kwamba Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa salla) amesema:

“Allaah amekadiria makadirio ya viumbe kabla ya kuumba mbingu na ardhi kwa miaka khamsini na wakati huo 'Arshi Yake ilikuwa juu ya maji.”¹⁹⁶

Kila kitu kimeshakadiriwa na kupangwa kwa mujibu wa ujuzi na uandishi wa Allaah. Yeye (Subhaanahu wa Ta'ala) ndiye Muumbaji mwenye kuyaendesha mambo kwa mujibu wa makadirio Yake. Hii ndio haki na ndio mfumo wa Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa'ah. Yule mwenye kuyaamini haya ndiye kapatia na yule mwenye kwenda kinyume na haya amepondoka kutoka katika haki.

¹⁹⁶ Muslim (2653).

61. Mlango kuhusu picha

Shaykh-ul-Islaam Muhammad bin 'Abdil-Wahhaab (Rahimahu Allaah) amesema:

1- Abu Hurayrah (Radhiya Allaahu 'anh) amesimulia kwamba Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Allaah (Ta'ala) amesema: “Ni nani dhalimu mkubwa kuliko yule ambaye anajaribu kuumba mfano wa viumbe Wangu? Hebu waumbe mdudu chungu, waumbe punje ya nafaka au waumbe chembe ya shayiri.”¹⁹⁷

Ameipokea al-Bukhaariy na Muslim.

2- Wamepokea vilevile kutoka kwa 'Aaishah (Radhiya Allaahu 'anhaa) ya kwamba Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Watu watakaokuwa na adhabu kali siku ya Qiyaamah ni wale wanaomuiga Allaah katika uumbaji Wake.”¹⁹⁸

3- Wamepokea pia kutoka kwa Ibn 'Abbaas (Radhiya Allaahu 'anhumaa) ambaye amesimulia ya kwamba amemsikia Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) akisema:

“Kila mtengeneza picha atakuwa Motoni. Ataifanya kila picha aliyoitengeneza kuwa na nafsi ambapo ataadhibiwa kwayo Motoni.”¹⁹⁹

Wamepokea tena ya kwamba Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

¹⁹⁷ al-Bukhaariy (5953) na (7559) na Muslim (2111).

¹⁹⁸ al-Bukhaariy (5954) na Muslim (2107).

¹⁹⁹ Muslim (2110).

“Atakayetengeneza picha duniani atakalifishwa kuipulizia roho, jambo ambalo hatoweza.”²⁰⁰

Muslim amepokea kutoka kwa Abul-Hayyaaj ambaye ameeleza kwamba 'Aliy (Radhiya Allaahu 'anh) alimwambia:

“Hivi nisikutume juu ya kazi aliyonituma kwayo Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam)? Usiache picha hata moja isipokuwa umeiharibu wala kaburi lililoinuka isipokuwa umelisawazisha.”²⁰¹

MAELEZO

Alichokusudia mwandishi kwa kuweka mlango huu ni kwamba picha ni miongoni mwa madhambi makubwa yanayoitia dosari Tawhiyd na yanaweza kumsababishia yule mfanyaji kupata ghadhabu za Allaah na kutumbukia Motoni na imani kupungua na kudhoofika. Watengeneza picha ni wale wanaoigiza uumbaji wa Allaah kwa njia ya kutengeneza picha za wanyama sawa kwa kutumia mkono au kwa kutumia nyenzo nyingine yoyote.

1- Abu Hurayrah (Radhiya Allaahu 'anh) amesimulia kwamba Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Allaah (Ta'ala) amesema: “Ni nani dhalimu mkubwa kuliko yule ambaye anajaribu kuumba mfano wa viumbe Wangu? Hebu waumbe mdudu chungu, waumbe punje ya nafaka au waumbe chembe ya shayiri.”

Swali hili limeulizwa kwa njia ya makanusho. Kwa msemu mwingine ni kwamba hakuna ambaye ni dhalimu zaidi kuliko huyu mtengeneza mapicha. Makusudio ya Hadiyth ni kutahadharisha kutokamana na kitendo hichi. Usulubu kama huu umekuja sehemu nyingi katika Qur-aan ikiwa ni pamoja na maneno Yake (Ta'ala):

²⁰⁰ al-Bukhaariy (5963) na Muslim (2110).

²⁰¹ Muslim (969).

وَمَنْ أَظْلَمُ مِمَّنِ افْتَرَىٰ عَلَى اللَّهِ كَذِبًا أَوْ كَذَّبَ بِآيَاتِهِ ۗ إِنَّهُ لَا يُفْلِحُ الظَّالِمُونَ

“Ni nani mdhalimu zaidi kuliko yule aliyemzulia Allaah uongo au anayekadhibisha alama Zake? Hakika madhalimu hawatofaulu.” (al-An’aam 06:21)

Allaah amesema:

“... kuliko yule ambaye anajaribu kuumba mfano wa viumbe Wangu?”

Bi maana anatengeneza picha kama picha Yangu. Kama kweli wana uwezo wa kufanya hivo, basi:

“Hebu waumbe mdudu chungu ...”

Waache waumbe mdudu chungu akiwa na sifa zake za kawaida kama vile usikizi, kutembea na nyenginezo. Pamoja na kipimo chake ni kiumbe wa ajabu mno:

“... waumbe punje ya nafaka.”

Waache waumbe punje ya nafaka au shayiri ikiwa na sifa zake za kawaida kama kumea, kuwanufaisha watu na nyenginezo. Ni vipi wataweza kuumba kiumbe kilicho na uhai ikiwa hawawezi kuumba kiumbe kisichokuwa na uhai na kumea?

3- Wamepokea pia kutoka kwa Ibn ‘Abbaas (Radhiya Allaahu ‘anhumaa) ambaye amesimulia ya kwamba amemsikia Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) akisema:

“Kila mtengeneza picha atakuwa Motoni. Ataifanya kila picha aliyoitengeneza kuwa na nafsi ambapo ataadhibiwa kwayo Motoni.”

Wanachuoni wote wamekubaliana juu ya kwamba kutengeneza picha za viumbe vyenye roho kwa njia ya masanamu vinyago ni katika madhambi makubwa. Ikiwa sio kwa njia ya masanamu vinyago, kama vile kuchora kuta, vibao na

nguo, baadhi ya wanafunzi wa Maswahabah wamejuzisha hilo. Hata hivyo wale maimamu wane na wanachuoni wengi wamekubaliana juu kwamba picha hizo pia zimeharamishwa na kwamba zina hukumu moja kama vile picha zenye kivuli. Maoni haya ndio sahihi zaidi kwa sababu Hadiyth ni zenye kuenea na zimekusanya zile picha za masanamu vinyago na zisizokuwa hivo na zimejumuisha pia zile picha za kisasa na nyenginezo. Miongoni mwa dalili zinazofahamisha kuwa hukumu ni yenye kuenea ni kwamba Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) siku moja wakati alipokuja kwa 'Aaishah na akaona picha kwenye pazia zake alighadhibika. Akasema:

“Hakika watu wa picha hizi ni wenye kuadhibiwa siku ya Qiyaamah na wataambiwa: “Vipeni uhai vile mlivyoviumba!”²⁰²

Katika pazia hakuna masanamu vinyago.

Picha za kisasa zina hukumu moja. Dalili ya hilo ni yale yaliyotokea ile siku ya ufunguzi wa mji wa Makkah ambapo Usamaah (Radhiya Allaahu 'anh) alimletea maji Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) akayafutia mapicha kutoka kwenye Ka'bah. Ni wajibu kutahadhari na hilo. Muislamu anatakiwa kujiepusha na madhambi haya. Ni wajibu kuziondosha na kuziharibu.

Muslim amepokea kutoka kwa Abul-Hayyaaj ambaye ameeleza kwamba 'Aliy (Radhiya Allaahu 'anh) alimwambia:

“Hivi nisikutume juu ya kazi aliyonituma kwayo Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam)? Usiache picha hata moja isipokuwa umeiharibu wala kaburi lililoinuka isipokuwa umelisawazisha.”

Kwa sababu Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) alikataza kuyajengea makaburi kwa sababu ni jambo linalopelekea katika shirki. Kadhalika picha

²⁰² al-Bukhaariy (2105) na Muslim (2107).

zinapelekea katika shirki. Kwa ajili hii shirki ilitokea wakati wa Nuuh (‘alayhis-Salaam) kwa sababu ya mapicha.

Kuhusu yale mahitajio ya watu ya picha hii leo, zinatakiwa kutumiwa wakati wa kutenzwa nguvu tu na wakati wa haja. Kwa njia hiyo mtu anayafanya hali ya kuwa si mwenye kupenda kwake mwenyewe. Mfano wa picha hizo ni kama zile zinazotumiwa katika vyeti vya vitambulisho.

Picha zinawazuia Malaika kuingia katika nyumba, kama ilivyofahamisha hivo Haidiyth Swahiyh²⁰³. Kunavuliwa katika hayo zile picha zenye kutwezwa. Picha kama hizi haifai kuzitengeneza, japokuwa ni zenye kutwezwa, lakini haziwazui Malaika kuingia katika nyumba. Mfano wa picha hizo ni zile zinazokuwa katika magodoro. Kadhalika mbwa ya ulinzi na mbwa ya kuelekeza njia haziwazui Malaika kuingia katika nyumba kwa sababu zimeruhusiwa. Kwa hiyo mtu akinunua godoro lililo na picha na akalilalia, haina neno kwa sababu ni lenye kutwezwa na Allaah ndiye mjuzi zaidi.

Uharamu ni wenye kuhusu pia zile picha za wale wapambanaji wa kiafghanistani. Jihaad inakuwa pasi na picha. Wala haitakikani kuwachukua video camera.

Kuwaning'iniza wanyama juu ni jambo halitakikani. Huku ni kuharibu mali bila faida yoyote. Baadhi wanaweza vilevile kutumia hoja kwamba mnyama ni picha pia. Kuna khatari vilevile baadhi wakaanza kuitakidi imani mbovu juu ya mnyama huo na kwamba anawazuia majini na mfano wa hayo.

Makatazo katika Hadiyth ni yenye kujumuisha vilevile picha kwa madhumuni ya mafunzo na mengineyo.

²⁰³ al-Bukhaariy (3322) na Muslim (2106).

62. Mlango kuhusu kuapa kwa wingi

Shaykh-ul-Islaam Muhammad bin 'Abdil-Wahhaab (Rahimahu Allaah) amesema:

1- Allaah (Ta'ala) amesema:

وَاحْفَظُوا أَيْمَانَكُمْ

“Hifadhini viapo vyenu.” (al-Maaidah 05:89)

2- Abu Hurayrah (Radhiya Allaahu 'anh) ameeleza kwamba amemsikia Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) akisema:

“Kiapo kinaweza kumshawishi mnunuzi kununua bidhaa, lakini kunaondosha na baraka.”²⁰⁴

Ameipokea al-Bukhaariy na Muslim.

3- Salmaan (Radhiya Allaahu 'anh) amesimulia ya kwamba Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Watu aina tatu hatowasemeza Allaah, hatowatakasa na watakuwa na adhabu kali: mzee mzinifu, mtu fakiri mwenye kiburi na mtu ambaye kamfanya Allaah ndio bidhaa yake; hanunui isipokuwa kwa kuapa na wala hauzi isipokuwa kwa kuapa.”²⁰⁵

Ameipokea at-Twabaraaniy kwa cheni ya wapokezi Swahiyh.

²⁰⁴ al-Bukhaariy (2087) na Muslim (1606).

²⁰⁵ at-Twabaraaniy katika "al-Mu'jam al-Kabiy" (6111). Swahiyh kwa mujibu wa al-Albaaniy katika "Swahiyh-ul-Jaami" (3072).

4- Imesihi kupokelewa kutoka kwa 'Imraan bin Huswayn (Radhiya Allaahu 'anh) ambaye ameeleza kwamba Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Watu bora katika Ummah wangu ni wale wa karne yangu, kisha wale watakaowafuatia, kisha wale watakaowafuatia. Kisha baadaye kutakuja watu wanaoshuhudia bila kuombwa kushuhudia, watakuwa makhaini na wala hawatoaminiwa, wanaweka nadhiri na wala hawatekelezi na kutadhihiri kwao unene.”

'Imraan amesema:

“Sikumbuki alisema baada ya karne yangu mara mbili au mara tatu.”²⁰⁶

Ameipokea Muslim.

5- Amepokea vilevile kutoka kwa Ibn Mas'uud (Radhiya Allaahu 'anh) ya kwamba Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Bora ya watu ni wa karne yangu, kisha watakaowafuatia, kisha watakaowafuatia. Halafu watakuja watu ambao ushahidi wao unatangukia viapo vyao na viapo vyao vinatangukia ushahidi wao.”²⁰⁷

6- Ibraahiym amesema:

“Pindi tulipokuwa wadogo walikuwa wakitupiga kwa kuapa na kwa kutoa ushahidi.”²⁰⁸

MAELEZO

²⁰⁶ al-Bukhaariy (2651) na Muslim (2535).

²⁰⁷ al-Bukhaariy (2652) na Muslim (2533).

²⁰⁸ al-Bukhaariy (6608) na Muslim (1639).

Mwandishi alichokusudia ni kwamba jambo la kuapa kwa wingi linaipunguza imani na Tawhiyd kwa sababu kuapa kwa wingi ni jambo linapelekea katika yafuatayo:

1- Kuchukulia wepesi na kutojali.

2- Uongo.

3- Kumdhanja uongo.

Mwenye kuapa sana hutumbukia katika uongo. Kwa ajili hiyo ndio maana inatakiwa kujiepusha na kuapa kwa wingi. Allaah (Subhaanahu wa Ta'ala) amesema:

1- Allaah (Ta'ala) amesema:

وَاحْفَظُوا أَيْمَانَكُمْ

"Hifadhini viapo vyenu."

Amri inapelekea uwajibu. Ni wajibu kuchunga viapo isipokuwa wakati wa haja. Muumini anatakiwa kuhifadhi na kutekeleza viapo vyake isipokuwa wakati wa haja, manufaa makubwa ya Kishari'ah, magomvi na mfano wake. Havitakiwi kukithirishwa. Kwa sababu kuna khatari mtu akamdhanja uongo.

2- Abu Hurayrah (Radhiya Allaahu 'anh) ameeleza kwamba amemsikia Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) akisema:

"Kiapo kinaweza kumshawishi mnunuzi kununua bidhaa, lakini kunaondosha na baraka."

Katika upokezi mwingine ametajwa "Mtume". Ni dalili inayofahamisha kwamba kuapa kwa wingi kunapelekea mtu kutumbukia katika makosa. Mtu huyu anaapa kwa sababu anataka kuuza bidhaa yake. Lakini anaingia khatarini kwa kukosa faida na kukosa baraka. Kwa hivyo anauza bidhaa yake kwa kuapa kwa

jina la Allaah kwamba iko namna hii na ile na matokeo yake akawaghuri wengine na huenda wakamsadikisha na wakainunua, lakini hata hivyo inakosa faida kwa sababu ya kule kuchukulia kwake wepesi wa kiapo.

Muslim amepokea kupitia kwa Abu Dharr (Radhiya Allaahu 'anh):

“Watu aina tatu hatowasemeza Allaah, hatowatakasa na watakuwa na adhabu kali: mwanaume mwenye kuvaa nguo ndefu yenye kuvuka kongo mbili za miguu, mzee mzinifu, mtu fakiri mwenye kiburi na mtu ambaye kamfanya Allaah ndio bidhaa yake; hanunui isipokuwa kwa kuapa na wala hauzi isipokuwa kwa kuapa.”²⁰⁹

Bidhaa inaweza kuuzika kwa kiapo cha uongo na kiapo cha ukweli, lakini kuapa kwa wingi ni jambo linamwingiza mtu katika makosa. Tamaa nyingi inaweza kumfanya muuzaji kuanza kudanganya. Kwa ajili hiyo ni wajibu kwa mtu kutahadhari. Viapo hivi vinapelekea kukosekana baraka na kuingia katika madhambi.

3- Salmaan (Radhiya Allaahu 'anh) amesimulia ya kwamba Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Watu aina tatu hatowasemeza Allaah, hatowatakasa na watakuwa na adhabu kali: mzee mzinifu, mtu fakiri mwenye kiburi na mtu ambaye kamfanya Allaah ndio bidhaa yake; hanunui isipokuwa kwa kuapa na wala hauzi isipokuwa kwa kuapa.”

Pamoja na kuwa mtu huyu ni fakiri lakini pamoja na hivyo anafanya kiburi. Tajiri anaweza kufanya kiburi kwa ajili ya mali zake, lakini fakiri huyu hana sababu yoyote ya kufanya kiburi. Hafanyi kiburi isipokuwa ni kwa sababu ni maumbile yake na ni sifa alionayo katika moyo wake.

²⁰⁹ Muslim (106).

Katika Hadiyth hii kuna matahadharisho juu ya sifa hizi akiwemo mzee mzinifu. Ni jambo kubwa kwa sababu kijana anaweza kutubia na kuachana na jambo hilo. Lakini huyu mzee hakuna kilichomfanya akaendelea kufanya hivo isipokuwa ni kwa sababu ni jambo limekita kabisa moyoni mwake. Wanachuoni wanasema kuwa Hadiyh hii ni dalili inayoonyesha kwamba dhambi inakuwa kubwa na khatari zaidi pale ambapo mtu anakuwa na uchache na udhaifu wa matamanivu.

4- Imesihi kupokelewa kutoka kwa 'Imraan bin Huswayn (Radhiya Allaahu 'anh) ambaye ameeleza kwamba Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Watu bora katika Ummah wangu ni wale wa karne yangu, kisha wale watakaowafuatia, kisha wale watakaowafuatia. Kisha baadaye kutakuja watu wanaoshuhudia bila kuombwa kushuhudia, watakuwa makhaini na wala hawatoaminiwa, wanaweka nadhiri na wala hawatekelezi na kutadhihiri kwao unene.”

'Imraan amesema:

“Sikumbuki alisema baada ya karne yangu mara mbili au mara tatu.”

Hata hivyo ni Hadiyth Swahiyh kutoka kwa 'Umar katika “al-Musnad” na Ibn Mas'uud (Radhiya Allaahu 'anhumaa) ya kwamba Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) alitaja karne mbili baada ya karne yake:

“Kisha baadaye kutakuja watu wanaoshuhudia bila kuombwa kushuhudia, watakuwa makhaini na wala hawatoaminiwa, wanaweka nadhiri na wala hawatekelezi na kutadhihiri kwao unene.”

Hii ina maana kwamba hali zitabadilika baada ya karne hizi tatu bora. Baada ya hapo kutakuwepo ukhaini, wanavunja nadhiri na wanashuhudia uongo kwa sababu ya udhaifu wa imani zao, ujinga kuenea na makosa mengi.

Ni wajibu kutekeleza nadhiri na ni miongoni mwa sifa za waumini. Hata hivyo nadhiri ni kitu kisichotakikana kwa sababu Hadiyth inasema:

“Hadiyth haileti kheri yoyote. Ni kitu kinachotoka kwa bakhili.”²¹⁰

Lakini akiweka nadhiri njema basi ni lazima aitekeleze. Ama kuhusu nadhiri ya maasi haifai kwake akaitekeleza ingawa ni wajibu kuitolea kafara:

“Kutadhihiri kwao unene.”

Kwa sababu ya kughafilika kwao na kuzama kwao katika neema na matamano. Lakini haina manaa kwamba kila ambaye ni mnene anatakiwa kuepukwa na ni mtu mbaya. Wanaweza kuwepo watu wanene ambao ni wazuri na wema. Hadiyth inaashiria ughafilikaji na upuuziaji wa kujiandaa na Aakhirah.

5- Amepokea vilevile kutoka kwa Ibn Mas'ud (Radhiya Allaahu 'anh) ya kwamba Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Bora ya watu ni wa karne yangu, kisha watakaowafuatia, kisha watakaowafuatia. Halafu watakuja watu ambao ushahidi wao unatangulia viapo vyao na viapo vyao vinatangulia ushahidi wao.”

Hadiyth inawahusu watu wote katika karne ile ambao ni Maswahabah (Radhiya Allaahu 'anhum). Ni watu bora baada ya Mitume. Kisha wale wataokaofuatia ambao ni wanafunzi wa Maswahabah. Kisha wale waliokuja baada ya wanafunzi wa Maswahabah:

“Halafu watakuja watu ambao ushahidi wao unatangulia viapo vyao na viapo vyao vinatangulia ushahidi wao.”

Haya yanatokana na uchache wa kujali kwao na upumbavu kwa sababu ya udhaifu na uchache wa imani.

²¹⁰ al-Bukhaariy (6608) na Muslim (1639).

6- Ibraahiym amesema:

“Pindi tulipokuwa wadogo walikuwa wakitupiga kwa kuapa na kwa kutoa ushahidi.”

Salaf walikuwa wakiwatia adabu watoto wao pindi wanaposhuhudia na kuapa ili wasije wakazowea kufanya hivo na matokeo yake wakaja kushuhudia uongo na wakaingia katika mikataba ya kidhuluma. Mtoto anapozowea tabia kama hii baadaye anapokuwa mkubwa anakuja kuchukulia wepesi. Hii ni dalili inayoonyesha kuwa Salaf walikuwa wakitilia umuhimu juu ya tabia njema na malezi mema kwa watoto wao. Hili ndio jambo la wajibu kwa kila muislamu.

63. Mlango kuhusu ahadi za Allaah na Mtume Wake

Shaykh-ul-Islaam Muhammad bin 'Abdil-Wahhaab (Rahimahu Allaah) amesema:

1- Allaah (Ta'ala) amesema:

وَأَوْفُوا بِعَهْدِ اللَّهِ إِذَا عَاهَدْتُمْ وَلَا تَنْفُضُوا الْأَيْمَانَ بَعْدَ تَوْكِيدِهَا وَقَدْ جَعَلْتُمُ اللَّهَ عَلَيْكُمْ كَفِيلًا إِنَّ اللَّهَ يَعْلَمُ مَا تَفْعَلُونَ

“Timizeni ahadi ya Allaah mnapoahidi na wala msivunje viapo baada ya kuvifunga na mmekwishamfanya Allaah kuwa ni mdhamini wenu; hakika Allaah anajua yale mnayoyafanya.” (an-Nahl 16:91)

2- Buraydah (Radhiya Allaahu 'anh) ameeleza ya kwamba Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) alipokuwa anateua kiongozi kwa jeshi au kikosi, basi humusia kumcha Allaah na kuwafanyia wema wale waislamu aliyo pamoja nao. Alikuwa akisema:

“Anzeni kupigana kwa jina la Allaah mpigane katika njia ya Allaah. Piganeni na kila mwenye kumkufuru Allaah, piganeni, msichukue kitu katika ngawira pasi na idhini, msivunje mkataba na wala msikatekate viungo vya maiti na wala msimuue mtoto. Ukikutana na adui wako katika washirikina mlinganie katika mambo matatu. Ikiwa atakubali kwa lolote katika haya matatu basi mkubalie na jizuie kumpiga vita. Mlinganie katika Uislamu. Akikukubalia hilo muitikie. Kisha mlinganie katika kuhama kutoka katika miji yao na kwenda katika miji ya Muhaajiruun na uwaambie ya kwamba ikiwa watafanya hivyo basi wana haki zote kama walizonazo Muhaajiruun na watakuwa na kama yale walionayo Muhaajiruun. Wakikataa kuhama kutoka katika miji yao waambieni ya kwamba watakuwa na hadhi kama ya mabedui wa Kiislamu na watapitishiwa hukumu ya

Allaah (Ta'ala); hawatokuwa na haki yoyote ya ngawira wala fai isipokuwa ikiwa watapigana Jihaad bega kwa bega wakiwa pamoja na waislamu. Ikiwa watakataa waombeni kodi. Wakikubali wakubalieni na jizuieni kupigana nao. Ikiwa watakataa muombeni Allaah msaada na piganeni nao. Utapowazingira watu waliomo ngomeni na wakakutaka ufunge nao mkataba wa Allaah na mkataba wa Mtume Wake, basi usifunge mkataba wa Allaah na mkataba wa Mtume Wake. Lakini badaba yake funga nao mkataba wako wewe na mkataba wa Maswahabah wako. Kwani hakika mtapotaka kuvunja mikataba yenu na mikataba ya Maswahabah wenu ni jambo jepesi kuliko kuvunja mkataba wa Allaah na mkataba Mtume Wake. Utapowazingira watu waliomo ngomeni na wakakutaka uwateremshe katika hukumu ya Allaah, usiwateremshe katika hukumu ya Allaah. Lakini badala yake wateremshe kwa hukumu yako. Kwani hakika hujui utapatia kwao hukumu ya Allaah au hapana."²¹¹

Ameipokea Muslim.

MAELEZO

Mlango unahusu kuadhimisha ahadi ya Allaah na Mtume Wake (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam). Unatahadharisha vilevie kuitumia vibaya na kuifunga baina ya watu kwa sababu kufanya hivo kunaweza kupelekea ikatumiwa vibaya. Ni wajibu kwa watawala wasivunge ahadi ya Allaah na Mtume Wake (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) kati ya watu. Badala yake wafunge kwa jina la maraisi, wafalme au watu wao. Huku ni kwa sababu ya kuadhimisha ahadi ya Allaah na Mtume Wake (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam). Ni katika kukamilisha Tawhiyd na imani. Kuvunja ahadi kama hii ni jambo linaipunguza Tawhiyd na ni njia inayopelekea ikachezewa.

1- Allaah (Ta'ala) amesema:

²¹¹ Muslim (1731).

وَأَوْفُوا بِعَهْدِ اللَّهِ إِذَا عَاهَدْتُمْ وَلَا تَنْفُضُوا الْأَيْمَانَ بَعْدَ تَوْكِيدِهَا وَقَدْ جَعَلْتُمُ اللَّهَ عَلَيْكُمْ كَفِيلًا إِنَّ اللَّهَ يَعْلَمُ مَا
تَفْعَلُونَ

“Timizeni ahadi ya Allaah mnapoahidi na wala msivunje viapo baada ya kuvifunga na mmekwishamfanya Allaah kuwa ni mdhamini wenu; hakika Allaah anajua yale mnayoyafanya.”

Yule mwenye kufunga mkataba kwa jina la Allaah na Mtume Wake (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) basi ni lazima atekeleze. Japokuwa atakuwa amekosea kufunga mkataba kwa jina la Allaah na Mtume Wake (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) lakini pamoja na hivyo ni lazima atekeleze. Haifai kwake akaivunja:

وَأَوْفُوا بِعَهْدِ اللَّهِ إِذَا عَاهَدْتُمْ وَلَا تَنْفُضُوا الْأَيْمَانَ بَعْدَ تَوْكِيدِهَا وَقَدْ جَعَلْتُمُ اللَّهَ عَلَيْكُمْ كَفِيلًا إِنَّ اللَّهَ يَعْلَمُ مَا
تَفْعَلُونَ

“Timizeni ahadi ya Allaah mnapoahidi na wala msivunje viapo baada ya kuvifunga na mmekwishamfanya Allaah kuwa ni mdhamini wenu; hakika Allaah anajua yale mnayoyafanya.”

Msivunje ahadi baada ya kuwa mmeshaifunga kwa viapo vikali. Timizeni kama alivyosema (Subhaanah):

وَأَوْفُوا بِالْعَهْدِ ۗ إِنَّ الْعَهْدَ كَانَ مَسْئُولًا

“Timizeni ahadi; hakika ahadi itakuwa ni yenye kuulizwa.” (al-Israa' 17:34)

Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Kila mdanganyifu atakuwa na bendera siku ya Qiyaamah na itasemwa: “Huu ni udanganyifu wa fulani mwana wa fulani.”²¹²

Haya ni matishio makali ambayo yanafahamisha kwamba ni lazima kutekeleza ahadi.

2- Buraydah (Radhiya Allaahu ‘anh) ameeleza ya kwamba Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) alipokuwa anateua kiongozi kwa jeshi au kikosi, basi humuusia kumcha Allaah na kuwafanyia wema wale waislamu aliyo pamoja nao. Alikuwa akisema:

“Anzeni kupigana kwa jina la Allaah mpigane katika njia ya Allaah. Piganeni na kila mwenye kumkufuru Allaah, piganeni, msichukue kitu katika ngawira pasi na idhini, msivunje mkataba na wala msikatekate viungo vya maiti na wala msimuue mtoto. Ukikutana na adui wako katika washirikina mlinganie katika mambo matatu. Ikiwa atakubali kwa lolote katika haya matatu basi mkubalie na jizue kumpiga vita. Mlinganie katika Uislamu. Akikukubalia hilo muitikie. Kisha mlinganie katika kuhama kutoka katika miji yao na kwenda katika miji ya Muhaajiruun na uwaambie ya kwamba ikiwa watafanya hivyo basi wana haki zote kama walizonazo Muhaajiruun na watakuwa na kama yale walionayo Muhaajiruun. Wakikataa kuhama kutoka katika miji yao waambieni ya kwamba watakuwa na hadhi kama ya mabedui wa Kiislamu na watapitishiwa hukumu ya Allaah (Ta’ala); hawatokuwa na haki yoyote ya ngawira wala fai isipokuwa ikiwa watapigana Jihaad bega kwa bega wakiwa pamoja na waislamu. Ikiwa watakataa waombeni kodi. Wakikubali wakubalieni na jizuieni kupigana nao. Ikiwa watakataa muombeni Allaah msaada na piganeni nao. Utapowazingira watu waliomo ngomeni na wakakutaka ufunge nao mkataba wa Allaah na mkataba wa Mtume Wake, basi usifunge mkataba wa Allaah na mkataba wa Mtume Wake. Lakini badaba yake funga nao mkataba wako wewe na mkataba wa Maswahabah wako. Kwani hakika mtapotaka kuvunja mikataba yenu na

²¹² al-Bukhaariy (1735).

mikataba ya Maswahabah wenu ni jambo jepesi kuliko kuvunja mkataba wa Allaah na mkataba Mtume Wake. Utapowazingira watu waliomo ngomeni na wakakutaka uwateremshe katika hukumu ya Allaah, usiwateremshe katika hukumu ya Allaah. Lakini badala yake wateremshe kwa hukumu yako. Kwani hakika hujui utapatia kwao hukumu ya Allaah au hapana.”

Maneno yake Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam):

“Mlinganie katika Uislamu.”

Kabla ya kila kitu walinganie kwanza katika shahaadah mbili. Kama ambavyo (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) alivyomwamrisha Mu‘aadh (Radhiya Allaahu ‘anh) wakati alipomtuma Yemen. Wakikubali shahaadah mbili na wakaitamka, ndipo uwafunze faradhi zengine.

Maneno yake Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam):

“... uwateremshe katika hukumu ya Allaah.”

Katika maamrishi na makatazo.

Maneno yake Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam):

“... waombeni kodi.”

Bi maana pale watapokataa kuingia katika Uislamu na wakakataa kuhama. Haya yanahusiana na mayahudi, manaswara na majusi. Allaah (Ta‘ala) amesema:

قَاتِلُوا الَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَلَا بِالْيَوْمِ الْآخِرِ وَلَا يُحَرِّمُونَ مَا حَرَّمَ اللَّهُ وَرَسُولُهُ وَلَا يَدِينُونَ دِينَ الْحَقِّ مِنَ الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ حَتَّى يُعْطُوا الْجِزْيَةَ عَنْ يَدٍ وَهُمْ صَاغِرُونَ

“Pambaneni na wale wasiomwamini Allaah na wala siku ya Mwisho na wala hawaharamishi aliyoyaharamisha Allaah na Mtume Wake na wala hawaiamini

na kuifuata dini ya haki katika wale waliopewa Kitabu – [pambaneni nao] mpaka watoe kodi kwa khiyari wakiwa ni wenye kudhalilika.” (at-Tawbah 09:29)

Sunnah imetaja watu ambao wanatakiwa kutoa kodi kwa kutokufungamanisha na Qur-aan imetaja kwa kufungamanisha mayahudi na manaswara. Sunnah imewafanya majusi wawe na hukumu hiyohiyo inapokuja katika kodi na si katika vichinjwa na wanawake.

Maneno yake Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam):

“... muombeni Allaah msaada na piganeni nao.”

Hii ni dalili inayoonyesha kuwa ni wajibu kumtaka msaada Allaah. Muumini anatakiwa kumtaka msaada Allaah wakati wa kupambana na maadui Wake na wala asitegemee nguvu zake mwenyewe.

Maneno yake Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam):

“Utapowazingira watu waliomo ngomeni...”

Mayahudi na manaswara walikuwa mara nyingi wakiwa katika ngome. Hawakuwa pamoja na mabedui huko jangwani.

Maneno yake Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam):

“... wakakutaka ufunge nao mkataba wa Allaah na mkataba wa Mtume Wake...”

Ni wajibu kwa waislamu kutovunja ahadi na mkataba. Vilevile wasifunge ahadi kwa jina la Allaah na Mtume Wake (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam). Kwa sababu ni sahali kuvunja ahadi kwa majina yao kuliko kwa jina la Allaah na Mtume Wake (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam). Hata kama matendo yote mawili hayafai, lakini baadhi ya shari na madhambi ni makubwa kuliko mengine.

Vivyo hivyo wasikubali kuhukumiwa kwa mujibu wa hukumu ya Allaah wakiomba hilo. Badala yake anatakiwa kuwahukumu kwa mujibu wa hukumu

ya wafuasi wake. Ni sawa akasema kuwa atafanya kila aliwezalo kuhukumu kwa mujibu wa Shari'ah inavosema, lakini asisemi ni kwa mujibu wa hukumu ya Allaah kwa sababu anaweza kukosea. Awawekee ijitahidi zake kwa mujibu wa vile Shari'ah inavosema. Kwa sababu akikosea anakuwa amemsema uongo Allaah. Kitendo hichi ni kwa sababu ya usalama na ni kwa sababu ya adabu ya Kishari'ah katika kufunga mikataba na ahadi na kumhukumu adui kwa njia inayomridhisha Allaah (Ta'ala).

64. Mlango kuhusu kumuapia Allaah

Shaykh-ul-Islaam Muhammad bin 'Abdil-Wahhaab (Rahimahu Allaah) amesema:

1- Jundub bin 'Abdillaah (Rahiya Allaahu 'anh) amesimulia kwamba Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Kuna mtu alisema: “Naapa kwa Allaah kwamba Allaah hatomsamehe fulani.” Allaah ('Azza wa Jall) akasema: “Ni nani huyo anayeniapia Mimi ya kwamba sintomsamehe fulani? Mimi nimemsamehe mtu huyo na nimeyaporomosha matendo yako.”²¹³

Ameipokea Muslim.

2- Katika Hadiyth ya Abu Hurayrah (Rahiya Allaahu 'anhu) imekuja ya kwamba mtu aliyesema hivi alikuwa ni mtu mwenye kufanya 'ibaadah. Abu Hurayrah (Radhiya Allaahu 'anh) amesema:

“Kaongea maneno ambayo yameiharibu dunia yake na Aakhirah yake.”

MAELEZO

Mlango huu ndani yake kuna matishio. Kumuapia Allaah ni kuthubutu kwa Allaah, kunaipunguza Tawhiyd na kuidhoofisha imani.

1- Jundub bin 'Abdillaah (Rahiya Allaahu 'anh) amesimulia kwamba Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Kuna mtu alisema: “Naapa kwa Allaah kwamba Allaah hatomsamehe fulani.” Allaah ('Azza wa Jall) akasema: “Ni nani huyo anayeniapia Mimi ya kwamba sintomsamehe fulani? Mimi nimemsamehe mtu huyo na nimeyaporomosha matendo yako.”

²¹³ Muslim (2621).

Jundub pia inaweza kusemwa Jundab.

Hadiyth hii ndani yake kuna matahadharisho ya kumuapia Allaah kwamba hatofanya kitu kadhaa kama vile kumsamehe fulani na mfano wake. Yote hii ni dhuluma na kuthubutu. Ni jambo lisilojuzu kwa sababu mtu hajui Allaah atachofanya na hana haki yoyote ya mtu huyo hata kama mtu huyu ni mtenda dhambi mkubwa. Wajibu wako ni kumuomba uongofu. Allaah anaweza kumsamehe pasi na wewe kujua. Haya yanaonyesha ukhatari wa ulimi. Ni wajibu kuuchunga ulimi wako na kutoongea namna hii kwa sababu ni jambo linaipunguza Tawhiyd na imani.

2- Katika Hadiyth ya Abu Hurayrah (Rahiya Allaahu 'anhu) imekuja ya kwamba mtu aliyesema hivi alikuwa ni mtu mwenye kufanya 'ibaadah. Abu Hurayrah (Radhiya Allaahu 'anh) amesema:

“Kaongea maneno ambayo yameiharibu dunia yake na Aakhirah yake.”

Kilichomfanya kuongea maneno haya mabaya ilikuwa ni ghera na 'ibaadah zake. Hii ni dalili inayoonyesha kuwa mtu anaweza kuingiwa na ghera mbaya ambapo akathubutu kumuapia Allaah. Anaweza kuwa ni mwenye ghera na anaamrisha mema na kukataza maovu pasi na elimu. Pengine anakataza maovu pasi na elimu. Kwa ajili hiyo ni wajibu mtu kushikamana na vigezo vya Kishari'ah katika kuamrisha mema na kukataza maovu na kukomeka na mipaka ya Allaah. Abu Hurayrah (Radhiya Allaahu 'anh) amesema:

“Kaongea maneno ambayo yameiharibu dunia yake na Aakhirah yake.”

Kwa sababu yalikuwa maneno khatari. Katika Hadiyth imekuja:

“Mja atatamka maneno asiyotia manani maana yake ambapo yakamfanya kutupwa Motoni umbali wa mashariki na mgharibi.”²¹⁴

²¹⁴ al-Bukhaariy (6477) na Muslim (2988).

Ameipokea Muslim.

Katika upokezi mwingine imekuja:

“Mja atatamka maneno kwa njia ambayo haikumbainikia yakaamsha hasira za Allaah ambapo Allaah akaandika hasira Zake katika ile Siku atayokutana Naye.”²¹⁵

²¹⁵ Maalik (1781), at-Tirmidhiy (2319), Ibn Maajah (3969) na al-Haakim (137). Swahiyh kwa mujibu wa al-Albaaniy katika "as-Swahiyhah" (888).

65. Haombwi Allaah kupitia viumbe Wake

Shaykh-ul-Islaam Muhammad bin 'Abdil-Wahhaab (Rahimahu Allaah) amesema:

1- Jubayr bin Mutw'im (Radhiya Allaahu 'anh) amesema:

“Alikuwa bedui kwa Mtume Muhammad (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) na kumwambia: “Ee Mtume wa Allaah! Watu wanaangamia, familia zina njaa na mali zinaangamia. Muombe Mola Wako atunyweshelee! Hakika sisi tunaomba maombezi kwa Allaah kupitia kwako na kwa maombi yako kwa Allaah.” Ndipo Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) akasema: “Allaah ametakasika! Allaah ametakasika!” Hakuacha kusabihi mpaka likajulikana hilo katika nyuso za Maswahabah wake. Kisha akasema Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam): “Ole wako! Je, unamjua ni nani Allaah? Hakika Jambo la Allaah ni kubwa zaidi kuliko hivyo. Hakika haombwi Allaah kwa yeyote yule katika viumbe Vyake.”²¹⁶

Ameipokea Abu Daawuud.

MAELEZO

Mwandishi ametaja mlango huu kwa sababu inahusiana na kuikamilisha Tawhiyd na imani. Yaliyotajwa katika Hadiyth ni miongoni mwa njia zinazopelekea katika shirki, kumuomba Allaah kupitia viumbe. Allaah ni mtukufu zaidi kuliko hivo. Allaah hatakiwi kuombwa kupitia viumbe Wake kwa njia ya kwamba mtu akasema:

“Namuomba Allaah kupitia kwako.”

²¹⁶ Abu Daawuud (4726) na at-Twabaraaniy katika "al-Mu'jam al-Kabiy" (1547). Dhaifu kwa mujibu wa al-Albaaniy katika "Dhwa'iyf Sunan Abiy Daawuud" (1017).

Lakini mtu anaweza kumuomba mwenzie kupitia viumbe wengine kwa kusema:

“Namuomba fulani kupitia kwako.”

Hili halina neno tofauti na kumuomba Allaah kupitia mtu. Haijuzu, kwa sababu Allaah ni mtukufu zaidi kuliko hivo. Kwani yule aombwaye ni mkubwa kuliko yule mwombezi. Kitu kama hicho hakistahiki kwa sababu Allaah ni mkubwa na mtukufu zaidi kuliko kila kitu. Allaah anatakiwa kuombwa kupitia majina na sifa Zake.

1- Jubayr bin Mutw'im (Radhiya Allaahu 'anh) amesema:

“Alikuwa bedui kwa Mtume Muhammad (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) na kumwambia: “Ee Mtume wa Allaah! Watu wanaangamia, familia zina njaa na mali zinaagamia. Muombe Mola Wako atunyweshelee! Hakika sisi tunaomba maombezi kwa Allaah kupitia kwako na kwa maombi yako kwa Allaah.” Ndipo Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) akasema: “Allaah ametakasika! Allaah ametakasika!” Hakuacha kusabihi mpaka likajulikana hilo katika nyuso za Maswahabah wake. Kisha akasema Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam): “Ole wako! Je, unamjua ni nani Allaah? Hakika Jambo la Allaah ni kubwa zaidi kuliko hivyo. Hakika haombwi Allaah kwa yeyote yule katika viumbe Vyake.”

Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) alikuwa akisema “Allaah ametakasika” wakati tunapotokea tukio kubwa, jambo lililompendeza au lililomchukiza, na mambo ambayo yamemshangaza au anayoyakemea. Kuna Hadiyth nyingi juu ya hilo kukiwemo ile Hadiyth kuhusu mkunazi na kwamba Ummah huu nusu ya watu wake watakuwa Peponi.

66. Mtume (صلى الله عليه وسلم) kuihami Tawhiyd na kuziba njia zote za shirki

Shaykh-ul-Islaam Muhammad bin 'Abdil-Wahhaab (Rahimahu Allaah) amesema:

1- 'Abdullaah bin ash-Shukhayr (Radhiya Allaahu 'anh) amesema:

"Nilifuatana na mjumbe wa Banuu 'Aamir kwa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam). Tukasema: "Wewe ndiye bwana wetu." Akasema: "Bwana ni Allaah (Tabaarak wa Ta'ala)." Tukasema: "Wewe ni mbora wetu kwa ubora na ni mkubwa wetu kwa ukarimu." Akasema: "Semeni msemayo, au baadhi yake tu, na wala asikupotezeni shaytwaan."²¹⁷

Ameipokea Abu Daawuud kwa cheni ya wapokezi nzuri.

2- Anas (Radhiya Allaahu 'anh) ameeleza kwamba kuna watu walisema:

"Ee Mtume wa Allaah! Ee mbora wetu na mtoto wa mbora wetu! Bwana wetu na mtoto wa bwana wetu." Ndipo akasema: "Enyi watu! Semeni msemayo, au baadhi yake tu, na wala asikupotezeni shaytwaan. Mimi ni Muhammad, ni mja wa Allaah na Mtume Wake. Sipendi mnipandishe zaidi ya cheo changu alichonipa Allaah ('Azza wa Jalla)."²¹⁸

Ameipokea an-Nasaa'iy kwa cheni ya wapokezi nzuri.

MAELEZO

Hapa mwandishi anazungumzia kuihami Tawhiyd kwa njia ya maneno. Tayari kuihami Tawhiyd kwa njia ya matendo kumeshatangulia. Mlango huu

²¹⁷ Abu Daawuud (4806) na al-Bukhaariy katika "al-Adab al-Mufrad" (211). Cheni ya wapoezi wake ni Swahiyh kwa mujibu wa al-Albaaniy katika "Mishkaat-ul-Maswaabiyh" (4900).

²¹⁸ Ahmad (13553) na an-Nasaa'iy (10078). Swahiyh kwa mujibu wa al-Albaaniy katika "Iswwaah-ul-Masaajid" (1/126).

unazungumzia kuihami mipaka ya Tawhiyd. Mipaka sio dhati yenyewe ya kitu. Kwa hiyo kichwa cha khabari ni chenye nguvu zaidi juu ya yale yaliyofungamana na Tawhiyd na maneno.

Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amehami Tawhiyd na akaihami mipaka ya Tawhiyd dhidi ya maneno na vitendo ili watu wasije kuisogelea Tawhiyd na kutumbukia ndani yake. Alitahadharisha (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) vilevile juu ya njia zote zinazopelekea katika shirki, jambo ambalo ni miongoni mwa ukamilifu wa ujumbe.

1- 'Abdullaah bin ash-Shukhayr (Radhiya Allaahu 'anh) amesema:

“Nilifuatana na mjumbe wa Banuu 'Aamir kwa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam). Tukasema: “Wewe ndiye bwana wetu.” Akasema: “Bwana ni Allaah (Tabaarak wa Ta'ala).” Tukasema: “Wewe ni mbora wetu kwa ubora na ni mkubwa wetu kwa ukarimu.” Akasema: “Semeni msemayo, au baadhi yake tu, na wala asikupotezeni shaytwaan.”

Ameipokea Abu Daawuud kwa cheni ya wapokezi nzuri.

Maneno yake Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam):

“Bwana ni Allaah (Tabaarak wa Ta'ala).”

Alisema (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) hivo kwa sababu ya unyenyekevu na kuchelea wasije kutumbukia katika upetukaji. Vinginevyo yeye (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) ndiye bwana wa wanaadamu. Lakini alisema hivo kwa sababu ya unyenyekevu na kwa kukhofia wasije kutumbukia katika kuchupa mipaka. Ni dalili inayoonyesha kuwa mtu akiambiwa na mwengine kwamba yeye ni bwana wao basi anatakiwa kusema:

“Bwana ni Allaah (Tabaarak wa Ta'ala).”

Anasema hivi ili asije kuingiwa na majivuno.

Maneno yake Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam):

“... na wala asikupotezeni shaytwaan.”

Bi maana shaytwaan asije kuwavuta katika mambo yasiyotakikana. Msimwache akakuingizeni katika shirki na kuvuka mipaka. Tumieni maneno yaliyozoeleka kama vile Abul-Qaasim, Mtume wa Allaah na Nabii wa Allaah. Msitumie maneno ambayo yanaweza kukuingizeni katika kuchupa mipaka. Allaah (Ta'ala) amesema:

أَيُّهَا الرَّسُولُ

“Ee Mtume!” (al-Maaidah 05:67)

يَا أَيُّهَا النَّبِيُّ

“Ee Nabii!” (al-Mumtahinah 60:12)

سُبْحَانَ الَّذِي أَسْرَى بِعَبْدِهِ لَيْلًا

“Utakasifu ni wa ambaye Alimsafirisha usiku mja Wake... ” (al-Israa' 17:01)

حَمْدٌ لِلَّهِ الَّذِي أَنْزَلَ عَلَىٰ عَبْدِهِ الْكِتَابَ وَلَمْ يَجْعَلْ لَهُ عِوَجًا

“Himdi zote anastahiki Allaah ambaye amemteremshia mja Wake Kitabu na wala hakukifanya kikawa na ukombo.” (al-Kahf 18:01)

Makusudio ya haya yote ni kufunga njia zote ziwezazo kuwapelekea watu kuchukulia wepesi shirki. Wakitumia maneno kama “bwana” na mfano wake katika upetukaji ambayo yanatumiwa na watu hii leo matokeo yake yanaweza kuwafanya wakaanza kumwabudu badala ya Allaah, wakamuomba, wakamtaka

msaada, kudai kwamba anajua mambo yaliyofichikana na mfano wake. Kama alivosema mwandishi wa “al-Burdah” wakati aliposema:

Ee kiumbe mbora! Sina mwengine zaidi yako wa kumkimbilia wakati wa majanga

Usiponitukuzi siku ya Qiyaamah na ukanishika mkono, nimeangamia.

Katika ukarimu wako ni pamoja na dunia hii na mali zake

na miongoni mwa elimu zako ni pamoja na elimu ya Ubao na Kalamu.

Kuvuka mipaka kulimpelekea akasema kwamba Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) ndiye ambaye atamwokoza siku ya Qiyaamah na kwamba yule ambaye hatookolewa na Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) basi ameangamia. Huu ni upetukaji mkubwa. Amesema vilevile kwamba Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) anayajua yaliyomo katika Ubao na katika Kalamu na kwamba yeye anakijua kila kitu.

Ni wajibu kwa muislamu kuuchunga ulimi wake na awe mkati na kati anapoongea sawa akiwa anamzungumzia Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) au mwengine. Ni lazima kwake kujipamba na adabu za Kishari’ah inapokuja kwa Mitume (Swalla Allaahu ‘alayhim wa sallam), waja wema na wanachuoni ili asije kutumbukia katika upetukaji waliyotumbukia ndani yake mayahudi na manaswara. Hatimaye wakaanza kuwaabudu Mitume wao, waja wao wema na wanachuoni na wakawaomba msaada. Wakatumbukia katika shirki kubwa ambayo ndio dhambi isiyosamehewa.

67. Mlango kuhusu maneno Yake (Ta'ala) “Hawakumkadiria Allaah inavyostahiki kukadiriwa!”

Shaykh-ul-Islaam Muhammad bin 'Abdil-Wahhaab (Rahimahu Allaah) amesema:

1- Allaah (Ta'ala) amesema:

وَمَا قَدَرُوا اللَّهَ حَقَّ قَدْرِهِ وَالْأَرْضُ جَمِيعًا قَبْضَتُهُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ وَالسَّمَاوَاتُ مَطْوِيَّاتٌ بِيَمِينِهِ

“Hawakumkadiria Allaah inavyostahiki kukadiriwa! Ardhi yote itakamatwa mkononi Mwake wa kuume siku ya Qiyaamah.” (az-Zumar 39:67)

2- Ibn Mas'ud (Radhiya Allaahu 'anh) amesema:

“Kuna mwanachuoni mmoja wa kiyahudi alikuja kwa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) na akamwambia: “Ee Muhammad! Sisi tunakuta kuwa Allaah ataziweka mbingu saba juu ya kidole, ardhi saba juu ya kidole, miti juu ya kidole, maji na vumbi juu ya kidole na viumbe vyengine vilivyobaki juu ya kidole. Halafu atasema: “Mimi ndiye Mfalme.” Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) akacheka mpaka magego yake yakaonekana kwa kusadikisha maneno ya mwanachuoni huyu. Kisha akasoma:

وَمَا قَدَرُوا اللَّهَ حَقَّ قَدْرِهِ وَالْأَرْضُ جَمِيعًا قَبْضَتُهُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ وَالسَّمَاوَاتُ مَطْوِيَّاتٌ بِيَمِينِهِ

“Hawakumkadiria Allaah inavyostahiki kukadiriwa! Ardhi yote itakamatwa mkononi Mwake wa kuume siku ya Qiyaamah.”

3- Katika upokezi mwingine wa Muslim imekuja:

“... milima na miti juu ya kidole. Kisha atavitikisa na atasema: “Mimi ndiye Mfalme, Mimi ndiye Allaah.”

Katika upokezi mwingine wa al-Bukhaariy imekuja:

“Allaah ataziweka mbingu juu ya kidole, maji na mchanga juu ya kidole na viumbe vyengine vilivyobaki juu ya Kidole.”

Ameipokea al-Bukhaariy na Muslim²¹⁹.

Muslim amepokea kupitia kwa Ibn 'Umar (Radhiya Allaahu 'anhumaa) ambaye ameeleza kwamba Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Allaah atazikunja mbingu siku ya Qiyaamah, kisha atazishika kwa mkono Wake wa kulia. Halafu atasema: “Mimi ndiye Mfalme! Wako wapi wenye jeuri? Wako wapi wenye kiburi?” Kisha atazikunja ardhi saba, kisha atazishika kwa mkono Wake wa kushoto kisha atasema: “Mimi ndiye Mfalme! Wako wapi wenye jeuri? Wako wapi wenye kiburi?”²²⁰

Imepokelewa kutoka kwa Ibn 'Abbaas (Radhiya Allaahu 'anhumaa) kwamba amesema:

“Hazikuwa mbingu saba wala ardhi saba katika kiganja cha Mwingi wa rehema isipokuwa ni kama chembe ya hardali katika kiganja cha mmoja wenu.”

Ibn Jariyr kasema: “Yuunus amenihadithia: Ibn Wahb ametukhabarisha: Ibn Zayd amesema: Baba yangu amenihadithia: Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Mbingu sana ukizilinganisha na Kursiy ni kama mfano wa vipande saba vya fedha vilivyotupwa katika ngao.”

²¹⁹ al-Bukhaariy (4811) na Muslim (2786).

²²⁰ Muslim (2788).

Abu Dharr (Radhiya Allaahu 'anh) amesema kuwa amemsikia Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) akisema:

“Kursiy ukiilinganisha na 'Arshi si kitu isipokuwa ni kama mfano wa kijipete cha chuma kilichotupwa katika uwanja mkubwa.”²²¹

4- Ibn Mas'ood (Radhiya Allaahu 'anh) amesema:

“Masafa ya baina ya mbingu ya dunia na inayofuatia ni miaka 500. Baina ya kila mbingu mpaka nyingine ni miaka 500. Baina ya mbingu ya saba na Kursiy ni miaka 500. Baina ya Kursiy na maji ni miaka 500. 'Arshi iko juu ya maji na Allaah Yuko juu ya 'Arshi na hakuna kinachofichikana Kwake katika matendo yenu.

Ameipokea Ibn Mahdiy kutoka kwa Hammaad bin Salamah, kutoka kwa 'Aaswim, kutoka kwa Zirr, kutoka kwa 'Abdullaah. al-Mas'uudiy amepokea mfano wahiyo, kutoka kwa 'Aaswim, kutoka kwa Abu Waa-iyI, kutoka kwa 'Abdullaah. Haafidhw adh-Dhahabiy (Rahimahu Allaah) amesema:

“Imepokelewa kwa njia nyingi.”

5- al-'Abbaas bin 'Abdil-Muttwalib (Radhiya Allaahu 'anh) amesimulia kwamba Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Hivi mnajua ni masafa ngapi baina ya mbingu na ardhi?” Tukajibu: “Allaah na Mtume Wake ndio wajuzi zaidi.” Akasema: “Baina yake kuna masafa ya miaka 500. Kutoka katika mbingu moja hadi nyingine ni mwendo wa miaka 500. Unene wa kila mbingu ni mwendo wa miaka 500. Baina ya mbingu ya saba na 'Arshi kuna bahari. Kutoka chini yake mpaka juu yake ni kama umbali wa baina mbingu na ardhi. Allaah (Subhaanahu wa Ta'ala) Yuko juu ya hivyo na hakuna kinachojificha katika matendo ya wanaadamu.”²²²

²²¹ Jaami'-ul-Bayaan (5/399) na Abuush-Shaykh katika "al-'Adhwamah" (2/587).

²²² Ahmad (1770), Abu Daawuud (4723), at-Tirmidhiy (3320), Ibn Maajah (193) na al-Haakim (3137). Dhaifu kwa mujibu wa al-Albaaniy katika "Dhwa'iyf-ul-Jaami'" (6093).

Ameipokea Abu Daawuud na wengineo.

MAELEZO

Mlango huu wa mwisho umekusanya sampuli zote tatu za Tawhiyd:

1- Allaah (Ta'ala) amesema:

وَمَا قَدَرُوا اللَّهَ حَقَّ قَدْرِهِ وَالْأَرْضُ جَمِيعًا قَبْضَتُهُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ وَالسَّمَاوَاتُ مَطْوِيَّاتٌ بِيَمِينِهِ

“Hawakumkadiria Allaah inavyostahiki kukadiriwa! Ardhi yote itakamatwa mkononi Mwake wa kuume siku ya Qiyaamah.”

Aayah hii inathibitisha ukubwa wa utukufu Wake (Subhaanahu wa Ta'ala) na kwamba atazikunja mbingu na ardhi. Aliye na sifa kama hii ana kila haki ya kuabudiwa na kutiwa. Yeye ndiye Mwenye ukamilifu katika majina, sifa na matendo Yake. Yeye hana anayefanana Naye, hana mshirika na wala halinganishwi na viumbe Wake. Yeye ni muweza wa kila jambo.

2- Ibn Mas'uud (Radhiya Allaahu 'anh) amesema:

“Kuna mwanachuoni mmoja wa kiyahudi alikuja kwa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) na akamwambia: “Ee Muhammad! Sisi tunakuta kuwa Allaah ataziweka mbingu saba juu ya kidole, ardhi saba juu ya kidole, miti juu ya kidole, maji na vumbi juu ya kidole na viumbe vyengine vilivyobaki juu ya kidole. Halafu atasema: “Mimi ndiye Mfalme.” Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) akacheka mpaka magego yake yakaonekana kwa kusadikisha maneno ya mwanachuoni huyu. Kisha akasoma:

وَمَا قَدَرُوا اللَّهَ حَقَّ قَدْرِهِ وَالْأَرْضُ جَمِيعًا قَبْضَتُهُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ وَالسَّمَاوَاتُ مَطْوِيَّاتٌ بِيَمِينِهِ

“Hawakumkadiria Allaah inavyostahiki kukadiriwa! Ardhi yote itakamatwa mkononi Mwake wa kuume siku ya Qiyaamah.”

Hadiyth inathibitisha kwamba Allaah ana sifa na kwamba Yeye (Subhaanah) ana mkono wa kuume na wa kushoto na kwamba yote miwili ni ya kuume, kama ilivyokuja katika Hadiyth nyingine. Mmoja unaitwa mkono wa kuume na mwingine unaitwa mkono wa kushoto, lakini inapokuja kimaana na utukufu mikono yake yote miwili ni ya kuume na haina aina yoyote ile ya mapungufu. Vivyo hivyo Hadiyth hii inathibitisha kiganja cha Allaah:

“Hazikuwa mbingu saba wala ardhi saba katika kiganja cha Mwingi wa rehema isipokuwa ni kama chembe ya hardali katika kiganja cha mmoja wenu.”

5- al-'Abbaas bin 'Abdil-Muttwalib (Radhiya Allaahu 'anh) amesimulia kwamba Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema:

“Hivi mnajua ni masafa ngapi baina ya mbingu na ardhi?” Tukajibu: “Allaah na Mtume Wake ndio wajuzi zaidi.” Akasema: “Baina yake kuna masafa ya miaka 500. Kutoka katika mbingu moja hadi nyingine ni mwendo wa miaka 500. Unene wa kila mbingu ni mwendo wa miaka 500. Baina ya mbingu ya saba na 'Arshi kuna bahari. Kutoka chini yake mpaka juu yake ni kama umbali wa baina mbingu na ardhi. Allaah (Subhaanahu wa Ta'ala) Yuko juu ya hivyo na hakuna kinachojificha katika matendo ya wanaadamu.”

Hadiyth hizi zinathibitisha sifa za Allaah na Allaah kuwa juu. Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa'ah wameafikiana juu ya kwamba Allaah yuko juu ya 'Arshi na juu ya viumbe Wote na kwamba ujuzi Wake umeenea kila mahali. Dalili juu ya hili hazidhibitiwi.

Hadiyth ya Ibn Mas'uud (Radhiya Allaahu 'anh) ni Swahiyh na nzuri. Vivyo hivyo Hadiyth ya al-'Abbaas, hata kama cheni ya wapokezi imekatika, inatiwa nguvu na zengine. Kuna mapokezi mengine yanayosema kwamba masafa ni 71, 72 na 73. Wanachuoni wameyaoanisha baina yake kwamba tofauti hizo zinatokamana na kasi ya ule mwendo. Kwa njia hiyo mwendo wa miaka 500 ni ngamia aliyebeba mizigo, mtu anayetembea kwa miguu na mwendo wa kawaida ilihali miaka 73 ni mwendo khafifu na wenye nguvu kiasi ambao kasi yake ni

mara sita ukilinganisha na ule mwendo mzito. Kwa hali yoyote ile zinafahamisha juu ya utukufu na ujuu wa Allaah na kwamba hakuna matendo ya wanaadamu wowote yanayofichikana Kwake.

Hadiyth zinafahamisha vilevile ujuu wa viumbe vilivyotajwa na namna masafa marefu yaliyo baina yake. Hata hivyo Mola wako na Muumbaji Wako (Jalla wa 'Alaa) ambaye kaviumba ni mtukufu na mkubwa zaidi.

Himdi zote zinamstahikia Allaah, Mola wa walimwengu. Swalah na salamu zimwendee Mtume wetu Muhammad, kizazi chake na Maswahabah wake.